

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

### **BUNGE LA TANZANIA**

---

### **MAJADILIANO YA BUNGE**

---

### **MKUTANO WA SITA**

**Kikao cha Nane – Tarehe 10 Februari, 2022**

*(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)*

### **D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu!

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:**  
Hati za kuwasilisha Mezani.

### **HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:

**MHE. KASSIM HASSAN HAJI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2021.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI:** Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2021.

**SPIKA:** Ahsante sana.  
Katibu.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:**

### **MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyo ada ninayo majina hapa ya Wabunge wengi kidogo amba wameomba kuuliza maswali ya kisera kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tutaanza na Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata fursa ya kuuliza swali kwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na kazi nzuri ili ofanywa na Kamati ya Mawaziri Nane ya kutatua migogoro kati ya hifadhi, hususan *TFC* na *TANAPA*, lakini kuna vijiji ambavyo bado havijafikiwa vikiwemo vijiji katika Wilaya ya Mbeya. Je, ni lini Kamati hii itarejea kukamilisha hilo zoezi muhimu kwa maeneo yaliyobaki nchi nzima? Nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu kwa swali hilo.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Serikali iliunda timu ya Mawaziri Nane kwa ajili ya kuhakiki vijiji ambavyo vina changamoto au migogoro kati ya vijiji hivyo na hifadhi. Mnatambua Waheshimiwa Wabunge tulipata taarifa za awali za utekelezaji huo na bado kazi hiyo inaendelea.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Njeza anahitaji kujuu lini kazi hiyo itakamilika, ili tuweze kwenda kule Mbeya. Nataka nimhakikishie kwamba, kazi ili ofanywa awali ambayo ilibaini vijiji vipatavyo mia tisa kama 75 hivi na kati ya hivyo ilithibitika kuwa vijiji mia tisa na 20 havikuwa na

matatizo na bado vilikuwa vinatakiwa kuishi huko kwenye maeneo ambayo tuliyahifadhi, lakini hayana tija. Bado Serikali inakusudia kutambua vijiji kadhaa vyenye migogoro ya aina hii katika vijiji na hifadhi, pale ambapo tunaona kwamba, uhifadhi wake hauna tija kwa malengo yaliyokusudiwa, vijiji hivyo vitapata nafasi ya kuendelea kushiriki shughuli za kijamii kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, pindi Kamati itakapokamilisha, tutakuja kutoa taarifa nyingine tena baada ya taarifa ya awali. Sasa, naielekeza Kamati ile pia, kuweka mpango kazi wa kwenda Mbeya Vijiji kuona huko ambako Mheshimiwa Mbunge anasema bado hatujafika, waone vijiji hivyo, lakini pia, aina ya mgogoro uliopo na nini tufanye baada ya kuhakiki. Kwa hiyo, Kamati ya Mawaziri wale nane itakapokamilisha kazi hiyo tutaipata.

Mheshimiwa Spika, nitoe wito, tunatambua tuna migogoro mingi, iko migogoro ya mipaka katika vijiji na vijiji vyenyewe, iko migogoro ya wafugaji na wakulima, bado nielekeze kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, hususan Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, lakini tunashuka chini kule kwa Watendaji wa Kata na Vijiji kuhakiki migogoro hii na tujiridhishe kuwa inakamilishwa hukohuko kwenye ngazi hiyo, badala ya kutegemea Mawaziri ambao wako hapa Dodoma wasafiri waje kwenye vitongoji na vijiji badala ya kuwa wamekamilisha kule na Mawaziri wapate unafuu wa kutekeleza hili. Ikkifika hatua hiyo ya kila mmoja kuwajibika kwenye nafasi yake hii migogoro itapungua kwa kiasi kikubwa, kama sio kuimaliza kabisa. Ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii muhimu. Kumekuwa na changamoto ya ukame kujirudiarudia nchini kwetu na matokeo yake ukame huu umeleta athari nyingi, ikiwemo mifugo kufa kwa kukosa malisho.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Waziri Mkuu, je, Serikali ina mkakati gani wa muda wa kati na wa muda mrefu wa kukabiliana na ukame huu hususan kwenye malisho ya mifugo? Nashukuru. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Komanya, Mbunge wa Meatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, amezungumzia ukame, anataka kujua mpango wa Serikali wa kukabiliana na ukame huu; ukame unaojitokeza mara nyingi nchini ni mabadiliko ya hali ya tabianchi ambayo yanaleta athari ya kukosekana kwa mvua na hasa pale ambapo athari hizo zinasababisha kutopata mvua kama ambavyo mwaka huu na mwaka uliopita hapa nchini kwetu, maeneo mengi yalikuwa makame kwa sababu hakuna mvua. Hii ni kutokana na mabadiliko ya tabianchi, lakini pia, ukame huu unatokana na uharibifu tu wa mazingira ambao wananchi wanaufanya kwenye maeneo yetu kwa kukata misitu na maeneo ambayo tunategemea sana kuwa na mvua.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, imeendelea kutoa elimu ya wananchi kuhifadhi mazingira kwenye maeneo yao ikiwemo misitu, ili isaidie kuleta mvua kwenye maeneo hayo kuachana na ukame. Hiyo ndio njia moja muhimu ambayo mimi naiona, lakini pia umehusisha maeneo ya malisho ya malisho ya mifugo. Kutokana na ukame huu ni kweli hatupati malisho na kwa hiyo, ni lazima pia tuhakikisha kwamba, tunaendelea kuhifadhi mazingira haya tupate mvua ili malisho mengi yaweze kupatikana.

Mheshimiwa Spika, ukiondoa ukame, lakini bado hata Wizara ya Mifugo na Uvuvi wanajitahidi sana kutoa elimu kwa wafugaji kuhakikisha kuwa wanafuga kitaalam kulingana na ukubwa wa malisho waliyonayo, ili kukabiliana na upungufu wa malisho ambayo kwa sasa yanakuwa hayapatikani kwa

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

sababu ya kuwa na mifugo mingi zaidi. Jana tumelizungumza hapa ndani ya Bunge juu ya Ngorongoro kule, uharibifu unaoendelea kule Ngorongoro itakwisha, lakini hili ni sisi wenyewe ndio tutaweza kukabiliana nalo na kwa kuwa Serikali imeweka mkakati wa kuelimisha umma juu ya uhifadhi wa mazingira, lakini pia Wizara ya Mifugo inaendelea kuwaelimisha wafugaji, ili tuanze kuandaa malisho kwa kuhifadhi malisho, lakini pia tuweze kuchimba visima kupata maji ya chini na kuanza kumwagilia kwenye maeneo ambayo tumeyatenga kama maeneo ya malisho.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla wake kwenye mifugo tumefanya jitihada kubwa sana za maeneo yetu yale ya *ranch*. Tumegawa vipande, vinaitwa *blocks* na kuwagawia wafugaji ili kila mmoja aweze kutunza maeneo hayo na ikiwezekana pia na kupanda nyasi ikiwa ni njia ya kupata malisho mapya, ili mifugo iweze kuendelea.

Mheshimiwa Spika, nitoe wito sasa kwa Watanzania, ili kukabiliana na ukame ambaao unaendelea ni lazima tuungane pamoja turekebishe, tuache tabia ya kukata miti na misitu kwenye maeneo tuliyonayo ili misitu hii iweze kutusaidia kupata mvua za kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitoe wito pia kwa ndugu zangu wafugaji waendelee kufuga kitaalam, tuwe na mifugo michache unayoweza kuihudumia ikiwemo kupata na malisho, ikiwezekana pia hata kuboresha malisho kwa mifugo uliyonayo badala ya kuwa ng'ombe zaidi ya 2,000 ambaao hauna uwezo wa kuwafuga na matokeo yake kukosa malisho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, huo ndio ujumbe wangu kwa swali ambalo Mheshimiwa Mbunge ameliuliza. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mbunge wa Jimbo la Msalala.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kumekuwepo na ongezeko la bei za bidhaa mbalimbali nchini kote, lakini hasa Mkoa wa Shinyanga, Wilaya ya Kahama, Jimbo la Msalala na hususan bidhaa hizo ni mafuta ya kula, sabuni, lakini pia vifaa vya ujenzi kama nondo, simenti. Ni nini sasa kauli ya Serikali juu ya ongezeko au mfumuko wa bei katika bidhaa hizi mbalimbali? Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Iddi Kassim, Mbunge wa Msalala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kumejitokeza siku za karibuni kupanda kwa bei kwa baadhi ya bidhaa zinazozalishwa hapa nchini. Upandaji wa bei hizni wakati mwagine ni wa makusudi unaofanywa na baadhi ya wafanyabiashara ambao sio waaminifu, lakini pia, upatikanaji wa malighafi. Viwanda vyote ambavyo vinazalisha hapa nchini vingi miongoni mwake vinategemea malighafi kutoka hapa nchini na malighafi zipo.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka siku tatu, nne zilizopita, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, amezungumza na Taifa kwa kuwaambia kwamba, uko mkakati wa baadhi ya wafanyabiashara waovu wasiokuwa na nia njema wa kupandisha bidhaa kwa makusudi tu; moja, kwanza wanazalisha kidogo sana ili kutengeneza upungufu mtaani ili bei ziweze kupanda. Mbili, kumekuwa na utamaduni sasa wa baadhi ya wafanyabiashara waovu kukaa pamoja na kujadili tu bei ziweje na kusababisha mfumuko wa bei. Serikali tumeligundua hilo na ndio kwa sababu, Waziri Dkt. Kijaji, ametoka hadharani kutueleza mkakati wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono kauli yake, lakini pia, natoa agizo kwa wafanyabiashara kuacha tabia hiyo ovu inayosababisha jamii kushindwa kupata bidhaa kwa gherama nafuu kwa sababu, wakati tunawekeana mikataba

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

na wakati tunajenga mazingira rahisi ya uwekezaji nchini, lengo la kwanza kubwa ilikuwa ni kupata bidhaa kwa wingi, kwa bei nafuu, lakini pia zipatikane wakati wote, sasa wengine wanaanza kukiuka masharti yetu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ametoa *ultimatum* kwao, nami narudia tena, hatutasita kuchukua hatua kwa wafanyabiashara ambao wanaweka mkakati tu wa kutaka kusumbua jamii kwa kununua bidhaa kwa bei ya juu bila sababu yoyote, kwa sababu, bidhaa tunazo, malighafi tunazo na viwanda viwo, uboreshaji ndani ya Serikali wa uwekezaji tumeufanya kwa kiasi kikubwa na kila siku tunakutana nao na wanaeleza namna ambavyo tungependa Serikali iwe na sisi Serikali tunafanya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili ambalo Mheshimiwa amelieleza, Serikali itaendelea kuchukua hatua kali na tutasimamia upandaji wa bidhaa hizi usiende kupanda mara zote. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nataka niagize taasisi yetu inaitwa *FCC*, ambayo inasimamia haki za wafanyabiashara katika kufanya biashara, ihakikishe inafanya ukaguzi wa kina kila bidhaa zinazozalishwa na mauzo yao, walinganishe na uzalishaji wao, uwezo wa kiwanda kwa mwaka, tuone kama je, wanazalisha kwa kiwango kilekile tulichokubaliana au wamepunguza uzalishaji kutengeneza upungufu? Pia tujue kwa nini wanapandisha bei, katika ya kiwanda na kiwanda bei zinatofautiana? Hili nalo tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niahidi kwamba, tutalifanyia kazi kupitia taasisi zetu za ndani ya Serikali, kama alivyoahidi Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Waziri Mkuu

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

swali. Mwaka 1994 aliyejekuwa Waziri Mkuu, Ndugu yetu Samuel Malecela, alitoa tamko juu ya mabasi yanayosafiri usiku na kusema yasisafiri usiku. Tamko lile halikuwa na sheria wala sera. Ni nini Serikali sasa inasema kwa kuwa, nchi yetu sasa imekuwa ni nchi ya katika uchumi unatakiwa uende mbele.

Mheshimiwa Waziri Mkuu unaonaje kwamba, mabasi hayo yaruhusiwe kutembea usiku na mchana ili tuweze kuongeza kipato, na hasa patola Taifa kwa Watanzania wote kwa kuwa, mabasi yakifanya mchana peke yake tunalala usiku bila kuingiza fedha yoyote? Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwakagenda, Mbunge wa Mbeya, lakini sio Mbeya Mjini, Mbunge wa Mkoa wa Mbeya, kama ifuatavyo:- (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mara kadhaa tumekuwa tukitoa maelekezo, hasa kwenye eneo la usafiri, kulingana na hali ya usalama iliyoko nchini. Wakati huo agizo hili lilitolewa kwa sababu, mara nyingi mabasi yalikuwa yanatekwa yanaposafiri na tulikuwa tunalazimika pia kuweka jeshi la polisi kila basi linaposafiri ili kuhakikisha kwamba, wasafiri wanasafiri salama.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, sasa usalama umeimarika nchini na Serikali inaendelea kuimarisha zaidi usalama nchini. Umuhimu wa hilo jambo upo, lakini nitawasiliana na vyombo vya ulinzi na usalama kuona kama, je, wamejiridhisha kwa kiasi gani kwa usalama huo, ili tuanze kuruhusu mabasi kufanya kazi wakati wote, ili kuboresha uchumi, lakini kuwafanya abiria kuwa na mipango binafsi ya kibashara ya kusafiri kutoka eneo moja mpaka eneo lingine katika kuendesha biashara zao kwa uhuru mkubwa.

Mheshimiwa Spika, katika hili lazima pia tutoe wito kwa Watanzania; kudumisha amani na usalama na utulivu nchini ni muhimu sana kwa sababu, malengo yetu ya kuboresha

uchumi wa nchi, kama nchi haiko salama hatutayafikia. Wito uliotolewa na Mheshimiwa Mwakagenda unaendelea kusisitiza na kuonesha umuhimu wa Taifa hili kuendelea kuwa salama ili wale wanaoamua kufanya biashara zao wakati wowote wafanye biashara hizo.

Mheshimiwa Spika, pia tumeanza kutoa wito hata kwenye mamlaka ya Serikali za Mitaa kupitia masoko yao makuu kuhakikisha kwamba masoko haya yanafanya kazi masaa 24 ili kuwaruhusu hata wanaokuwa *busy* mchana kutwa kwenye ofisi zao waweze kufanya hivyo wanapopata muda wa mapumziko ambao pia ni usiku kama ambavyo tunaona kwenye nchi zilizoendelea za wenzetu, watu wanaenda *shopping center*, biashara zinafanywa masaa 24 na sasa tunataka Tanzania hiyo pia ijitekeze kuanzia kwenye masoko yetu, kwenye usafiri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimeagiza vyombo vya ulinzi hasa Jeshi la Polisi kupitia Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya waendelee kufanya tathmini hiyo kwa haraka ili tupate taarifa hiyo tuweze kutoa vibali hivyo vya kusafiri nyakati hizo ili kazi ziendeleee. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Swali langu linahusu huduma ya umeme.

Mheshimiwa Spika, natambua, nathamini na vilevile naipongeza Serikali kwa juhudhi kubwa sana za kuhakikisha kwamba Taifa hili linakuwa na umeme wa uhakika. Nafahamu vilevile kwamba kumekuwa na *initiatives* nyingi za Serikali ikiwemo hii ambayo imetolewa tarehe 30 Juni, 2014 ambayo ni ya *Electricity Supply Industry Reform Strategy and Roadmap*. Katika utafiti huo inaonekana kuna matatizo makubwa ya *generation, transmission* pamoja na *distribution*.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, sasa *TANESCO* inaonekana kuhemewa na kazi hii hasa kwa kuwa tunakwenda kuwa na umeme mkubwa kutoka Mwalimu Nyerere *Hydropower Supply*. Kwa hali hiyo, Serikali haionti kwamba muda muafaka sasa wa kwenda kuifumua *TANESCO* ili tuwe na makampuni matatu ya *generation* peke yake, *transmission* peke yake pamoja na *distribution* kama ilivyo katika nchi nyine na hata majirani zetu wa Kenya, Uganda, *South Africa* na kwingineko? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu swali hili unao uhuru wa kulijibu, kwa sababu nilikuwa nafuatilia, sehemu ya mwanzo alikuwa anaeleza sera nzima ya mambo ya umeme, lakini hapa mwishoni naona yuko mahususi. Kwa hiyo, unao uhuru wa kulijibu ama naweza kumwagiza Mheshimiwa Mbunge alete swali ambalo litajibowi na Waziri anayehusika.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba ridhaa yako angalau hili eneo la mwisho naweza kulitolea ufanuzi kama ambavyo Mheshimiwa Abbas Tarimba, Mbunge wa Kinondoni, mwanamichezo alivyouliza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, shirika letu la umeme nchini linafanya kazi kubwa sana. Kazi hiyo kubwa ambayo inafanywa kwa sasa, lenyewe ndiyo linazalisha, lakini *TANESCO* pia inasafirisha umeme na inafanya kazi ya kugawa. Unapofanya jukumu hili, pia tunaangalia na maslahi ya Taifa, kwamba maeneo haya unaweza ukawa umeyakatakata ukawapa watu tofauti tofauti ikakuletea athari kwenye usalama wa nchi. Pale ambako nchi inahitaji umeme wakati wote, halafu mmoja mionganoni mwao anafanya mambo anayoyataka tu, halafu ukashindwa kufikia malengo ya kupeleka umeme kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, tunapokea ushauri wake. Hali tuliyonayo sasa nchini, maeneo yote yanayozalisha umeme tunaendelea kuzalisha umeme. Tuna maeneo ya maji; tunapopata mvua za kutosha kama sasa maji yamejaa,

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

mfano Kidatu na Mtera, tunayo maji ya kutosha na uzalishaji unaendelea. Kwa hiyo, eneo hili halina matatizo. Kwenye eneo la gesi pale Kinyerezi uzalishaji unaendelea. Pia maeneo mengine tunayotumia mafuta yanaendelea pia na uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, *TANESCO* kwa sasa maeneo yote ya uzalishaji, uzalishaji upo. Changamoto tuliyonayo sasa ni miundombinu iliyopo kwenye maeneo hayo ya uzalishaji. Hii inasababisha pia hata sasa naona kuna baadhi ya maeneo umeme unakatika, lakini ni kwa sababu ya kukosekana miundombinu. Sasa nini mkakati wa Serikali?

Mheshimiwa Spika, moja, tumewapa kazi *TANESCO* kufanya tafiti. Wanaweza kuja kwenye hatua hiyo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameipendekeza. Pale ambapo tutakuwa tumejipanga na tunaona nani tunampa jukumu la kuzalisha, nani anasafirisha lakini pia msambazaji ni nani? Zinaweza kuwa ni taasisi za Serikali ambazo pia lengo lake ni moja. Kwa hiyo, tukifika hapo kupitia utafiti unaoendelea sasa na Shirika letu la Nmeme Nchini, tutaweza kufikia hatua nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pili, suala la usambazaji, kama ambavyo mmeona Serikali leo ina mkakati wa kupeleka umeme mpaka vijiji, hii hatua tutaifikia kwa sababu tumefanya kazi nzuri sana na leo umeme unapatikana mpaka vijiji. Bado kazi hiyo inaendelea na malengo yetu kufikia Desemba mwaka huu tuwe tumefikia vijiji vyote nchini kupata umeme. Kwa nini? Tuna uhakika wa uzalishaji na bado tunaendelea kutafuta maeneo mengine ya uzalishaji, bado pia shirika letu limetoa nafasi kwa taasisi kuja kuwekeza kwenye uzalishaji. Kwa hiyo, nchi yetu itakuwa na umeme wa kutosha na kwa maana hiyo, eneo la uzalishaji halina matatizo kabisa. Tutajiimarisha pia kwenye eneo la miundombinu ya kwenye eneo la uzalishaji, usafirishaji na ugawaji kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nachukua ushauri wake, tutaufanya kazi na hivi *TANESCO* wanafanya kazi hiyo. Tukishakamilisha haya, tutatoa taarifa kwenu Waheshimiwa

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Wabunge na hasa Mheshimiwa Mbunge ambaye ametoa pendekezo hili, tutakupa mrejesho wa hatua ambayo tutaiflikia. Ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Upungufu wa watumishi katika Halmashauri zetu limekuwa ni tatizo kubwa sana; na kwa mfano tu, Halmashauri yangu ya Mkalama ina upungufu wa zaidi ya walimu 800; na kwa kuwa nchi yetu sasa haina tatizo la wataalam na vijana wengi wanasubiri ajira:-

Mheshimiwa Spika, kwa nini sasa Serikali isianze kujaza nafasi wazi mara moja pale mtumishi anapostaifu au anapotangulia mbele ya haki kwa sababu mtumishi huyo tayari yuko kwenye bajeti inayoendelea, badala ya utaratibu wa sasa wa kusubiri Halmashauri ziombe vibali jambo ambalo huchukua muda mrefu na linaongeza ukubwa wa tatizo? Ahsante. (*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Mkalama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ndani ya Serikali kuititia Wizara ya Ofisi ya Rais, Utumishi imeweka utaratibu mzuri tu wa kupata watumishi katika kuziba mapengo au watumishi wapya. Pale ambapo inatokea bahati mbaya mtumishi ametangulia mbele za haki, tunao utaratibu wa kujaza pia kwa kutangaza nafasi mpya, lakini hili linafanya baada ya kufanya uhakiki wa kina kwa vipindi vyta miezi mitatu, miezi sita au mwaka ili kuona tuna upungufu wa watumishi kwa kiasi gani; na wangapi wa kada ipi wanahitajika kujazwa?

Mheshimiwa Spika, kuititia Wizara ya Utumishi, Tume ya Utumishi wanacho kitengo maalum ambayo pia wanafanya uratibu kuititia Wizara zote na mahitaji yake. Kwa

hiyo, unaweza kuona tunachelewa kutangaza nafasi hizo kwa sababu kwanza lazima tupate *data base* ya mapengo ya watumishi wa Serikali kwa kada na Idara, ili tuone Idara hii tutakapotangaza, mahitaji ni mangapi kwa ajili ya Wizara zote; ili tutakapotangaza, tunatangaza mara moja kwamba tunahitaji watumishi 1,000 halafu wanagawiwa kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kazi hii inapofanywa katika kipindi cha miezi sita au mwaka tunaona kama inachelewa lakini inasaidia Serikali pia kutambua idadi ya wafanyakazi waliopo na mahitaji, lakini pia na kuziba, halafu tuendelee kusimamia maslahi yao wakati wote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba zoezi hilo la kuziba mapengo linaendelea, kuanzisha sekta mpya na kujaza sekta hizo. Kwa ujumla vibali hivi vinapokamilika utafiti huu, tunaomba kibali kwa Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Rais Mama Samia tunamwona anatoa vibali wakati wote kwa ajili ya kuajiri kada mpya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwahakikishie tu kwamba kazi hiyo inaendelea kufanyika na mamlaka husika hupeleka takwimu na taarifa Wizara ya Utumishi kuititia Tume ya Utumishi na zinatangazwa wakati wote. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mohamed Said Issa, Mbunge wa Jimbo la Konde.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kumwuliza Waziri Mkuu swali langu.

Mheshimiwa Spika, Chama cha Soka cha Zanzibar ZFA mpaka leo kimeshindwa kupata uanachama wa *FIFA* na sababu kubwa iliyotolewa ni kwamba Tanzania tayari ni mwanachama wa *FIFA*. Najua kuna juhudhi zinazofanyika ili Zanzibar iwe mwanachama wa *FIFA*, lakini kwa vile imekosa

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

kupata uanachama kwa sababu ya kutumika jina la Tanzania kupata uanachama: Je, Serikali inaisaidia vipi Zanzibar kuweza kupata kuititia Chama cha Soka cha Tanzania ambayo ni *TFF*, zile faida ambazo inazipata kwa ajili ya kuendeleza soka la Tanzania iweze kupeleka pia Zanzibar kabla ya Zanzibar hajitatua changamoto iliyopo katika usajili wa *FIFA*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu swali hilo litajibiwa na Mheshimiwa Waziri wa Michezo anayehusika. Katibu utalipangia siku atauliza kama swali la msingi. Mheshiniwa Ester Amos Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Waziri Mkuu, mwaka 2018 tulipitisha Sheria ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na lengo kuu liliikuwa kuunganisha mifuko na vile vile kuhakikisha maslahi ya wafanyakazi yanaboreshwani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuitisha sheria hiyo, matarajio ya wafanyakazi hayakuzingatiwa na matokeo yake, Hayati John Pombe Magufuli alisitisha matumizi ya sheria ile. Mpaka sasa hivi baada ya kusitishwa, ongezeko la watumishi wanaostaafu kwa hiyari limeongezeka, ongezeko la fao la kujitoa limeongezeka na mifuko imekuwa ikilemewa kulipa mafao ya wastaafu kutokana na watu kutokujua hatima yao na kuamua kuwahi kustaafu kabla ya wakati.

Je, ni lini Serikali mtaleta mabadiliko ya sheria ambayo tayari mlili-*commit* zaidi ya mara tatu, hamkufanya hivyo; ili sasa wastaafu wetu wawe na uhakika wa maisha yao baada ya kustaafu kwamba yamezingatiwa kwenye sheria na kile walichokitaka? (*Makofu*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bulaya, Mbunge wa Musoma... (*Kicheko*)

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, ni Mkoa wa Mara, siyo Musoma, maana nitakuwa na mgogoro na Mheshimiwa Mathayo. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri jambo hili liko Ofisi ya Waziri Mkuu, nafahamu mchakato wote ni kwamba kweli tulikuwa na mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii ambayo inashughulikia mafao ya watumishi waliostaafu. Tulikuwa na LAPF chini ya Ofisi ya Rais, wakati huo ilikuwa Waziri Mkuu, tukawa na mifuko mingi, lakini tukaipunguza mifuko hii tukaacha michache ili iweze kulipa vizuri maslahi kwa watumishi waliostaafu. Sasa tuna NSSF ambayo pia inashughulikia sekta binafsi na wachache sekta rasmi, na pia kuna PSSSF baada ya kuwa tumebadilisha sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, ulipaji wa mafao unaendelea siyo kwa kiasi kikubwa, ni kwa sababu mifuko hii illipoanzishwa tulikuta madeni mengi na makubwa. Kazi ambayo inafanywa sasa ni kulipa madeni ya wastaafu wa muda mrefu na tunaendelea kulipa wale wanaostaafu ili angalau kukamilisha hili, tufike hatua ya kuweza kulipa madeni pindi mtumishi anapostaaafu na kuendelea kulipwa mafao yao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mabadiliko ya sheria yapo na kanuni zilitengenezwa. Kwa sasa tunaangalia kama kanuni na sheria hizi zinaweza kutufikisha hatua nzuri ya kulipa mafao kwa wakati. Tayari Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Kazi, Ajira na Vijana ndio anasimamia jambo hili; na wakati wote amekuwa na vikao na mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii ili kuhamkisha kwamba inalipa kulingana na wakati aliostaafu mtumishi; wale wa zamani na walioko sasa. Ulipaji unaendelea. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tunayo madai, lakini pia tunaendelea kupata changamoto za kutokamilisha ipasavyo kulipa wadai wote kwa sababu ya yale madeni. Serikali iliwhahi kutoa fedha kwa ajili kuongezea uwezo wa mifuko yetu ili iweze kulipa mafao na kazi hiyo inaendelea. Kwa hiyo, tutaendelea kufanya mapitio ya sheria hizo na Waziri wa Nchi yuko hapa, anaendelea kusimamia. Malengo yetu ni kulipa

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

watumishi wote wanaostaafu kwa wakati na hatua hii nina uhakika tutaifkia. Ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, subirini kidogo. Makof yasubiri kidogo ili mumpigie akiwa ameshamaliza. Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushukuru sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Ahsante sana, muda wako umekwisha. (*Makof*)

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc - KATIBU WA BUNGE:**

### **MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Maswali ya kawaida, tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Amina Ali Mzee, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalii lake.

Na. 81

### **Chuo cha DMI Kutumika Kukabiliana na Changamoto za Ajira**

**MHE. AMINA ALI MZEE** aliuliza:-

Je, Serikali inatumiaje Chuo cha Bahari cha DMI kuendeleza vijana wa Kitanzania ili kukabiliana na changamoto za ajira?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA,  
AJIRA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PATROBAS P. KATAMBI)**  
aliuju:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Amina Ali Mzee, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Bahari Dar es Salaam (*DMI*) ni Chuo cha Serikali ambacho kimeanzishwa kwa Sheria

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

ya Bunge Na. 22 ya mwaka 1991 Chuo kinatoa elimu na mafunzo katika sekta ya usafiri wa njia ya maji na hivyo kina mchango mkubwa katika kukuza ajira nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto za ajira, Chuo cha *DMI* kina kitengo maalum cha uwakala wa ajira za mabaharia (*DMI Crewing Agency*). Kitengo hiki kilianza kazi mwaka 2018. Kina usajili Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (*TASAC*) kwa ajili ya kutafuta ajira na mafunzo melini kwa vijana wa Tanzania kwa meli za ndani na nje ya nchi yetu hususan kwenye mashirika mbalimbali ya meli ikiwemo *Azam Maritime, Zan Fast Ferry, TPA Kyera, Greece Marine Company* na Verba *Shipping Company*.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa kuwawezesha wahitimu wa Chuo cha *DMI* na mabaharia wa Tanzania kupata ajira katika meli za Kimataifa, Serikali inaendelea na taratibu za kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kusimamia masuala ya Bahari duniani (*IMO Convention – Maritime Labour Convention*). Kuridhiwa kwa mkataba huu, kutawezesha kutoa mafunzo na ajira kwa mabaharia takriban 150 ambao ni sawa na 25% ya wahitimu kwa mwaka. Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Amina Ali Mzee, swali la nyongeza.

**MHE. AMINA ALI MZEE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, natambua wanufaika wakubwa ni vijana Watanzania: Je, Serikali ina mpango gani wa kupanga fedha kwa ajili ya kukiendeleza chuo hiki? (*Makofii*)

**SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Patrobas Katambi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PATROBAS P. KATAMBI):**

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, tayari Serikali imeshakuwa na mpango wa kujenga jengo hilo litakalokuwa na urefu wa ghorofa sita na tayari fedha zimeshatengwa kwa ajili ya shughuli hiyo. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Amina kwa kuwa mafatiliaji.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, tuna habari nyingine njema ambayo Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan ameshatoa zaidi ya shilingi bilioni 54 kwa ajili ya kuwasaidia vijana zaidi ya 150,000 ambao wataenda kupata mafunzo mbalimbali katika vitengo hivyo ikiwemo uchumi wa bahari. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtaturu, swali la nyongeza.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Chuo hiki cha Bandari ni chuo ambacho kiko kwenye ukanda huu wa Afrika Mashariki, na ni chuo muhimu sana kwa ajili ya mafunzo haya; na kwa sababu vijana wanaokwenda kufundishwa pale wanahitaji kufundishwa kwa vitendo; na kwa sababu chuo hiki kina tatizo la kuwa na meli ya mazoezi. Je, ni lini Serikali sasa itatenga fedha kwa ajili ya kununua meli ya mazoezi kwa ajili ya kuwasaidia vijana kwa ajili ya mafunzo ya vitendo? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Abbas Mwinyi, swali la nyongeza.

**MHE. CAPT. ABBAS ALI MWINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niulize...

**SPIKA:** Samahani Mheshimiwa, samahani kidogo, Mheshimiwa Naibu Waziri alikuwa hajajibu bado. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mtaturu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ameuliza ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya mafunzo. Nimhakikishie tu Mheshimiwa kwamba, katika suala hili, pamoja na mambo mengine ya uboreshaji wa chuo hicho, ikiwa ni sambamba na ujenzi unaoendelea, zipo pia fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya vifaa vya kufundishia na kwenye hili suala la meli ni sehemu ya mpango huo. Kwa hiyo kulingana na upatikanaji wa fedha tutalikamilisha hilo na Serikali hii imekuwa ikifanya kazi kwa *speed*, tutalikamilisha. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abbas Mwinyi, swali la nyongeza.

**MHE. CAPT. ABBAS ALI MWINYI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa chuo hiki kinatoa mafunzo ya aina mbili, yaani nadharia pamoja na *practical*. Sasa swali ni kwamba, je, Serikali inahakikishajie kwamba kwa wale ambao wanamaliza nadharia na wanatakiwa wafanye *practical*, hiyo *practical* inapatikana katika meli gani? Nini mchango mchango wa Serikali katika kuhakikisha kwamba upande wa pili wa *practical* unapatikana? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PATROBAS P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abbas Mwinyi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ameuliza katika eneo la mafunzo, hasa katika *practical training*. Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Wakala wa TAESA ambaye yuko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, tumekuwa tukitoa mafunzo hayo kwa wahitimu, lakini pia kuna mpango maalum wa chuo chenyewe wa utoaji wa mafunzo ya mabaharia ambao wanahitimu hapo. Kwa mfano ukiangalia takriban zaidi ya vijana 3,000 waliomaliza katika chuo hicho wamepewa mafunzo. Tunatarajia baada ya marekebisho haya na ukarabati wa chuo pamoja na ongezeko la majengo tayari

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

tutakuwa na uwezo wa kudahili vijana 4,500 hadi 6,500 na hawa wote wanaingia kwenye mpango wa mafunzo. Tumekuwa tukiwapeleka kwenye meli za Wakala binafsi au wawekezaji binafsi pamoja na zile za Serikali.

Mheshimiwa Spika, sasa katika ule mpango wa kupata meli yetu wenye kwa ajili ya chou, nao utasaidia katika kufanya *practical training* ili kuwajengea vijana wetu *competence* na *performance* katika kazi hii. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 82

### **Ujenzi wa Stendi Mpya – Geita Mjini**

**MHE. COSTANTINE J. KANYASU** aliuliza:-

Je, nini kinakwamisha ujenzi wa stendi mpya ya Geita Mjini na lini sasa ujenzi huo utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa stendi ya kisasa ya mabasi kwenye eneo la ukubwa wa hekta 6.9 unaendelea na upo katika hatua ya usanifu ambapo unafanyika pamoja na usanifu wa miradi mingine ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami nzito zenye urefu wa kilometra 15.4.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, kazi za ujenzi wa stendi ya kisasa ya mabasi imepangwa kuanza mwaka wa fedha 2022/2023, baada ya kukamilika kwa usanifu. Mradi huu umepangwa kutekelezwa na Serikali kuititia Mkopo wa Benki ya Dunia. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Constantine Kanyasu, swali la nyongeza.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwanza naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa stendi hii ulikuwa ni sehemu ya ujenzi wa barabara miaka sita iliyopita, ambapo ilikuwa ni sehemu ya fedha za mkopo ya *World Bank* na baada ya muda uli-*phase out* na fedha hizi zikabaki kwenye Mfuko wa Serikali. Sasa swali langu namba moja; kwa kuwa mkopo huu ulikuwa wa pamoja, fedha zilizobaki kwenye utekelezaji wa mradi huu wa awali zilienda wapi?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, nashukuru kwa ujio wa mradi wa pili wa *World Bank* ambao ni *TACTIC* ambao unatarajia kuanza hivi karibuni. Sasa kilichosababisha stendi isijengwe awamu ya kwanza ni kwa sababu utangazaji wa miradi unakwenda kwa awamu. Wanatangaza barabara moja baada ya nyingine na mradi mwingine baada ya mwingine na matokeo yake mradi una-*phase out* na fedha zinaisha. Je, kwa nini Wizara isiwashauri wafadhili, miradi hii ikatangazwa kwa pamoja ili weze kutekelezwa kwa pamoja kuepuka tatizo lilitotokea hapo awali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyingeza ya Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini, kama ifuatavyo:-

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Kanyasu kwa kuwasemea kwa dhati kabisa wananchi wa Geita Mjini. Pili, nimhakikishie kwamba mradi wa ujenzi wa stendi ya kisasa, pamoja na kwamba ulisanifiwa na kupangwa kufanyika pamoja miaka sita iliyopita, changamoto ilijoitokeza iliкуwa ni upungufu wa fedha katika kutelekeza mradi wa stendi hiyo. Stendi hiyo ni ya kisasa, ni kubwa na inahitaji fedha nyngi na ndiyo maana kwenye awamu ile ya kwanza haukuweza kukamilika.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi, kwamba kwenye mwaka wa fedha 2022/2023, tayari usanifu umefanyika na uko hatua za mwisho na utatekelezwa kuititia mradi wa *TACTIC* ambapo tutajenga barabara za lami kilometra 15 pamoja na stendi hii ya kisasa katika Mji wa Geita. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Joseph Tadayo, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa hitaji la stendi lililoko Jimbo la Geita Mjini ni sawa kabisa na lile lililoko katika Jimbo la Mwanga; na kwa kuwa mwezi Novemba mwaka jana Mheshimiwa Rais alipotembelea Mkoa wa Kilimanjaro aliwaahidi wananchi wa Mwanga stendi ya kisasa pale Mwanga.

Swali langu je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hii ya Mheshimiwa Rais kwa wananchi wake wa Mwanga? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Joseph Tadayo, Mbunge wa Mwanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ahadi ya Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan tayari tumeshaipokea Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tumeshaifanyia tathmini na tunatafuta fedha wakati wowote ahadi hiyo itatekelezwa. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari kazi imeanza kwa ajili ya kujenga stendi ya kisasa pale Mwanga. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Ezra Chiwelesa, swali la nyongeza.

**MHE. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii.

Kwa kuwa hitaji hili la stendi katika Mji wa Geita ni sawasawa na kilio cha muda mrefu cha wananchi wa Biharamulo cha kupata stendi ya kisasa pale, ni lini sasa Serikali itaanza ujenzi wa stendi ya kisasa katika Mji wa Biharamulo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ezra Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa miundombinu ya stendi za kisasa, ujenzi wa barabara pamoja na ujenzi wa masoko vyote ni vipaumbele katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kazi ambayo Serikali tumeelekeza, kwanza halmashauri zifanye tathmini ya uwezo wa mapato yao ya ndani na kuweka kipaumbele cha kuanza ujenzi wa miundombinu hiyo, zikiwemo stendi za kisasa kwa kutumia mapato ya ndani kwa zile halmashauri zenyne uwezo wa mapato ya ndani. Zile halmashauri ambazo hazina uwezo wa mapato ya ndani waandae maandiko ya miradi ya kimkakati ya stendi hizo na kuyawasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na Wizara

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

na Mipango ili tufanye tathmini na kutafuta fedha za kuwezesha kujenga stendi za kisasa za kimikakati katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Ezra Chiwelesa kwamba, wafanye tathmini Biharamulo waone uwezo wao wa mapato ya ndani, lakini kama hautoshi walete mradi wa kimkakati ili fedha itafutwe kwa ajili ya kujenga stendi ya kisasa pale Biharamulo. Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Japhet Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri; kwa kuwa katika eneo la *TaCRI* pale Mbimba Vwawa lilitengwa kwa ajili ya kujenga stendi kubwa ya Mkoa wa Songwe. Je, ni lini stendi hiyo itaanza kujengwa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mbunge wa Mbozi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba baada ya stendi ya mkoa kukosekana katika Mkoa wa Songwe ulifanyika mpango wa kuandaa eneo kwa ajili ya ujenzi wa Stendi ya kisasa ya Mabasi ya Mkoa wa Songwe katika eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge amelitaja. Nimhakikishie kwamba lengo la Serikali bado liko vile vile na mipango inafanyika ya tathmini ya mahitaji ya fedha na kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga stendi ile. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mpango bado upo na taratibu za kutafuta fedha zinaendelea ili tuanze ujenzi. Nakushukuru sana. (*Makofii*)

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Issa Ali Mchungahela, Mbunge wa Lulindi.

Na. 83

### **Vituo vya Afya vya Nagaga na Mnavira**

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA** aliuliza:-

Je, ni lini Vituo vya Afya vya Nagaga na Mnavira vitakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Jimbo la Lulindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali iliipatia Halmashauri ya Masasi shilingi milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Nagaga ambapo ujenzi umekamilika na huduma zimeanza kutolewa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Halmashauri ya Masasi katika mwaka wa fedha 2021/2022, imetenga shilingi milioni 23 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa nguzo na paa kwenye njia za watembea kwa miguu (*walkways*).

Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 2009 hadi 2018 kiasi cha Shilingi milioni 110 kilitumika kwa ajili ya ukamilishaji wa boma la *OPD* la zahanati ya Mnavira. Kati ya fedha hizo shilingi milioni 68 zilitolewa na Serikali na shilingi milioni 42 nguvu za wananchi. Ujenzi wa jengo hilo la Zahanati ya Mnavira umekamilika na huduma zinaendelea kutolewa.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, shilingi milioni 500 zimepelekwa Halmashauri ya Masasi kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Chikoropola na Chikundi ambapo ujenzi wa vituo hivi unaendelea. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHOLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa sababu mazingira ya ukamilishaji wa vituo hivi umechangiwa kwa namna moja au nyingine kuonekana kwamba kuna maeneo ambayo bado hayajakamilika, kwa mfano Nagaga, Mnavira pamoja na Chiungutwa kuna fedha ambazo hazijatimia pale, kwa sababu bajeti nzima ilikuwa shilingi milioni 500 lakini wamepewa shilingi milioni 400 na hivyo kusababisha baadhi ya majengo kama vile wodi ya akinamama pamoja na majengo ya *ultrasound*/kutokamilika.

Je, ni lini sasa Serikali itakamilisha majengo haya yaliyokosekana? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Lulindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa vituo vya afya nchini kote unakwenda kwa awamu. Tunapeleka fedha awamu ya kwanza, tunajenga majengo ya kipaumbele ili kuwezesha vituo kuanza kutoa huduma za msingi, lakini tunatafuta fedha kwa ajili ya awamu ya pili ili kukamilisha majengo hayo. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo fedha ambazo zilipelekwa Nagaga na Mnavira zilikamilisha sehemu ya kwanza ya majengo, lakini milioni 100 ambayo inabaki

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

itapelekwa ili kukamilisha wodi ya wanawake pamoja na jengo hilo la *ultrasound*. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Edward Kisau Olelekaita, Mbunge wa Kiteto, sasa aulize swali lake.

Na. 84

### **Ujenzi wa Mabwawa ya Maji-Kiteto**

**MHE. EDWARD O. KISAU** aliuliza:-

Je, ni lini ahadi iliyotolewa wakati wa kampeni za Urais ya ujenzi wa mabwawa mawili ya maji katika Wilaya ya Kiteto itatekelezwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa *Engineer Maryprisca Mahundi*, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Edward Kisau Olelekaita, Mbunge wa Jimbo la Kiteto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama katika Wilaya ya Kiteto kwa sasa ni asilimia 52.58. Katika kuboresha huduma ya majisafi na salama katika Wilaya ya Kiteto, Serikali katika mwaka fedha 2021/2022, inatekeleza miradi katika Vijiji 21 vya Nchinila, Engusero, Ngipa, Nasetani, Ngarenaro, Mafichoni, Kibaya Kati, Kanisani Bomani, Magubike na Msakasaka. Vijiji vingine ni Jangwani, Magungu, Kaloleni, Majengo Mapya, Msikitini, Vumilia, Esuguta na Kiperesa.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi hiyo unahusisha ujenzi wa matangi 11 yenyewe jumla ya ujazo wa litu 1,325,000, ulazaji wa mabomba umbali wa kilometra 99.49 na ujenzi wa vituo 69 vya kuchotea maji. Utekelezaji wa miradi

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

hiyo umefikia wastani wa asilimia 10 na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2022.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa muda mrefu, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022, imefanya mapitio ya usanifu wa Bwawa la Maji la Dongo na usanifu wa ukarabati wa Mabwawa ya Dosidosi na Kijungu na taratibu za kupata wakandarasi zitakamilika kabla ya mwezi Juni, 2022. Ujenzi wa Bwawa la Dongo pamoja na ukarabati wa Mabwawa ya Dosidosi na Kijungu unatarajiwa kuanza katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023.

**SPIKA:** Mheshimiwa Edward Olelekaita, swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na niseme kwa dhati kabisa kwamba nimefurahishwa sana na majibu ya Serikali na wananchi wangu wa Dosidosi, Kijungu na Dongo watakuwa wamesikia haya.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa mradi ule wa milioni 400 wa Kaloleni uliotokana na fedha za UVIKO na kwa kweli niishukuru Wizara ya Maji na meneja wa *RUWASA* aliyeko pale ni mzuri sana, anafanya kazi vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, sasa swali langu dogo tu, je, ni lini Wizara ya Maji watakuwa tayari twende Kiteto, hususan pale Dongo, ili tukatembelee mradi mkubwa wa bwawa hili ambalo limewekwa kwenye mpango wa Serikali?Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa maji, majibu kwa ombi hilo la kwenda kwa Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Olelekaita kama ifuatavyo:-

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimepokea pongezi zote na tuendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu anaendelea kutoa fedha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kufika Kiteto, niko tayari, nitafika Kiteto na tutafanya kazi. Sisi tunasema na kutenda, tutafika Kiteto.

**SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, sasa aulize swali lake.

Na. 85

### **Hitaji la Umeme Wilaya ya Chunya**

**MHE. MASACHE N. KASAKA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itafikisha umeme kwenye vijiji ambavyo bado havijafikiwa Wilayani Chunya pamoja na Makao Makuu ya Kata za Nkung'ungu, Lualaje, Mafyeko na Kambikatoto?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu – Mzunguko wa Pili unaolenga kufikisha miundombinu ya umeme katika vijiji vyote ambavyo vilikuwa havijafikiwa na huduma ya umeme Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) kwa niaba ya Serikali umeingia mkataba na Kampuni ya *M/S Electrical Transmission and Distribution Construction and*

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

*Maintenance Company Limited* kutekeleza mradi huu katika Mkoa wa Mbeya ambao utekelezaji wake umekwishaanza kwa Mkandarasi kukamilisha uhakiki na kuagiza vifaa vitakavyotumika katika ujenzi.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kupeleka umeme katika Wilaya ya Chunya unahusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo kilovoti 33 zenye urefu wa kilomita 245.5; kilomita 12 ya njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 0.4; ufungwaji transfoma 12 za KVA 50; pamoja na kuunganisha wateja wa awali 814. Gharama ya mradi ni Shilingi bilioni 10.656 na utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2022.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, swali la nyongeza.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake hayo. Nami nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Wilaya ya Chunya katika REA Awamu ya Pili tumepata vijiji 12; lakini katika vijiji 12, vijiji 10 vinapita kwenye misitu ambayo iko chini ya TFS. Sasa mradi huu unapopita, TFSimekwamisha huu mradi inasubiri mpaka iweze kupata malipo ya fidia ili mradi uweze kuendelea, kitu ambacho kinashangaza sana.

Je, ni lini sasa Serikali itakaa na taasisi nyingine ya Serikali TFS waweze kujadiliana ili malipo yaweze kufanyika na mradi huu uweze kutekelezeka na wananchi waweze kunufaika kama ambavyo wanategemea? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwenye kila kijiji kitapata *transfomer* ya KVA 50 ambapo usambazaji wake wake wa umeme ni wastani wa kilometra moja ambayo inahudumia takribani watu 68:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza *transfomer* yenyе ukubwa zaidi ya KVA 50 ili wananchi wengi zaidi waweze kunufaika na huduma hii ya umeme?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Stephen Byabato Lujwahuka, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia masuala ya wananchi na hasa kwenye hili eneo la fidia. Kwanza naishukuru Serikali kwamba ilishirikiana na wananchi na kuwaomba miradi yote ya *REA* isiwe miradi inayohitaji fidia katika maeneo ambayo miradi inapita. Nawashukuru wananchi kwa niaba ya Serikali walikubali ombi hilo kwa sababu umeme ni kwa mahitaji yetu sote.

Mheshimiwa Spika, kwanza niseme kwamba mradi wa *REA* hauna fidia kwa wananchi. Ila kwa wenzetu wa *TFS* wamekuwa wanazo kanuni ambazo zinazelekeza kwamba maeneo yao yaktaka kutumika kwa shughuli nyingine, basi fidia itolewe. Nasi mara kadhaa tumefanya mazungumzo nao ili eneo hili liondoke na kikao cha mwisho kimefanyika wiki hii na tunatarajia kabla ya mwezi huu tutakuwa tumekamilisha jambo hili, ili sasa kama ambavyo tunapeleka miradi ya umeme katika maeneo ya wananchi bila kuwafidia na *TFS* ambayo ni taasisi ya Serikali pia, Isifidiwe kwa kutumia eneo kwa ajili ya shughuli za wananchi. Tuna uhakika jambo hili litakamilika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika awamu hii ya pili eneo la Mbeya lakini pia Katavi, Simiyu na Morogoro yapo maeneo yanahitaji *attention* ya namna hiyo na tayari tunayafanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwenye jambo la pili, ni kweli kwamba wateja ambao wamefikishiwa umeme kwa kipindi hiki, siyo wote wanaouhitaji, lakini Serikali imejitahidi sana kwa hizo shilingi trillioni moja na bilioni 250 kupeleka angalau kwa wateja wa awali katika maeneo ya mijini. (*Makofii*)

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na Wabunge wengine wote kwamba Serikali inayo mradi mwagine wa *densification* ambayo ni jazilizi; inayo mradi mwagine wa *Peri-Urban* wa kupeleka miradi ya umeme huko na pia *TANESCO* wanaendelea, kila mtu atapata umeme kwa kadiri Serikali inavyojitahidi kufikisha umeme katika maeneo hayo. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anton Mwantona, swali la nyongeza.

**MHE. ANTON A. MWANTONA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuuliza swali la nyongeza katika Wizara hii ya Nishati. Jimbo la Rungwe lina vijiji 99. Katika vijiji 99, vijiji 66 vilikuwa kwenye mradi wa *REA II*/na vijiji 33 viko kwenye mradi wa *REA III*; lakini katika vijiji 66 ni vijiji 41 tu ndiyo vilikamilishiwa umeme, lakini vijiji 25 havikukamilishiwa umeme katika awamu ya pili ya *REA*.

Mheshimiwa Spika, Waziri alikuja kufanya ziara kule kwetu kwenye ufunguzi wa *REA III* tarehe 28 mwezi wa Nane akasema kuna fedha ilibaki kwenye *REA II*, shilingi bilioni 2.4 kwa ajili ya kupeleka umeme kukamilisha mradi wa umeme kwenye *REA II*. Akasema, ndani ya miezi miwili huo mradi utakamilika na wananchi watapata umeme.

Mheshimiwa Spika, la kusikitisha, mpaka leo umeme bado haujafika na kazi bado haijaanza. Nilikuwa naomba Waziri atoe kauli hapa, ni lini mradi wa umeme *REA II* vijiji 25 katika Jimbo la Rungwe utaanza? Ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mbunge wa Rungwe kwa swali lake. Naomba kutoa majibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwenye mradi wa *REA III round* ya kwanza zilikuwepo *lots* 29 na *lots* 8 bado hazijakamilika katika eneo hilo la Rungwe na maeneo mengine. Kama

tulivyosema, kulikuwa na kucheleta kwa sababu ya kucheleta kupatikana kwa vifaa na maeneo kama hayo, lakini Serikali tayari imeilagiza *REA* kuhakikisha inakamilisha miradi hiyo na wakandarasi kabla ya mwezi wa tatu mwaka huu. Kwa hiyo, vile viporo vyote ambavyo vilibakia kwenye mradi wa *REA II, REA III round one*, vyote tunatarajia viwe vimekamilika kabla ya kwisha kwa mwezi wa Tatu mwaka huu 2022 eneo la Rungwe likiwemo. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nikukumbushe tu, mwezi wa Tatu ni mwezi ujao; na hapa tunarudi muda siyo mrefu kwenye Bunge la Bajeti. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Afya. Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 86

**Changamoto ya ukosefu wa dawa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini**

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje katika kupunguza ama kumaliza kabisa changamoto ya ukosefu wa dawa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini?

**SPIKA:** Simwoni aliyesimama. Ah, Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imapeleka Bohari ya Dawa (*MSD*) shilingi bilioni 333.8 kwa ajili ya ununuzi wa dawa na

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

vifaa tiba ambapo sasa Bohari ya Dawa ipo katika hatua mbalimbali za manunuzi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupeleka fedha kwa ajili ya manunuzi, Serikali imetoa shilingi bilioni 18 kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha dawa eneo la Idofoi, Mkoani Njombe ambacho kitakuwa na uwezo wa kuzalisha vidonge ndani ya siku mbili vya kutosha nchi nzima kwa miezi mitatu na ujenzi umefikia 70%. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kiwanda cha kuzalisha *gloves* kilichopo Njombe kimekamilika kwa asilimia 100 na sasa kipo kwenye majaribio; na kikamilika kitawezeku kidhi mahitaji ya nchi kwa 85%. Aidha, kiwanda cha Keko kimefufuliwa na kinazalisha kwa sasa aina 12 za dawa. Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na pia nashukuru kwa majibu sana ya Serikali. Naendelea kuipongeza Serikali kwa juhudini azofanya kuhakikisha kwamba upatikanaji wa dawa unakuwa ni mzuri. Pia naishukuru Serikali, inajitahidi kuhakikisha kwamba wazee wanapata vitambulisho vya kupata dawa bure na pia wanaendelea kupata vitambulisho vingine. Hata hivyo nina swali la nyongeza kwa Serikali.

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba wazee wanaendelea kupata stahiki za dawa kwa mwendelezo mzuri bila usumbufu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi anavyofuatilia matatizo ya akina mama wa Mkoa wa Pwani kwa ukaribu sana hasa kwenye mahospitali yetu; vile vile kwa jinsi ambavyo anafuatilia watoto wa kike kule mashulenii,

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

niliona *procedure* yake nzuri sana inayofuatilia kwa karibu sana watoto wakike wa Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, kwanza niseme kama tulivyo sema, mmeona Rais wetu Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan ametoa shilingi bilioni 338.8, shilingi bilioni 495 na umeona shilingi bilioni 18. Kwa kipindi cha miezi tisa tu zimekwenda zaidi ya shilingi bilioni 846. Maana yake ni nini? Shida siyo fedha, ni kujipanga.

Mheshimiwa Spika, kikubwa Waziri wa Afya Mheshimiwa Ummy Mwalimu pamoja na Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Bashungwa wameshatoa maelekezo kwa ma-RMO wote na ma-*DMO* wote kuhakikisha kila hospitali na kila kituo cha afya na zahanati, wana dirisha la wazee kwenye hospitali zao na kunakuwepo na daktari na mtu maalum wa kuwashudumia wazee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile kuhakikisha kwamba kunakuwepo na dawa eneo husika na wazee wapate vitambulisho vyao kwa sababu kuna utaratibu wa wazee kupata vitambulisho vyao. Pia tumeshawaelekeza *MSD*, vituo vyetu vikiomba dawa wapeleke ndani ya siku tatu dawa ziwe zimefika kituoni na kama hawana *item* hiso, ndani ya masaa 24 wawe wamewaruhusu vituo vinunue dawa kwa sababu imeonekana vituo vinakuwa na fedha za *basket fund*, na *own source* lakini wanashindwa kununua dawa kwa sababu hawajapewa ruhusa ya kufanya hivyo kama taratibu zinavyotaka na *MSD*. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa John Marco Sallu, Mbunge wa Handeni Vijiji, sasa aulize swalii lake.

Na. 87

**Ujenzi wa barabara ya kutoka Kwamsisi hadi Mkata**

**MHE. JOHN M. SALLU** aliuliza:-

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya kutoka Kwamsisi mpaka Mkata kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Marko Sallu, Mbunge wa Handeni Vijiji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Kwamsisi hadi Mkata yenye urefu wa kilometra 35 ni sehemu ya barabara ya *Mkalamo Junction* hadi Mkata yenye urefu wa kilometra 73.1. Barabara hii ni ya mkoa na inahudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*).

Mheshimiwa Spika, sehemu ya barabara hii kutoka *Mkalamo Junction* hadi Kwamsisi yenye urefu wa kilometra 38.51 iliingizwa katika mradi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Pangani – Tungamaa – Mkwaja hadi Mkange yenye urefu wa kilometra 95.2. Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami amepatikana ambaye ni *China Railway 15 Group* na Mkataba umesainiwa tarehe 6 Septemba, 2021. Gharama za ujenzi ni shilingi bilioni 94.539 na muda wa utekelezaji wa mradi huo ni miezi 48.

Mheshimiwa Spika, sehemu iliyobaki ya Kwamsisi hadi Mkata iliingizwa katika mpango wa *Rise (Roads to Inclusion and Socioeconomic Opportunities)* ambao inafadhiliwa na Benki ya Dunia. Mradi huu upo katika hatua ya manunuzi ya kumpata Mhandisi Mshauri atakayefanya kazi ya upembuzi yakini na usanifu wa kina na kuandaa nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Ahsante. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa John Sallu, swali la nyongeza.

**MHE. JOHN M. SALLU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Kule handeni kuna barabara inayotoka Magore - Turiani mpaka Handeni. Barabara hii ina ahadi nyingi za viongozi wa Serikali na vile vile barabara hii inaunganisha Mkoa wa Tanga na Morogoro na ni barabara fupi kwa kuja Jijini Dodoma.

Sasa niulize, ni lini Serikali itamalizia kile kipande cha Turiani - Handeni kwa kiwango cha lami? Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa John Marco Sallu, Mbunge wa Handeni Vijiji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia barabara zinazopita katika jimbo lake. Kwa swali alilouliza, nataka nimhakikishie kwamba dhamira ya Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan ni kuifungua Tanzania; na kuifungua Tanzania ni kuhakikisha kwamba miundombinu na hasa barabara zinajengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja ya Magole - Turiani hadi Handeni ni sehemu ya barabara inayotoka Korongwe - Handeni - Mzia -Turiani - Magole kwenda Kilosa hadi Mikumi. Barabara hii iko kwenye mpango, kwa hiyo, Serikali inatafuta fedha, maana imeshajenga Magole hadi Turiani; sasa hivi inatafuta fedha za kujenga Turiani kwenda Handeni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba iko kwenye mpango wetu na hata kwenye vitabu vya bajeti inaonekana hivyo. Kwa hiyo, avute Subira, barabara itakamilishwa kwa kiwango cha lami. Ahsante. (*Makofii*)

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa nyakati tofauti hapa Bungeni na pia kwenye ziara za viongozi katika Jimbo langu ikiwemo ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu mwezi Oktoba mwaka 2021, niliombwa Serikali iweze kujenga barabara njia nne kwenda Kipatimu kwa kiwango cha lami ambayo ina urefu wa kilometra 50.

Mheshimiwa Spika, nashukuru Serikali imeanza kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami katika kipande cha kilometra 1.4 katika eneo la mteremko mkali wa Kilimangoge pamoja na eneo la Kijiji cha Ngorongoro:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kumalizia eneo lililobaki la kilometra 48.6? (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kumba Ndulani, Mbunge wa Kilwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika ziara hiyo nami nilikuwepo na Mheshimiwa Waziri Mkuu kweli aliahidi kwamba barabara hiyo itajengwa. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii tumeichukua na tunaiingiza kwenye mpango kwa ajili ya kujenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, pia napokea pongezi kwamba tayari tumeshaanza kujenga hizo kilometra chache. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba kadiri Serikali itakavyopata fedha, hizi kilomita 48.6 zilizobaki tutajenga barabara kwa kiwango cha lami kuanzia Njia Nne hadi Kilwa Kipatimu.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Barabara ya Kimara - Mavurunza – Kinyerezi ya kilometra saba maarufu kama *Kikwete Highway* iliahidiwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete mwaka 2010 na ilikuwepo kwenye llani za Uchaguzi tatu; mwaka 2010, 2015 na 2020.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua, ni lini ujenzi wa barabara hii utaanza? Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo Mbunge wa Ubungo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba moja ya vipaumbele vyta Serikali ni ahadi za viongozi na hasa viongozi wa Kitaifa. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara aliyoitaja ya Kimara kwenda Kinyerezi ambayo iliahidiwa na Mheshimiwa Rais tutajenga kwa kiwango cha lami kadiri fedha zitakavyoendelea kupatikana. Tunajua baada ya kuwa na Stendi ya Magufuli, hii barabara ni muhimu sana kwa sasa kupunguza msongamano kwenye barabara zetu za Mji wa Dar es Salaam. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Timotheo Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. TIMETHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Barabara ya Magokweni - Maramba – Daluni – Mashewa Mpaka Korongwe ni barabara muhimu sana kwa uchumi na ulinzi na usalama wa nchi yetu; na kumekuwa na ahadi za viongozi za muda mrefu.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, nataka kujuua, ni lini Serikali itatengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami? (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mnzava, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge atakuwa shahidi, baada ya Bunge tulilomaliza hii barabara, nimeitembelea kuanzia Mabokweni mpaka Korogwe na hasa kutokana na umuhimu wa hii barabara.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutafuta fedha. Hata hivyo, kitu tunachokifanya sasa hivi kwa jinsi ilivyopita kwenye miinuko tutaanza kwanza kujenga barabara katika hali zile zenye changamoto ngumu kujenga vipande vifupi vifupi kwa njia ya lami ili njia ipitike kwa muda wote wakati Serikali inatafuta fedha kujenga barabara yote kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 88

### **Ujenzi wa barabara ya Mtwara Pachani mpaka Tunduru**

**MHE. DAIMU I. MPAKATE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Mtwara Pachani, Lusewa, Nalasi hadi Tunduru yenyeye urefu wa kilomita 320 kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Mtwarapachani – Lusewa – Nalasi – Tunduru yenyeye urefu wa kilomita 300 ni barabara ya mkoa na inahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina pamoja na utayarishaji wa nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami imekamilika mwaka 2020. Baada ya usanifu kukamilika na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, wakati tukisubiri upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi, Serikali itaendelea kuifanya matengenezo mbalimbali barabara hiyo ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka. Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, jumla ya shilingi milioni 1,960.583 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo mbalimbali na ukarabati wa madaraja kwenye barabara hii. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Daimu Mpakate, swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pia nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Serikali imesema inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ile kwa kiwango cha lami na kuna maeneo ambayo hivi sasa magari hayapiti yanakaa siku mbili, tatu kufika mwisho wa safari, kama maeneo ya kutoka Mkandu mpaka Mbesa, eneo la Lusewa mpaka kufika Ligunga na eneo la Majiwe mpaka Milonji ambayo yamekuwa ni maeneo korofi kwa muda mrefu. Je, Serikali

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

haioni sasa haja ya kuweka lami laini katika maeneo hayo ili magari yaweze kupita kwa urahisi?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; kwa kuwa barabara hii hajjawahi kukanyagwa na Naibu Waziri wala Waziri wa Ujenzi, naomba anipe *commitment* ya yeye na mimi kufuatana kwenda kukagua barabara hiyo ili aone adha wanayoipata wananchi katika maeneo hayo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maeneo aliyyoyataja ya Lusewa, Mbesa, Malonji nadhani ni jana magari mengi yamekwama. Jana tulitoa maelekezo kwa Mameneja wote wa TARURA Mkoa, naamini watakuwa wanansikia na watakuwa pengine wako *site* eneo hilo ili waweze kukwamua magari hayo.

Mheshimiwa Spika, hii barabara sasa hivi mwaka huu tumeitengeneza kwa changarawe barabara yote ya kilometra hizi 320. Kwa hiyo nimhakikishie Mbunge kwamba Mhandisi wa Mkoa ninavyosema hivi yuko *site* kukwamua hayo magari yaliyokwama.

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na naamini pamoja na Mheshimiwa wa Namtumbo, kwa sababu barabara hii ndiyo barabara muhimu sana kwa watu wa Tunduru na Namtumbo niombi baada ya hapa tupange ziara tutembelee hiyo barabara. Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, swalii la nyongeza.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Jiji la Arusha linakua kwa kasi sana na kusababisha misongamano mbalimbali, kwa hiyo napenda kufahamu; je, ni lini Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi itaanza rasmi ujenzi wa barabara ya lami ya kutoka pale Kiserian (Moshono) kuunga na *bypass* na ile ya Ngaramtoni kwenda mpaka Mianzini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mrisho Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa kujenga hiyo barabara ya kuanzia Moshono kwenda *bypass* na tayari tumeshaanza, labda ni kuikamilisha tu. Kwa hiyo Serikali bado itaendelea kujenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kwa barabara ya pili alioitaja ya kuanzia Mianzini kwenda Ngaramtoni yenye urefu wa kilometra 18, ninavyoongea hapa ipo kwenye hatua za manunuzi kuanza kujenga yote kilometra 18 kwa kiwango cha lami. Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hassan Zidodu Kungu, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa Serikali iko katika mpango wa kutafuta pesa ya kujenga barabara hiyo ya Mtwara Pachani – Tunduru Mjini.

Je, Serikali haioni haja ya kujenga angalau kilometra tano tu za lami ambapo barabara hiyo inapita Tunduru Mjini Na ofisi zote za Serikali pamoja na taasisi za Kiserikali ziko kwenye barabara hiyo ambapo hakuna lami kabisa na zipo mjinini kabisa? (*Makofii*)

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara nyingi zinazopita katika ofisi zipo ambazo tunazihudumia sisi, lakini pia na TAMISEMI. Tumelichukua hili, tutakutana na wenzetu wa TAMISEMI tuone namna ya kutafuta fedha ili miji hii iweze kupata lami angalau kwa uchache kama miji mingine. Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, swali la nyongeza.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Barabara ya kutoka Kilindi – Kiteto – Chemba mpaka Singida ni barabara ya kimkakati ya kuchochea uchumi kwenye mikoa hii minne na wilaya zake. Bajeti hii tunayokwenda kumaliza ilikuwa inaze lakini mpaka sasa michakato yake bado ni mirefu na hatuoni dalili ya kwenda kuanza ujenzi wa barabara hii. Je, ni lini sasa ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami unaanza? Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoisema ni sehemu ya barabara inayoanzia Kilindi – Kiberashi – Kiteto hadi Kwamtoro, Singida. Naomba nimhakikishie kwamba kama

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

nilivyosema, barabara hii ndiyo inayopita kwenye Bomba la Mafuta la kutoka Tanzania kwenda Uganda. Kwa hiyo Serikali ya Awamu hii ya Sita imejipanga kuhakikisha kwamba kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha barabara hii inaanza kujengwa. Hivi ninavyoongea barabara hii inaanza kujengwa kwa kiwango cha lami, tuko kwenye hatua za manunuzi kwa barabara hii. Ahsante. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni, sasa aulize swali lake.

Na. 89

### **Uchakavu wa vituo vya polisi vya zamani na nyumba za askari – Zanzibar**

**MHE. USSI SALUM PONDEZA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itafanya ziara kwenye Vituo vya Polisi vya zamani na nyumba za kuishi Askari Unguja na Pemba ili kushuhudia uchakavu uliopo na ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya Vituo vya Polisi nchini kwa Mwaka 2021/2022?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilishatembelea na kuona uchakavu wa vituo vya polisi na nyumba za makazi ya askari huko Zanzibar na maeneo mengine ya Tanzania Bara. Zoezi la kufanya tathmini ya uchakavu kujua gharama zinazohitajika ili kufanya ukarabati zinaendelea nchi nzima. Zoezi hili litakapokamiliika, Serikali itatenga fedha kwa ajili ya

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

ukarabati kulingana na upatikanaji wa fedha kwa mwaka ujao (2022/2023) kama ilivyofanyika mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Serikali ya mwaka 2021/2022, Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi 2,000,000,000 kwa ajili ya ukarabati wa Vituo yya Polisi na ujenzi wa nyumba za askari. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ussi Pondeza, swali la nyongeza.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nina swali dogo kabisa la nyongeza la kumuuliza.

Mheshimiwa Spika, tathmini hiyo ambayo imefanywa ya vituo vibovu na nyumba chakavu za askari, lakini katika Jimbo langu la Chumbuni nina vituo viwili ambavyo ni vibovu ambavyo vimefungwa zaidi ya miaka minne. Nataka nimuulize Mheshimiwa Waziri; yuko tayari kuambatana na mimi kwenda katika jimbo langu kwa ajili ya ukarabati wa vituo vyangu ambavyo nimekuwa navidai sasa ni awamu ya pili? Ni lini na yeye yuko tayari nami niko tayari naomba, anisaidie kwa jambo hili. (*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, najua katika jimbo lake Kituo cha Kiwanda cha Soda Maruhubi na Kituo cha Chumbuni ndivyo ambavyo vimeathirika sana. Nimwahidi mbele yako kwamba tarehe 22 na 23 mwezi huu wa Februari nitakuwa Zanzibar. Pamoja na mambo mengine nitakayofanya ni kutembelea Vituo yya Chumbuni. Ahsante sana. (*Makof*)

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Juma Usange, swali la nyongeza.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naitwa Juma Usonge.

Mheshimiwa Spika, Mko wa Kaskazini Unguja ni mkoa ambao unaongoza kwa shughuli za kitalii kwa Zanzibar, lakini pia *population* ya watu ni kubwa sana. Naiomba sana Serikali kuititia Mheshimiwa Waziri; wamejipangaje Wizara hii ili kuhakikisha Mko wa Kaskazini Unguja unakuwa na idadi kubwa ya Vituo vya Polisi, ingawa sasa hivi kuna Vituo vitano tu vya Polisi? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

### **NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Juma Usonge Hamad, Mbunge wa Chaani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, tumefanya tathmini ili tuweze kuona uchakavu wa vituo vilivyopo kwa madhumuni ya kuvifanyia ukarabati. Kwa hiyo baada ya kumaliza zoezi hilo, kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar tutaona maeneo mengine yanayohitaji kuimarishwa ulinzi ili tuweze kuona namna ya kuviongezea nguvu. Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zuena Bushiri, swali la nyongeza.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa matatizo yaliyopo Unguja na Pemba yanafanana sawa na matatizo yaliyopo katika Kituo cha Polisi cha Gonja Maore. Kituo hiki kilijengwa tangu mwaka 1958, kilijengwa kipindi cha Mkoloni. Nyumba zake zote zimechakaa sana, Kituo cha Polisi kimechakaa sana, miundombinu yake hasa maeneo ya

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

*toilets hayafai. Je, ni lini sasa Serikali itakwenda kufanya ukarabati katika nyumba hizo? Ahsante sana. (Makof)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**  
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Zueno Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kweli naomba nitumie nafasi hii kusema kwamba Wizara inatambua uchakavu wa vituo na makazi ya askari katika maeneo mbalimbali nchini. Ndiyo maana tunesema tunafanya tathmini ili kuona kiwango cha uchakavu, tuandae mpango kabambe wa kukarabati vituo hivi. Kwa hiyo, Kituo cha Mheshimiwa Mbunge cha Gonja Maore tutakifuatilia ili kuona katika mwaka ujao nini tunaweza kufanya kukirekebisha kiweze kutoa huduma kwa wananchi wa Gonja. Ahsante sana. (Makof)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abdulwakil Ahmed Yahya, swalii la nyongeza.

**MHE. AHMED YAHYA ABDULWAKIL:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Naomba nimuulize swalii Mheshimiwa Naibu Waziri; kwa kuwa Jimbo la Chukwani wananchi wamejenga kituo kipyaa cha ghorofa moja na mpaka sasa kimefikia asilimia 85, bado asilimia 15 kimalizike.

Naomba Serikali itoe kauli lini kituo kile kitamalizika na kuanza kutumika na hasa ukitia maanani kwamba lilitokea wimbi kubwa la mauaji katika eneo lile? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**  
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Yahya, kama ifuatavyo:-

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, napokea ombi au swalı lenye mwelekeo wa ombi la Mheshimiwa Yahya, kwamba katika vitu ambavyo tutaviangalia kule ambako wananchi wamejitokeza wakachangia nguvu zao na rasilimali zao nyingine kupitia Mfuko wetu wa tozo tunaweza kuwasaidia ili kukamilisha vituo hivyo. Kwa hiyo katika tathmini itakayofanyika kwa Mheshimiwa Mbunge pia tutapazingatia. Ahsante sana. (*Makofî*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Lucy John Sabu, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalı lake.

Na. 90

### **Kuweka Dirisha la Vijana Kwenye Benki za Serikali nchini**

**MHE. LUCY J. SABU** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka Dirisha Maalum la Vijana kwenye kila Benki za Serikali nchini ili kuwawezesha vijana kupata mitaji na mikopo yenyе riba nafuu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swalı la Mheshimiwa Lucy John Sabu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania inatekeleza sera na mikakati mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha kuwa riba za mikopo zinashuka ili kuwezesha makundi yote likiwemo kundi la vijana yanapata mikopo yenyе riba nafuu na kuweza kushiriki vyema katika shughuli za kiuchumi.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Benki za Serikali zinatoa huduma za mikopo kwa makundi yote likiwemo kundi la vijana kwa kuzingatia taratibu za utoaji mikopo za mabenki ambapo kwa wale wenye vigezo hupatiwa mikopo bila usumbufu wowote.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kutambua umuhimu wa kundi la vijana katika suala zima la upatikanaji wa mikopo yenye riba nafuu kwa ajili ya kuwawezesha kufanya shughuli za kiuchumi, Serikali ilianzisha programu maalum ya utoaji mikopo ya uwezeshaji yenye riba nafuu kwa vikundi vyatwanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2019 ambapo halmashauri zote zinatakiwa kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya kutoa mikopo kwa makundi hayo. Vijana wengi nchini wameendelea kunufaika na mikopo hiyo hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha vijana wote wanaokidhi vigezo na masharti ya kupata mikopo wanapatiwa mikopo ili kuendesha shughuli zao na hatimaye waweze kuwa na mchango kwenye ukuaji wa uchumi na pato la Taifa letu. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Sabu, swali la nyongeza.

**MHE. LUCY J. SABU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Ninalo swali moja dogo la nyongeza; kwa kuwa vijana wengi kutokidhi vigezo na masharti yatolewayo na mabenki.

Je, Serikali haioni haja ya kuweka kigezo cha miradi ama *business plan* ili vijana wengi waweze kukopesheka? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Lucy John Sabu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swalii hilo, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa juhudii zake za kuwatetea vijana. Ni kweli kwamba vijana walio wengi wanamaliza masomo na wengine ni hodari sana, wana uwezo mzuri wa kielimu, lakini hawakopesheki kwa sababu hawana dhamana. Serikali italicchukua hili kulipeleka kwa wataalam wetu kulifanyia uhakiki, ikionekana jambo hili linapendeza, basi *business plan* itatumika kama ni kigezo cha dhamana katika benki za Serikali.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa tumalizie Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalii lake.

Na. 91

**Kurudisha masomo ya ziada ya kazi za mikono mashulenii**

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA** aliuliza: -

Je, Serikali haioni umuhimu wa kurudisha masomo ya ziada ya kazi za mikono kama vile useremala, upishi, ushonaji, kilimo na ujenzi katika shule za msingi na sekondari ili kupunguza changamoto ya ajira?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba sasa kujibu swalii la Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kufundisha masomo ya kazi za mikono kama vile Useremala, Upishi, Ushonaji, Kilimo na Ujenzi ili kuwajengea wanafunzi stadi mbalimbali za maisha zitakazowasaidia kukabiliana na changamoto ya upatikanaji wa ajira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutilia mkazo masomo ya ziada ya kazi za mikono katika ngazi mbalimbali za elimu. Kwa mfano, katika ngazi ya Elimu ya Msingi, Stadi za Useremala, Upishi, Ushonaji, Kilimo na Ujenzi hufundishwa katika somo la Stadi za Kazi kuanzia Darasa la Tano. Pia, masomo ya ziada ya kazi za mikono yamekuwa yakifundishwa kama masuala mtambuka kuititia vilabu vya masomo. Katika ngazi ya sekondari, stadi na maarifa haya hufundishwa katika somo la *Home Economics* pamoja na masomo ya ufundi yakiwemo ya useremala na ujenzi. Vilevile, somo la Kilimo hufundishwa ngazi ya sekondari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inaendelea na mapitio ya mitaala ya elimu na mafunzo katika ngazi mbalimbali kwa lengo la kuboresha elimu na mafunzo yatolewayo ili yaweze kutoa stadi mbalimbali na kukidhi mahitaji ya jamii kwa maendeleo ya Taifa letu. Hivyo, nawaomba wadau mbalimbali wa elimu kuendelea kushiriki kikamilifu katika mchakato huu kwa kutoa maoni na ushauri utakaosaidia kuboresha elimu yetu. *Nakushukuru.* (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Najma Murtaza Giga swali la nyongeza.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namshukuru Mheshimiwa Waziri na naipongeza sana Serikali kwa kupokea mashauri mengi ya Waheshimiwa na kuyafanya kazi. Hata hivyo, nina maswali mafupi mawili ya nyongeza. Swali langu la kwanza, ni lini Serikali sasa itaweza kukamilisha mapitio hayo na kazi hii kuwa nzuri zaidi kwa manufaa ya vijana wetu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa vile Baraza la Mitihani la Taifa (*NECTA*) pamoja na Elimu ya Juu ni masuala

ya Muungano: Je, Serikali haioni umuhimu wa kushirikiana na Wizara ya Elimu Zanzibar ili manufaa ambayo watayapata vijana wetu wa Tanzania Bara na Zanzibar waweze kupata? (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba sasa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Giga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la uratibu au upitiaji upya wa mitaala yetu ni agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akihutubia Bunge tarehe 22 Aprili, 2021. Nasi kama Wizara, baada ya maagizo yale, tulianza kuyafanya kazi kwa haraka. Nimhakikishie Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba kazi ile inaendelea vizuri na tumeanza kukusanya hayo maoni; tulianzia pale Dar es Salaam, baadaye tukaenda Zanzibar na baadaye tulifanya hapa Dodoma na kazi hiyo bado inaendelea. Kazi hii inatarajija kukamilika baada ya miaka mitatu na miezi tisa. Tunatarajia mtaala huu mpya utaanza kutumika ifikapo Januari, 2025. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika eneo la pili ambalo amezungumzia namna gani Wizara hizi mbili katika maeneo haya, namna gani yanawenza kufaidika? Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, eneo ambalo tupo tofauti na wenzetu wa Tanzania Visiwani ni katika eneo la elimu ya msingi; lakini upande wa sekondari tunatumia mtaala wa aina moja na upande wa Vyuo Vikuu tunatumia mtaala wa aina moja.

Mheshimiwa Spika, nimwondoe wasiwasi, wakati tunafanya mapitio ya mitaala yetu hii, tunashirikiana kwa karibu sana na Taasisi ya Elimu ya Zanzibar, nayo vilevile inafanya mapitio ya mitaala hiyo ili basi ile Tanzania tunayoihitaji iweze kufikiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakushuruku sana.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na kujibwa na Serikali. Naishukuru Serikali kwa majibu waliyoyatoa.

Kabla sijaleta matangazo yaliyopo hapa, nitoe ufanuzi kidogo kuhusu maswali. Leo Waheshimiwa Wabunge wengi mlikuwa mnasimama lakini mlikuwa mnasikia wengine wakiitwa. Leo nilikuwa naangalia ambaao hawana maswali kabisa ya nyongeza. Kwa hiyo, kama unalo moja au mawili ndiyo maana hujapata hiyo fursa. Mtu mwenye mengi zaidi kwa sasa anayo matano na hao hawazidi wawili. Kundi linalofuata wanayo manne. Kwa hiyo, ukiona hujaitwa, hiyo ndiyo sababu. Hakuna sababu nyingine yoyote. (*Makofi*)

Kwa hiyo, leo walikuwa wanaangaliwa ambaao hawajapata fursa na Mbunge allyeuliza swali la pili ni mmoja tu. Kwa hiyo, wengine wote hawakuwa na swali kabisa. Kwa hiyo, tutaendelea kufanya hivyo ili kila Mbunge apate fursa ya kuuliza maswali. Hiyo haimaanishi wenyewe maswali matano hawatapata fursa, wataendelea kupata, lakini tunaangalia zaidi wale ambaao hayajapata fursa kabisa. (*Makofi*)

Sasa hilo nimeona nifafanue; na hapa kuna Mbunge anataka ufanuzi, kama hawajasimama! Maana yake unatunzwa muda kwa ajili ya maswali mengine ambayo wameomba wale ambaao hawana nafasi. Kwa hiyo, usije kusema swali hili nimesimama peke yangu lakini Spika bado hajaniona. Aah, nimekuona, lakini inabidi nitunze muda kwa ajili yule ambaye hana swali anayekusudia kusimama swali la mbele. Kwa hiyo, mambo yataenda vizuri tu, hakuna mtu ataonewa Waheshimiwa Wabunge, msiwe na wasiwasi. (*Makofi*)

Nilete tangazo la wageni tulionao siku ya leo hapa Bungeni. Kwanza ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, ambaye ni Naibu Waziri wa Kilimo; na hawa ni wafanyakazi wa Kampuni ya *Agriedo* inayoendesha *Incubation Herb* kwa ajili ya vijana wanaofanya kilimo kutoka

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mkoa wa Iringa, wakiongozwa na Mhasisi na Mtendaji Mkuu wa *Agriedo* Ndugu Hadija Jabiri ambaye pia ni mwanzilishi wa Kampuni ya *GBR* inayofanya usafirishaji wa mazao ya mbogamboga na matunda. Karibuni sana, sana wageni wetu. (*Makofi*)

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano wa Mazingira kutoka Zanzibar, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Baraza la Vijana Taifa, Ndugu Yunus Juma Ali. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Jackson Kiswaga, ambaye ni mpiga kura wake kutoka Kalenga, Mkoani Iringa na huyu ni Ndugu Daniel Eliuta Mwangile. Karibu sana. (*Makofi*)

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Mwita Waitara ambaye ni Katibu wa Mbunge kutoka Tarime, Mkoa wa Mara, huyu ni Ndugu Remy Pascal Mkapa. Karibu sana. (*Makofi*)

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Zaituni Swai, ambaao ni Waandishi wa Habari kutoka Mkoani Arusha na hawa ni Ndugu Teodoila Mrema na Ndugu Jane Edward. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi ambaao ni Mwenyekiti wa Jumuia ya Wazazi, Kata ya Maretadu, Ndugu Stanley Hayashi na mdogo wake Ndugu Samuel Kobe. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Condester Sichalwe, ambaye ni Diwani wa Kata ya Ivuna - Momba, Mkoani Songwe na huyu ni Mheshimiwa Eric Mkamba. Karibu sana Mheshimiwa Diwani. (*Makofi*)

Pia tunao wageni wa walolitembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wanafunzi 90 na walimu 10 kutoka Shule ya Msingi Shalom ya Njiro, Jijini Arusha. Karibuni sana, sana vijana wetu na walimu wenu na tunawatachia kila

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

la heri katika masomo yenu. Tunaamini mmepeata fursa ya kujifunza jambo moja ama mawili. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tena, watu wanaoruhusiwa kupita hapa mbele kwenye huu mzunguko Siwa ikiwa hapa mbele ni hawa Wahudumu wa Bunge na siyo Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, hata kama unakuja kuleta hoja hapa mbele, usikatize mbele ya Siwa. Kama unakaa upande huu, basi hakikisha umekaa upande ambaao utashuka kutokea upande ule unaotoka, usikatize kwenye huu mzunguko Siwa ikiwa hapa mbele. Kwa sababu Siwa ndio Mamlaka yetu sisi Wabunge, kwa hiyo, usikatize hapa katikati Mheshimiwa Mbunge. Wale ambaao hawapo, akiwa jirani yako, mkumbushe. Hairuhusiwi kukatiza mbele ya Siwa. Wanaoruhusiwa kukatiza ni Wahudumu. Wabunge lazima tutoke kwenye hizi pande.

Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. Baada ya kusema hayo, anaingia sasa Mwenyekiti kuendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. David M. Kihenzile) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA KAMATI**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na  
Maendeleo ya Jamii kuhusu Shughuli za Kamati  
kwa mwaka 2021na Taarifa ya Kamati ya  
Kudumu ya Masuala ya Ukimwi kuhusu  
shughuli za Kamati kwa  
mwaka 2021

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Stanslaus Nyongo. (*Makofii*)

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kukushukuru kwa kunipa fursa hii adhimu ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa Majukumu na shughuli za Kamati kwa kipindi cha mwaka 2021/2022. Hii ni Taarifa ya Mwaka ya Kwanza ya Kamati kuwasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, taarifa hii imegawanyika katika maeneo makuu yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Kwanza ni utangulizi wenyewe kueleza Muundo, Majukumu ya Kamati na kuainisha shughuli zilizotekelizwa na Kamati; Sehemu ya Pili, inaeleza kuhusu namna Kamati iliyotekeliza majukumu yake na yaliyobainika wakati wa utekelezaji huo; vile vile Sehemu ya Tatoo inatoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati; na Sehemu ya mwisho ni Hitimisho la taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane, Sehemu ya Sita fasili ya (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii imepewa jukumu la kusimamia shughuli za Wizara tatu yaani: -

- (a) Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa wakati huo;
- (b) Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo; na
- (c) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Nyongeza ya Nane, Sehemu ya Saba ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, imemeanisha majukumu ya Kamati za Kisekta ikiwemo Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuwa ni pamoja na:-

**NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

- (a) Kushughulikia Bajeti ya Wizara inazosisimamia;
- (b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba iliyopendekezwa kuridhiwa na Bunge ilio chini ya Wizara inazosisimamia;
- (c) Kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara hizo pamoja Taasisi zilizo chini yake; na
- (d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu shughuli zilizotekeliza na Kamati; katika kipindi cha mwaka 2021/2022, Kamati ilipata wasaa wa kutekeleza majukumu yake mbalimbali ambayo imepewa kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge. Shughuli ambazo Kamati imezitekeleza ni pamoja na:-

- (a) Kujifunza shughuli au kuhusu shughuli zinazotekeliza na Wizara inazosisimamia pamoja na taasisi zake;
- (b) Kufanya ziara na ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2020/2021;
- (c) Kupokea, kuchambua na kujadili taarifa za utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021 na mwelekeo wa bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022;
- (d) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za utendaji wa Wizara na taasisi inazosisimamia;
- (e) Kupokea, kuchambua na kujadili taarifa za utendaji na utekelezaji wa bajeti wa Wizara na Taasisi kwa kipindi cha nusu mwaka, yaani Julai – Desemba 2021;
- (f) Kushiriki semina za mafunzo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Pili ya taarifa hii, ilikuwa ni kuchambua kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Katika kipindi cha mwaka 2021/2022, Kamati ya

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii imefanikiwa kutekeleza majukumu yake ya Kikanuni kwa kufanya yafuatayo: -

(i) Kujifunza kuhusu shughuli za Wizara inazozisimamia, kwa sababu kufuatia uchaguzi Mkuu uliofanyika Mwezi Oktoba, 2020, idadi kubwa ya Wabunge waliochaguliwa walikuwa ni wapya ambao pia ilipelekea idadi kubwa ya Wajumbe wa Kamati nao kuwa wapya. Upya huo wa Wajumbe wa Kamati ulilazimu uwepo wa vikao vya kuwezesha kujifunza muundo na majukumu ya Wizara inazozisimamia ili kuweza kuzishauri vyema.

Hivyo basi, katika vikao vya mwezi Januari, 2021 Kamati ilikutana na Wizara inazozisimamia na kuelimishwa kuhusu Muundo na Majukumu ya Wizara na Taasisi zake inazozisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vikao hivi viliwezesha Wajumbe wa Kamati kuelewa kuhusu muundo na majukumu yanayotekelawa na Wizara hizo pamoja na Taasisi zake. Aidha, Wajumbe walipata wasaa wa kutosha wa kuuliza maswali kwa lengo la kupata ufanuzi, pia kutoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ambapo Kamati ina imani kuwa kama yatakelezwaa ipasavyo, basi yatasaidia kuboresha utendaji wa Wizara hizo na Taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulifanya ukaguzi wa miradi mbalimbali kwa kuzingatia matakwa na Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka 2020. Kamati yetu ilifanikiwa kufanya ziara katika mikoa miwili ambapo ni Dodoma na Dar es Salaam.

Awali, Kamati ilipanga kufanya ziara katika mikoa mitatu ikiwemo Arusha na kukagua jumla ya miradi tisa. Hata hivyo, kufuatia msiba ambao ulilikumba Taifa letu wa kuondokewa na aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Kamati ilisitisha ziara katika mikoa hasa katika Mkoa wa Arusha.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanikiwa kukagua jumla ya miradi minne iliyo chini ya Wizara zake kama ifuatavyo:-

- (i) Mradi wa Upanuzi wa Usikivu wa *TBC (Expansion of TBC Coverage Na. 4279)*;
- (ii) Mradi wa Taasisi ya Saratani (*Ocean Road*);
- (iii) Mradi wa Taasisi ya Mifupa Muhimbili (*MOI*);
- (iv) Mradi wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete; na
- (v) Mradi wa Vifaa Tiba wa Idofi kule Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati ilipokea taarifa za miradi mingine minne ambayo haikuweza kutembelewa katika Mkoa wa Arusha. Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna Mradi wa Ujenzi Tume ya Nguvu za Atomiki, yaani Arusha; Miradi ya Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela, Arusha, Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo cha Ufundis Arusha na Mradi wa Ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Monduli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa za kina kuhusu hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi hiyo zilikuwa ni sehemu ya taarifa za Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara hiyo zillizowasilishwa Bungeni kuanzia mwezi Aprili hadi Juni, 2021. Pia tulipokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri Kamati za Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na Mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni Na. 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, mara baada ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa za Utekelezaji wa

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Maoni ya Kamati na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa za kina za uchambuzi wa Bajeti za Wizara tatu ambazo kwa sasa zimekuwa nne zinazosimamiwa na Kamati pamoja na maoni na ushauri wa Kamati zilizowasilishwa katika Mkutano wa Tatoo wa Bunge la Bajeti uliokamilizika Mwezi Juni, 2021. Aidha, Kamati inaendelea kusisitiza baadhi ya maoni ambayo inaona bado hayajatekeleza kikamilifu katika taarifa hii.

Katika vikao vya Kamati vilivyo fanyika mwezi Agosti ,2021 na Oktoba, 2021, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa za Utendaji wa Wizara na Taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukianza na Wizara ya Elimu; kupitia Wizara hii, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili taarifa na utekelezaji wa taasisi zifuatazo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokea Chuo cha Ufundji Arusha, ambapo tuliweza kugundua kwamba kuna upungufu wa watumishi ikilinganishwa na ikama iliyopo; vilevile kuna upungufu wa madarasa na maabara kulingana na idadi ya wanafunzi. Kamati ilitaarifiwa kuwa Chuo kimeshawasilisha ombi la fedha kumaliza jengo ambalo linagharimu shilingi bilioni 2.1; uUhaba wa malazi kwa wanafunzi kwani kwa sasa Chuo kina idadi ya wanafunzi 3,809 na mabweni ya Chuo kwa sasa yana uwezo wa kuchukua wanafunzi 884 sawa na 23% tu, wanafunzi wa kiume wakiwa 698 na wa kike wakiwa 186.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wa Taarifa hiyo, Kamati imebaini masuala mbalimbali yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, kumekuwa na ongezeko la wanafunzi wa kike kutoka 389, ambapo ilikuwa ni mwaka 2015/2016 hadi 704 mwaka 2020/2021. Sawa na ongezeko la asilimia 80.97 jambo ambalo ni jema na Kamati inapongeza sana kwa hatua hiyo.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili, Chuo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kimeshafanya tafiti katika maeneo mbalimbali ya sayansi, teknolojia na ubunifu. Ikiwa ni pamoja na kufanya utafiti, ubunifu na ukarabati wa vifaa tiba, katika mahospitali mbalimbali nchini na hivyo kupunguza gharama na mzigo kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Chuo hakitengewi bajeti ya kutosha ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo, hususan ujenzi wa mabweni, jambo ambalo limekuwa ni kikwazo kwa watoto wa kike kujunga katika Chuo, lakini pia katika utendaji wa Chuo suala hili limekuwa ni kilio kwa Kamati kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tulipitia Sera ya Elimu ya Mafunzo ya Mwaka, 2014. Kamati ilipokea Taarifa kuhusu utekelezaji wa Sera ya Elimu ya Mafunzo ya mwaka, 2014 na kuifahamu, lakini pia kuona ni kwa kiasi gani Sera inaendana na mabadiliko ya sasa ya dunia, hasa katika karne hii ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka, 2014 iliandaliwa ikiwa ni matokeo ya kuhuishwa na hatimaye, kufutwa kwa Sera ya Elimu ya Mafunzo ya mwaka, 1995. Sera ya Elimu ya Ufundu ya Mwaka, 1996 na Sera ya Taifa ya Elimu ya Juu ya mwaka, 1999 na Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilize Hotuba ambayo ni ya kwetu sisi wenyewe, ya Kamati. (*Makofii*)

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sera iliandaliwa kwa lengo la kutoa mwelekeo wa elimu na mafunzo nchini kwa kuzingatia mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, kisayansi na kiteknolojia na changamoto ya elimu ya mafunzo ya kitaifa, kikanda na kimataifa. Ili kuongeza fursa, ufanisi na ubora wa

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

elimu ya mafunzo nchini na kufikia kiwango cha rasilimali watu kwa nchi yenye uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa, tangu kutungwa kwa Sera hii kumekuwa na mafanikio mbalimbali kama vile kuongezeka kwa upatikanaji wa vifaa, uboreshaji wa mitaala, sayansi, teknolojia na ubunifu. Kutolewa kwa elimu bure kwa shule za msingi na sekondari, pia kuongezeka kwa wanafunzi na ufaulu pamoja na miundombinu ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo, Kamati imebaini uwepo wa changamoto ambazo zimekuwa kikwazo katika utekelezaji mzuri wa Sera hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, ikiwa ni uhaba wa walimu, wakufunzi, wahadhiri na mafundi sanifu wa maabara za shule, kulingana na mahitaji katika ngazi zote za elimu na mafunzo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia vinavyoendana na mabadiliko ya sasa ya sayansi na teknolojia katika ngazi zote za elimu na mafunzo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, uwekezaji mdogo katika elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi pamoja na elimu ya juu katika fani ya sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati. Kamati inaona ni wakati muafaka sasa kwa Serikali kuanza kuzifanya kazi changamoto hizi, ili iweze kuboresha elimu nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipitia vile vile kuona Chuo cha Sayansi cha Teknolojia cha Mbeya, ambapo tuliona kwamba Chuo hiki sasa kimeweza kudahili wanafunzi 6,817. Kati yao, wanafunzi wa kike wako 1,500 na wa kiume ni 5,000 sawa na ongezeko la asilimia 20, ikilinganishwa na mwaka wa 2019/2020 ambapo wanafunzi walikuwa 5,678 waliodahiliwa. Pia kutoa huduma ya ushauri wa kitaalamu kupitia wataalam wake kupitia kampuni yake, ya *MCB Company Limited* na hususan ushauri elekezi kibashara.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Kimejikita zaidi katika sekta ya ujenzi pamoja na usimamizi wa miradi mbalimbali katika sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Chuo hiki, Kamati imebaini kuwa Chuo kina changamoto mbalimbali zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, ni upungufu wa miundombinu ya kujifunzia na kufundishia ikiwemo madarasa, karakana na maabara;

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuna upungufu wa mabweni; na

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu idadi ndogo ya wanafunzi wa kike wanaojiunga katika Chuo hiki. Tulipitia vile vile katika Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ambapo Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili taarifa zifuatazo katika Wizara hii:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwanza ilikuwa ni taarifa ya Baraza la Michezo Tanzania ambapo Kamati ilibaini, changamoto zilizokuwa zikilikumba Baraza hili na changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, uhaba wa rasilimali fedha za kusaldia timu za Taifa;

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili, miundombinu isiyokidhi matakwa ya kikanuni hasa viwanja vya michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Kutokuzingatia misingi ya utawala bora na uongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, mawasiliano hafifu baina ya Baraza la Michezo na Makatibu Tawala wa Mikoa pamoja na Wilaya.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni usimamizi mbovu wa masharti ya mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Kamati za Michezo za Mikoa hazijawezeshwa vya kutosha kutengeneza bajeti ya kutosha ili kuweza kuratibu vyema michezo katika ngazi hizo za chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tuliweza kupitia na kupata ripoti kutoka katika Bodi ya Filamu Nchini. Pamoja na kupokea taarifa ya mafanikio na changamoto, Kamati imebaini masuala yafuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, kuibuka wimbi la baadhi ya wasanii kuchafua wenzao hivyo kuna haja ya Wizara kuchukua hatua, kwa kuhakikisha maadili ya wasanii yanazingatia hadhi na tasnia ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, uharamia wa kazi za wasanii bado unaendelea hivyo, ipo haja ya kuweka mikakati na kudhibiti ili wasanii hao waweze kunufaika na jasho lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, zile *script* za filamu zetu baadhi hazipo katika lugha fasaha na hivyo kushindwa kuvutia soko la ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, kutokuwa na ubora wa tafsiri za cinema zetu za maandishi na maneno yanayotafsiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, tuliweza kupitia Baraza la Kiswahili la Taifa, Kamati ilielezwa baadhi ya changamoto ambazo BAKITA inakumbana nazo. Hasa, ni ufinyu wa rasilimali fedha katika kubidhaisha Kiswahili na uhaba wa watumishi. Katika kupitia, kuchambua na kujadili Taarifa hii ya BAKITA Kamati imebaini masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, bado jitihada zinatakiwa kwa Wizara kutengeneza Kiswahili kuwa bidhaa, kwa kufunganisha na sekta zingine kwa mfano sekta ya utalii.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, idadi ya wanafunzi wanaosoma Kiswahili katika ngazi za Vyuo bado ni ndogo. Hivyo, Wizara inashauriwa iweke mikakati ya kuhamasisha vijana wa Kitanzania, kujifunza Kiswahili kama sehemu ya mikakati ya kubidhaisha Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kutokwa na mkakati wa kutumia Balozi zetu kuanzisha vituo vya kutoa mafunzo ya lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumepitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Wazee ya wakati huo. Kwa upande wa Wizara hii, Kamati ilipokea, ikachambua na kujadili:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, hatua iliyofikiwa katika maandalizi ya Muswada wa Bima ya Afya kwa wote. Kamati ilipokea na kujadili Taarifa hii kuhusu hatua iliyofikiwa katika maandalizi ya Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa watu wote. Taarifa hiyo ilieleza masuala mbalimbali ikiwemo pamoja na namna Wizara, ilivyoanza kufanya maandalizi ya kutunga Sheria ya Bima ya Afya kwa wote toka mwaka, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa katika hatua za awali, tafiti mbalimbali zilifanyika katika maeneo mbalimbali ya ugharamiaji wa huduma za afya na kufuatiwa na maandalizi ya mkakati wa ugharamiaji wa huduma za afya wa mwaka, 2016. Mkakati huo ulilenga kuhakikisha kuwa kila mwananchi anatumia bima ya afya katika kupatiwa huduma za afya/matibabu. Baada ya kuwasilisha mkakati huo ngazi za maamuzi za mwaka 2016, ilibainika kuwepo kwa uhitaji wa kutunga Sheria itakayotumika kutekeleza mkakati wa kugharamia. Hivyo Wizara ilishauriwa kuandaa Waraka mahususi wenye lengo la kutunga Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilielezwa kuwa taratibu mbalimbali zimekuwa zikifuatwa katika kuhakikisha Sheria ya Bima ya Afya kwa wote inatungwa, kwa kuzingatia

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

maelekezo ya llani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka, 2020. Yanayolenga kufikia bima ya afya kwa wote kwa kuimarisha Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (*NHIF*) na Mfuko wa Afya ya Jamii (*CHF*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Wizara kuchukua mwelekeo huo, mchakato wa maandalizi ya Muswada wa kutunga Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote umechukuwa muda mrefu, kutokana na suala la ugharamiaji wa bima ya afya kwa watu wasio na uwezo kabisa ambao ni asilimia 26.4 ambao ilhitaji kupata ufumbuzi ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa, suala hilo tayari limepata ufumbuzi ambapo Serikali imejipanga kuwa itatenga fedha kupitia bajeti ya kila mwaka. Ili kugharamia kadi za bima za afya za watu wasiokuwa na uwezo kulingana na orodha ya kaya zenyе mahitaji hayo. Aidha, kwa sasa Wizara inategemea kuwasilisha kwa mara ya mwisho waraka katika ngazi ya *Inter Ministerial Technical Committee* na baadae kufikishwa katika Baraza la Mawaziri ili Muswada huo wa Sheria wa Bima ya Afya kwa Wote uanze kuandaliwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokea Taarifa hiyo na kueleza masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, Sheria itakayotungwa iħakikishe kunakuwepo na uboreshaji wa upatikanaji wa huduma kama dawa, vipimo ili kuepuwa usumбуfo ambao wananchi wamekuwa wakiupata hasa walipokuwa na ule mfumo wa *CHF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ili kuhakikisha huduma zinaboreshw, changamoto ya uhaba wa watumishi katika Sekta ya Afya lazima ipatiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Sheria iwe wazi kuhusu masuala ya udhibiti na usimamizi. Ianzishwe Mamlaka ya Udhibiti (*Regulatory Authority*) ya Bima ya Afya badala ya kutumia (*TIRA*) *Tanzania Insurance Regulatory Authority*.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, Serikali ihakikishe kunakuwa na *ring-fenced budget* ya Mfumo wa Bima ya Afya, hasa ikizingatiwa kuwa kuna wengi hawana uwezo ili kuepuka Mfuko huo kufilisika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ili kuboresha utoaji wa huduma ya Afya Sheria itakapokuja sekta binafsi, ziruhusiwe na kuwepo na ubunifu utakaowezesha wananchi kuchagua vifurushi wanavyoona vinafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara hiyo hiyo ya Afya kuhusiana na Bohari Kuu ya Dawa (*MSD*); Kamati ilipokea taarifa hiyo ya *MSD*, ambayo ilieleza masuala mbalimbali kama hali ya fedha, rasilimali watu na upatikanaji wa dawa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati illelezwa kuwa hali ya upatikanaji wa dawa imeimarika kwa sasa ikilinganishwa na hapo awali, kutokana na fedha za dawa zimeanza kuwa *ring-fenced* na kutolewa kila mwezi. Utaratibu huu umewezesha uwepo wa uhakika wa upatikanaji wa dawa kwa wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa changamoto, Kamati ilielezwa changamoto zifuatazo ambazo *MSD* inakumbana nazo kuwa ni pamoja na:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa viwanda vyatanya ndani vyatanya kutengeneza dawa na hivyo, kuongeza gharama za manunuvi ya bidhaa kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, taarifa ya ukosefu wa dawa (*out of stock*) zimekuwa zikichelewa kutolewa katika vituo vyatanya afya, jambo linalosababisha vituo vyatanya afya kutokupata dawa kwa wakati. Ipo haja ya Taarifa hizi kutolewa mapema kwa vituo vyatanya afya ili waone namna ya upatikanaji wa dawa hizo.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ipo haja ya kufanya marekebisho ya Sheria iliyounda *MSD* ili kuruhusu sasa *MSD* kufanya kazi ya uzalishaji wa dawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, mfumo wa utendaji wa *MSD* ni mzuri sana ipo haja ya kuiweka mifumo hii rasmi kisheria, ili kuwezesha maboresho yanayoendelea kufanya kutekelezwa kwa wakati hata wakati Mkurugenzi aliye po anapokuwa nje ya kazi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende kwenye maoni na ushauri na mapendekezo ya Kamati yetu. Baada ya maelezo ya kina kuhusu shughuli zilizotekelizwa na Kamati pamoja uchambuzi wake, naomba kuwasilisha Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze na maoni ya jumla. Kwanza, Miundombinu ya Sekta ya Elimu ya Afya:-

KWA KUWA kumekuwa na kilio cha muda mrefu cha uhaba wa miundombinu ya elimu na afya; (*Makofii*)

NA KWA KUWA Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan kupitia fedha za mkopo wa kupambana na UVICO 19 amejenga madarasa na vituo vya Afya nchi nzima;

HIVYO BASI Bunge inatoa pongozi kwa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuelekeza fedha hizo, katika ujenzi wa miundombinu ya Elimu ya Afya hapa nchini pamoja na elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, uhaba wa watumishi:-

KWA KUWA changamoto ya watumishi katika Sekta ya Afya, Elimu, Maendeleo ya Jamii na Utamaduni, Sanaa na Michezo bado ni kubwa;

NA KWA KUWA upungufu wa watumishi hawa umekuwa ukileta athari katika utoaji wa huduma mbalimbali;

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

HIVYO BASI Bunge linaitaka Serikali kutoa kipaumbele cha ajira, kwa sekta hizi mbili muhimu hususan sekta ya afya na sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la bajeti:-

KWA KUWA utekelezaji wa majukumu ya Wizara, unategemea kutengwa kwa bajeti ya kutosha lakini pia utolewaji wa fedha hizo;

NA KWA KUWA bajeti finyu na utolewaji usioridhisha umekuwa ukiathiri, utekelezaji bora wa majukumu ikiwemo utoaji wa huduma kwa wananchi;

HIVYO BASI Bunge lako linaitaka Serikali kuziangalia sekta hizi, kwa jicho la pekee kwa kuzitengea fedha za kutosha, lakini pia, kuhakikisha bajeti hizo zilizoldhinishwa na Bunge zinatolewa zote na kwa wakati ili kuleta ustawi bora wa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Wizara ya Afya:-

KWA KUWA upatikanaji wa huduma za afya kwa wote ni haki ya msingi ya kila mwanadamu, lakini pia ni utekelezaji wa lengo Na. 3 la Malengo ya Milenia;

NA KWA KUWA mpaka sasa ni asilimia 26 tu ya Watanzania ndiyo wanaofikiwa na Huduma ya Bima ya Afya;

HIVYO BASI Bunge lako linaitaka Serikali kuhakikisha kuwa inaleta Muswada wa Sheria wa Bima ya Afya kwa Wote mapema iwezekanavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na watoto njiti:-

KWA KUWA watoto njiti wamekuwa wakipata changamoto mbalimbali za kiafya zinazowafanya washindwe kuishi kama watoto wengine;

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

NA KWA KUWA ukosefu wa huduma bora hupelekea watoto hao kupoteza maisha;

HIVYO BASI Bunge lako linashauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, Serikali ije na mkakati wa kuwalinda na kuhakikisha watoto hawa wanapata Bima ya Afya mapema baada ya kuzaliwa, ili kuwapunguzia gharama za matibabu wazazi wanaopata watoto hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Wizara ifanye mapitio ya likizo za wazazi wanaojifungua watoto njiti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na *MSD*:-

KWA KUWA Bohari Kuu ya Dawa imekuwa ikifanya kazi kubwa ya kuhakikisha kunakuwepo ufanisi katika upatikanaji wa dawa na vifaa tiba;

NA KWA KUWA tayari Bohari imeanza uzalishaji wa dawa nchini jambo ambalo linapunguza gharama ya ununuzi wa dawa kutoka nje ya nchi;

HIVYO BASI Bunge linaishauri Serikali kuongeza Bajeti ya *MSD* ili iweze kuzalisha, kununua dawa na vifaa tiba vyta kutosha na hivyo kuondoa changamoto ya ukosefu wa dawa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie. Kumekuwa hakuna ulinganifu wa usambazaji na usimamizi wa matumizi ya dawa katika ngazi zote za huduma za afya (kuanzia mikoani hadi zahanati). Kutokuwa na ulinganifu huo kunapelekea uhaba wa dawa, katika baadhi ya hospitali wakati hospitali zingine hazina dawa... (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa nimekuongeza dakika mbili naomba uhitimishe.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, tunaomba/tunashauri Bunge kuwe na mfumo madhubuti wa kusimamia, usambazaji na matumizi ya dawa hizo kulingana na mahitaji katika eneo husika. Vile vile, naomba maoni yote na mapendekezo ya Kamati yaliyomo basi yaweze kuingia, kwenye *Hansard* na yaweze kuchukuliwa maamuzi na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile kwenye Wizara ya Elimu zoezi la uboreshaji wa mitaala linapaswa kujumuisha katika ngazi nydingine za Vyuo vya Ufundii na Vyuo Vikuu ambazo nazo pia mitaala yake ina changamoto. Muda wa kukamilika wa zoezi hili la kuanza kutumia mitaala mipyä ambayo inasemwa iwe mpaka mwaka 2026 ni mrefu mno. Wizara ione namna ya kufupisha jambo hili ili liweze kutumia muda mfupi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda naomba kuhitimisha kwamba natoa pongezi kwa Mawaziri wote tuliofanya nao kazi, ambaao ni Dkt. Dorothy Gwajima aliyekuwa Waziri wa Afya. Vilevile nitoe pongezi sana kwa Naibu wake Dkt. Godwin Mollel. Pia pongezi kwa Mheshimiwa Profesa Ndalichako ambaye naye tulifanya naye kazi na sasa hivi, tuna Waziri mpya na Mawaziri wote na watumishi wote wa Bunge ambaao tumefanya nao kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiumuhimu wa pekee niwapongeze sana Wajumbe wa Kamati yangu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, ambaao tumefanya nao kazi kwa weledi wa hali ya juu. Hivyo basi, nichukue fursa hii na naomba sasa, kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA SHUGHULI ZA  
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO  
YA JAMII KWA MWAKA 2021/2022**

-----

**SEHEMU YA KWANZA**

**UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kukushukuru kwa kunipa fursa hii adhimu ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa Majukumu na shughuli za Kamati kwa kipindi cha Mwaka 2021/2022. Taarifa hii ni Taarifa ya Mwaka ya kwanza ya Kamati kuwasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, Taarifa hii imegawanyika katika maeneo makuu yafuatayo:-

- i) Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi wenyewe kueleza Muundo, Majukumu ya Kamati na kuainisha shughuli zilizotekeliza na Kamati;
- ii) Sehemu ya Pili inaeleza kuhusu namna Kamati ilivyotekeliza Majukumu yake na yaliyobainika wakati wa utekelezaji huo;
- iii) Sehemu ya Tatu inatoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati; na
- iv) Mwisho ni Hitimisho la Taarifa hii.

**1.1 Muundo na Majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane 6 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii imepewa jukumu la kusimamia shughuli za Wizara tatu (3) zifuatazo: -

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

- (a) Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto;
- (b) Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo; na
- (c) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Aidha, Nyongeza ya Nane, 7 (1) (a-d) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, imeainisha Majukumu ya Kamati za Kisekta ikiwemo Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuwa ni pamoja na: -

- a) Kushughulikia Bajeti ya Wizara inazozisimamia;
- b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;
- c) Kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara hizo pamoja Taasisi zilizo chini yake; na
- d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

### **1.2 Shughuli zilizotekelizwa na Kamati**

**Mhesimiwa Spika**, katika Kipindi cha Mwaka 2021/2022, Kamati ilipata wasaa wa kutekeleza majukumu yake mbalimbali ambayo imepewa kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge. *Shughuli ambazo Kamati imezitekeleza ni pamoja na:-*

- (a) Kujifunza kuhusu Shughuli zinazotekelizwa na Wizara inazozisimamia pamoja na Taasisi zake;
- (b) Kufanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021;
- (c) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na mwelekeo wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;

- (d) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za utendaji wa Wizara na Taasisi inazozisimamia;
- (e) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za utendaji na utekelezaji wa bajeti wa Wizara na Taasisi kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba 2021); na
- (f) Kushiriki Semina za mafunzo

### **SEHEMU YA PILI**

---

## **2.0 UCHAMBUZI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha mwaka 2021/2022, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii imefanikiwa kutekeleza majukumu yake ya Kikanuni kwa kufanya yafuatayo: -

### **2.1 Kujifunza kuhusu shughuli za Wizara inazozisimamia**

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia uchaguzi Mkuu wa Taifa uliofanyika Mwezi Oktoba 2020, Idadi kubwa ya Wabunge waliochaguliwa walikuwa ni wapya ambao pia walipelekea idadi kubwa ya wajumbe wa Kamati nao kuwa wapya. Upya huo wa Wajumbe wa Kamati ulilazimu uwepo wa vikao vya kuweza kujifunza muundo na majukumu ya Wizara inazozisimamia ili kuweza kuzishauri vyema. Hivyo basi, katika vikao vya mwezi Januari 2021, Kamati ilikutana na Wizara inazozisimamia na kuelimishwa kuhusu:-

- a) Muundo na Majukumu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Idara Kuu Afya) pamoja na Taasisi zilizo chini yake ambazo ni Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Mfuko Wa Taifa Wa Bima ya Afya (NHIF), Hospitali ya Magonjwa ya Kuambukiza – Kibong’oto, Hospitali za Rufaa za Mikoa, Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), Hospitali ya Afya

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

ya Akili –Mirembe, Maabara ya Mkemia Mkuu Wa Serikali, Bohari Kuu ya Dawa (MSD), na Taasisi ya Chakula na Lishe – (TFNC); na Taasisi ya ya Moyo ya Jakaya Kikwete - (JKCI)

b) Muundo na Majukumu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Idara Kuu Maendeleo ya Jamii) pamoja na Taasisi zilizo chini yake ambazo ni Taasisi ya Ustawi wa Jamii Kijitonyama na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru;

c) Muundo na Majukumu wa iliyokuwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na zilizokuwa Taasisi zake ambazo ni Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC); Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN); Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA); Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA); Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA); Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSuBa); Taasisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA); Bodi ya Filamu Tanzania; Baraza la Michezo la Taifa (BMT); na Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya; na

d) Muundo na Majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Taasisi zake ambazo ni Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA); Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundsi Stadi (VETA); Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundsi (NACTE); Tume ya Vyuo Vikuu (TCU); Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA); Taasisi ya Elimu Tanzania (TET); Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB); Vyuo vikuu vya umma; Tume ya Taifa ya UNESCO na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH).

**Mheshimiwa Spika**, Vikao hivi viliwezesha Wajumbe wa Kamati kuelewa kuhusu muundo na majukumu yanayotekelzwa na Wizara hizo pamoja na Taasisi zake. Aidha, Wajumbe walipata wasaa wa kutosha wa kuuliza maswali kwa lengo la kupata ufanuzi lakini pia kutoa maoni, ushauri na mapendekozo mbalimbali ambayo ni imani ya Kamati kuwa kama yatakelezwa ipasavyo basi yatasaidia kuboresha utendaji wa Wizara hizo na Taasisi zake.

## 2.2      **Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ilifanikiwa kufanya Ziara katika Mikoa miwili ambayo ni Dodoma na Dar Es Salaam. Awali Kamati ilipanga kufanya ziara katika Mikoa mitatu ikiwemo Arusha na kukagua jumla ya Miradi 9. Hata hivyo, kufuatia msiba mzito ambao ulilikumba Taifa letu wa kuondokewa na aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Kamati ilikatisha ziara katika Mkoa wa Arusha.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanikiwa kukagua jumla ya miradi minne (4) ilio chini ya Wizara mbili ambazo ni pamoja na iliyokuwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (Mradi 1) na iliyokuwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Miradi 3) kama ifuatavyo: -

- (i) Mradi wa Upanuzi wa Usikivu TBC (Expansion of TBC Coverage) (Namba ya Mradi 4279)
- (ii) Mradi wa Taasisi ya Saratani Ocean Road – ORCI (Mradi Namba 5412);
- (iii) Mradi wa Taasisi ya Mifupa Muhimbili – MOI (Mradi Namba 5491); na
- (iv) Mradi wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete – JKCI (Mradi Namba 5419)
- (v) Mradi wa Vifaa Tiba wa Idofi Njombe

Aidha, Kamati ilipokea Taarifa za Miradi mingine minne (4) ambayo haikuweza kutembelewa katika Mkoa wa Arusha. Miradi hiyo ni kama ifuatavyo: - Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Tume ya Nguvu za Atomiki Arusha, Miradi ya Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela – Arusha, Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo cha Ufundi Arusha na

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mradi wa Ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Monduli.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa za kina kuhusu hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa Miradi hiyo zilikuwa ni sehemu ya Taarifa za Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara hizo zilizowasilishwa Bungeni kuanzia mwezi Aprili hadi Juni, 2021.

### **2.3 Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa Maoni na Ushauri Kamati na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, mara baada ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa za utekelezaji wa Maoni ya Kamati na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara inazosimamia kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika**, katika vikao hivyo, Kamati ilipata wasaa mzuri wa kuchambua, kuhoji na kujadili utekelezaji wa bajeti ya Wizara inazosimamia kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Aidha, Kamati ilipata wasaa wa kuchambua, kuhoji, kujadili na hatimaye kutoa maoni, ushauri na mapendekezo muhimu kwa Bajeti ya Wizara hizo tatu zilizo chini ya usimamizi wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa za kina za Uchambuzi wa Bajeti za Wizara tatu (ambazo kwa sasa zimekuwa nne) zinazosimamiwa na Kamati pamoja na maoni na ushauri wa Kamati ziliwasilishwa katika Mkutano wa Tatoo wa Bunge la Bajeti uliomalizika Mwezi Juni, 2021. Aidha, Kamati itaendelea kuyasisitiza baadhi ya maoni ambayo inaona bado hayajatekelezwa kikamilifu katika Taarifa hii.

## 2.4 Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za Utendaji wa Wizara na Taasisi

**Mheshimiwa Spika**, Katika vikao vya Kamati vilivyo fanyika mwezi Agosti 2021 na Oktoba 2021, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa za Utendaji wa Wizara na Taasisi zake kama ifuatavyo:-

### 2.4.1 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

**Mheshimiwa Spika**, kupitia Wizara hii, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili taarifa na utekelezaji wa Taasisi zifuatazo: -

#### a. Chuo cha Ufundi Arusha

**Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Ufundi Arusha kilianzishwa mwaka 1978 kwa madhumuni ya kutoa mafunzo ya ufundi sanifu katika ngazi ya Cheti ("Full Technician Certificate" - FTC) ili kupata wataalamu wenye sifa na ujuzi katika fani mbalimbali za ufundi. Mnamo mwaka 2007 Chuo kilipandishwa hadhi ya kiuendeshaji kupitia Gazeti la Serikali No. 78 la mwaka 2007 (The National Council for Technical Education (Arusha Technical College) Establishment Order GN. No. 78 of 30th March, 2007) na kufanyiwa marekebisho kupitia Gazeti la Serikali Na. 302 la mwaka 2015 (The National Council for Technical Education (The Grant of Autonomous Status to the Arusha Technical College) Order No. 302 of 24th July, 2015)).

**Mheshimiwa Spika**, Chuo kinatoa mafunzo ya ufundi stadi katika ngazi mbalimbali (level I, II na III) na elimu ya ufundi kwa ngazi za Astashahada, Stashahada na Shahada katika fani mbalimbali katika michepwo ya Sayansi, Teknolojia na Ufundi.

**Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Ufundi Arusha kinawajibika kuhakikisha kinatoa mchango wake katika kufanikisha malengo makuu ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP)

wa 2016/2017- 2020/2021 na ule wa 2021/22-2025/26. Katika kutekeleza hayo, Chuo kina majukumu makuu matatu ambayo ni Kutoa elimu na mafunzo ya Ufundi; Kufanya utafiti; na Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Jamii.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea Taarifa ya utendaji wa chuo hiki ambayo kwa ujumla inaridhisha. Hata hivyo, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Chuo hiki, changamoto zimekuwa kikwazo katika utekelezaji bora wa majukumu yake. Changamoto ambazo Kamati ilielezwa ni pamoja na: -

- i. Upungufu wa watumishi ikilinganishwa na ikama;
- ii. Upungufu wa madarasa na maabara kulingana na idadi ya wanafunzi. Kamati ilitaarifiwa kuwa Chuo kimeshawasilisha ombi la fedha za kumalizia jengo ambayo ni shilingi **2,107,488,976.00**;
- iii. Uhaba wa malazi kwa wanafunzi kwani kwa sasa Chuo kina idadi ya **wanafunzi 3,809** na mabweni ya Chuo kwa sasa yana uwezo wa kuchukua **wanafunzi 884** sawa na **asilimia 23.2 tu** (698 wa kiume na 186 wa kike).

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi wa Taarifa hiyo, Kamati imebaini masuala mbalimbali yafuatayo kuhusu Chuo hiki: -

- i. Kumekuwa na ongezeko la wanafunzi wa kike kutoka **389** mwaka 2015/2016 hadi **704** mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko la **asilimia 80.97** jambo ambalo ni jema na Kamati inapongeza sana;
- ii. Chuo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kimeshafanya tafiti katika maeneo mbalimbali ya sayansi, teknolojia na ubunifu ikiwa ni pamoja na kufanya utafiti, ubunifu na ukarabati wa vifaa tiba katika hospitali mbalimbali nchini na hivyo kupunguza gharama na mzigo kwa Serikali
- iii. Chuo hakitengewi bajeti ya kutosha ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo hususan za Ujenzi wa Mabweni jambo ambalo limekuwa kikwazo kwa watoto wa kike kujunga na Chuo lakini

pia katika utendaji wa Chuo. Suala hili limekuwa ni kilio cha Kamati kwa muda mrefu.

iv. Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela, Arusha (Nelson Mandela Arusha Institute of Science and Technology NM –AIST)

**Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Afrika ya Nelson Mandela ya Sayansi na Teknolojia ilianzishwa mwaka 2009 kama Taasisi yenye "Hadhi Maalum" (*unique status*) kwa ajili ya kujikita katika kuinua na kuleta matokeo bora ya Sayansi, Uhandisi, Teknolojia na Uvumbuzi katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Jangwa la Sahara. Katika Hati Idhini ya kuanzishwa kwake, Kifungu cha 3(3) kinasema kuwa:- "*The University shall have a unique status of catering for Eastern African region and modus operandi as well as conditions of services for its staff commensurate with that unique status*". Aidha, Kifungu cha 3(4) cha Hati Idhini ya Taasisi pia kinasema: "*The unique status shall enable the University to maintain comparability and staff mobility with sister institutions in the African Institutions of Science and Technology (AISTs) network, and thereby attract, motivate and retain its staff*".

**Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Nelson Mandela ina majukumu ya msingi matatu yafuatayo:-

- i. Ufundishaji na ujifunzaji katika ngazi ya umahiri na uzamivu;
- ii. Utafiti na ubunifu unaojibu matatizo ya jamii na viwanda (utakaondoa pengo katи ya jamii na viwanda); na
- iii. Utoaji wa utaalamu wa kuboresha huduma kwa umma na jamii kupitia wataalamu waelekezi.

**Mheshimiwa Spika**, katika Taarifa ya utendaji iliyowasilishwa mbele ya Kamati, Taasisi pamoja na mambo mengine ilionesha kuwa 'katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Taasisi imetekeleza majukumu mbalimbali kama vile:-

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

- i. Kuendelea kutoa mafunzo katika programu 28; ambapo 16 ni Shahada za Umahiri (Masters) na 12 ni za Uzamivu (PhD)
- ii. Kuendelea kufanya tafiti mbalimbali takribani 23 ikiwa ni pamoja na Mfumo unaoweza kukusanya na kuchambua takataka kulingana na tabia zake yaani "Waste Management System"; Mifumo ya utambuzi wa madhara ya matumizi mabaya ya dawa "Improving the Pharmacovigilance System using Natural Language Processing on Electronic Medical Records"; Ugunduzi wa mfumo wa TEHAMA unaoweza kumsaidia mfugaji wa kuku kugundua dalili za awali za ugonjwa wa "Occidiosis", "Salmonellosis" na Newcastle"; Utafiti wa namna ya kuboresha uzalishaji wa migomba inayostahimili ugonjwa wa mnyauko; Mfumo wa TEHAMA unaomsaidia mkulima kujua viuatilifu vyenye ubora/vilivyo sajiliwa. Mfumo huo unawasilliana na "data base" ya mamlaka ya Usajili na Udhibiti wa Viuatilifu Tanzania (TPRI); na Ubunifu wa Utengenezaji wa kirutubisho kiitwacho OmeOmega-3 DHA Super food kwa ukuaji wa ubongo na akili ya mtoto. OmeOmega-3 DHA Superfood ni chakula chenye lishe asilia yenye utajiri wa omega-3 DHA ambayo husaidia kuimarisha afya na ukuaji wa ubongo na akili ya mtoto.

**Mheshimiwa Spika**, licha ya kazi nzuri inayofanywa na Taasisi hii, Kamati ilielezwa Changamoto ambazo kwa kiasi kikubwa zimekuwa kikwazo katika utendaji bora wa Taasisi. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

- i. Ufinyu wa Bajeti unaoathiri uendeshaji wa shughuli za chuo ikiwemo kushindwa kulipa stahiki za walimu;
- ii. Miundombinu haba isiyokidhi mahitaji ya idadi ya wanafunzi waliopo kwani uwezo ni kuhudumia wanafunzi 500 ila waliopo ni 600 sawa na upungufu wa **asilimia 16.7**
- iii. Uhaba wa Rasilimali watu hususan wa kada ya Wanataaluma hasa ikizingatiwa wengine wanastaafu.

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wa Taarifa hii, Kamati imebaini mambo yafuatayo: -

- i. Taasisi haijaweza kutangaza kazi zake hususan za ubunifu na utafiti na hivyo jamii kotonufaika na tafiti hizo;
- ii. Taasisi haijaweza kubuni miradi mingi ambayo inaweza kusaidia kuwa chanzo cha mapato na hivyo kupunguza changamoto ya bajeti; na
- iii. Gharama/bei kubwa ya bidhaa/vifaa vinavyozalishwa ambavyo wananchi hawawezi kumudu.
- iv. Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea Taarifa kuhusu utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 kwa lengo la kuifahamu lakini pia kuona ni kwa kiasi gani Sera inaendana na mabadiliko ya sasa ya dunia hasa katika karne hii ya Sayansi na Teknolojia.

**Mheshimiwa Spika**, Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 iliandaliwa ikiwa ni matokeo ya kuhuishwa na hatimaye kufutwa kwa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995, Sera ya Elimu ya Ufundji na Mafunzo (1996), Sera ya Taifa ya Elimu ya Juu (1999) na Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa Elimu Msingi (2007). Sera iliandaliwa kwa lengo la kutoa mwelekeo wa elimu na mafunzo nchini kwa kuzingatia mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, kisayansi na kiteknolojia na changamoto za elimu na mafunzo kitaifa, kikanda na kimataifa, ili kuongeza fursa, ufanisi na ubora wa elimu na mafunzo nchini na kufikia viwango vya rasilimali watu kwa nchi yenye uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa malengo saba ambayo Sera inapanga kutekeleza kuwa ni:-

- i. Mfumo, miundo na taratibu nyumbufu kumwezesha Mtanzania kuijendeleza kwa njia mbalimbali katika mikondo ya kitaaluma na kitaalamu;

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

- ii. Elimu na mafunzo yenye viwango vya ubora unaotambulika kitaifa, kikanda na kimataifa;
- iii. Upatikanaji wa fursa mbalimbali za elimu na mafunzo nchini;
- iv. Ongezeko la rasilimali watu kulingana na vipaumbele vya Taifa;
- v. Usimamizi na uendeshaji madhubuti wa elimu na mafunzo nchini;
- vi. Mfumo endelevu wa ugharimiaji wa elimu na mafunzo nchini; na
- vii. Mfumo wa elimu na mafunzo unaozingatia masuala mtambuka

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa, tangu kutungwa kwa Sera hii kumekuwa na mafanikio mbalimbali kama vile kuongezeka kwa upatikanji wa vifaa, uboreshaji wa mitaala, sayansi, Teknolojia na ubunifu, kutolewa kwa elimu bure kwa shule za msingi na Sekondari, kuongezeka kwa wanafunzi na ufaulu pamoja na miundombinu ya elimu.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo, Kamati imebaini uwepo wa changamoto ambazo zimekuwa kikwazo katika utekelezaji mzuri wa Sera. Changamoto hizo ni pamoja na:-

- i. Uwezo wa kuhimili mabadiliko ya mahitaji ya kitaaluma na kitaalamu kulingana na mahitaji ya soko;
- ii. Miundombinu isiyokidhi mahitaji kutokana na ongezeko la wanafunzi;
- iii. Uhaba wa Walimu, Wakufunzi, Wahadhiri na Mafundi Sanifu wa Maabara za Shule kulingana na mahitaji katika ngazi zote za elimu na mafunzo nchini;

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

- iv. Uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia vinavyoendana na mabadiliko ya sasa ya sayansi na teknolojia katika ngazi zote za elimu na mafunzo;
- v. Uwekezaji mdogo katika Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi pamoja na Elimu ya Juu katika fani za sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati;

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona ni wakati muafaka sasa kwa Serikali kuanza kuzifanyia kazi changamoto hizi ili kuboresha Elimu yetu.

### i. Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST)

**Mheshimiwa Spika**, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) kilianzishwa mwaka 2012 kwa lengo la kutoa mafunzo katika ngazi za Shahada za Uhandisi na Teknolojia pamoja na Stashada za Ufundu katika fani mbalimbali. Aidha, kuanzia mwaka wa masomo 2019/20 Chuo kimefanikiwa kuanza kutoa mafunzo ya Shahada ya Uzamili na Uzamivu wa Uhandisi Ujenzi na TEHAMA.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa majukumu makuu matatu ya Chuo kama ifuatavo: -

- i. Kutoa mafunzo katika nyanja mbalimbali za Sayansi na Teknolojia kuanzia ngazi ya Astashahada hadi Shahada ya Uzamivu;
- ii. Kufanya tafiti zenyе kuchochea ukuaji wa matumizi ya Sayansi na Teknolojia; na
- iii. Kutoa ushauri elekezi kwa umma, mashirika binafsi na kwa mtu mmoja mmoja.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Chuo kimefanikiwa kutekeleza majukumu yake mbalimbali. Mafanikio ambayo Chuo imeyapata ni pamoja na:

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

- i. Kudahili wanafunzi **6,817**. Kati yao, wanafunzi wa kike ni 1,510 (22%) na wa kiume ni 5,307 (78%) sawa na ongezeko la **asilimia 20** ikilinganishwa na mwaka wa masomo 2019/20 ambapo wanafunzi **5,678** walidahiliwa.
- ii. Kuingia makubaliano na Taasisi 21 na Mashirika ya Kimataifa ili kusaidiana katika masuala ya kitaaluma ili kuweza kuboresha utoaji wa elimu bora;
- iii. Kuendelea kuhakikisha wanafunzi wote wanafanya mafunzo kwa vitendo katika mashirika na makampuni mbalimbali na hivyo kumfanya mwanafunzi kuelewa kwa kina kile anachojifunza kwa nadharia. Vilevile, Mafunzo hayo yamekuwa ni sehemu ya kuongeza umahiri na uzoefu wa kazi utakaowasaidia wanafunzi kuajiriwa au kujajiri;
- iv. Kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu kupitia wataalam wake kupitia kampuni yake ya MCB Company Limited na hususan ushauri elekezi kibiashara na kimejikita zaidi katika sekta ya ujenzi pamoja na usimamizi wa miradi ya mbalimbali ya Serikali na sekta binafsi. Vilevile, Chuo kinatoa huduma za ushauri elekezi zisizo za kibiashara kwa lengo la kusaidia jamii kutatua changamoto zake kupitia wataalam waliopo Chuoni. hata hivyo utoaji wa huduma ni sehemu ya chanzo cha mapato ya ndani. Katika kipindi cha Mwaka 2020/2021 Chuo kimesanifu na kusimamia miradi ya Ujenzi 39 yenye thamani ya jumla ya Shillingi Bilioni 6.46.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Chuo, Kamati imebaini chuo kina changamoto mbalimbali zifuatazo: -

- i. Upungufu wa Miundombinu ya kujifunzia na kufundishia ikiwemo madarasa, karakana na maabara
- ii. Upungufu wa mabweni;
- iii. Upungufu wa Watumishi;
- iv. Upungufu mkubwa wa vifaa vyta kufundishia na vilivyopitwa na wakati; na
- v. Idadi ndogo ya wanafunzi wa kike wanaojiunga na Chuo.

## **Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar Es Salaam (DUCE)**

**Mheshimiwa Spika**, Chuo Kishiriki cha Elimu Dar Es Salaam (DUCE) ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam (UDSM) na kimepitia mabadiliko mbalimbali kuanzia mwaka 1964 hadi mwaka 2005 kilipokuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu. Chuo kilianzishwa ikiwa ni jitahada za Serikali kutatua changamoto ya upungufu wa walimu na wataalam wa Sekta ya Elimu uliochochewa na ongezeko kubwa la udahili wa wanafunzi katika shule za msingi na Sekondari hasa wakati wa kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Msingi (MMEM) na Mpango wa Maendeleo ya Sekondari (MMES).

**Mheshimiwa Spika**, majukumu makuu matatu (3) ya DUCE ambayo ina vitivo vitatu na jumla ya Programu 10 ni kama ifuatavyo: -

i. Kufundisha Programu mbalimbali kama vile Elimu ya Jamii, Elimu ya Sayansi na Elimu. Aidha, Chuo kimefanikiwa kuanzisha kitengo cha elimu cha wenyewe mahitaji maalum na kuna kitengo cha Elimu maalaum (*Special Education Unit*) ikiwa ni pamoja na kuajiri Wataalam wa mahitaji maalum kama vile Wakalimani wa lugha za alama, wataalam wa kuandika na kusoma nukta nundu na fani nyinginezo;

ii. Kufanya tafiti na ubunifu katika maeneo mbalimbali ya Elimu ambapo msisitizo umewekwa kwenye tafiti zinazotatua changamoto za jamii na mchango katika maendeleo ya Taifa. Kwa mfano Chuo kimetengeza vipukusi (*sanitizers*) wakati wa ugonjwa wa UVIKO 19 na hivyo kupunguza gharama kwa Chuo kununua; na

iii. Kutoa ushauri wa Kitaalam na huduma kwa jamii katika maeneo ya ubobezi wao hususan katika sayansi, elimu, insia na sayansi za jamii ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo kazini kwa walimu kuhusu mbinu mpya na bora za ufundishaji na usimamizi wa shule.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafaniko hayo, Kamati imebaini Chuo kinakumbana na changamoto mbalimbali zikiwemo: -

- i. Ufinyu wa Eneo la Chuo kwani ukubwa wa eneo ni ekari 52.9 ambalo halitoshelezi mahitaji. Chuo kimeandaa mpango kabambe (Master Plan) utakaowezesha ujenzi uwa kwenda juu (Vertical Extension)
- ii. Utiegemezi wa fedha kutoka Serikali Kuu na iliahidiwa kuwa Chuo kitabuni vyanzo vipyta vyta mapato kwa kufanya tafiti mbalimbali ili kuweza kupata fedha za kutosha ili kupanua miundombinu yake.
- iii. Uhaba wa Watumishi hasa wahadhiri, madereva na wakaguzi wa ndani. Chuo kimejipanga kutumia wanafunzi tarajali (*Interns*) na wahadhiri wa muda wakati kikisubiri vibali vyta ajira.
- iv. Uhaba wa Malazi. Chuo kina uwezo wa kudahili wanafunzi 5560 lakini uwezo wa mabweni ni kuchukua wanafunzi 1018 sawa na **asilimia 18.3 tu** ya mahitaji.

### **2.4.2 Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili taarifa zifuatazo kutoka Wizara hii: -

#### **a. Baraza la Michezo la Taifa (BMT)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea Taarifa ya Baraza la Michezo la Taifa (BMT) pamoja na wadau wao kwa lengo la kufahamu kazi zao lakini pia mafanikio na changamoto wanazokumbana nazo pamoja na mipango ya kukabiliana na changamoto hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Baraza la Michezo la Taifa liliundwa kwa Sheria Na. 12 ya mwaka 1967 ambayo pamoja na mambo mengine inabainisha majukumu ya BMT. Majukumu hayo ni pamoja na:

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

- i. Kuendeleza, kustawisha na kudhibiti aina zote za michezo ya ridhaa na kulipwa kwa kushirikiana na Vyama/Mashirikisho ya Michezo;
- ii. Kuhimiza na kutoa fursa za ushirikiano mionganoni mwa Vyama veya Michezo;
- iii. Kuidhinisha mashindano na matamasha ya Kitaifa na Kimataifa yanayoandaliwa na Mashirikisho/Vyama veya Michezo;
- iv. Kuandaa baada ya kushauriana na Vyama veya Michezo vinavyohusika na mashindano ya Kitaifa na Kimataifa ili kubadilishana uzoefu na kukuza mahusiano ya kirafiki na Mataifa mengine;
- v. Kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuwezesha kuwepo kwa fursa za michezo kwa ngazi zote na kujitahidi kujenga moyo wa uanamichezo na nidhamu ya hali ya juu kwa Wanamichezo; na
- vi. Kusajili Vyama, Vilabu na Mashirikisho ya Michezo.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa fedha 2020/2021, Baraza limetekeleza majukumu mbalimbali iliyojiwekea. Majukumu hayo ni pamoja na: -

- i. Kufanya Maboresho ya Kanuni za BMT na Kanuni za Msajili ili kuleta ufanisi katika utendaji kazi na kupanua wigo wa ukusanyaji wa mapato;
- ii. Kuhakikisha Vyama na Mashirikisho ya Michezo yanaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya Utawala Bora kwa kufanya mapitio ya Katiba za Vyama na Mashirikisho ya Michezo;
- iii. Kusajili Vyama 15 na Vilabu veya Michezo 150;

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

- iv. Kuidhinisha/Kutoa Vibali vya Kufanya Shughuli za Michezo kwa Vyama/Vilabu vya Michezo ili kuwezesha uratibu, ufuatilaji na tathmini;
- v. Kutoa Ushauri wa Kitaalamu na Kiutawala kwa Vyama/Vilabu vya Michezo katika kutekeleza majukumu yao;
- vi. Kuratibu Michezo ya UMISSETA na UMITASHUMTA Kwa kushirikiana na Wizara ya elimu na Wizara ya Ofisi ya Rais TAMISEMI na
- vii. Kuratibu Ushiriki wa Timu za Taifa katika Mashindano Mbalimbali ya Kimataifa kwa Kushirikiana na Vyama na Mashirikisho ya Michezo

**Mhesimiwa Spika**, Kamati ilibaini changamoto ambazo zimekuwa zilkilikumba Baraza. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo: -

- i. Uhaba wa Rasilimali Fedha za Kusaidia Timu za Taifa
- ii. Miundombinu isiyokidhi matakwa ya kikanuni hasa viwanja vya michezo
- iii. Vilabu na vyama vya mikoa kutekeleza kanuni za leseni, katiba n.k
- iv. Kutokuzingatia misingi ya Utawala bora na uongozi.

**Mhesimiwa Spika**, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini masuala yafuatayo: -

- i. Mawasiliano hafifu baina ya BMT na Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya;
- ii. BMT na wadau wake kama TFF hawajatumia fursa mbalimbali zilizopo kuzisaidia klabu ambazo hazina uwezo kupata wadhamini na ili kuweza kushiriki vyema katika mechili mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa;

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

- iii. Usimamizi mbovu wa masharti ya mkataba
- iv. Kamati za Michezo za Mikoa hajijawezeshwa vya kutosha (kutengewa bajeti ya kutosha) ili kuweza kuratibu vyema michezo katika ngazi hizo na za chini zaidi; na
- v. Wizara haijaweza kutumia ipasavyo wanamichezo wake waliochanja chanjo ya UVIKO - 19 ili kuhamasisha jamii umuhimu wa kupata chanjo ya UVIKO - 19.

### **b. Sera ya Maendeleo ya Michezo ya Mwaka 1995**

**Mheshimiwa Spika**, Sera ya Maendeleo ya Michezo ilitungwa mnamo Mwaka 1995 ikiwa ni hatua ya kuhakikisha kunakuwepo na Mwongozo madhubuti wa kusimamia na kuendeleza michezo nchini. Sera ilitungwa kwa malengo yafuatayo: -

- i. Kuhamasisha umma kushiriki katika michezo na mazoezi ya viungo;
- ii. Kuhakikisha kunakuwepo upatikanaji wa viwanja vya michezo na zana bora na za kutosha kwa ajili ya kuimarisha maendeleo ya michezo;
- iii. Kuandaa na kutayarisha wataalamu wa kutosha katika fani na taaluma mbalimbali za michezo;
- iv. Kuhakikisha timu na wachezaji wetu wanafanya vizuri katika mashindano na michezo ya Kitaifa na kimataifa;
- v. Kufanya utafiti katika michezo ya jadi kwa lengo la kuifufua na kuiendeleza; na
- vi. Ushirikiano na mataifa mengine katika utoaji wa elimu ya michezo na ushiriki michezo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa kwa kipindi cha miaka 26 tangu kutungwa kwa Sera hii kumekuwa na baadhi ya mafanikio mbalimbali, katika utekelezaji wake. Baadhi ya

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

mafanikio hayo ni pamoja na: - kuimarika kwa ushiriki wa wananchi katika michezo, kuongezeka kwa wataalam na miundombinu ya michezo inayomilikiwa na wadau mbalimbali pamoja na Timu za Taifa na wachezaji kufanya vizuri katika michezo na mashindano mbalimbali kimataifa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa changamoto, Kamati ilielezwa changamoto zilizopo katika kufikia malengo ya Sera kuwa ni pamoja na: -

- i. Upungufu wa rasilimali fedha za kugharamia maendeleo ya michezo; Uhaba wa wataalamu wa michezo katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo;
- ii. Upungufu kwa miundombinu na vifaa vyta michezo vinavyokidhi mahitaji kwa makundi mbalimbali katika jamii; na
- iii. Ushiriki mdogo wa wadau katika kutekeleza majukumu waliyokasimiwa na Sera ikiwemo shughuli za michezo kutopewa kipaumbele stahiki katika Taasisi za Elimu.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini yafuatayo: -

- i. Utekelezaji wa sera una changamoto kutokana na ukosefu wa fedha unaosababisha uhaba wa zana za michezo ambazo ni nyenzo muhimu katika kuhamamisha michezo nchini;
- ii. Serikalli haijawekeza vyta kutosha katika kuzalisha walimu na wataalam wa michezo kwani hawana hata Muundo wa utumishi (*scheme of service*);
- iii. Tozo za vilabu zipo juu na hivyo kufanya vilabu vidogo kushindwa kuingia kwenye ligi;
- iv. Viwanja vyta michezo vilivyopo havikidhi mahitaji;
- v. Michezo ya jadi imesahaulika hivyo ipo haja ya kuchagua mikoa ya kimkakati kwa ajili ya utekelezaji wake;

vi. Mlolongo wa usajili wa Timu unafanya baadhi kushindwa kusajiliwa hivyo kuna haja ya kuboresha na kurahisisha utaratibu wa usajili; na

vii. Uvamizi wa viwanja vya michezo umeendelea kushamiri hivyo kuna haja ya Serikali kuweka mkakati madhubuti wa kukabiliana nalo.

### c. Bodi ya Filamu

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea Taarifa ya utendaji wa Bodi ya Filamu ambayo ilieleza masuala mbalimbali kama Dhima, Dira, Majukumu, Muundo na Hali ya Watumishi katika Bodi hiyo. Aidha, Kamati ilielezwa kuhusu namna Bodi ilivyotekeleza majukumu yake katika mwaka wa fedha 2020/2021, mafanikio waliyoyapata pamoja na changamoto walizonazo.

**Mheshimiwa Spika**, majukumu ya Bodi ya Filamu Tanzania yamebainishwa kwenye Sheria ya Filamu na Michezo ya kuigiza Na.4 ya Mwaka 1976 ambayo ni pamoja na: -

- i. Kusimamia maendeleo ya Tasnia ya Filamu;
- ii. Kusimamia na kuratibu utayarishaji wa filamu na michezo ya kuigiza;
- iii. Kuhakiki na kupanga katika madaraja filamu/picha jongevu kabla ya kuzipeleka sokoni;
- iv. Kusimamia urasimishaji wa sekta ya filamu (Utoaji wa leseni za uendeshaji wa shughuli za Filamu, vitambulisho vya wadau pamoja na kufanya ufuatiliaji wa uzingatiaji wa Sheria); na
- v. Kuandaa, kuratibu na kuendesha warsha, vikao, mijadala na mafunzo ya kujenga weledi kwa wadau wa filamu, utoaji wa tuzo na uendeshaji wa matamasha.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa katika kipindi cha Mwaka 2020/2021, katika utekelezaji wa majukumu haya, Wizara imepata mafanikio mbalimbali yafuatayo:

- i. Kuhamasisha wadau kuanzisha miundombinu ya usambazaji kupitia vituo vya Televisheni katika visimbusi vyenye channeli zinazoonesha filamu za Kitanzania
- ii. Kuhusu ajira, kwa mujibu wa takwimu za Bodi ya Filamu zinaonesha kuwa, filamu moja ndefu ya kitanzania huajiri wastani wa watu 20 na tamthilia wastani wa watu 100. Hivyo kutokana na idadi ya filamu ndefu 1,048 na tamthilia 30 zilizozalishwa katika kipindi cha kati ya Januari hadi Desemba, 2020 pekee, inakadiriwa kuwa sekta ya filamu ilichangia kiasi cha ajira 25,000; na
- iii. Katika kutetea haki za wasanii, Kamati illyoundwa na Bodi ya Filamu imehakikisha inashughulikia malalamiko yakiwemo 44 na tayari 27 yamesuluhihwa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo, Kamati ilielezwa changamoto ambazo Bodi inakumbana nazo kama ifuatavyo: -

- i. Uwekezaji mdogo wa kifedha kutoka Serikalini katika eneo la filamu, jambo linalosababisha Taasisi kushindwa kutekeleza miradi ya kimkakati kama vile uandaaji wa filamu za kizalendo, mafunzo pamoja na uratibu wa shughuli kama vile matamasha na tuzo za filamu.
- ii. Filamu nyingi kukosa ubora unaokidhi viwango vya ushindani katika soko la ndani (Kitaifa) na nje (Kimataifa) kutokana na uhaba wa mitaji katika kuwezesha utayarishaji wa kazi hizo;
- iii. Uwekezaji mdogo katika tasnia ya filamu ikiwemo miundombinu na vifaa vya utayarishaji wa filamu bora;
- iv. Weledi mdogo mionganoni mwa wadau wa filamu jambo ambalo husababisha biashara ya filamu kuendeshwa katika mtazamo wa kipaji badala ya ubobevu na taaluma; na

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

v. Uharamia wa kazi za filamu "Film Piracy" ambao pia husababisha ukosefu wa masoko kwa mazao ya filamu yanayozalishwa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini masuala yafuatayo: -

i. Kumeibuka wimbi la baadhi ya wasanii kuchafua wenzao hivyo kuna haja ya Wizara kuchukua hatua kwa kuhakikisha maadili ya wasanii yanazingatia hadhi ya Tasnia hii;

ii. Ushirikiano mdogo unaotolewa wa waandaji wa filamu na wasanii wanaopeleka muziki nje ya nchi

iii. Uharamia wa kazi za wasanii bado unaendelea hivyo ipo haja ya kuweka mikakati ya kudhibiti ili wasanii hao waweze kunufaika na jasho lao;

iv. *Script* za filamu zetu baadhi hazipo katika lugha fasaha na hivyo kushindwa kuvuta soko la ndani na nje; na

v. Uandaaji wa baadhi ya filamu zetu hauna uhalisia na hivyo kushindwa kuvutia watazamaji.

vi. Kutokuwa na ubora tafsiri za cinema zetu za maandishi na za maneno

### d. Baraza la Kiswahili la Taifa

**Mheshimiwa Spika**, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) limeundwa kwa Sheria ya Bunge Na. 27 ya mwaka 1967 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 1983 na 2016. Majukumu ya Baraza kwa mujibu wa Sheria ni kama ifuatavyo:-

i. Kusimamia na kuhimiza matumizi fasaha na sanifu ya Kiswahili;

ii. Kukuza na Kusambaza misamiati na istilahi za Kiswahili;

**NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

- iii. Kutoa na kuimarisha huduma za Kiswahili za tafsiri, ukalimani na ithibati;
- iv. Kuandaa mazingira wezeshi kwa ajili ya kubidhaisha Kiswahili;
- v. Kushiriki katika Maendeleo ya Kiswahili Afrika na Duniani;
- vi. Kuingiza TEHAMA katika kusaidia maendeleo ya Kiswahili;
- vii. Kuimarisha uwezo wa rasilimali watu na uboreshaji wa mazingira ya kazi; na
- viii. Ujenzi wa mfumo endelevu wa mapato.

**Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa majukumu yake kwa Mwaka 2020/2021, BAKITA imefanikiwa kufanya yafuatayo: -

- i. Kutoa Semina ya Matumizi ya Kiswahili kwa waandishi na watangazaji wa redio na Televisheni;
- ii. Kutoa Elimu ya Matumizi ya Lugha kwa Umma Kupitia Vipindi vya Redio na Televisheni na Uandishi wa Makala;
- iii. Kuandaliwa kwa Mfumo wa Kusajili na Kutunza Kanzidata ya Wataalamu wa Kiswahili ambapo hadi kufikia Juni, 2021 jumla ya Wataalamu 1,320 wa Kiswahili walikuwa wamejisajili katika kanzidata ya Kiswahili;
- iv. Kununua Vifaa vya Mafunzo vya kisasa kwa Wakalimani vyenye thamani ya Milioni 187.5
- v. Baraza limefungua Kituo cha Kufundisha Kiswahili kwa Wageni pamoja na kuendesha mtihani wa kupima ujuzi wa kiwango cha lugha kwa wageni na wote wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya kigeni.
- vi. Wizara kupitia Baraza imeandaa Mkakati wa Taifa wa Kubidhaisha Kiswahili kwa Mwaka (2021-2031) ambao utekelezaji wake utagharimu takribani Shilingi Bilioni 15.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa changamoto ambazo BAKITA inakumbana nazo, Kamati ilielezwa changamoto Kuu mbili ambazo ni ufinyu wa Rasilimali Fedha Katika Kubidhaisha Kiswahil na Uhaba wa Watumishi

**Mheshimiwa Spika**, katika kuititia, kuchambua na kujadili Taarifa hii ya BAKITA, Kamati imebaini masuala yafuatayo:

- i. Bado jitihada zinatakiwa kwa Wizara kutengeneza Kiswahili kuwa bidhaa kwa kukifungamanisha na sekte nyingine kama Utalii,
- ii. Idadi ya wanafunzi wanaosoma Kiswahili katika ngazi ya vyuo bado ni ndogo hivyo Wizara inashauriwa iweke mkakati wa kuhamasisha vijana wa kitanzania wajifunze Kiswahili kama sehemu ya mikakati ya kukibidhaisha Kiswahili.
- iii. Wizara haijachagua maeneo ya kimkakati kuweza kikitambulisha kiswahili sanifu cha Tanzania kuwa maarufu kwani zipo nchi nyingine wanaotumia Kiswahili, hivyo ni bora kutengeneza ushindani baina ya nchi hizo na Tanzania kutengeneza Kiswahili sanifu, kukipiga chapa (Brand) kwa lengo la kukipa umaarufu na kutambulika duniani pote.
- iv. Kutokuwa na mkakati wa kutumia balozi zetu kuanzisha vituo vya kutoa mafunzo ya lugha ya Kiswahili.
- v. Idadi ya Wakalimani waliopo nchini bado ni ndogo ipo haja ya kutoa mafunzo ya kutosha ya ukalimani ili kupata idadi ya wakalimani wakutosha kwa lengo la kuokoa gharama zitokanazo na ukalimani;

#### **2.4.3 Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Wizara hii, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili taarifa zifuatazo: -

**a. Hatua iliyofikiwa katika maandalizi ya Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa kuhusu hatua iliyofikiwa katika maandalizi ya Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote. Taarifa hiyo ilieleza masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na namna na Wizara ilivyoanza kufanya maandalizi ya kutunga Sheria ya Bima ya Afya kwa wote tangu mwaka 2012. Kamati ilielezwa kuwa katika hatua za awali, tafiti mbalimbali zilifanyika katika maeneo mbalimbali ya ugharamiaji wa huduma za afya na kufuatiwa na maandalizi ya mkakati wa ugharamiaji wa huduma za afya wa mwaka 2016. Mkakati huo ulilenga kuhakikisha kuwa kila mwananchi anatumia bima ya afya katika kupatiwa huduma za afya/matibabu. Baada ya kuwasilisha Mkakati huo katika ngazi za maamuzi mwaka 2016, ilibainika kuwepo kwa uhitaji wa kutungwa kwa Sheria itakayotumika kutekeleza mkakati wa ugharamiaji na hivyo Wizara ilishauriwa kuandaa Waraka mahususi wenye lengo la kutunga Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote.

**Mheshimiwa Spika**, ilielezwa kuwa taratibu mbalimbali zimekuwa zikifuatwa katika kuhakikisha Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote inatungwa kwa kuzingatia maelekezo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 yanayolenga **kufikia bima ya afya kwa wote kwa kuimarisha Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF)**. Pamoja na Wizara kuchukua mwelekeo huo, mchakato wa maandalizi ya Muswada wa kutunga Sheria ya Bima ya Afya kwa wote umechukwa muda mrefu kutokana na suala la ugharamiaji wa bima ya afya kwa watu wasio na uwezo (**asilimia 26.4**) ambalo lilihitaji kupata ufumbuzi ndani ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa, suala hilo tayari limepata ufumbuzi ambapo Serikali imejipanga kuwa inatenga fedha kuititia bajeti ya kila mwaka ili kugharamia kadi za bima ya afya za watu wasio na uwezo kulingana na orodha ya kaya zenye mahitaji hayo. Aidha, kwa sasa Wizara inategemea kuwasilisha kwa mara ya mwisho waraka katika

ngazi ya *Inter Ministerial Technical Committee (IMTC)* na baadae kufikishwa katika Baraza la Mawaziri ili Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote uanze kuandaliwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea Taarifa hiyo na kuelekeza masuala yafuatayo: -

- i. Sheria itakayotungwa ihakikishe kunakuwepo na uboreshaji upatikanaji wa huduma kama dawa, vipimo ili kuepuka usumbufo ambao wananchi wamekuwa wakipata hasa walio katika mfuko wa CHF;
- ii. Ili kuhakikisha huduma zinaboreshw, changamoto ya uhaba wa watumishi katika Sekta ya Afya lazima ipatiwe ufumbuzi;
- iii. Sheria iwe wazi kuhusu masuala ya Udhhibit na usimamizi. Ianzishwe Mamlaka ya udhibiti (regulatory authority) ya Bima ya Afya badala ya kutumia TIRA;
- iv. Serikali ihakikishe kunakuwa na *ring fenced budget* ya Mfuko wa Bima ya Afya hasa ikizingatiwa kuwa kuna wengi hawana uwezo ili kuepuka mfuko kufilisika;
- v. Wizara iendelee kuelimisha na kuhamasisha jamii umuhimu wa kuendelea kupata chanjo ya ugonjwa wa Korona
- vi. Wizara iruhusu Madaktari bingwa kutumia usoefu wao kutoa dawa wanazoona zinafaa kwa wagonjwa bila ya kuwapangia; na
- vii. Ili kuboresha utoaji wa huduma za afya, Sheria itakapokuja, Sekta binafsi ziruhusiwe na kuwepo na ubunifu utakaowezesha wananchi kuchagua vifurushi wanavyoona vinafaa.

**viii. Bohari Kuu ya Dawa nchini (MSD)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea Taarifa hiyo ya MSD ambayo ilieleza masuala mbalimbali kama Hali ya fedha, Rasilimali watu na Upatikanaji wa dawa nchini.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa hali ya upatikanaji wa dawa imeimarika kwa sasa ikilinganishwa na hapo awali kutokana na fedha za dawa zimeanza kuwa *ring fenced* na zinatoka kila mwezi. Utaratibu huu umewezesha uwepo wa uhakika wa upatikanaji wa dawa wakati wote.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa changamoto, Kamati ilielezwa changamoto zifuatazo ambazo MSD inakumbana nazo kuwa ni pamoja na: - Ukosefu wa viwanda vya ndani vya kutengeneza dawa na hivyo kuongeza gharama za manunuzi ya bidhaa nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini yafuatayo: -

- i. Taarifa ya ukosefu wa dawa (out of Stock) zimekuwa zikichelewa kutolewa katika vituo vya afya Jambo linalosababisha vituo vya afya kutopata dawa kwa wakati. Ipo haja ya Taarifa hizi kutolewa mapema kwa vituo vya afya ili waone namna ya upatikanaji wa dawa hizo;
- ii. Ipo haja ya kufanya marekebisho ya Sheria iliyounda MSD ili kuruhusu kufanya kazi ya uzalishaji wa dawa;
- iii. Mifumo ya utendaji wa MSD ni mizuri sana ipo haja ya kuiweka mifumo hii rasmi na kisheria ili kuwezesha maboresho yanayoendelea kufanyika kutekelezwa wakati wote hata wakati Mkurugenzi anayefanya haya maboresho asipokuwepo kazini

### **iv. Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA)**

**Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ni Wakala wa Serikali wenyewe jukumu la kulinda afya ya jamii kwa kuhakiki ubora, usalama na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi. TMDA imeundwa kwa mujibu wa Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura 219 na inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakala za Serikali, Sura 245 na marekebisho yake ya mwaka 2009.

**Mheshimiwa Spika**, majukumu ya TMDA yameainishwa katika Kifungu Na. 5 cha Sheria ya Dawa na Vifaa tiba, Sura 219 ambayo ni pamoja na:-

- i. Kudhibiti utengenezaji, uingizaji, usambazaji na uuzaaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi;
- ii. Kukagua viwanda vya utengenezaji na maeneo ya kuhifadhi, kusambaza na kuuzia bidhaa zinazodhibitiwa na Mamlaka ili kuhahikisha vigezo vilivyowekwa vinafikiwa;
- iii. Kutathmini na kusajili bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi ili kuhakikisha zinakidhi vigezo vinavyotakiwa kabla ya kuruhusiwa kwenye soko la Tanzania;
- iv. Kutoa vibali vya kuendesha biashara za bidhaa zinazodhibitiwa na Mamlaka;
- v. Kufanya uchunguzi wa kimaabara ili kuhakiki usalama na ubora wa bidhaa zinazodhibitiwa;
- vi. Kufuatilia katika soko bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi, kukusanya taarifa na kutathmini madhara yatokanayo na matumizi na kuchukua hatua stahiki;
- vii. Kuhamasisha matumizi sahihi ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi; na
- viii. Kuelimisha na kutoa taarifa sahihi kwa wadau na wananchi kwa ujumla juu ya bidhaa zinazothibitiwa na Mamlaka.

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/2021, TMDA iliendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Mpango kazi na Bajeti ya yake ya mwaka 2020/2021. Kazi na mafanikio ambayo TMDA imeyapata ni kama ifuatavyo: -

- i. Kukusanya Shilingi Bilioni 31.3 sawa na asilimia 101 ya lengo la kukusanya Shilingi Bilioni 31.1 kwa mwaka 2020/21;

**NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

- ii. Kupata cheti cha umahiri cha kiwango cha ISO 9001: 2015 katika mifumo ya utendaji ya udhibiti wa bidhaa na kuendelea kushikilia cheti hicho mwaka hadi mwaka;
- iii. Kudumisha umahiri wa mifumo ya udhibiti wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi inayotambuliwa na WHO iitwayo Maturity Level – 3 (ML -3)
- iv. Maabara ya uchunguzi wa dawa kupata hadhi ya kutambuliwa na Shirika la Afya Duniani (WHO)
- v. Kuweka mfumo mahiri wa TEHAMA wa kupokea na kuchakata maombi ya usajili wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi (Regulatory Information Management System – RIMS) ambapo kwa sasa wateja wanawasilisha maombi kwa njia ya mtandao (online) na kupata vyeti vya usajili vinavyotolewa kielektroniki;
- vi. Kuchakata maombi ya vibali vya kuingiza nchini na kusafirisha nje ya nchi bidhaa (Import and Export permits) ndani ya saa 24; na
- vii. Kukamata na kuteketeza tani 62.44 za dawa, vifaa tiba na vipukusi duni na bidhaa bandia zinazokadiriwa kuwa na thamani ya TZS 749,975,535.00.

**Mhesimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati kuhusu TMDA umebaini yafuatayo: -

- i. Kuna changamoto katika uteketezaji wa dawa zilizokwisha muda wake hivyo TMDA isimamie ipasavyo zoezi hilo ili kuepuka gharama za kuteketeza, TMDA ifanye ukaguzi wa bidhaa viwandani na mipakani kabla bidhaa hizo hazijaingizwa sokoni;
- ii. TMDA na kazi zake bado hazijulikani ipasavyo kwa wananchi ipo haja ya kutoa elimu kwa Umma;
- iii. Bado vifaa tiba kama x-ray vinavyonunuliwa nchini vina teknolojia ambayo wataalamu wetu wengi hawawezi

kuvitengeneza vinapoharibika hivyo ipo haja ya kununua kwa kuzingatia teknolojia rahisi;

iv. Watumishi wengi wanakaimu nafasi na hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi na kwa kujiamini; na

v. Jamii haina elimu ya kutosha ya matumizi ya dawa na uhifadhi wake ipo haja ya kutoa elimu.

#### **vi. Makazi ya Wazee Nchini**

**Mheshimiwa Spika**, Historia ya Makazi ya Wazee na Wasiojiweza ambayo ilianzishwa katika nyakati tofauti kuanzia miaka ya 1930 na baada ya uhuru. Madhumuni ya kuanzishwa kwa makazi haya yalikuwa ni kutoa huduma kwa waathirika wa ugonjwa wa ukoma ambaao walikuwa wakitengwa na jamii zao. Baada ya uhuru Makazi haya yalitumika kuwahudumia wazee na wasiojiweza ambaao hawakuwa na ndugu au jamaa wa kuwatunza ikijumuisha wazee waliokuwa vibarua katika mashamba ya mkonge, kahawa na miwa yaliyokuwa yakimilikiwa na walowezi, pamoja na wafungwa wa vifungo vya muda mrefu baada ya kumaliza kutumikia vifungo vyao.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, Tanzania ilikadiriwa kuwa na Wazee 2,507,568. Kati ya hao wanawake ni 1,307,358 na wanaume 1,200,210 ambaao ni sawa na asilimia 5.6 ya wananchi wote. Vilevile, Taarifa ya Taifa ya Makadirio ya Watu ya kwa mwaka 2013-2035 (National Population Projection Report – 2013 - 2035) kwa mwaka 2020/2021 inaonesha kuwa Tanzania inakadiriwa kuwa na wazee 2,524,559 (wanawake 1,318,940 na wanaume 1,205,619).

**Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendesha na kusimamia jumla ya makazi 15 katika Mikoa mbalimbali nchini. Aidha, yapo pia Makazi ya Wazee 20 yanayomilikiwa na Taasisi Binafsi na Mashirika ya Dini yenye jumla ya wahudumiwa 537 (wanawake 242 na wanaume 295) hadi kufikia Juni, 2021.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Makazi hayo ni pamoja na Msimbazi (Dar es Salaam), Missionery of Charity (Dar es Salaam), Mji wa Huruma (Mara), Nazareth (Morogoro), Kisosora (Tanga), Joy and Love - Missionary of Charity Hombolo (Dodoma), Iduguta Nzega (Tabora), Busanda (Shinyanga), Igabiro (Kagera), Kindwiti (Pwani), Rasbura (Lindi).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa Changamoto kuu katika makazi ya wazee ni kuendelea kuwepo kwa miundombinu chakavu katika baadhi ya Makazi ya Wazee.

**Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa;**

- i. Hali ya Makazi ya Wazee siyo ya kuridhisha hivyo Wizara iwe na wakaguzi hasa hasa katika vituo binafsi ili kuhakikisha viwango na vigezo vya kuanzishwa kwake vinazingatiwa na hivyo kuondoa adha hii kwa Wazee;
- ii. Jamii hajatambua umuhimu na jukumu la kulea wazee kuwa ni lao na hivyo kuendelea kuwaacha wazee hawa kuishi katika Makazi ya Wazee
- iii. Usajili wa Makazi ya Wazee haupo katika mgawanyo ulio sawa kwani baadhi ya mikoa inayo makazi mengi wakati mingine haina.

### **SEHEMU YA TATU**

---

#### **3.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo ya kina kuhusu shughuli zilizotekelizwa na Kamati pamoja uchambuzi wake naomba kuwasilisha Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kama ifuatayo: -

##### **3.1 Maoni ya Jumla**

###### **a. Miundombinu ya Sekta ya Elimu na Afya**

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na kilio cha muda mrefu cha uhaba wa miundombinu ya Elimu na Afya;

**NA KWA KUWA**, Mhe. Rais Mama Samia Suluhu Hassan kupitia fedha mkopo wa kupambana na UVIKO 19 amejenga madarasa na vituo vya Afya nchi nzima;

**KWA HIYO BASI** Bunge inatoa pongezi kwa Mhe. Rais Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuelekeza fedha hizo katika ujenzi wa miundombinu ya Elimu na Afya Nchini.

**i. Uhaba wa Watumishi**

**Mheshimiwa Spika**, changamoto ya Watumishi katika Sekta ya Afya, Elimu, Maendeleo ya Jamii na Utamaduni, sanaa na Michezo bado ni kubwa;

**NA KWA KUWA** upungufu wa Watumishi hawa umekuwa ukileta athari katika utoaji wa huduma mbalimbali nchini;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaitaka Serikali kutoa kipaumbele cha ajira kwa Sekta hizi muhimu hususan Sekta ya Afya na elimu.

**ii. Bajeti**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizi unategemea utengwaji wa bajeti ya kutosha lakini pia utolewaji wa fedha hizo

**NA KWA KUWA**, bajeti finyu na utolewaji usiroridhisha umekuwa ukiathiri utekelezaji bora wa majukumu ikiwemo utoaji wa huduma kwa wananchi

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaitaka Serikali kuzingalia Sekta hizi kwa jicho la pekee kwa kuzitengea fedha za kutosha lakini pia kuhakikisha bajeti hizo zilizoidhinishwa na Bunge zinatolewa zote na kwa wakati ili kuleta ustawi bora wa huduma kwa wananchi.

**3.2 Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto**

**a. Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** upatikanaji wa huduma za afya kwa wote ni haki ya msingi ya kila mwanadamu lakini

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

pia ni utekelezaji wa lengo Namba 3 la Malengo ya Maendeleo Endelevu;

**NA KWA KUWA** mpaka sasa ni asilimia 26 tu ya Watanzania ndiyo wamefikiwa na Huduma ya Bima ya Afya nchini;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaitaka Serikali kuhakikisha kuwa inaleta Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote mapema iwezekanavyo.

### **iii. Watoto Njiti,**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** watoto njiti wamekuwa wakipata changamoto mbalimbali za kiafya zinazowafanya washindwe kuishi kama watoto wengine;

**NA KWA KUWA**, ukosefu wa huduma bora hupelekea watoto hao kupoteza maisha;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linashauri hoja zifuatazo,

i. Serikali ije na mkakati wa kuwalinda na kuhakikisha watoto hawa wanapata Bima ya afya mapema baada ya kuzaliwa ili kuwapunguzia gharama za matibabu wazazi wanaopata watoto njiti.

ii. Wizara ifanye mapitio ya likizo ya uzazi kwa wanaojifungua watoto njiti na kuwaongezea likizo ya uzazi.

### **iv. Bohari Kuu ya Dawa (MSD)**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Bohari Kuu ya Dawa imekuwa ikifanya kazi kubwa ya kuhakikisha kunakuwepo ufanisi katika upatikanaji wa dawa na vifaa tiba nchini nchini;

**NA KWA KUWA** tayari Bohari imeanza uzalishaji wa dawa nchini jambo ambalo linapunguza gharama ya ununuzi wa dawa kutoka nje ya nchi;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linashauri Serikali kuongeza Bajeti ya MSD ili iweze kuzalisha na kununua dawa na vifaa tiba vya

kutosha na hivyo kuondoa changamoto ya ukosefu wa dawa nchini;

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** kumekuwa hakuna ulinganifu wa usambazaji, usimamizi na matumizi ya dawa katika ngazi zote za huduma za afya (kuanzia mikoani hadi zahanati)

**NA KWA KUWA** Kutokuwa na ulinganifu huo kunapelekea uhaba wa dawa katika baadhi ya hospitali wakati hospitali nyingine zikiwa na dawa nyingi tofauti na uhitaji.

**KWA HIYO BASI** Bunge linashauri kuwe na mfumo madhubuti wa kusimamia usambazaji na matumizi ya dawa hizo kulingana na mahitaji ya mkoa

**v. Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA)**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA TMDA** imekuwa ikifanya ukaguzi katika maduka na kubaini dawa zilizokwisha muda wake, zilizoingizwa kinyume na utaratibu na zinazopaswa kuteketezwa;

**NA KWA KUWA** zoezi la uteketezaji limekuwa likiigharimu Serikali fedha nyingi

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaitaka TMDA

i. kufanya ukaguzi wa bidhaa viwandani na mipakani ili kudhibiti uingiaji wa dawa kinyume na taratibu

ii. TMDA kusimamia sheria, taratibu, kanuni na miongozo kuhusu udhibiti, usambazaji na uuzaaji wa dawa nchini

**vi. Makazi ya Wazee**

**Mheshimiwa Spika KWA KUWA** hali ya Makazi mengi ya Wazee nchini siyo ya kuridhisha;

**NA KWA KUWA** hali hiyo mbaya ya baadhi ya makazi ya wazee imekuwa adha kubwa kwa wazee wetu kutokana na

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

ukosefu wa huduma muhimu za kijamii hasa kwa maeneo ya pembezoni;

### **KWA HIYO BASI**, Bunge linaitaka Serikali

- i. Kuwa na wakaguzi wa Vituo vya Wazee ili kuhakikisha viwango na vigezo vya kuanzishwa kwake vinazingatiwa na hivyo kuondoa adha kwa Wazee; na
- ii. Serikali/Wizara iweke vigezo vitakavyosaidia usajili wa Makazi ya Wazee kuwa katika mgawanyo ulio sawa kwa mikoa yote nchini.

### **3.3 Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia kazi iliyofanywa na Kamati kuptitia Wizara na changamoto ambazo Kamati illizibaini, Kamati inatoa hoja zifuatazo: -

#### **a. Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA)**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Mkakati wa Serikali ni kubidhaisha Kiswahili ili kiweze kujulikana lakini kuleta faida za kiuchumi nchini;

**NA KWA KUWA**, ili kuweza kubidhaisha Kiswahili mikakati mbalimbali inapaswa kuwepo;

### **KWA HIYO BASI**, Bunge linaitaka Serikali

- i. Kutafuta bidhaa itakayouzika sambamba na Kiswahili mfano Utalii, hii itasaidia bidhaa hizi kuuzika ipasavyo;
- ii. Iweke mkakati maaalum wa Kitaifa wa kuwafikia wanafunzi katika kutoa mafunzo ya Kiswahili kwa kuwa idadi ya Wanafunzi nchini ni kubwa lakini wanoonekana kusoma Kiswahili ni wachache, hii itasaidia kufikia malengo yaliyokusudiwa katika kubidhaisha Kiswahili;
- iii. Wizara iweke mikakati maaalum ya kukitambulisha Kiswahili sanifu cha Tanzania kama bidhaa duniani.

iv. Kuwe na mkakati wa kutumia balozi zetu kuanzisha vituo vya kutoa mafunzo ya lugha ya Kiswahili.

**vii. Baraza la Michezo Tanzania (BMT)**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Sekta ya Michezo ni moja ya Sekta muhimu kwa uchumi wa Taifa letu;

**NA KWA KUWA** Sekta hii bado inakumbana na changamoto mbalimbali ambazo ni kikwazo kwa ukuaji wake

**KWA HIYO BASI**, Bunge linatoa ushauri ufuatao: -

i. BMT iboreshe mawasiliano na Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya kwani hao ndiyo wenyeviti wa Baraza la Michezo kwenye maeneo yao; na

ii. Kamati za Michezo za Mikoa ziwezeshwe kwa kutengewa bajeti ya kutosha ili kuweza kuratibu vyema michezo katika ngazi hizo na za chini zaidi.

**viii. Bodi ya Filamu**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** nchi nydingi ikiwemo India zimenufaika kiuchumi; kisiasa na kijamii kupitia tasnia ya Filamu;

**NA KWA KUWA** nchi yetu bado hatujanufaika ipasavyo kutokana na changamoto mbalimbali zinazoikumba Tasnia hii;

**KWA HIYO BASI**, Bunge lina hoja zifuatazo: -

i. Mkakati uwewe kuwezesha kukamatwa maharamia wa kazi za wasanii ili wachukuliwe hatua na wasanii hao waweze kunufaika na kazi zao;

ii. Mkakati uwewe kuhakikisha “script” za filamu zetu zinakuwa katika lugha fasaha ili kuvuta soko la ndani na nje; na

iii. Uandaaji wa Filamu zetu uwe na uhalsia ili kuweza kuvutia watazamaji

#### **ix. Viwanja vya Michezo**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** unapoongelea michezo suala la viwanja bora vinavyokidhi mahitaji ni jambo ambalo haliepukiki,

**NA KWA KUWA** changamoto ya uhaba wa viwanja vya michezo nchini ni kubwa

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaitaka Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi kuanza ujenzi wa viwanja bora vya michezo nchini.

#### **3.4 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

##### **a. Mfumo wa Elimu na Mitaala**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** utajiri na mafanikio ya Taifa lolote kwa kiasi kikubwa yanategemea aina ya Mfumo wa Elimu na Mtaala ambao Taifa unao;

**NA KWA KUWA** Mfumo wetu wa Elimu na Mtaala umeonekana kuwa na changamoto jambo ambalo limefanya Serikali kuamua kuititia upya mtaala wa Elimu kwa ngazi zote ya Elimu ya Msingi, Sekondari na Elimu ya juu;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linatoa hoja zifuatazo: -

i. Zoezi la uboreshaji wa Mitaala linapaswa kujumisha ngazi nyingine za Vyuo vya Ufundı na Vyuo Vikuu ambazo nazo pia mitaala yake ina changamoto;

ii. Muda wa kukamilika kwa zoezi hili na kuanza kutumika kwa mitaala mipyä mwaka 2026 ni mrefu hivyo Wizara ione namna ya kuharakisha jambo hili bila kuathiri ubora.

##### **a. Chuo cha Ualimu Mtwara**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** katika jitihada za kupanua elimu ya vyuo vikuu na kupunguza tatizo la upungufu wa

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

walimu Serikali iliamua kubadili vyuo vya ualimu vya Dar es Salaam, Iringa na Mtwara kuwa vyuo vikuu vishiriki.

**NA KWA KUWA** Tayari vyuo vya Dar es Salaam na Iringa vimeshabadilishwa.

**KWA HIYO BASI** Bunge linashauri Serikali kuendeleza mchakato wa kubadili chuo cha ualimu Mtwara kuwa Chuo Kikuu kishiriki ili kutimiza azma yake.

### **b. Vyuo vya Ufundi**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** nchi yetu ipo kwenye Uchumi wa Kati wa Viwanda ambao unategemea zaidi wataalamu kutoka kada ya katika wanaozalishwa na Vyuo vya Ufundi;

**NA KWA KUWA** uzalishaji wa kada hii ya katika umekuwa wa kusuasua kutokana na kada hii kutopata mikopo ya Elimu;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linashauri Serikali kuanza kutoa Mikopo kwa wanafunzi wa Vyuo vya katika hususani vyuo vya ufundi ili kuweza kuzalisha wataalam wa kutosha katika fani mbalimbali za uzalishaji.

### **c. Chuo cha Ufundi Arusha**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Chuo cha Ufundi Arusha kimekuwa ni kimbilio la vijana wengi katika kujipatia elimu ya ufundi wakiwemo watoto wa kike;

**NA KWA KUWA** Chuo kinakumbana na changamoto ya uhaba wa miundombinu hususan mabweni, madarasa na maabara jambo linaloathiri wanafunzi kuijunga na wengine kulazimika kupanga mtaani;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaitaka Serikali kupeleka fedha za kutosha kukamilisha ujenzi wa miundombinu hiyo ya mabweni, madarasa na maabara.

**SEHEMU YA NNE**

**4.0 HITIMISHO**  
**4.1 Shukrani**

**Mheshimiwa Spika**, kwanza nikupongeze kwa kushinda nafasi ya Uspika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. kwa mara nyingine naomba kutumia nafasi hii tena kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, nakupongeza kwa kazi kubwa unayofanya ya kuliongoza Bunge letu vizuri. Nawashukuru pia Wenyeviti wote wa Bunge kwa kazi nzuri wanayofanya.

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kuwashukuru Mawaziri wote tuliofanya nao kazi ambao ni Mhe. Dkt. Dorothy Onesphoro Gwajima (Mb) -Aliyekuwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Manaibu wake Mhe. Dkt. Godwin Oloyce Mollel (Mb) na Mhe. Mwanaidi Ali Khamis (Mb); Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako (Mb) – aliyekuwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na Naibu Waziri wake Mhe. Omary Juma Kipanga (Mb); Mhe. Innocent Lugha Bashungwa (Mb) - Aliyekuwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, na Naibu wake Mhe. Pauline Philip Gekul (Mb) kwa mashirikiano mema tuliyokuwa nayo. Kipekee niwapongeze kwa kuteuliwa na kuwakaribisha kwenye Kamati Mhe. Adolph Faustine Mkenda (Mb) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Elimu; Mhe. Ummy Ally Mwalimu (Mb) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Afya; mhe. Dorothy Onesphoro Gwajima (Mb) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum; pamoja na Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa (Mb) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo. Aidha, nawashukuru Makatibu Wakuu wote na Manaibu Makatibu Wakuu wa Wizara hizi zote kwa ushirikiano mzuri wanaoutoa kwa Kamati wakati wote.

**Mheshimiwa Spika**, namshukuru sana Makamu Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Aloyce John Kamamba (Mb) kwa ushirikiano anaonipa mimi pamoja na Kamati kwa ujumla. Kipekee zaidi

nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa kushiriki vizuri katika shughuli za Kamati na hivyo kurahisisha kazi yangu kama Mwenyekiti wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Aloyce John Kamamba, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Eng. Samwelii Hhayuma, Xaday Mb- Mjumbe
5. Mhe. Husna Juma Sekiboko, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Tecla Mohamedi Ungele, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Kassim Hassan Haji, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Francis Leonard Mtenga, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Latifa Khamis Juakali, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Kabula Enock Shitobelo, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Bernadeta Kasabago Mushashu, Mb-Mjumbe
14. Mhe. Fatma Hassan Toufiq, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Neema Kichiki Lugangira, Mb - MJumbe
16. Mhe. Mussa Ramadhani Sima, Mb - Mjumbe
17. Mhe. George Ranwell Mwenisongole, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Dkt. Paulina Daniel Nahato, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Salome Wycliffe Makamba, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Abdallah Dadi Chikota, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Khamis Kassim Ali, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Khalifa Mohamed Issa, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Hassan Zidadu Kungu, Mb - Mjumbe
24. Mhe. Nashon William Bidyanguze, Mb - Mjumbe
25. Mhe. Hamisi Shabani Taletale, Mb - Mjumbe
26. Mhe. Prof. Kitila Alexander Mkumbo, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru sana Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi (*ndc*) kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake wakati wote kikamilifu. Pamoja nao namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein (*ndc*), Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili na Makatibu wa Kamati Ndg. Chacha Nyakega,

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Happiness Ndalu na Ndg. Francisca Haule na Msaidizi wa Kamati Ndugu Jane Ndulesi kwa kuisaidia Kamati wakati wote na kwa kuratibu vyema shughuli zote za Kamati.

### **4.2      Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Stanslaus Haroon Nyongo, Mb

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA  
NA MAENDELEO YA JAMII**

10 Februari, 2022

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante hoja imetolewa na imeungwa mkono. (*Makofî*)

Sasa namuita Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Masuala ya UKIMWI, Mheshimiwa Fatma Toufiq asome taarifa yake. (*Makofî*)

**MHE. FATMA H. TOUFIQ - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba taarifa hii yote iingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) kama illiyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa kipindi cha Januari, 2021 hadi Februari, 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kwa niaba ya Kamati niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya mwaka Kuhusu Majukumu na Shughuli Zilizotekelizwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa kipindi cha Januari, 2021 hadi Januari, 2022. Taarifa hii inawasilishwa kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu kama inavyoolekezwa katika masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020. Sehemu ya kwanza inahusu utangulizi ambapo inafafanua muundo, majukumu pamoja na maelezo ya jumla kuhusu utekelezaji wa shughuli za Kamati; sehemu ya pili inazungumzia uchambuzi na matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati; na sehemu ya tatu Kamati imetoa mapendekezo na hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi zilizosimamiwa na Kamati ni pamoja na Kamati kufuatilia kwa ukaribu utendaji wa kazi zilizo chini yake ambazo ni *TACAIDS* na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyaa pamoja na utekelezaji wa sera na mipango inayohusu udhibiti wa UKIMWI na dawa za kulevyaa katika Wizara na Taasisi za Umma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni imeipa Kamati majukumu yafuatayo:-

- (a) Kusimamia utekelezaji wa masuala yote yanayohusu UKIMWI katika sekta zote;
- (b) Kusimamia shughuli zote za Serikali za kudhibiti na kutokomeza ugonjwa wa Kifua Kikuu;
- (c) Kufuatilia utekelezaji wa sera na mipango ya Serikali kuhusu UKIMWI na Kifua Kikuu na Udhibiti wa dawa za kulevyaa;

**NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

- (d) Kujadili hatua za kudhibiti UKIMWI, Kifua Kikuu na Dawa za Kulevy;
- (e) Kushughulikia Bajeti za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy; na
- (f) Kushughulikia magonjwa yasiyoambukiza ambayo yanachangia vifo vingi sana kwa wananchi kwa kukosa ufahamu juu ya magonjwa haya pamoja na kutokufanya mazoezi na kutokuwa na desturi ya kupima afya mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufuatilia majukumu ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACAIDS*), Kamati ilibaini uwepo wa changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:-

- (a) Uwepo wa changamoto ya takwimu ambazo siyo sahihi za wananchi waliojitokeza kupima na kuanza kutumia dawa za *ARV's* ambapo baadhi ya wananchi wanapima sehemu moja na kuhamia sehemu nyingine kuchukua dawa kwa kuogopa unyanyapaa mionganoni mwa jamii inayowazunguka hali ambayo inaleta mkanganyiko wa kujua takwimu halisi na sahihi za maambukizi kwa eneo husika.
- (b) Ufinyu wa Bajeti inayotengwa na Serikali kwa ajili ya kutekeleza afua mbalimbali za UKIMWI kwa kiasi kikubwa inategemea fedha za wafadhili kutoka nje kwa zaidi ya 90% hali inayopunguza ufanisi wa Tume katika mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI ili kufikia malengo ya 95, 95, 95 ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 umeonesha kwamba shilingi bilioni moja zilitengwa kwa ajili ya Mfuko wa Kudhibiti Ukimwi, (*Aids Trust Fund – ADF*). Pamoja na Serikali kuonesha nia njema na nzuri ya kutenga fedha kwa ajili ya ATF bado Kamati inaona upo umuhimu wa Serikali kufanya uchambuzi na upembusi wa kina wa vyanzo mbalimbali vya mapato kwa ajili ya kutunisha Mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy, Mamlaka imekuwa haitengewi bajeti kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Mojawapo ya athari za kutotengewa fedha za maendeleo ni kuwepo kwa changamoto ya vituo vichache vyta kliniki za kutolea dawa ya *methadone* kwa waraibu wa dawa za kulevy ambapo huduma hiyo ya tiba inatolewa tu kwa baadhi ya hospitali za Mikoa ya Dar es Salaam, Songwe, Mbeya, Tanga na Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupitia taarifa za Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, Kamati imebaini kuwa wafanyabiashara wa dawa za kulevy wameendelea kuwa wabunifu kwa kubuni mbinu mbalimbali kwa kutumia gharama yoyote ile ili kufanikisha kusafirisha dawa za kulevy kwenda maeneo mbalimbali duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya njia hizo ni pamoja na kumeza pipi au kete tumboni; kujifunga mwilini (*Binding*): kuweka ndani ya maiti za binadamu; kuficha ndani ya vifaa mbalimbali kama vile mabegi, sabuni, *perfume*, tairi za magari, mipira, soli za viatu, vitabu, vinyago, bidhaa za makopo na kutumia *diplomatic bags* na njia nyingine nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ushauri wa Kamati kuwa Wizara iendelee kushirikiana na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy katika kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa Maofisa Usalama wa Viwanja vyta Ndege ambao hufanya ukaguzi wa abiria na mizigo ili kutambua dawa hizo kitaalamu pamoja na mbinu zinazoweza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati inaishauri Wizara kuongeza ushirikiano na Taasisi mbalimbali kwa kubadilishana taarifa za kihalifu hasa kwa kuangalia mapito ya abiria wanaohisiwa kusafirisha dawa haramu za kulevy.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI, Kamati imebaini matokeo ya 90 tatu (95, 95, 95) kwa mwaka 2020, ilikadiriwa kuwa Tanzania ina

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

watu takribani 1,700,000 wanaoishi na Virusi vya UKIMWI. Mpaka mwisho wa robo ya Oktoba – Desemba, 2020, takribani WAVIU milioni 1.4, sawa na 83% ya WAVIU wote walikuwa wanatambua hali zao. WAVIU milioni 1.36 sawa na 98% walikuwa kwenye tiba na matunzo ya ARV na 92% ya waliokuwa kwenye tiba ya ARV walikuwa na kiwango cha chini cha VVU mwilini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ushauri wa Kamati kuwa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI uongeze kasi ya huduma za Upimaji wa kwa hiari na ushauri nasaha na kuimarisha zaidi upimaji wa VVU; pili, Serikali iweke mikakati ya kuongeza idadi ya vituo vya huduma za upimaji VVU ili kusogeza huduma karibu na wananchi; tatu, Wizara kuimarisha utokomezaji wa maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto ikiwa ni pamoja na kuimarisha ufuutiliaji wa akina mama wenye maambukizi na watoto wao baada ya kujifungua na wakati wa kunyonyesha; na nne, Serikali iendelee kutekeleza mikakati ya Tohara ya Hiari kwa Wanaume na mkakati huu upewe kipaumbele katika mikoa yenye kiwango cha chini cha tohara na kiwango cha juu cha maambukizi ya VVU ikiwemo Mikoa ya Geita, Iringa, Kagera, Katavi, Kigoma, Mara, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga, Singida, Simiyu, Songwe na Tabora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Taifa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma mwaka 2019 inakadiriwa kuwa na wagonjwa wa *TB*137,000. Kati ya hao wagonjwa 82,166 sawa na 59% waligundulika na kupatiwa matibabu. Aidha, zaidi ya 44% ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI (WAVIU) husababishwa na *TB*. Takwimu hizi zinadhahirisha ya kuwa *TB* bado ni janga la Kitaifa hapa nchini mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kwamba Serikali kwa kutumia vyanzo mbalimbali inatarajiwa kutumia kiasi cha shilingi trilioni 12.6 ndani ya kipindi cha miaka mitano ijayo sawa na wastani wa shilingi trilioni 2.3 kila mwaka ili kupunguza 15% ya vifo visivytarajiwa vinavyosababishwa na magonjwa yasiyoambukiza. Aidha, Kamati imebaini kuwa,

zaidi ya 55.6% ya bajeti ya Wizara ya Afya imeelekezwa katika huduma za Saratani, Moyo, Mishipa ya Damu, Kisukari, Figo, Selimundu na magonjwa sugu ya mfumo wa hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kwamba, kwa kuwa magonjwa yasiyoambukizwa yamekuwa ni tishio kwa afya ya Watanzania wengi zaidi ya 73%, Kamati inashauri Wizara ya Afya kuweka utaratibu wa pamoja wa shughuli za udhibiti wa magonjwa yasiyoambukiza katika sekta zote kushiriki kwenye mazoezi, lishe bora, athari za afya kimazingira na mipango miji, zinaratibowi nje ya sekta ya afya.

Pili, Kamati inashauri kufanyike uwekezaji mkubwa katika Hospitali za Rufaa na Mikoa ambapo itasaidia kusogeza huduma za magonjwa yasiyoambukiza karibu zaidi na wananchi na hivyo kupunguza mzigo wa matibabu kwa mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwango cha maambukizi kiwango cha maambukizi kwa vijana wenye umri wa miaka 15 hadi 24 wanachangia kiwango chao cha maambukizi kuwa 40%, yaani 28,000 ya maambukizi yote Kitaifa, kama ilivyo katika takwimu 2016/2017, kwa mujibu a utafiti huo, inakadiriwa vijana 23,000 hupata maambukizi mapya kwa mwaka ikiwa ni theluthi moja ya maambukizi yote 72 kwa mwaka nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kwamba vijana ambao ndiyo nguvu kazi ya Taifa bado wapo nyuma katika zile 95-95-95 ambazo nimezibainisha hapo mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri ni kwamba, kuwepo na mipango mikakati ya Wizara kuhusu kuboresha mitaala ya elimu ili kujumuisha elimu ya afya ya uzazi kuanzia elimu ya msingi. Kamati inaishauri Serikali kwamba sheria zote zinazokinzana na Wizara nyingine zifanyiwe marekebisho ili ziweze kukidhi mahitaji kulingana na wakati uliopo pamoja na kupunguza vitendo vya ukatili wa kijinsia. Sheria ya Ndoa ifanyiwe mapitio ya haraka ili kupunguza maambukizi ya VVU.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara ya Madini, Kamati imebaini ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna utaratibu wa kuhamasisha matumizi ya kondomu za kike pamoja na upatikanaji wake kwa ajili ya kuwezesha wanawake kuzitumia na kujikinga dhidi ya Maambukizi ya VVU; na pili, kukosekana kwa mwongozo na mikakati ya namna ya kuratibu afua za UKIMWI katika maeneo ya migodi pamoja na waratibu wa kusimamia ipasavyo madawati ya UKIMWI katika kila mgodi ambapo wananchi watakuwa wanapata taarifa na huduma wanazostahili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri kuwa Wizara ya Madini na Tume ya Madini kushirikiana na wadau mbalimbali katika kupambana na kusimamia maambukizi ya magonjwa ya UKIMWI na Kifua Kikuu migodini illi kulinda afya za watu wanaojishughulisha na uchimbaji madini na biashara nyingine kwenye maeneo ya wachimbaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Kamati inaishauri Wizara ya Madini iendelee kusimamia wamiliki wa migodi kuwa na mipango na mikakati ya kudhibiti maambukizi ya UKIMWI na *TB* migodini kwa kuwa Sekta ya Madini inaendelea kukua kwa kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Wizara ya Uvubi, Kamati ilibaini kwamba Mkoa wa Ruvuma una kiwango kikubwa cha maambukizi, yaani 7.0%, ikifuatiwa na Mkoa wa Dar es Salaam wenye 6.9%, Pwani 5.9%, Mara 4.5%, Kagera 4.8%, Mwanza 4.2%, Geita 4.7%, Mtwara 4.1%, Katavi 5.9% na Rukwa 6.2%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, sababu zinazochangia ni kuwepo kwa kiwango kidogo cha matumizi ya kondomu kwa wanaume na wanawake wenye wapenzi zaidi ya mmoja. Wavuvi na jamii zinazowazunguka kutokuwa na tabia ya kupima na kufahamu afya zao; uelewa mdogo juu ya elimu ya UKIMWI na Kifua Kikuu katika mialo na kambi za wavuvi ambapo hupelekea ngono zembe.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilitoa ushauri kuhusu mambo ya msingi yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Wizara iuunde Kamati za Afya zitakazoshirikiana kutoa elimu-rika katika mialo ya wavuvi wa samaki ili ziweze kufuatilia masuala yote yahuyohusu afya na elimu kuhusu kujikinga na maambukizi ya VVU na Kifua Kikuu; pili, Kamati inasisitiza elimu zaidi kuhusu matumizi ya vifaa-kinga itolewe ili kupunguza maambukizi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia masharti ya Kanuni ya (10)(c) ya Sehemu ya Tatu, Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 Kamati hii ilifanya ziara ya kikazi katika Mikoa ya Njombe, Mbeya na Songwe. Lengo la ziara lilikuwa ni kutembelea na kukagua afua zinazotekelawa na Serikali pamoja na sekta binafsi katika ngazi mbalimbali za kitaasisi na jamii katika kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu, Ukoma na matumizi ya dawa za kulevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa mambo yaliyobainishwa na Kamati katika wa ziara, kwa kuwa muda siyo rafiki sana na tunayo kwenye vishkwambi, hii mtaipitia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende 2.4 kuhusu uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020 na mchakato wa bajeti wa mwaka fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri ililoutoa kuhusu Bajeti za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Taasisi hizo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Taarifa hizo ziliwasilishwa Bungeni kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu Bunge Toleo la Juni, 2020 mnamo tarehe 29 Machi, 2021. Kwa hiyo, taarifa hiyo ambayo ipo 2.42 ipo pale ukurasa wa 10 wa taarifa hii hadi namba 2.43 katika ukurasa wa 11 wa taarifa hii.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa makadirio ya matumizi; Tume ya Kudhibiti UKIMWI katika mwaka wa fedha 2021/2022 Fungu 92 inatarajia kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi milioni tano ambayo yanatarajiwa kupatikana kutokana na uuza ji wa vifaa chakavu na tozo kutokana na matumizi ya Ukumbi wa Mikutano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha wa 2021/2022 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania - Fungu 92 imeombewa jumla ya shilingi 4.3, kati ya fedha hizo, shilingi 1.3 sawa na 32% kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na shilingi bilioni 2.9 sawa na 68% ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida kwa upande wa matumizi ya kugharamia miradi ya maendeleo. Uchambuzi umeonesha kama bajeti ilivyoombwa ilipungua kwa 72%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta – Fungu 71 taarifa zipo pale; mafunzo na semina kwa Wajumbe wa Kamati inaonesha pale. Katika kipindi cha Januari, 2021 hadi Januari, 2022, Kamati kwa kushirikiana na wadau wa masuala ya UKIMWI, Kifua Kikuu, Dawa za Kulevyta na magonjwa yasiyoambukiza, walipata mafunzo kutoka kwa Wizara na taasisi zifuatazo: Wizara ya Afya, Tume ya Kudhibiti UKIMWI (*TACAIDS*), Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*NACIP*), Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma (*NTLP*), Shirika la *Walter Reed Program Tanzania*, *Phyte Exponent*, *UNICEF* na *TAN – CIDA*. Hawa ni baadhi ya wadau ambaao walitoa semina pamoja na mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu ni maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACAIDS*); upatikanaji wa Fedha za ndani kwa ajili ya Afua za UKIMWI:-

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

KWA KUWA, Kamati imebaini kwamba Bajeti ya Maendeleo ya fedha za ndani ya TACA/DSkwa mwaka 2020/2021 ilitengewa shilingi bilioni moja na mwaka 2021/2022 imeendelea kutengewa kiasi hicho hicho cha fedha, yaani shilingi bilioni moja;

NA KWA KUWA, bado Tume inahitaji kuongezewa fedha zaidi ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu;

NA KWA KUWA, suala la utekelezaji wa afua za UKIMWI linahitaji nguvu nyingi sana za Serikali, wananchi na wadau;

KWA HIYO BASI, Kamati inaishauri Serikali iweke mikakati mahususi ya kutenga fedha za ndani kwa ajili ya udhibiti wa UKIMWI badala ya kutegemea fedha za wafadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Kudhibiti UKIMWI (ATF):

KWA KUWA, Serikali ilianzisha Mfuko wa UKIMWI wa Taifa mwaka 2015 kwa ajili ya kuongeza nguvu za kupambana na UKIMWI hapa nchini;

NA KWA KUWA, pamoja na malengo mengine Mfuko huu ulilenga kuwezesha nchi kuwa na uwezo wa kifedha wa kupambana na UKIMWI;

NA KWA KUWA, Mfuko huu bado una changamoto ya kutojitosheleza kifedha kwa kukosa vyanzo endelevu vya mapato kwa ajili ya mwitiko wa afua za UKIMWI na kutegemea fedha za wafadhili kwa 90%;

NA KWA KUWA, lengo la Mfuko huu ni kuhakikisha Serikali inatenga fedha zake za ndani kwa ajili ya kupambana na janga hili;

KWA HIYO BASI, Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kuliangalia suala hili kwa uzito unaostahili ili Mfuko wa ATF uweze kuwa na vyanzo vya mapato vya ndani. Aidha, Serikali ifikie mahali ipate ufumbuzi wa upatikanaji wa

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

fedha hizo. Kwa kufanya hivyo, tutapunguza utegemezi mkubwa wa fedha za wafadhili ambapo kwa sasa fedha hizo zimeambatana na masharti magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mapendekezo ya Kamati kuwa, mtazamo wa kufikia malengo ya kufikia 95, 95, 95 ifikapo mwaka 2030, inamaanisha wigo wa uhitaji wa dawa za ARV's unazidi kuongezeka wakati wafadhili wanapungua. Hivyo hatuna budi kujipanga ili tusifikie wakati ambapo mahitaji yatazidi uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaume kutojitokeza kupima VVU na kufanya tohara:-

KWA KUWA, Kamati imebaini takwimu zinaonesha wanaume wenyе umri mkubwa bado hawajitokezi kupima na kutambua hali ya afya zao za maambuki ya UKIMWI ikilinganishwa na wanawake;

NA KWA KUWA imebainika kuwa ufanyaji wa tohara hupunguza kwa kiasi kikubwa maambukizi ya VVU kwa 60% na kusaidia uwezekano wa kuambukiza saratani ya mlango wa shingo ya kizazi kwa akina mama;

NA KWA KUWA, malengo ya Umoja wa Mataifa yanataka kila nchi kufikia 95, 95, 95 ifikapo mwaka 2030;

KWA HIYO BASI, Kamati inashauri kuwa Serikali kuhakikisha juhudzi zinafanyika za kutoa elimu kuhusu umuhimu wa wanaume kujitokeza kupima afya zao na kufanya tohara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaume kutojitokeza kupima VVU na kufanya tohara:-

KWA KUWA Kamati imebaini takwimu zinaonesha wanaume wenyе umri mkubwa bado hawajitokezi kupima na kutambua hali ya afya zao za maambuki ya UKIMWI ikilinganishwa na wanawake.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

NA KWA KUWA, imebainika kuwa ufanyaji wa tohara hupunguza kwa kiasi kubwa maambukizi ya VVU kwa asilimia 60 na kusaidia uwezekano wa kuambukiza saratani ya mlango wa shingo ya kizazi;

NA KWA KUWA malengo ya Umoja wa Mataifa yanataka kila nchi kufikia 95 tatu ifikapo mwaka 2030;

HIVYO BASI Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha juhud zinafanyika za kutoa elimu kuhusu umuhimu wa wanaume kujitokeza kupima afya zao na kufanya tohara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Suala la Ukatili wa Kijinsia:-

KWA KUWA vitendo vya ukatili wa kijinsia vimeendelea kuwepo na kuleta athari ndani ya familia na jamii kwa ujumla.

NA KWA KUWA tarehe 25 Novemba, 2021, Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya uzinduzi wa maadhimisho ya kampeni ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia Tanzania yaliyofanyika Kitaifa katika Mkoa wa Dar es Salaam kwenye Kaulimbiu isemayo "Ewe Mwananchi: Komesha Ukatili wa Kijinsia Sasa".

NA KWA KUWA zaidi ya asilimia 20 ya wanawake wenye umri kati ya miaka 15 na 29 wanafanyiwa ukatili wa kijinsia hapa nchini.

NA KWA KUWA Kamati imebaini kuwa ukatili wa kijinsia huchangia kuwepo kwa maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwa wanawake na wasichana na wanaume.

HIVYO BASI ni ushauri wa Kamati kuwa Serikali kuelimisha, kukemea na kuchukua hatua kwa pamoja ili kupinga aina zote za ukatili wa kijinsia katika jamii ambazo husababisha maambukizi ya UKIMWI. Aidha, Serikali iendelee kutekeleza Mpango Kazi wake wa Kitaifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto unaolenga kupunguza kiwango cha ukatili dhidi ya wanawake na watoto katika jamii kwa asilimia 50 ifikapo 2022.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maambukizi ya VVU kwa vijana:-

KWA KUWA takwimu zinaonesha kuwa vijana 80 huambukizwa kila siku, kwa mwezi ni vijana 2400, sawa na maambukizi 28,800 kwa mwaka.

NA KWA KUWA vijana wenyе umri kati ya miaka 15 na 24 wanachangia maambukizi kwa asilimia 24 ya maambukizi ya kitaifa ambapo kiwango cha maambukizi kwa wasichana ni asilimia 2.1 na wavulana ni 0.6.

NA KWA KUWA sababu kubwa zinazochangia kuongezeka kwa maambukizi mapya kwa wasichana rika balehe ni kufanya ngono wakiwa na umri chini ya miaka 15 na wavulana kufanya ngono kwa asilimia 14.

HIVYO BASI Kamati inaishauri Serikali kuendelea kushirikiana na wadau, wazazi na walezi kutoa mafunzo ya malezi bora ya afya ya uzazi kwa vijana walioko shulen na nje ya shule na hatua za mabadiliko ya tabia. Aidha, Wizara kuongeza utoaji wa huduma rafiki za afya kwa vijana rika balehe walioko shulen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maambukizi Kutoka kwa Mama Kwenda kwa Mtoto:-

KWA KUWA Kamati imebaini kuwa yapo maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto ambapo kati ya watoto 1,800,000 waliozaliwa hapa nchini kwa mwaka watoto wapatao 10,000 wanazaliwa na maambukizi ambayo ni sawa na asilimia 0.6.

HIVYO BASI Kamati inaishauri Serikali kuweka mkakati madhubuti wa kutoa elimu ya maambukizi kwa akinamama wajawazito pindi wanapofikia wiki 12 baada ya ujauzito wapime virusi vya UKIMWI, kupima VVU wiki 14 baada ya kujifungua na kuhamasisha kupima VVU wakati wa kunyonyesha.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua muda sio rafiki sana, lakini 3.2 inazungumzia kuhusu Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyaa:-

KWA KUWA majukumu ya Mamlaka ya Kudhibiti na kupambana na Dawa za Kulevyaa ni udhibiti wa dawa za kulevyaa na kufanya uelimishaji kwa jamii.

NA KWA KUWA jukumu la pili na la tatu ni kimkakati zaidi ikilinganishwa na jukumu la kwanza na utekelezaji wake unahitaji rasilimali fedha za kukidhi ukubwa wa tatizo la athari za biashara na matumizi ya dawa za kulevyaa, ilihali bado elimu ya matumizi ya madhara ya dawa za kulevyaa hajjawafikia wanajamii.

HIVYO BASI Kamati inashauri Serikali kuiwezesha Mamlaka kwa kutenga fedha kwenye Bajeti yake kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Fedha zitakazoisaidia Mamlaka kuimarisha programu za kuimarisha na kutoa elimu ya madhara ya matumizi ya dawa za kulevyaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapambano ya Dawa za kulevyaa:-

KWA KUWA tafiti zinaonesha kuwa mbinu mbalimbali zinatumika kusafirisha dawa za kulevyaa ikiwa ni pamoja na kubeba mizigo ya kawaida na kuficha ndani ya bidhaa nydingine na hata kutumia maiti.

HIVYO BASI Kamati inashauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwekeze katika vitendea kazi vya kisasa vitakavyorahisisha zoezi zima la upekuzi na ukamataji wa dawa za kulevyaa zinazoingizwa nchini kupitia njia mbalimbali, lakini pia vitakavyolinda afya za watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, najua muda sio rafiki, maelezo yanaendelea ukurasa wa 20.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Kutokuwepo na Sera ya Dawa za Kulevy:-

KWA KUWA mpaka sasa Tanzania haina Sera ya Taifa ya Kupambana na Dawa za Kulevy ambayo umuhimu wake ungeimarisha mapambano yaliyo ndani ya matumizi ya biashara ya dawa za kulevy.

HIVYO BASI Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya mchakato wa kuandaa Sera ya Taifa ya kudhibiti na kupambana na Dawa za Kulevy Nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kifua Kikuu, inaelezea pale ukurasa wa 21. Sambamba na hilo, Magonjwa Yasiyoambukiza, yanaelezewa pale ukurasa wa 22. Naomba nitoe ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba, Wizara ya Afya, iweke uratibu wa pamoja kuhakikisha shughuli za udhibiti wa magonjwa yasiyoambukiza katika Sekta zote kushiriki kwenye mazoezi, lishe bora, athari za kimazingira na mipango miji, ziratibiwe na Sekta ya Afya. Mambo mengine yamezungumzwa kule, najua mnazo kwenye vishkwambi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye Hitimisho. Kwa namna ya pekee napenda kumshukuru sana Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelwa Mwihambi na watendaji wake wote kwa ushirikiano aliouonesha kwa Kamati na Makatibu ambao ni Bi. Asia Msangi, Bi. Happiness Ndalu pamoja na Bi. Pamela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Ajira, Vijana na Walemauvu) Mheshimiwa Jenista Mhagama na Naibu Waziri, Mheshimiwa Ummy Nderiananga, Patrobas Katambi. Vilevile napenda kumpongeza Waziri mpya wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Ajira, Vijana na Walemauvu), Mheshimiwa Pindi Hazara Chana. Pamoja na hao Kamati inampongeza Mkurugenzi Mtendaji wa Kudhibiti UKIMWI, Dkt. Leonard Maboko, Kamishna Generali wa

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Kupambana na Dawa za Kulevyta, Ndugu Gerald Kusaya na Watendaji wote wa Tume na Mamlaka kwa ushirikiano walioipatia Kamati kwa kipindi cha mwaka mzima ambapo waliweza kufika mbele ya Kamati kila walipohitajika na kutoa ufanuzi wa masuala mbalimbali kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuwapongeza Waziri wa Afya, Naibu Waziri wa Afya, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wote, lakini pia niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa uchapakazi wao wakati wote na kutekeleza majukumu ya kamati kwa mwaka mzima. Wamefanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo kuhusu shughuli zilizotekelizwa, uchambuzi, matokeo na utekelezaji wa shughuli za Kamati, Maoni na Mapendekezo, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako lipokee, Ilijadili na kuikubali Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo kwa ajili ya utekelezaji wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

### **KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI TAARIFA YA SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA KWA KIPINDI CHA JANUARI, 2021 HADI JANUARI, 2022**

---

#### **SEHEMU YA KWANZA**

##### **1.0      UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa niaba ya Kamati niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Mwaka kuhusu majukumu na shughuli zilizotekelizwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa kipindi cha Januari, 2021 hadi Januari, 2022. Taarifa hii inawasilishwa kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu (3) kama inavyoelekezwa katika masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020. Sehemu ya Kwanza inahusu utangulizi ambapo inafafanua muundo, majukumu pamoja na maelezo ya jumla kuhusu utekelezaji shughuli za Kamati. Sehemu ya Pili inazungumzia uchambuzi na matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Sehemu ya Tatu Kamati imetoa mapendekezo na hitimisho.

### **1.1. Muundo na Majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane, Sehemu ya Tatu, Kanuni ya 10 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, Kamati ya Masuala ya UKIMWI imepewa jukumu la kusimamia shughuli za Taasisi mbili ambazo ni Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACAIDS*) na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyा.

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni imeipa Kamati majukumu yafuatayo:-

- (a) kusimamia utekelezaji wa masuala yote yanayohusu UKIMWI katika sekta zote;
- (b) kusimamia shughuli zote za serikali za kudhibiti na kutokomeza ugonjwa wa kifua kikuu;
- (c) kufuatilia utekelezaji wa sera na mipango ya serikali kuhusu UKIMWI, kifua kikuu na udhibiti wa dawa za kulevyा;
- (d) kujadili hatua za kudhibiti UKIMWI, kifua kikuu na dawa za kulevyा
- (e) kushughulikia Bajeti za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyा; na
- (f) kushughulikia Magonjwa Yasiyoambukiza ambayo yanachangia vifo vingi sana kwa wananchi kwa kukosa

ufahamu juu ya magonjwa haya pamoja na kutokufanya mazoezi na kutokuwa na desturi ya kupima afya mara kwa mara.

### **1.2. Utaratibu uliotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imetumia utaratibu ufuatao katika kutekeleza majukumu yake:-

- (a) Kufanya vikao na Wizara na Taasisi kwa kuwaomba kufika mbele ya Kamati ili kutoa taarifa juu ya jambo au suala mahususi ambalo Kamati ilipenda kupata taarifa zake kutoka kwa Watendaji wa Wizara na Taasisi hizo;
- (b) Kufanya ziara kwa ajili ya kukagua shughuli zinazotekelawa katika kushughulikia masuala ya UKIMWI, Kifua Kikuu, Dawa za Kulevyaa na Magonjwa Yasiyoambukiza;
- (c) Kushiriki semina, tamasha na warsha mbalimbali kuhusiana na Masuala ya UKIMWI, Kifua Kikuu, Dawa za Kulevyaa na Magonjwa Yasiyoambukiza; na
- (d) Kufuatilia utekelezaji wa Majukumu ya Wizara na Taasisi hizo.

### **1.3. Shughuli zilizotekelawa na Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Februari, 2021 hadi Januari, 2022, Kamati imetekelawa shughuli zifuatazo:-

- (a) Kufuatilia utekelezaji wa Afua mbalimbali za UKIMWI, dawa za kulevyaa, kifua kikuu na magonjwa yasiyoambukiza katika Wizara na baadhi ya Taasisi za umma;
- (b) Kupata mafunzo mbalimbali kuhusiana na masuala ya UKIMWI na Dawa za Kulevyaa;
- (c) Kufanya ziara maeneo mbalimbali yanayojihusisha na mapambano ya UKIMWI na Dawa za Kulevyaa kwa lengo la kuona na kutoa ushauri kuhusiana na maeneo hayo;

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

(d) Kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Bajeti za Tume ya Kudhibiti UKIMWI na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

(e) Kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

### **SEHEMU YA PILI**

## **2.0 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii inaelezea utekelezaji wa shughuli za Kamati kwa kipindi cha Januari, 2021 hadi Januari, 2022 kwa kuzingatia masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge hususan Kanuni ya 10 ya Sehemu ya Tatu, Nyongeza ya Nane, Toleo la Juni, 2020. Mpango Kazi uliandaliwa na kutekelezwa katika kipindi hicho ambao matokeo ya utekelezaji wake yamefanyiwa uchambuzi katika Sehemu hii.

### **2.1 Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi zinazosimamiwa na Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifuatilia kwa ukaribu utendaji kazi wa Taasisi zilizo chini yake ambazo ni TACAIDS na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta pamoja na utekelezaji wa Sera na Mipango inayohusu Udhibiti wa UKIMWI na Dawa za Kulevyta katika Wizara na Taasisi za Umma nchini kama ifuatavyo:-

#### **2.1.1 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS)**

**Mheshimiwa Spika**, Katika kufuatilia majukumu ya Tume hii Kamati ilibaini uwepo wa changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:-

(a) Uwepo wa changamoto ya takwimu ambazo si sahihi za wananchi waliojitokeza kupima na kuanza kutumia dawa za ARVs ambapo baadhi ya wananchi wanapima sehemu moja na kuhamia sehemu nyingine kuchukua dawa kwa kuogopa unyanyapaa mionganoni mwa jamii inayowazunguka hali ambayo inaleta mkanganyiko wa kujua takwimu halisi na sahihi za maambukizi kwa eneo husika.

(b) Ufinyu wa Bajeti inayotengwa na Serikali kwa ajili ya kutekeleza afua mbalimbali za UKIMWI kwa kiasi kikubwa inategemea fedha za wafadhili kutoka nje kwa zaidi ya asilimia 90 hali inayopunguza ufanisi wa Tume katika mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI ili kufikia malengo ya 95-95-95 ifikapo mwaka 2030.

### **2.1.2 Mfuko wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (*Aids Trust Fund - ATF*)**

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na hatua nzuri ya Serikali ya kuanzisha Mfuko wa Udhagini wa UKIMWI (ATF) tangu mwaka 2015 mpaka sasa Serikali haijaweza kubainisha njia bora ya utatuzi wa kutunisha Mfuko wa (ATF) ingawa Kamati imekuwa ikitoa taarifa mara kwa mara kuhusiana na suala hili. Aidha takwimu zinaonesha kuwa, zaidi ya asilimia 90 ya gharama za UKIMWI kwa mwaka zinafadhiliwa na Wadau wa Maendeleo wa Serikali ya Marekani na Mfuko wa Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria (*Global Fund*).

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Mfuko wa Udhagini wa UKIMWI kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 unaonesha kuwa shilingi bilioni moja (1,000,000,000/=) zimetengwa kwa ajili ya ATF. Pamoja na Serikali kuonesha nia njema na nzuri ya kutenga fedha kwa ajili ya ATF bado Kamati inaona upo umuhimu wa Serikali kufanya uchambuzi na upembusi wa kina wa vyanzo mbalimbali vya mapato kwa ajili ya kutunisha Mfuko huu. Aidha bado kiwango kinachotengwa ni kidogo sana ukilinganisha na mahitaji na pia utekelezaji wa utoaji wa fedha hizo bado ni wa kiwango cha chini. Kamati inaona ni muhimu Serikali kufanya uchambuzi wa vyanzo mbalimbali vya mapato vya uhakika kwa ajili ya kutunisha Mfuko huu. Ni

maoni ya Kamati kuwa Serikali kuona umuhimu wa kutenga fedha zake za ndani kwa ajili ya udhibiti wa UKIMWI. Aidha iweke mipango mbalimbali madhubuti ya kupata vyanzo vingine nya mapato vitakavyosaidia kupata fedha zaidi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Nijambo jema bajeti ya UKIMWI kwa kiasi kikubwa itokane na fedha zetu za ndani. Uwepo wa vyanzo nya uhakika kwa ajili ya Mfuko huu kutafungua milango kwa wadau wengine wenyewe nia na maslahi na suala husika kujitokeza kuunga mkono jitihada za Serikali; kwa mfano, sekta binafsi kujumuisha nguvu zao pamoja kwa ajili ya kuchangia Mfuko wa Udhaminii wa UKIMWI

### **2.1.3 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyaa (DCEA)**

**Mhesimiwa Spika**, ajenda ya kupambana na dawa za kulevyaa ni kubwa na inapaswa kuangaliwa kwa uzito wa pekee. Katika utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka ya Kudhibiti Kupambana na Dawa na Kulevyaa, Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

- (a) Tangu kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyaa, Mamlaka imekuwa haitengewi bajeti kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Mojawapo ya athari za kutotengewa fedha za maendeleo ni kuwepo kwa changamoto ya vituo vichache nya kliniki za kutolea dawa ya *methadone* kwa waraibu wa dawa za kulevyaa ambapo huduma hiyo ya tiba inatolewa kwa baadhi ya hospitali za Mikoa ya Dar es Salaam, Songwe, Mbeya, Tanga na Arusha.
- (b) Kutokuwepo kwa Sera ya Taifa ya Kupambana na Dawa za Kulevyaa ni suala lenye uzito mkubwa na hivyo linahitaji msukumo wa ziada.
- (c) Elimu kuhusu matumizi na madhara ya dawa za kulevyaa na uelewa mdogo juu ya madhara ya dawa za kulevyaa na njia sahihi za kupambana na tatizo la dawa za kulevyaa mionganoni mwa wananchi/jamii bado haijawafikia wananchi wengi na hivyo kuongezeka kwa vitendo nya

utumiaji dawa za kulevyta na kuongezeka kwa unyanyapaa mionganii mwa waraibu walioacha matumizi ya dawa hizo pindi wanaporudi katika familia zao.

(d) Kukosekana kwa mfumo maalum katika ngazi ya jamii kwa ajili ya kuwatambua waraibu wa dawa za kulevyta. Kwa sababu hiyo kunakuwa na upungufu wa mwitikio wa Kitaifa wa kupambana na tatizo hilo; hii ni pamoja na kukosekana kwa elimu ya kutosha kuhusu matumizi na madhara ya dawa za kulevyta kama ilivyofanyika kwa mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU/UKIMWI.

#### **2.1.4 Taasisi za Umma za Kisekta Zinazotekeleza Sera za Ukimwi na Dawa za Kulevyta**

##### **(a) Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta (DCEA)**

**Mheshimiwa Spika**, tatizo la dawa za kulevyta ni suala mtambuka na hivyo linahitaji nguvu ya pamoja kutoka kwa wadau mbalimbali katika kukabiliana nalo. Mamlaka ina majukumu yake ikiwa ni pamoja na kuunganisha jitihada za wadau na kuwajengea uwezo iii kuongeza tija katika mapambano dhidi ya matumizi na biashara ya dawa za kulevyta. Aidha tatizo la dawa za kulevyta linavuka mipaka ya nchi na hivyo huhusisha mataifa mbalimbali. Mamlaka pia inahusika katika kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa ili kuongeza jitihada za kikanda na kimataifa katika kukabiliana na tatizo la dawa za kulevyta duniani.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka 2020 jumla ya kilo **13,230.23** za Bangi, kilo **11,804.87** za Mirungi, kilo **4.52** za Cocaine na kilo **349.81** za Heroin zimekamatwa. Katika ukamataji huo jumla ya kesi **7,361** zimefunguliwa zikihuisha watuhumiwa **9,265** ambapo watuhumiwa **751** ni wanawake na watuhumiwa **8,514** ni wanaume. Aidha Mamlaka imefanikiwa kufanya ukaguzi katika makampuni **106** yanayojihuisha na uingizaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevyta katika Vituo vya Forodha vya Tarakea, Holili, Namanga, Tunduma, Kasumulo, Mabamba,

Manyovu na makampuni ya kusafirisha vifurushi. Mamlaka pia imeweza kuzuia uingizwaji wa kemikali bashirifu zilizokuwa ziingizwe kinyume na sheria kiasi cha kilo **57,600** kwa mwaka 2020.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Mamlaka katika kupambana na dawa za kulevyta na kukamilisha Mwongozo wa Uanzishwaji na Uendeshwaji wa Nyumba za Upataji Nafuu (*Guidelines for Management of Sober Houses in Tanzania*); Kamati imebaini kuwa bado hakuna Nyumba za Upataji Nafuu za Serikali. Kamati inaona ipo haja ya Serikali kuona umuhimu wa kuchukua hatua ya kujenga nyumba za upataji nafuu kwa ajili ya waathirika wa dawa za kulevyta ili kuipunguzia jamii gharama zinazotozwa na asasi za kiraia.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini uwepo wa ukubwa wa mipaka ya nchi ardhini na baharini na kuongezeka kwa njia za videnyo zisizo rasmi huchangia kufanya doria au udhibiti wa uingizwaji wa dawa za kulevyta kutofanyika kwa ukamilifu. Ni maoni ya Kamati kuwa Serikali ianzishe Ofisi za Mamlaka za Kanda zitakazoimarišha udhibiti na mapambano dhidi ya dawa za kulevyta nchini. Vilevile Mamlaka kuanzisha Maabara yenye uwezo wa kufanya tafiti na utambuzi wa dawa za sasa na bidhaa mpya zinazoingizwa sokoni.

**Mheshimiwa Spika**, Utafiti unaonesha kwamba kumekuwepo na ongezeko kubwa la Magonjwa ya Akili, UKIMWI, Kifua Kikuu na Homa ya Ini mionganoni mwa waathirika wa dawa za kulevyta na hivyo kuathiri tiba mionganoni mwao na jamii kwa ujumla. Hivyo basi ni maoni kuwa Serikali ione umuhimu wa kuchukua hatua ya kuongeza huduma za tiba ili kuwafikia waathirika wengi zaidi ikiwepo kuongeza vituo vyta tiba ya *methadone* katika mikoa iliyo na ongezeko la maambukizi ya UKIMWI na waathirika wa dawa za kulevyta.

**(b) Wizara ya Habari, Mawasiliano na Uchukuzi**

**Mheshimiwa Spika**, viwanja vya ndege nchini vimeripotiwa mara kwa mara kukamata watuhumiwa wa usafirishaji wa dawa haramu za kulevyia. Matumizi ya njia hii ya usafiri yameongezeka kutokana na uharaka wa usafiri wenyewe ambao huwavutia zaidi wasafirishaji ambao wengi humeza dawa hizo na usafiri huu unaweza kumfanya mhusika kuunganisha safari ili aweze kukwepa mkono wa sheria na kuwepo eneo lolote kwa muda mfupi. Hata hivyo uwepo wa mifumo rasmi ya udhibiti imerahisisha wahusika kutambulika haraka tofauti na njia nyngine za usafirishaji.

**Mheshimiwa Spika**, wafanyabiashara wa dawa za kulevyia wameendelea kuwa wabunifu kwa kubuni mbinu mbalimbali na kwa kutumia gharama yoyote ili kufanikisha kusafirisha dawa za kulevyia kwenda maeneo mbalimbali duniani. Baadhi ya njia hizo ni pamoja na kumeza pipi/kete tumboni; kujifunga mwilini (*Binding*); kuweka ndani ya maiti za binadamu; kuficha ndani ya vifaa mbalimbali kama vile mabegi, sabuni, perfume, tairi za magari, mipira, soli za viatu, vitabu, vinyago, bidhaa za makopo na kutumia *diplomatic bags* na njia nyngine nyngi. Ni ushauri wa Kamati kuwa Wizara iendelee kushirikiana na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyia (DCEA) katika kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa Maofisa Usalama wa Viwanja vya Ndege ambao hufanya ukaguzi wa abiria na mizigo ili kutambua dawa hizo kitaalamu pamoja na mbinu zinazoweza kutumika. Kamati inaishauri Wizara kuongeza ushirikiano na Taasisi mbalimbali kwa kubadilishana taarifa za kihalifu hasa kwa kuangalia mapito (*routings*) ya abiria wanaohisiwa kusafirisha dawa haramu za kulevyia.

**Mheshimiwa Spika**, uingizaji wa dawa za kulevyia pia hufanyika kirahisi katika maeneo ya mipaka kama bandari na fukwe iwapo maeneo hayo hayajarasimishwa. Njia hii hutumika kutokana na maeneo yasiyo rasmi hayana mamlaka za Serikali zinazosimamia Sheria mbalimbali za nchi ambazo zinadhibiti utaratibu wa forodha, uingiaji wa watu, uingiaji wa bidhaa ikiwa ni pamoja na bidhaa zinazohitaji usimamizi mahsus kama dawa za kulevyia. Kamati inaishauri

Wizara ya Habari, Mawasiliano na Uchukuzi kutenga bajeti ya vyanzo vya ndani vya Taasisi zilizo chini yake kwa ajili ya kununua vifaa vipya na vya kisasa kama boti za kufanya doria pamoja na kukarabati vifaa vilivyopo, sambamba na kuweka mbwa maalumu wa kunusa na kubaini dawa haramu za kulevyta katika maeneo mbalimbali ya viwanja vya ndege na bandari zote.

**(c) Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (NACP)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa kiwango cha maambukizi ya VVU kimeshuka kutoka asilimia 7 mwaka 2003/04 hadi kufikia asilimia 4.7 mwaka 2016/17. Kiwango cha maambukizi kwa wanawake ni kikubwa (asilimia 6.3) ikilinganishwa na wanaume (asilimia 3.4). Pamoja na kushuka kwa kiwango cha maambukizi ya VVU, Matokeo ya tisini tatu (90, 90, 90) kwa mwaka 2020 illkadiriwa kuwa Tanzania ina watu takribani 1,700,000 wanaoishi na Virusi vya UKIMWI. Mpaka mwisho wa robo ya Oktoba - Desemba 2020, takribani WAVIU milioni 1.4, sawa na asilimia 83 ya WAVIU wote walikuwa wanatambua hali zao za VVU. WAVIU milioni 1.36 sawa na asilimia 98 walikuwa kwenye tiba na matunzo ya ARV na asilimia 92 ya waliokuwa kwenye tiba ya ARV walikuwa na kiwango cha chini cha VVU mwilini.

Wajumbe walijadili na kuibua hoja mbalimbali ambazo zillhitaji ufanuzi kisha kutoa ushauri wa namna ya kuimarisha Mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI kama ifuatavyo:-

(i) Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI uongeze kasi ya huduma za Upimaji wa kwa hiari na ushauri nasaha na kuimarishwa zaidi upimaji wa VVU. Aidha, Serikali iweke mikakati ya kuongeza idadi ya vituo vya huduma za upimaji VVU ili kusogeza huduma karibu na wananchi, kutumia mbinu mbalimbali za utoaji huduma ikiwemo upimaji binafsi, kuhakikisha upatikanaji wa vitendanishi vya upimaji pamoja na kutoa elimu na kuongeza uelewa wa wananchi ili kupunguza unyanyapaa.

- (ii) Wizara kuimarisha utokomezaji wa maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Aidha, Serikali iweke mikakati ya kuimarisha huduma za utoaji wa tiba za ARVs kwa mama wajawazito na wanaonyonyesha wenyе maambukizi ya VVU ikiwa ni pamoja na kuimarisha ufuutiliaji wa akina mama wenyе maambukizi na watoto wao baada ya kujifungua. Pia inasisitiza kuimarisha ugunduzi wa hali ya VVU kwa watoto wachanga na kuwaweka kwenye matibabu.
- (iii) Kuimarisha ufuasi endelevu wa dawa za ARVs kwa kuwashirikisha watoa huduma ngazi ya jamii na mama mwambata ili kuboresha utoaji wa tiba kinga kwa wenzi wasio na maambukizi na kuimarisha ushirikishaji wa wanaume katika kliniki za mama na mtoto.
- (iv) Serikali kuendelea kutekeleza mkakati wa Tohara ya Hiari kwa Wanaume ili kupunguza uwezekano wa maambukizi kutoka kwa mama mwenye maambukizi kwenda kwa mwanaume. Mkakati huu upewe kipaumbele katika Mikoa yenye kiwango cha chini cha tohara na kiwango cha juu cha maambukizi ya VVU Geita, Iringa, Kagera, Katavi, Kigoma, Mara, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Njombe, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga, Singida, Simiyu, Songwe na Tabora.

**(d) Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma (NTLP)**

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania ni miongoni mwa nchi 30 zenyе maambukizi makubwa ya ugonjwa wa TB zinazochangia **asilimia 87** ya wagonjwa wote duniani. Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani, kwa mwaka 2019 kulikuwa na wagojwa wapya wa TB **milioni 10** ambao kati yao **milioni 1.4** sawa na **asilimia 14** walifariki. Mwaka 2019 Tanzania ilikuwa na wagonjwa wapya wa TB **137,000**. Kati ya hao wagonjwa **82,166** sawa na **asilimia 59** waligundulika na kupatiwa matibabu.

**Mheshimiwa Spika**, zaidi ya **asilimia 44** ya vifo vya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI (WAVIU) husababishwa na TB. Takwimu hizi zinadhihirisha ya kuwa TB bado ni janga la

kitaifa hapa nchini mwetu kama ilivyo pia janga la kidunia tangu ilipotangazwa hivyo mwaka 1993. Aidha Kamati imebaini upungufu wa mashine za *Gene-Xpert* ambazo hutumika kupimia ugunduzi wa TB. Kamati ilibaini na kutoa ushauri kuhusu mambo ya msingi yafuatayo:-

- (i) Serikali kuendelea kuboresha huduma za ugunduzi wa TB kwa kupanua teknolojia mpya ya vinasaba ya Gene-Xpert inayotoa majibu kwa haraka ndani ya saa mbili na mashine za hadubini ambazo hutoa majibu baada ya saa 48 katika Halmashauri zote nchini na kuimarisha mfumo wa usafirishaji wa sampuli kwa vituo vilivyo mbali na maabara ili kuhakikisha kila mhisiwa wa TB anafanyiwa uchunguzi. Aidha kuhakikisha halmashauri zote zinatekeleza mfumo wa uchunguzi na ugunduzi wa TB katika vituo vyetu ulioboreshwa "*Quality Improvement in TB case detection*" katika vituo vya kutolea huduma za afya.
- (ii) Serikali iendelee kutoa elimu kwa jamii kuhusu athari na dalili za TB na Ukoma na namna ya kukabiliana na magonjwa haya kwa kuitia redio, televisheni, vipeperushi na mitandao ya kijamii (*facebook, tweeter n.k.*). Aidha Wizara iwajengee uwezo watoa huduma za TB ngazi ya jamii ikiwepo vikundi vya wagonjwa waliowahi kuugua TB na kupona (*Ex-TB patient*) katika halmashauri zote nchini ili waweze kutoa elimu, kuhamasisha jamii, kusimamia matibabu nyumbani na kutoa rufaa kwa walio na dalili kwenda kwenye vipimo. Aidha Kamati inasilitiza kwamba Serikali iendelee kutekeleza kampeni mbalimbali za uhamasishaji na upimaji wa TB na VVU kwa wananchi katika makazi duni yenye msongamano au sehemu za kazi zenye mazingira hatarishi kama vile maeneo ya migodi, magerezani na makazi duni, miji mikubwa na shule za bweni. Vilevile Kampeni maalumu zifanyike katika vijiji vyote vyenye idadi ya wagonjwa wengi wa Ukoma. Kampeni hii ihushe pia kufanya ufuutiliaji wa kaya zenye wagonjwa na watu wao wa karibu (*contact tracing*) na kutoa tiba kinga.

**(e) Wizara ya Afya**

**Mheshimwa Spika**, Kamati ilikutana na Wizara ya Afya ili kupokea taarifa kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa Yasiyoambukiza. Kamati ilielezwa sababu zinazochangia kuongezeka kwa magonjwa yasiyoambukiza ikiwa ni pamoja na ulaji usiofaa ambapo watu wengi wanatumia sana chakula cha wanga chenye sukari nyingi, kutofanya mazoezi, kutumia chumvi na sukari nyingi na imebainika kuwa, wananchi wengi hawana tabia ya kufanya mazoezi. Serikali kwa kutumia vyanzo mbalimbali inatarajiwa kutumia kiasi cha **Shilingi Trilioni 12.6** ndani ya kipindi cha miaka mitano ijayo ambayo ni sawa na wastani wa **trilioni 2.3** kila mwaka ili kupunguza **asilimia 15** ya vifo visivytarajiwa vinavyosababishwa na magonjwa yasiyoambukiza. Aidha Kamati imebaini kuwa, zaidi ya **asilimia 55.6** ya bajeti ya Wizara ya Afya imeelekezwa katika huduma za Saratani, Moyo, Mishipa ya Damu, Kisukari, Figo, Selimundu na magonjwa sugu ya mfumo wa hewa. Kwa ujumla bajeti hii imelenga zaidi katika upatikanaji wa bidhaa za afya hususani dawa na vifaa tiba ambavyo vinaongeza gharama kwa wananchi na taasisi zinazotoa huduma hizo. Takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) zinaonesha kuwa magonjwa haya yanakadiriwa kusababisha **asilimia 71** ya vifo vyote ulimwenguni.

**Mheshimiwa Spika**, tathmini ya haraka (*Rapid Assessment*) za matibabu zilizofanywa na Chama cha Kisukari nchini ili kutambua gharama ilibainika kuwa, zaidi ya shilingi **bilioni 290** zinahitajika kwa mwaka kama gharama za Dawa kwa wagonjwa **milioni 1.5** wenye kisukari na shinikizo la juu la damu pekee. Gharama hizi ni karibu sawa na asilimia **20** ya bajeti yote ya Wizara ya Afya. Changamoto ya huduma za upasauji wa Moyo au upandikizwaji figo ambazo zaidi ya Shilingi **Milioni 20** zinahitajika kwa ajili ya huduma hizo kwa mtu mmoja, huku gharama za usafishaji damu kwa wagonjwa wa figo zikifikia **laki 3** kwa "awamu" moja ambapo mgonjwa anahitaji kupatiwa huduma hizo angalau mara tatu kwa wiki na kufanya uhitaji wa angalau **Shilingi milioni moja** kwa kila wiki

sawa na **shilingi milioni 52** kwa mwaka kwa mgonjwa kwa maisha yake yote.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini na kutoa ushauri kuhusu mambo ya msingi yafuatayo:-

- (i) Kwa kuwa Magonjwa Yasiyoambukiza yamekuwa ni tishio kwa kwa afya za Watanzania wengi kwa zaidi ya **asilimia 73** na pengine kupelekea vifo; na Kwa kuwa, bado elimu ya Magonjwa Yasiyoambukiza hajjawafikia wananchi wengi; Kamati inaishauri Wizara ya Afya kuweka uratibu wa pamoja wa shughuli za udhibiti wa magonjwa yasiyoambukiza katika Sekta zote kushiriki kwenye mazoezi, lishe bora, athari za kimazingira na mipango miji, zinaratibiwa nje ya Sekta ya Afya. Pamoja na wananchi kuwa na uelewa mzuri wa baadhi ya visababishi, bado hali ya kimaisha, mila, desturi na umaskini umewazuia kutekeleza kwa vitendo baadhi ya mambo ambayo yangeweza kuwakinga dhidi ya magonjwa haya.
- (ii) Kuwepo na sheria ya uchangiaji wa gharama za matibabu ambayo ni kitu muhimu na inaweza kusaidia wananchi na Taasisi kuweza kumudu gharama zitokanazo na magonjwa haya. Uundwaji wa Sheria hii unaweza kusaidia wananchi na Serikali kuwekeza zaidi kwenye kinga na udhibiti wa magonjwa. Kamati inasitisiza Sheria itakayoundwa iendane na uanzishwaji wa Mfuko wa Afya (*Health Fund*) ambapo wananchi watachangia kutoka kwenye vyanzo mbalimbali. Aidha sheria hii ibainishe kodi ya nyongeza ya bidhaa hatarishi (*Sin Tax*) kama tumbaku, pombe, vyakula vyenye sukari nyingi na chumvi nyingi itatumika kwenye huduma za Afya kama sehemu ya kurejesha kwenye jamii ilioathirika, lakini pia mkakati wa kudhibiti uzalishaji holela wa bidhaa zenye madhara kiafya ili kupunguza uhatarishi.
- (iii) Kamati inashauri kufanyike uwekezaji mkubwa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ambapo itasaidia sana kusogezza huduma za Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza karibu zaidi na wananchi na hivyo kupunguza mzigo wa matibabu kwa mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla. Kwa kuwa gharama za uendeshaji ni kubwa kuliko kiasi ambacho Hospitali za Rufaa

za Mikoa (RRH) zinaweza kumudu, Serikali itenye ruzuku maalum ambazo ingeweza kupatikana kama tozo maalum zitokanazo na biashara ya bidhaa zinazochochea magonjwa haya kama Tumbaku, vinywaji vyenye sukari nyingi, pombe na sehemu ya Bima za Magari kama “social responsibility” kwa makampuni au bidhaa hizo.

(iv) Kuwepo na uratibu wa pamoja wa huduma za kinga dhidi ya Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza na uanzishwaji wa Mkakati wa “*Health in All Policies*” ambao unasisitiza kuwa suala la Afya lipewe kipaumbele katika kila Sekta linaweza kusaidia katika uratibu wa kinga na udhibiti wa magonjwa haya.

(v) Wizara ya Fedha na Mipango inashauriwa kutengeneza kifungu kinacholindwa kwa ajili ya huduma za kuzuia na kudhibiti magonjwa Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza. Aidha kipengele hiki kwa uwiano wa asilimia tofauti kitokee katika kila sekta ili sekta hizo zishiriki katika utekelezaji wa mikakati ya kitaifa inayoainishwa kutekelezwa katika sekta hizo.

#### **(f) Wizara ya Afya – (NACP)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto ambapo ilipokea na kujadili Taarifa kuhusu utekelezaji wa Makubaliano ya Kimataifa ya kuwakinga mabinti walio katika rika balehe dhidi ya VVU/UKIMWI. Kamati ilielezwa kwamba, Serikali ya Tanzania imeingia makubaliano mbalimbali ya kimataifa kwa lengo la kudhibiti VVU na UKIMWI kwa makundi mbalimbali hususani vijana. Moja ya makubaliano ya Kimataifa ambayo Tanzania imeingia ni pamoja na Kuwakinga Mabinti Walio katika rika balehe Dhidi Ya VVU “*Global HIV Prevention Coalition*” ya Mwaka 2017 yanayoratibiwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na UKIMWI (*UNAIDS*). Tanzania inakadiriwa kuwa asilimia 25 ya watu wote ni vijana (NBS - Sensa, 2012). Inakadiriwa kuwa wasichana walio na umri kati ya miaka 10 hadi 19 ni 12,439,677 ambao wamegawanyika katika umri wa miaka 10 hadi 14 ambao ni 6,743, 218 na miaka 15 hadi 19 ni 5,696,459. (NAlIA 2021/22 - 2024/25). Aidha kundi

hili linahitaji kupewa kipaumbele katika masuala ya kinga, tiba na matunzo ya VVU na UKIMWI kwa mustakabali wa Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya utafiti wa viashiria vya VVU na UKIMWI ya Mwaka 2016/17 inakadiriwa kuwa vijana rika balehe zaidi ya **108,361** wenyе umri kati ya miaka 10 hadi 19 wanaishi na VVU. (NAIA 2021/22 - 2024/25). Aidha, kiwango cha maambukizi kwa vijana wenyе umri wa miaka 15 hadi 24 wanachangia kiwango chao cha maambukizi kuwa **asilimia 40**, yaani 28,000 ya maambukizi yote kitaifa. (THIS 2016/17).

Kwa mujibu wa utafiti huo inakadiriwa kuwa **Vijana 23,000** hupata maambukizi mapya kwa mwaka ikiwa ni theluthi moja (**31%**) ya maambukizi yote **72,000** kwa mwaka nchini.

**Mheshimiwa Spika**, sababu kubwa ambazo ni hatarishi zinazochangia kuongezeka kwa maambukizi mapya kwa mujibu wa tafiti zinaonesha kuwa asilimia 9.1 ya wasichana rika balehe huanza ngono wakiwa na umri chini ya miaka 15 na wavulana asilimia 14.3 hufanya ngono na watu wasio rasmi (*High cohabiting behaviour in this age category*), uelewa mdogo kuhusu maswala ya elimu ya afya ya uzazi, VVU na UKIMWI, wazazi na walezi kutokuongea kwa uwazi kuhusiana na masuala ya afya ya uzazi, utumiaji wa pombe uliopitiliza, utumiaji wa dawa za kulevyia, kutokutumia kondomu "kuuza mechi kwa kutumia rim ya gari", ukatili wa kijinsia, vijana wa kiume kutokufanya tohara ambapo huchangia asilimia 60 ya maambukizi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba vijana ambao ndio nguvu kazi ya Taifa bado wapo nyuma katika 95 (3); ambayo 95 ya kwanza wapo nyuma katika suala la kupima na kufahamu afya zao; 95 ya pili wapo nyuma katika kutumia dawa za ARVs; na 95 ya tatu wapo nyuma katika kutumia dawa za kufubaza makali ya VVU. Kamati ilibaini na kutoa ushauri kuhusu mambo ya msingi yafuatayo:-

(i) Wizara kutenga bajeti ya vyanzo vya ndani ili kutekeleza afua ambazo ndio njia za msingi katika kujikinga na VVU na kuweka

mazingira wezeshi ya utoaji huduma rafiki za VVU na afya ya uzazi kwa vijana wa umri wa rika balehe;

(ii) Serikali iendelee kushirikiana na wadau mbalimbali kutoa mafunzo ya malezi bora ya afya ya uzazi kwa vijana walioko shuleni na nje ya shule na hatua za mabadiliko ya tabia. Aidha ni vizuri Wizara kuongeza utoaji wa huduma rafiki za afya kwa vijana rika balehe;

(iii) Kuwepo na mipango mikakati ya Wizara kuhusu kuboresha mitaala ya elimu ili kujumuisha elimu ya afya ya uzazi kuanzia elimu ya msingi. Aidha elimu iendelee kutolewa katika jamii na shuleni na Wizara inasitizwa kubuni kampeni na mikakati mbalimbali ili kuyafikia makundi mengi zaidi. Kwa sasa UKIMWI unaonekana kama kitu cha kawaida watu hawaogopi; hivyo elimu itolewe na maeneo ambayo redio na TV haziwafikii wananchi vitumile vikundi vya asili vinavyojihusisha na kutoa burudani ili elimu iwafikie watu hadi ngazi za vijiji.

(iv) Kamati inaishauri Serikali kwamba Sheria zote zinazokinzana na Wizara zingine zifanyiwe marekebisho ili ziweze kukidhi mahitaji kulingana na wakati uliopo pamoja na kupunguza vitendo vya ukatili wa kijinsia. Sheria ya Ndoa ifanyiwe mapitio haraka ili kupunguza maambukizi ya VVU;

(v) Kuwepo kwa dawati la jinsia kwenye shule za msingi na sekondari ili kusaidia watoto wanaopata athari za unyanyasaji wa kingono. Pia ni vema Wazazi wapewe elimu ya kuweza kuongea na watoto wao kuhusu mabadiliko ya mwili na elimu ya afya ya uzazi kwa watoto kwa kuwa watoto siku hizi wanawayahi kubalehe kuanzia darasa la nne.

### **(g) Wizara ya Madini**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana na Wizara ya Madini ili kujadii hali ya Virusi vya UKIMWI kwenye Migodi ya Tanzania ambapo ilibaini yafuatayo:-

(i) Takwimu za hali ya Maambukizi ya VVU na UKIMWI Migodini hazikuweza kubainisha ukubwa wa tatizo na hatua

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

zitakazochukuliwa za kukabiliana na janga hilo kwa kuzingatia muktadha wa 95 95 95;

(ii) Hakuna utaratibu wa kuhamasisha matumizi ya kondomu za kike pamoja na upatikanaji wake kwa ajili ya kuwezesha wanawake kuzitumia na kujikinga dhidi ya Maambukizi ya VVU; na

(iii) Kukosekana kwa mwongozo na mikakati ya namna ya kuratibu afua za UKIMWI katika maeneo ya Migodi pamoja na waratibu wa kusimamia ipasavyo Madawati ya UKIMWI katika kila Mgodi ambao wananchi watakuwa wanapata taarifa na huduma wanazostahili.

Kufuatia yaliyobainika, Kamati ilitoa ushauri kuhusu mambo ya msingi yafuatayo:-

(i) Kwa kuwa, wachimbaji wadogo ni kundi kubwa na linahitaji jicho la pekee; na kwa kuwa, kundi hili linawakilisha nguvu kazi kubwa ya Taifa; na kwa kuwa, kundi hili ni miongoni mwa kundi lenye maambukizi makubwa ya UKIMWI; na kwa kuzingatia hilo, Kamati inaishauri Wizara ya Madini na Tume ya Madini kushirikiana na wadau mbalimbali katika kupambana na kusimamia maambukizi ya magonjwa ya UKIMWI na Kifua Kikuu migodini ili kulinda afya za watu wanaojishughulisha na uchimbaji madini na biashara zingine kwenye maeneo ya wachimbaji.

(ii) Kamati inaishauri Wizara ya Madini iendelee kusimamia wamiliki wa migodi kuwa na mipango na mikakati ya kudhibiti maambukizi ya UKIMWI na TB migodini kwa kuwa, Sekta ya Madini inaendelea kukua kwa kasi na hatimaye kufikia mchango wa **asilimia 10** kwenye pato la Taifa ifikapo mwaka 2025 kama ilivyoelekezwa kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025; hivyo basi ni muhimu Serikali kuchukua hatua.

### **(h) Wizara ya Uvuvi**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Wizara ya Uvuvi Kamati ilibaini kwamba Mkoa wa Ruvuma

una kiwango kikubwa cha maambukizi (**asilimia 7.0**) ikifuatiwa na Mkoa wa Dar es Salaam 6.9%, Pwani 5.9%, Mara 4.5%, Kagera 4.8%, Mwanza 4.2%, Geita 4.7%, Mtwara 4.1%, Katavi 5.9% na Rukwa 6.2%. Aidha, Sababu zinazochangia kuwepo kwa kiasi kikubwa cha mambukizi ya VVU ni pamoja na wavulana na wasichana kuanza mahusiano ya ngono katika umri mdogo; kiwango kidogo cha matumizi ya kondomu kwa wanaume na wanawake wenye wapenzi zaidi ya mmoja; kiwango kidogo cha watu wanaojua hali zao za afya; wavuvi na jamii zinazowazunguka kutokuwa na tabia ya kupima na kufahamu afya zao; uelewa mdogo juu ya elimu ya UKIMWI na Kifua Kikuu katika mialo na kambi za wavuvi ambapo hupelekeea ngono zembe.

Kufuatia yaliyobainika, Kamati ilitoa ushauri kuhusu mambo ya msingi yafuatayo:-

(i) Wizara iuunde Kamati za Afya zitakazoshirikiana kutoa elimu rika katika mialo ya wavuvi wa samaki ili ziweze kufuatilia masuala yote yahuyohusu afya na elimu kuhusu kujikinga na maambukizi ya VVU na Kifua Kikuu. Aidha, msisitizo zaidi wa elimu kuhusu matumizi ya vifaa kinga itolewe ili kupunguza maambukizi katika maeneo hayo;

(ii) Wizara ya Afya kwa kushirikiana na TACAIDS kuongeza kasi ya kiwango cha upimaji wa VVU katika mialo na kambi za wavuvi hususani maeneo yote yenye kuambatana na ugumu wa mazingira ya shughuli za uvuvi. Aidha, Wizara ishirikiane na mamlaka nyingine za Serikali kwa kuandaa mikakati ya kuboresha mawasiliano na upatikanaji wa taarifa juu ya maambukizi ya VVU na Kifua Kikuu katika maeneo yote ya uvuvi na kambi;

(iii) Kwa kuwa, Wizara ya Uvuvi inafanya kazi kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Asasi za Kiraia katika kukabiliana na maambukizi ya UKIMWI na Kifua Kikuu; Kamati inashauri Sekta ya Uvuvi kuongezewa rasilimali zinazotengwa kwa ajili ya kuwasaidia waathirika wa UKIMWI katika maeneo ya uvuvi pamoja na sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika kufadhili masuala ya UKIMWI katika Sekta ya Uvuvi. Aidha, Wizara

ifanye sensa ya uvuvi katika maeneo ya uvuvi ili kubaini huduma zinazotolewa kuhusiana na Ugonjwa wa UKIMWI na Kifua Kikuu.

## **2.2 Ziara zilizofanywa na Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia masharti ya Kanuni ya (10)(c) ya Sehemu ya Tatu, Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, yanayoitaka Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Serikali kuhusu UKIMWI na Udhibiti wa Dawa za Kulevyta, Kamati hii ilifanya ziara ya kikazi katika Mikoa ya Njombe, Mbeya na Songwe tarehe 1 – 5 Machi, 2021. Lengo la ziara lilikuwa ni kutembelea na kukagua Afua zinazotekelezwa na Serikali pamoja na sekte binafsi katika ngazi mbalimbali za kitaasisi na jamii katika kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu, Ukoma na matumizi na biashara ya dawa za kulevyta.

## **2.3 Malengo ya Ziara katika maeneo yaliyotembelewa**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kutekeleza ratiba ya ziara, Kamati ilipokea na kujadili taarifa za maeneo/vituo ilivyovitembelea, pamoja na kushuhudia utoaji wa huduma mbalimbali za masuala ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Madawa ya Kulevyta.

Kwa ujumla taarifa zilizowasilishwa na kujadiliwa na ukaguzi uliofanywa ulilenga kubaini mambo makubwa yafuatayo: -

- a) Mwitikio wa UKIMWI kwa ujumla kwenye Halmashauri za Wilaya;
- b) Hali ya maambukizi ya VVU na upatikanaji wa dawa za kufubaza makali ya VVU pamoja na tiba ya magonjwa nyemelezi kwa muktadha wa malengo ya 95-95-95;
- c) Utekelezaji wa afua za UKIMWI mahala pa kazi mionganoni mwa Watumishi; mafanikio na changamoto;

- d) Udhibiti wa biashara na matumizi ya dawa za kulevy ya pamoja na huduma ya utoaji *Methadone* kwa watumiaji wa dawa za kulevy, Mafanikio na changamoto;
- e) Ukusanyaji, usimamizi na matumizi ya takwimu za Masuala ya UKIMWI katika ngazi mbalimbali za utoaji huduma za afya; na
- f) Shughuli zinazofanywa na Vikundi mbalimbli vya Watu wanaishi na VVU ( KONGA )

#### **2.4 Uchambuzi wa mambo yaliyobainishwa na Kamati wakati wa ziara**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati katika maeneo tajwa uliweza kubaini mambo ya msingi kuhusu mafanikio na changamoto zillizopo pamoja na hatua zinazochukuliwa. Kamati ilibua hoja pamoja na kutoa ushauri na mapendeleko ya hatua za kuchukua ili kuimarisha mapambano dhidi ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Dawa za Kulevy.

Baadhi ya mambo ya msingi ambayo Kamati ilibaini ni pamoja na yafuatayo: -

#### **a) Utoro wa kutumia dawa za kufubaza makali ya VVU kutokana na umbali wa vituo vya kutolea dawa**

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na changamoto kubwa ya watu wanaoishi na VVU kutoroka kutumia dawa za kufubaza makali ya VVU kwa kiasi kikubwa umechangiwa na umbali wa vituo vya kutolea dawa, gharama za usafiri na ukizingatia wateja wengi wanatoka nje ya Halmashauri zao, au wengine kukubali kutumia lakini kutoendelea na hivyo kutofubaza VVU. Wateja wengi hutoa taarifa zisizo sahihi kuhusu makazi yao na mawasiliano yao, vilevile kuwepo kwa unyanyapaa ambao husababisha mteja kwenda kuchukua dawa katika vituo vilivyoko mbali na maeneo anayoishi. Kamati inataka kufahamu ni hatua gani mahsusii zinachukuliwa kukabiliana na utoro huo? Ni maoni kwamba, Serikali kwa kushirikiana na

Halmashauri zote kufanya Ukaguzi Maalum (*Special Survey*) ili kubaini sababu za hali hiyo kisha kushauri hatua madhubuti za kuchukua. Kuwepo na mikakati madhubuti ya kuendelea kutoa elimu kuhusu umuhimu wa ufuasi mzuri wa dawa na kuhudhuria kliniki kwa wakati.

**b) Tabia Hatarishi za Maambukizi ya VVU mionganoni mwa Vijana, Matumizi ya vidonge vya kuzuia mimba (P2) mionganoni mwa wasichana**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini ongezeko la matumizi ya vidonge vya kuzuia mimba mionganoni mwa wasichana hasa wenye umri katika miaka 10 - 24. Licha ya kuwa na lengo la kuzuia mimba, matumizi ya vidonge hivi ambavyo vimekuwa vikiuzwa kwa bei ya chini yamekuwa yakichochea maambukizi ya Virusi vya UKIMWI. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, baadhi ya wasichana wamekuwa wakiogopa zaidi mimba kuliko maambukizi ya VVU na hivyo wamekuwa wakitumia vidonge vya P2 kama njia mbadala ya kuzuia mimba na kuacha kutumia kondomu ambazo zingewakinga dhidi ya maambukizi ya VVU, magonjwa ya ngono na mimba zisizotarajiwa.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukabiliana na tabia hii hatarishi Kamati inashauri kwamba, wakati wa mauzo ya dawa za kuzuia mimba (P2) ni vizuri zikauzwa pamoja na kondomu kwa lazima ili kuwawezesha wasichana kuwa na tabia ya kutumia kondomu hizo bila ya kunyanyapaliwa. Aidha, uzoefu unaonesha iwo watakuwa na hizo kondomu basi wasichana wengi watazitumia ili kupunguza maudhi na madhara ya dawa za kuzuia mimba.

**Mheshimiwa Spika**, dawa hizi huharibu mzunguko wa hedhi na mfumo wa *hormone* za wasichana. Mara nyingi wasichana wakitaka wavulana watumie kondomu huwa wanapata tatizo la upatikanaji wake kwa kuwa maduka ya dawa yenye kuuza kondomu yanakuwa yamefungwa wakati wa usiku. Matumizi ya kondomu huwa hayapendwi na wavulana kwa kuwa wanajua wasichana watatumia dawa za kuzuia mimba ambapo huchangia kasi kubwa ya tabia

hatarishi inayopelekea kupata maambukizi mapya kwa vijana hususani wasichana. Ununuaji wa kondomu na dawa ya P2 kwa pamoja utasaidia kupunguza unyanyapaa mionganoni mwa vijana na kusaidia kufanya utafiti wa maambukizi ya VVU kwa wasichana.

c) Matumizi ya Pombe Kali Mionganoni mwa Vijana (*double double*)

**Mheshimiwa Spika**, licha ya Tanzania kuwa na Sheria ya Vileo na sheria nyingine ambatanishi, lakini matumizi holela ya pombe zenye asilimia kubwa ya kilevi yamekithiri mitaani na kusababisha madhara makubwa kwa jamii hasa vijana ambao ni nguvu kazi ya Taifa. Pamoja na juhudhi kubwa na kazi nzuri iliyofanywa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa kushirikiana Serikali ya kupiga marufuku matumizi ya pombe za pakti maarufu kama **VIROBA** hivi sasa imebainika kuwa vijana watumiaji wa pombe hizo wamegeukia kwenye chupa ndogo za plastiki zinazouzwa kwa bei nafuu *double kick* *yenye ujazo 200 ml na kilevi 43%, hanson's choice ujazo 200 ml na kilevi 40%, ananas cuca yenye ujazo 200 ml na kilevi 40%, rivella yenye ujazo 200 ml na kilevi 40% na gordon's yenye ujazo 200 ml na kilevi 43%*. Matumizi ya pombe kali mionganoni mwa vijana yamekuwa yakisababisha kubadilika kwa tabia, kuongezeka kwa ajali za barabarani na kuathirika kwa ini na figo. Pombe hii vilevile husababisha mihemuko kwa vijana kuwa na hamu ya kujamiihana, inahisiwa kuwa pombe hizi huwekewa madawa ya kulevyaa au dawa za kuongeza nguvu za kiume. Aidha, matumizi ya pombe mionganoni mwa vijana yamekuwa yakichochea kasi ya maambukizi ya VVU kwa sababu ya kutotumia kondomu wakati wa kujamiihana kutokana na ulevi.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa vijana wanaotumia dawa za kupunguza makali ya VVU (ARV), pombe hupunguza ufanisi wa dawa hizo. Kutokana na ulevi baadhi ya vijana huacha kutumia dawa katika vipindi na muda walioachagua baada ya kulewa na kuharibu ratiba ya dozi zao hivyo kuchangia kushuka kwa kinga mwilini na kushindwa kufubaza virusi kwa wakati. Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka

za kupiga marufuku utengenezaji wa pombe zenyé kilevi kikubwa ambazo zinawekwa kwenye chupa ndogo za plastiki. Aidha, kiwango cha chini kiwe miligramu 300 ili kupunguza matumizi mabaya ya pombe hizi ambapo zinauzwa hata sehemu za washona viatu na maeneo yasiyo rasmi.

**d) Mchango wa Baraza la Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (NACOPHA) katika mapambano dhidi ya UKIMWI**

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na ushirikiano mzuri kati ya NACOPHA kuitia Konga zake na Halmashauri katika kuratibu na kuhamasisha upimaji wa VVU, utoaji wa elimu ya ufuasi sahihi wa dawa za kupunguza makali ya VVU (ARV), upimaji wa uwangi wa virusi mwilini, kwa kushirikiana na viongozi wa dini hutoa elimu ya kupinga ukatili wa kijinsia kwa watoto na wanawake, hufuatilla watoro wa dawa (*LTFU*) na kuwarudisha kwenye huduma za tiba na matunzo na utoaji wa elimu ya lishe bora kwa WAVIU na jamii kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, Baraza kwa kushirikiana na Konga hutoa elimu ya kupinga unyanyapaa na ubaguzi kwenye jamii kwa kuzingatia miongozo ya Serikali pamoja na kutoa elimu kwa watu wanaoishi na VVU ya kuijunga kwenye huduma ya uzazi wa mpango. Kwa mfano, Konga ya Halmashauri ya Mji wa Njombe imefanikiwa kuwarudisha takribani watu **960** waliopotea kwenye huduma ya matunzo na dawa (*LTFU*), kati yao wanawake **635** na wanaume **325**. Vilevile imefanikiwa kuwarudisha kwenye huduma jumla ya wanafunzi **94**, kati yao wanaume ni **39** na wanawake **55** katika shule tatu za msingi na tano za sekondari.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza NACOPHA kuitia Konga ya Halmashauri ya Mji wa Njombe kwa kufanikiwa kuwarudisha kwenye huduma ya tiba na matunzo baadhi ya WAVIU waliopotea. Kamati inaamini kwamba, Baraza kwa kushirikiana na Serikali upo uwezekano mkubwa wa kufikia malengo tarajija ya Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI wa 95 95 95 ifikapo mwaka 2025 na kufikia 0 0 0 ifikapo mwaka 2030.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Baraza kupitia Konga ya Halmashauri ya Mji wa Njombe kufanikiwa kuwarudisha wateja kwenye tiba na matunzo; Konga ya Halmashauri ya Mji wa Mbeya nayo imefanikiwa kuhamasisha uundwaji wa vikundi wezeshi 7 ambavyo vinafanya shughuli mbalimbali za kiuchumi na kujiongezea kipato ambacho huwasaidia kujikimu kimaisha na kuboresha afya zao kama ufugaji wa kuku, nguruwe, kilimo cha matunda, kilimo cha chakula, ufugaji wa nyuki, ushonaji, biashara ndogo ndogo na uatikaji wa miche ya parachichi. Kamati inapongeza juhudzi zinazofanywa na Baraza kupitia Konga za kuhakikisha WAVIU wanajikwamua kiuchumi na kupunguza tatizo la ajira. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kupitia Halmashauri zote kuangalia uwezekano wa kuwasaidia kupata mikopo yenyereba nafuu kupitia mabenki, taasisi za fedha na kupitia mikopo ya Halmashauri ya Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu.

**e) Msongamano wa Wafungwa Gerezani na Maambukizi ya Kifua Kikuu**

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na msongamano wa wafungwa na mahabusu katika Magereza mengi nchini ambapo mazingira halisi ya vyumba vyake havina mzunguko wa kutosha wa hewa, hali inayoweza kuchochea maambukizi ya Ugonjwa wa Kifua Kikuu kwa haraka. Pamoja na hatua za awali za upimaji na kuanzishiwa dawa kwa wanaokutwa na Kifua Kikuu, Kamati inataka kufahamu ni hatua gani mahsusizi zinachukuliwa kwa waliopo magerezani kiasi cha kuyafanya magereza yasiwe na wagonjwa wa Kifua Kikuu. Aidha, yapo masuala ya jumla kwenye Jeshi la Magereza yanayohitaji kuangaliwa kwa haraka na kwa makini kama ifuatavyo:-

(i) Msongamano wa mahabusu ni mkubwa sana magerezani kuliko hata idadi ya wafungwa ambao ndio hasa wanatakiwa kutunzwa na Jeshi la Magereza. Hali hii ni hatarishi kwa maambukizi ya kifua kikuu na hata upatikanaji wa takwimu zinazohusu masuala ya UKIMWI na kutotoa picha halisi ya maambukizi ili kuwezesha kufanya maamuzi sahihi

ya hatua za kuimarisha afua zinazochukuliwa. Serikali iangalie uwezekano wa kuzifanya marekebisho sheria ili kutenganisha mahabusu na wafungwa badala yake mahabusu wahifadhiwe na Jeshi la Polisi na wafungwa wahifadhiwe na Jeshi la Magereza. Mabadiliko hayo ya sheria vilevile yaruhusu mahabusu hao kufanya kazi kwa muda wote wanaposubiri hukumu za kesi zao au ushahidi kukamilika. Utaratibu huo utasaidia pia kupunguza idadi ya mahabusu wanaohifadhiwa gerezani kwa miaka mingi sana na kesi zao kuchukua muda mrefu kutokana na ushahidi kuchelewa kukamilika na hivyo kuliongezea Jeshi la Magereza mzigo wa kuwatunza kwani mahabusu hawaruhusiwi kufanya kazi yoyote ya uzalishaji tofauti na wafungwa.

(ii) Endapo Jeshi la Polisi litaruhusiwa kutunza mahabusu, kuna uwezekano mkubwa wa kuongezeka kwa uangalifu katika kutambua ni watuhumiwa wepi wapelekwe mahabusu na ni wepi masuala yao yatatuliwe bila kuwekwa mahabusu.

**f) Mahusiano ya Ugonjwa wa Homa ya Ini na VVU kwa Waraibu wa Dawa za Kulevyta**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea Kliniki ya *Methadone* ya Hospitali ya Kanda Mbeya na kubaini kuwa hakukuwa na takwimu zilizozungumzia ugonjwa wa Kifua Kikuu na Homa ya Ini B na C kwa waraibu wanaotumia dawa za kulevyta wanaoishi na VVU. Aidha, kumekuwepo na changamoto ya walioathirika na dawa za kulevyta kuwa na magonjwa mengine licha ya uraibu ikiwemo magonjwa ya akili, Kifua Kikuu na UKIMWI ambayo huathiri kasi ya upataji nafuu na kudhoofisha tiba na ushiriki mdogo katika kuchangia Pato la Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwepo maambukizi ya juu sana ya ugonjwa wa homa ya ini mionganoni mwa waraibu wa dawa za kulevyta. Hali hii ni hatarishi kwa jamii nzima. Katika taarifa yao ilielezwa kuwa jumla ya **waraibu 345** wanatumia dawa ya *methadone* kila siku, kati ya hao **wanaume ni 329** sawa na **asilimia 95.4** na **wanawake 16** sawa na **asilimia 4.6**. Hivyo, Kamati inasisitiza kuwa, pamoja na

kutoa huduma za *methadone* kwa waraibu ni muhimu kliniki zote kuwepo na takwimu na kuimarisha utoaji huduma za Kifua Kikuu na Homa ya Ini kwa uzito unaostahili.

### **(i) Mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea Mkoa wa Songwe katika Halmashauri ya Mji wa Tunduma-Mombasa, takwimu zinaonesha kiwango cha maambukizi ya VVU ni takribani watu **43,819** wanaoishi na VVU. Aidha, jumla ya WAVIU **39,267** sawa na **asilimia 89.6** ya watu wanaokadirisha kuambukizwa VVU wanatambua hali zao za maambukizi na **asilimia 99** ya wote waliobainika kuambukizwa VVU wapo katika tiba na matunzo ya ARVs.

Mkoa uliweza kuwafikia wanaume wapatao **57,202** sawa na **asilimia 42.5** na wanawake wapatao **77,394** sawa na **asilimia 57.5** kwa huduma ya upimaji, ambapo kati yao **wanaume 1,883** sawa na **asilimia 40.15** na **wanawake 2,806** sawa na **asilimia 9.84** waligundulika kuwa na maambukizi ya VVU na wote waliunganishwa katika huduma ya tiba na matunzo. Kundi lenye kiwango kikubwa cha maambukizi ni umri kuanzia miaka 25 - 49 kwa **asilimia 37.5** na kundi la umri kati ya 20 - 24 kwa **asilimia 11.4**. Kamati imebaini uwepo mwamko na mwitikio mdogo wa wanaume kujitokeza kupima na kufahamu hali zao za maambukizi. Hali hii inachangia kurudisha nyuma kasi ya mapambano dhidi ya UKIWMV/VVU. Ni maoni ya Kamati kuwa ili kufikia malengo tarajiwa ya Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI wa 95 95 95 ifikapo mwaka 2025 na kufikia 0 0 0 ifikapo mwaka 2030, mkoa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wanaojihusisha na mapambano ya UKIMWI waweke mikakati madhubuti ya kuhakikisha wanaume wanapima.

**Mheshimiwa Spika**, imebainika kwamba, pamoja na Mkoa wa Songwe kuwa mionganini mwa mikoa yenye kiwango cha juu cha upatikanaji wa chakula, bado kuna kiwango ya kiwango kikubwa cha udumavu kwa **watoto 28,080**, ambayo ni sawa na **asilimia 43.3** ya watoto wenye umri chini ya miaka 5. Kamati inaiomba Serikali ihakikishe elimu ya lishe

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

inaendelea kutolewa katika vituo vyote vya tiba na matunzo juu ya umuhimu wa kula vyakula mchanganyiko kwa kuzingatia makundi matano ya vyakula vilivyopo katika jamii zetu. Aidha, ni vema upimaji wa hali ya lishe ufanyike kwa wateja wa vituo vya tiba na matunzo kwa wateja wanaogundulika na changamoto ya lishe na chakula dawa. Vilevile uwepo ufuatilaji kwa kuwatumia watoa huduma ngazi ya jamii na kutumia mtandao wa WAVIU wanaojishughulisha na shughuli za kilimo na ufugaji ili kuongeza kipato na kudumu kwenye mlo kamili. WAVIU kwa kutumia Konga zao waendelee kusaidiana kwa kupeana elimu ya lishe na kuuziana vyakula wanavyozalisha kwa bei nafuu ili watu wengi zaidi waweze kumudu.

### **(ii) Ziara katika Kliniki ya Methadone ya Hospitali ya Kanda Mbeya**

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 5 Machi, 2021 Kamati ilifanya ziara katika Kliniki ya Methadone Hospitali ya Kanda Mbeya ambayo ililenga kukagua shughuli zinazofanywa na Kliniki hiyo. Kliniki ya Methadone Mbeya ilianzishwa mwaka 2017 kwa lengo la kutoa tiba kwa waraibu wa dawa za kulevyta ili kuimarisha na kuboresha afya pamoa na maisha yao kwa ujumla. Huduma hii hutolewa kwa kushirikiana na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Vilevile hushirikiana na Wadau wa Maendeleo wa Shirika la Walter Reed (WRP-T), ambaye ndiye mfadhili mkuu katika kliniki na huduma za kijamii katika kufanya maandalizi na rufaa kwa waraibu wa dawa za kulevyta. Aidha, kituo hushirikiana na taasisi zisizo za kiserikali katika kutoa huduma za utengamao ambazo ni KIHUMBE na SETA.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Februari, 2021, Kliniki hii ilikuwa na jumla ya **waraibu 345** ambao wanatumia dawa ya *methadone* kila siku; kati ya hao **wanaume ni 329** sawa na **asilimia 95.4** na wanawake 16 sawa na asilimia 4.6. Kliniki pia hutoa huduma ya dawa za ARVs, magonjwa ya akili, Kifua Kikuu, magonjwa ya zinaa na magonjwa nyemelezi. Vilevile kliniki ina jumla ya wateja wenye maambukizi ya UKIMWI 45,

ambao ni sawa na asilimia 13 na wanapata huduma ya tiba na matunzo. Wapo wagonjwa 5 wa Kifua Kikuu ambao ni sawa na asilimia 1.2 ya wagonjwa wote katika kliniki.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza juhudini zinazofanywa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Wadau mbalimbali wa Mkoa wa Mbeya hususani Walter Reed (*WRF*) katika mapambano dhidi ya dawa za kulevyta. Kwa kuwa suala la mapambano ya dawa za kulevyta ni mtambuka na linahitaji kuunganisha nguvu za wadau mbalimbali ili kuimarisha na kuboresha afya na maisha ya waraibu waweze kujikwamua kiuchumi baada ya kupona wasijiingize katika masuala ya uhalifu tena; ni maoni ya Kamati kuwa wakati umefika sasa wa Serikali kushirikiana na asasi zisizo za kiserikali kubuni namna sahihi na ya kimkakati ya kuwafikia watu walioathirika na dawa za kulevyta ili iwe njia rahisi ya kuwatambua, kuwashirikisha, kuwasaidia na kuwawezesha kufanya shughuli nyingine za kiuchumi. Kwa kufanya hivyo tutajenga Taifa ambalo ni imara.

### **(iii) Ziara katika Mkoa wa Tanga na Arusha**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ziara ya kutembelea vituo vya kutolea tiba kwa waraibu wa dawa za kulevyta (MAT-CLINICS), nyumba za upataji nafuu (Sober Houses) pamoja na asasi za kiraia zinazowaibua, kuwandaa na kuwapeleka waraibu wa dawa za kulevyta katika vituo vya matibabu. Kamati ilitembelea maeneo yafuatayo Mkoani Tanga: Kituo cha Huduma ya Methadone Hospitali ya Bombo, Asasi ya Gift of Hope, Nyumba za upataji nafuu za Gift of Hope, Course on Recovery Foundation na Tanga Drug Free. Mkoani Arusha Kamati ilitembelea maeneo yafuatayo: Kituo cha Huduma ya Methadone Hospitali ya Mount Meru, Asasi ya YCR, Nyumba za upataji nafuu za Tanzania Sobriety Change Foundation (Arusha Recovery), Tanzania Sobriety Change Foundation (Njiro Recovery) na Tanzania Sobriety Change Foundation (Meru Recovery). Ziara hii ilifanyika tarehe 13 – 17 Septemba, 2021.

**Mheshimiwa Spika**, katika ziara hii Kamati ilibaini Maafisa Ustawi wa Jamii hawazitembelei mara kwa mara nyumba za upataji nafuu ili kujionea changamoto zinazozikabili. Vilevile uwepo wa changamoto ya ukosefu wa fedha za kuendeshea vituo na elimu ya stadi za kazi kwa waraibu wanaotunzwa katika nyumba hizo. Aidha, uwepo wa nyumba za upataji nafuu zinazomilikiwa na watu binafsi katika Mikoa ya Tanga na Arusha kunasababisha gharama kubwa za matunzo ya waraibu ambapo jamii nyingi hushindwa kuzimudu na hivyo kushindwa kuwapeleka katika nyumba hizo.

**Mheshimiwa Spika**, ni maoni ya Kamati kuwa Halmashauri kwa kushirikiana na Serikali waweke mkakati wa pamoja wa kupata maeneo maalum kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za upataji nafuu (*Sobber Houses*) na ujenzi wa sehemu za ujasiriamali katika mikoa hiyo kwa kuwa inaongozwa kuwa na waraibu wengi zaidi kuliko mikoa milgine.

#### **(iv) Ziara katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini**

**Mheshimiwa Spika**, Shirika la HJF Medical Research International (HJFMRI) - Walter Reed Program Tanzania ni mionganini mwa Wadau wa Maendeleo, wanaoshirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutekeleza afua mbalimbali za kuutokomeza UKIMWI katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Taasisi hii inafadhiliwa na Mpango wa Dharura wa Rais wa Marekani wa kukabiliana na UKIMWI (PEPFAR) kupitia Walter Reed Army Institute of Research (WRAIR) - Idara ya Ulinzi ya Marekani (US. DoD).

**Mheshimiwa Spika**, mnamo mwezi Septemba, 2021, Kamati kwa kushirikiana na Shirika la Walter Reed (W-RPT) lilitanya ziara katika Mikoa ya Mbeya, Songwe, Rukwa na Katavi kwa lengo la kujifunza na kuona utekelezaji wa Miradi ya afua za UKIMWI, Kifua Kikuu, Dawa za Kulevyta inayofanywa na Shirika hili. Aidha, kuona mafanikio na changamoto ili kuishauri Serikali katika afua zote zinazohusu UKIMWI, Kifua Kikuu na Dawa za Kulevyta.

Katika ziara hiyo Kamati ilibaini mambo mbalimbali yafuatayo ambayo Serikali kwa kushirikiana na wadau wanaweza kutafuta ufumbuzi wa changamoto hizo:-

- (a) Kuwepo kwa idadi kubwa ya maambukizi ya VVU katika Mkoa wa Mbeya asilimia 9.3, Wilaya ya Kyela asilimia 4.2.
- (b) Kuwepo kwa kiwango kikubwa cha wanaume wenye umri mkubwa ambao hawajafanya tohara ambapo huchangia kwa kiasi kikubwa maambukizi ya UKIMWI kwa asilimia 60 na uwezekano wa kumwambukiza mwenza saratani ya shingo ya kizazi.
- (c) Kuwepo kwa idadi kubwa ya Watoto wanaozaliwa na kuishi na maambukizi ya VVU katika Mikoa hiyo.
- (d) Uwepo wa utoro wa dawa na kutohudhuria kliniki na hivyo kushindwa kufubaza virusi nya UKIMWI.

## **2.5      Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2019/2020 na Mchakato wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri ilioutoa kuhusu Bajeti za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Taasisi hizo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Taarifa hizo ziliwasilishwa Bungeni kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu Bunge Toleo la Juni, 2020 mnamo tarehe 29 Machi, 2021.

### **2.5.2    Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania - Fungu 92**

#### **a) Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika**, upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge ni jambo la msingi katika kufanikisha utekelezaji wa mpango wa bajeti unaopitishwa na Bunge. Kwa kuzingatia

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

hilo, Kamati ilichambua taarifa ya upatikanaji wa fedha ili kujiridhisha iwapo fedha imepatikana kama ilivyokusudiwa. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa Uchambuzi wa Kamati unaonesha kwamba hadi kufikia mwezi Februari 2021 Fungu 92, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania ilikuwa imepokea kiasi cha **asilimia 71.4** ya Bajeti yake. Uchambuzi zaidi ulionesha kuwa pamoja na kuwa bajeti ya miradi ya maendeleo ilikuwa ni **asilimia 64** ya Bajeti yote ya Tume hii, fedha zilizopatikana kwa ajili ya Maendeleo zilizidi uwiano huo kwa kufikia **asilimia 71** ya fedha zote zilizopokewa. Takwimu hizo, zinaonekana katika Jedwali Namba 1.

### **Jedwali Na 1: Ulingenisho wa uwiano wa bajeti na Upatikanaji wa fedha hadi Mwezi Februari, 2021**

BAJETI ILYCIDHINSHWA			UPATIKANAJI WA FEDHA HADI FEBRUARI		
Mchanganuo	kiasi	%	Mchanganuo	kiasi	%
Jumla	7,689,447,000.00	100	Jumla	5,488,985,666.62	100
Kawaida	2,788,708,000.00	36	Kawaida	1,588,246,666.62	29
Maendeleo	4,900,739,000.00	64	Maendeleo	3,900,739,000.00	71
Ndani	1,000,000,000.00	20	Ndani	3,900,739,000.00	100
Nje	3,900,739,000.00	80	Nje	0	0

### **Chanzo: Taarifa ya Tume (TACAIDS) ya Makadirio ya Matumizi ya Mwaka 2021/2022**

**Mheshimiwa Spika**, licha ya uwiano huo wa fedha zilizopatikana kwa ajili ya miradi ya maendeleo kuonekana mkubwa, fedha za nje kwa ajili hiyo, zimechukuwa asilimia 100 ya fedha za maendeleo zilizopatikana. Tafsiri ya matokeo hayo ni kuwa, Tume haikupata kiasi chochote cha fedha za ndani za maendeleo. Hali hii inaoenesha utegemezei mkubwa wa kibajeti kwa ajili ya miradi ya maendeleo inayohusu mapambano dhidi ya UKIMWI. Ni maoni ya Kamati kuwa uwiano uliojitekeza kuhusu upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida ni jambo linalohitaji kurekebishwa ili kujimarishe katika kupambana na janga la UKIMWI kwa mustakabali wa taifa.

### **2.5.3 Upatikanaji wa Fedha za Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyा (DCEA) - Fungu 91**

**Mheshimiwa Spika**, Fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyा (Fungu 91), zilitarajiwа kuwezesha mapambano na udhibiti wa dawa za kulevyा. Aidha, Taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati zilionesha kuwa kati ya shilingi **9,033,345,000.00** zilizoidhinishwa na Bunge, Mamlaka imepokea jumla ya shilingi **5,308,281,428.00**. Kiasi kilichopokewa ni sawa na asilimia 59 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Mamlaka hii kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati unaonesha kuwa Bunge liliidhinisha asilimia 68 ya bajeti ya Mamlaka kwa ajili ya Uendeshaji na asilimia 32 ya bajeti kwa ajili ya mishahara. Ulinganisho umeonesha kuwa, kiasi cha fedha zillizopatikana kwa ajili ya mishahara ni asilimia 23 ya fedha iliyopokewa, na kiasi kilichopokewa kwa ajili ya uendeshaji ni asilimia 77 ya fedha yote iliyopokewa. Tafsiri ya matokeo hayo ni kuwa uzito uliotolewa na Bunge kuhusu uwiano kati ya bajeti ya mishahara na bajeti ya uendeshaji unatofautiana na uzito wa uwiano unaojitekeza katika kiasi cha fedha zilizopokewa kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 2.

#### **Jedwali Na. 2: Ulinganisho wa Bajeti iliyoidhinishwa na kiasi kilichopokewa**

BAJETI ILIYOIDHINISHWA			FEDHA ILIYOPOKEWA		
Mchanganuo	Kiasi	% Jumla		Kiasi	% Jumla
Uendeshaji	6,167,415,000.00	68		4,111,610,000.00	23
Mishahara (PE)	2,865,930,000.00	32		1,196,671,428.00	77

**Chanzo: Taarifa ya Mamlaka Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2021/2022**

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

### **2.6      *Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi***

#### **2.6.1    Tume ya Kudhibiti UKIMWI**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2021/2022 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kuititia **Fungu 92** inatarajia kukusanya maduhuli ya jumla ya **shilingi 5,000,000.00**, ambayo yanatarajiwa kapatikana kutokana na uuzaaji wa vifaa chakavu na tozo kutokana na matumizi ya Ukumbi wa Mikutano.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa makadirio ya matumizi katika Mwaka wa Fedha wa 2021/2022 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania - **Fungu 92** inaombewa jumla ya shilingi **4,317,818,000**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 1,389,470,000** sawa na **asilimia 32** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na shilingi **2,928,348,000** sawa na **asilimia 68** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Uchambuzi wa Kamati umeonesha kuwa makadirio haya yameongezeka kwa shilingi **139,640,000.00** ambayo ni sawa na **asilimia 8.9** ikilinganishwa na fedha zilizoidhinishwa na Bunge pamoja na uhamisho wa fedha kwa mwaka 2020/2021 kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 3.

**Jedwali Na. 3 Ulinganisho wa Bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka 2020/21 na Makadirio ya matumizi kwa mwaka 2021/22**

BAJETI ILIYOIDHINISHWA 2020/21			MAKADIRIO 2021/22		
Mchanganuo	kiasi	%	Mchanganuo	kiasi	%Tofauti
Jumla	7,689,447,000.00	100	Jumla	4,317,818,000	-44
Kawaida	2,788,708,000.00	36	Kawaida	2,928,348,000	+ 5
Maendeleo	4,900,739,000.00	64	maendeleo	1,389,470,000	-72

**Chanzo: Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta kuhusu Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/21**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa matumizi ya kugharamia miradi ya maendeleo, uchambuzi umeonesha kuwa bajeti inayoombwaa imepungua kwa asilimia 72 ambacho ni kiasi

kikubwa cha tofauti. Kwa kawaida fedha zinazotumika kugharamia miradi ya maendeleo kwa Tume hii hutumika kwa ajili ya shughuli mbalimbali zinazohusu mapambano dhidi ya Janga la UKIMWI. Kwa uchambuzi huu, ni wazi mpango wa shughuli hizo umeacha mambo mengi yaliyopangwa kwa mwaka wa fedha unaoisha kwa kiwango cha asilimia 72. Jambo hili lina hatari kubwa kwa ustawi wa wananchi ambao ndio lengo la serikali kwa mujibu wa Ibara ya 8 (1) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa maoni ya Kamati, hali hii yenye athari hasi katika mapambano dhidi ya UKIMWI inafaa kurekebishwa.

#### **2.6.2 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy - Fungu 91**

**Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa makadirio ya matumizi kwa ajili ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 umeonesha kuwa kiasi kinachoombwa ni **Shilingi 8,529,789,000.00** ambapo **Shilingi 6,167,415,000** sawa na **asilimia 72** ya fedha yote inayoombwa ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi **2,362,382,000**, sawa na **asilimia 28** ni Mishahara. Makadirio haya yamepungua kwa kiasi cha shilingi **503,548,000** sawa na **asilimia 6** ikilinganishwa na bajeti ya Fungu hili iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/2021 kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 4 la Taarifa hii.**

**Jedwali Na. 4 Ulinganisho wa Bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka 2020/2021 na Makadirio ya Matumizi kwa mwaka 2021/2022**

BAJETI ILIYOIDHINISHWA 2020/21			MAKADIRIO 2021/22		
Mchanganuo	kiasi	%	Mchanganuo	kiasi	% Tofauti
Jumla	9,033,345,000.00	100	Jumla	8,529,789,000.00	6
Mishahara	2,865,930,000.00	32	Mishahara	362,382,000.00	87
OC	6,167,415,000.00	68	OC	6,167,415,000.00	0
Maendeleo	0	0	Maendeleo	0	-72

**Chanzo: Taarifa ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy kuhusu Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022**

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi umebainisha kuwa bajeti ya mishahara imepungua kwa kiasi kikubwa kufikia pungozo la asilimia 87. Tofauti hiyo ni kubwa na ilitoa mashaka kwa Kamati. Kwa mujibu wa Kanuni ya 117 ya Kanuni za Kudumu za Bunge (3)(2), Kamati ya Bajeti ilipitia na kuchambua masuala muhimu ya kibajeti yaliyojitokeza katika Fungu 91 ambapo majibu ya Serikali ni kuwa kiasi cha shilingi **503,548,000** kimezingatiwa katika Fungu 21 – Hazina kupitia Kasma ya *Salary Adjustment* ambazo zitatumika kulipa Makamishna wa Tume wanaotarajiwa kuteuliwa wakati wa utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2021/2022.

### **2.7 Mafunzo na Semina kwa Wajumbe wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Februari, 2021 hadi Januari, 2022, Kamati kwa kushirikiana na Wadau wa Masuala ya UKIMWI, Kifua Kikuu, Dawa za Kulevyaa na Magonjwa Yasiyoambukiza, walitoa mafunzo mbalimbali yaliyolenga kuwajengea uwezo Wajumbe kuhusiana na utekelezaji wa afua hizi hapa nchini. Mafunzo haya yalitolewa kwa njia ya semina kutoka kwa Taasisi zifuatazo: -

#### **(a) Semina kuhusu shughuli mbalimbali zinazofanywa na Shirika la Walter Reed**

**Mheshimiwa Spika**, Shirika la HJF Medical Research International (HJFMRI) - Walter Reed Program Tanzania ni mionganoni mwa Wadau wa Maendeleo, wanaoshirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kutekeleza afua mbalimbali za kuutokomeza UKIMWI katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Taasisi hii inafadhiliwa na Mpango wa Dharura wa Rais wa Marekani wa kukabiliana na UKIMWI (PEPFAR) kupitia Walter Reed Army Institute of Research (WRAIR) - Idara ya Ulinzi ya Marekani (US. DoD).

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 2 Agosti, 2021, Shirika hili liliendesha semina kwa Wajumbe kuhusu shughuli mbalimbali wanazozifanya katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ya Mbeya, Songwe, Rukwa na Katavi. Katika mafunzo haya Wajumbe walipata fursa ya kufahamu utekelezaji wa afua

zote za mapambano dhidi ya VVU, ikiwa ni pamoja na huduma za kinga na tiba na afua ya tohara ya hiari kwa wanaume ili kufikia malengo ya UNAIDS ya 95-95-95 ya kutokomeza UKIMWI ifikapo 2030.

**Mheshimiwa Spika**, Wajumbe wanaipongeza Walter Reed kwa jitihada wanazofanya kupunguza maambukizi ya VVU. Aidha ni ushauri wa Kamati kuwa huduma hii itolewe pia katika Mkoa wa Ruvuma ambao ni mojawapo ya Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kwa sababu mila na desturi zao zinafanana kama inavyofanyiwa Mikoa mingine ya Nyanda hiyo. Vilevile Mkoa wa Dodoma nao ufikiwe kwa kuwa hivi sasa ni Makao Makuu ya Nchi na kuna mwingiliano mkubwa wa watu kutokana na Serikali kuhamishia shughuli zake mkoani hapa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefurahishwa sana na shughuli mbalimbali zinazofanywa kwa ari kubwa na Shirika hili kwa Wananchi wa mikoa iliyotajwa na kuwaomba Wadau wengine wa Maendeleo kuiga mfano mzuri unaofanywa na Walter Reed. Kamati imeshuhudia Shirika hili likifanya kazi kwa pamoja na Viongozi wa Serikali, Wabunge, Viongozi wa Dini na Vijana na makundi mbalimbali.

**(b) *Semina kuhusu Mfuko wa Udhagini wa Udhibiti wa UKIMWI (AIDS Trust Fund - ATF)***

**Mheshimiwa Spika**, Wajumbe wa Kamati walipewa mafunzo kuhusu Mfuko wa Udhagini wa Kudhibiti wa UKIMWI Tanzania (*The Tanzania AIDS Trust Fund - ATF*) ambao ulianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 6 ya Mwaka 2015 kufuatia mabadiliko ya Sheria Na. 22 ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*Tanzania Commission for AIDS (Amendment Act)*). Katika mafunzo haya Waheshimiwa Wajumbe walielezwa kuwa Mfuko huu ulianzishwa kwa lengo la kuongeza mchango wa Serikali na taasisi binafsi katika suala zima la UKIMWI na changamoto zake. Ilielezwa kuwa asilimia 60 ya fedha za Mfuko huu zinatumika kununulia dawa za ARVs kupunguza makali ya VVU/UKIMWI kwa watu wazima, wanawake na watoto. Wajumbe walifahamishwa kuwa vyanzo vyta fedha

vyo Mfuko huu ni pamoja na Bajeti ya Serikali, chanzo cha uwekezaji wa muda mfupi, ubunifu wa Bodi na michango ya taasisi mbalimbali pamoja na watu mmoja mmoja. Malengo matatu yaliwekwa wakati wa kuanzisha Mfuko huu kwanza ni kuongeza mchango wa fedha za ndani za mwitikio wa UKIMWI kutoka asilimia 7 mwaka 2015 mpaka asilimia 30 mwaka 2018; kuongeza mchango wa sekta binafsi katika mapambano dhidi ya UKIMWI kutoka asilimia 8 mwaka 2015 mpaka asilimia 15 mwaka 2018; na kuongeza mchango wa Serikali katika mapambano dhidi ya UKIMWI kufikia shilingi bilioni 300 kwa mwaka. Aidha, Wajumbe walielezwa kuwa Bodi inaweza kutoa fedha za ruzuku kwenye maeneo yenye changamoto kwa wakati husika.

**Mheshimiwa Spika**, Kupitia semina hii Wajumbe walipata uelewa juu ya mwenendo wa ruzuku ya fedha za Mfuko inayotolewa ambapo unafuata utaratibu ufuatao: asilimla 60 ununuzi wa dawa za ARVs, dawa za magonjwa nyemelezi, vifaa na bidhaa za maabara, kondomu na kadhalika; asilimia 25 kwa shughuli za kinga, elimu, mawasiliano kuhusu kinga na magonjwa nyemelezi na asilimia 15 ya mwisho kwa ajili ya mazingira wezeshi kama utafutaji fedha, ufanyaji tathmini na uendeshaji wa Mfuko wenyewe.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa Mfuko huu unakabiliwa na changamoto ya kukosa chanzo cha uhakika cha fedha ni maoni ya Kamati kuwa Serikali itenye fedha za ndani za kutosha kwa ajili ya kuuendesha Mfuko huu. Kamati inaendelea kusisitiza kuwa kutegemea fedha za wafadhili kununulia dawa ni tatizo kwani tayari wameshajitoa kufadhili baadhi ya maeneo kama ununuzi wa dawa za *septrine*. Aidha dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI (ARVs) bado zinanunuliwa na wafadhili hali ambayo inatishia maisha ya Watanzania hasa ukizingatia kuwa wanaweza kugoma kuendelea kutufadhili.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri kwamba Serikali iongeze fedha za UKIMWI kutoka vyanzo vya ndani kwa mfano inaweza kuchukua asilimia moja kutoka kwenye tozo ya simu iende kwenye Mfuko huu. Vilevile uwekwe utaratibu

utakaosaidia sekta binafsi kuchangia kiasi cha mapato yao kwenye Mfuko kupunguza athari ya UKIMWI katika jamii inayotuzunguka. Semina hii ilifanyika tarehe 11 Aprili, 2021 katika Ukumbi Na. 20 uliopo Jengo la Utawala Annex, Bungeni Dodoma.

(c) *Semina kuhusu matumizi ya Dawa ya Phyte Exponent*

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 24 Aprili, 2021 Taasisi ya Prime Afro Health Care ilipata fursa ya kutoa elimu kwa Wajumbe kuhusu matumizi ya dawa ya Phyte Exponent iliyofanyika katika Ukumbi Na. 33, Jengo la Utawala Annex, Bungeni Dodoma. Kamati ilielimishwa kuwa *Phyte Exponent* imetengenezwa na baadhi ya virutubisho ambavyo vimewekwa vitu vinavyofanya kazi kama dawa. Katika mafunzo haya Wajumbe walielezwa kuhusu faida inayopatikana na dawa hii ambayo inasaidia sana kuponya wagonjwa wanaosumbuliwa na UVIKO 19 pamoja na maradhi mengine mbalimbali. Wajumbe vilevile walipata uelewa juu ya faida ya dawa ya *Phyte Exponent* ambapo ilielezwa kuwa kutokana na tafiti mbalimbali zilizofanywa kwa baadhi ya madaktari na wananchi wa kawaida waliokuwa wameathirika na Virusi vya UKIMWI, baada ya kutumia dawa hii majibu yalionesha hawakuwa tena na maambukizi ya VVU mwilini mwao.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri kuwa ni muhimu kuwepo na mkakati wa kupunguza gharama za uzalishaji ili Watanzania wengi zaidi waweze kuitumia. Vilevile Kamati maoni kuwa kijengwe kiwanda hapa hapa nchini ambacho kitazalisha dawa hii na kuisambaza kwa wananchi wengi zaidi. Suala la kuwaelimisha wananchi kabla ya kuitumia dawa hii ni la muhimu sana ili kuepusha madhara yanayoweza kutokea kwa kutofahamu namna ya utumiaji.

(d) *Semina kuhusu Wasichana Balehe na Wanawake Vijana*

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 28 Juni, 2021 semina kuhusu Mradi wa Kusaidia Wasichana Balehe na Wanawake Vijana ilitolewa na TACAIDS kwa Wajumbe wa Kamati. Wajumbe

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

walielimishwa kuwa Mradi huu unatekelezwa katika Halmashuri 12 za Mikoa ya Dodoma (5), Singida (3) na Morogoro (4) unaowafikia Wasichana Balehe na Wanawake Vijana walio ndani na nje ya shule wenye umri wa miaka 10 - 24. Katika semina hiyo ilielezwa kuwa Tanzania inakadiriwa kuwa na idadi ya watu wanaokaribia milioni 60. Asilimia 63 wako chini ya umri wa miaka 25 na kundi la vijana balehe wa miaka 10 – 19 wako asilimia 23. Wasichana balehe na wanawake vijana nchini wanakabiliwa na changamoto mbalimbala za kijamii na kiuchumi ikiwemo za umaskini katika kaya na jamii kwa jumla. Wajumbe walipata wasaa wa kuelewa matatizo yanayowakabili wasichana walioko masomoni kutoka katika kaya maskini ikiwemo kuacha shule mapema; kukosa elimu ya ufundi stadi; kukosa stadi za maisha; kupata watoto au mimba katika umri mdogo; ndoa za utotoni; maambukizi ya VVU; na ukatili wa kijinsia na unyanyasaji.

Wajumbe walielimishwa kuwa Lengo Kuu la Mradi ni kuwasaidia wasichana walioko shulenii kuhitimii elimu na walio nje ya mfumo wa elimu kuwezesha kijamii na kiuchumi ili kujikimu kimaisha wakiwa salama dhidi ya VVU na UKIMWI. Takwimu za Utafiti wa Viashiria vya VVU Tanzania (THIS, 2017) zinaonesha kwamba vijana (wenye umri wa miaka 15 - 24) wanachangia asilimia 40 ya maambukizi mapya kila mwaka na ambapo asilimia 80 ya maambukizi hayo kwa vijana yapo kwa wasichana.

**Mheshimiwa Spika**, ni ushauri wa Kamati kuwa Mradi huu ufile katika Mikoa yote Tanzania ambayo hajafikiwa kwa mfano Mkoa wa Lindi ambaa unakabiliwa na tatizo la uongezeko kwa mimba za utotoni, utoro shulenii na kadhalika. Vilevile Mkoa wa Kigoma nao unakabiliwa na umaskini na mimba za utotoni. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha Mradi huu unawafikia pia watoto wa kiume kwani nao wanahuusika kwenye maambukizi ya VVU na wengine hawafiki shulenii wanawekwa kwenye majumba.

### **(e) Semina Kuhusu Makuzi ya Mtoto**

**Mheshimiwa Spika**, UNICEF ilifanya mafunzo kuhusu makuzi ya mtoto tarehe 26 Juni, 2021 iliyofanyika katika Ukumbi

*Namba 20, Jengo la Utawala Annex uliopo Bungeni Dodoma. Wajumbe walipata fursa ya kufahamu juu ya madhara ya lishe duni katika miaka miwili ya mwanzo ya mtoto kuwa inaweza kukwamisha ukuaji wa viungo na ubongo na hivyo kuwa na madhara yasiyorekebishika kielimu, ajira na mustakabali wake. Wakati tumebaini hilo kwa miaka kadhaa sasa kumekuwepo na maendeleo kidogo katika kuwapatia watoto lishe bora na salama. Kufuatia mlipuko wa COVID-19 hali ya lishe inaweza kuwa mbaya zaidi kwa kuwa baadhi ya familia zimelazimika kupunguza ununuzi wa vyakula vyenye lishe kutokana na hali ngumu ya maisha. Kamati ilielezwa kuwa uchambuzi uliofanyika katika nchi 91 umebaini kuwa ni nusu tu ya watoto wenge umri wa kuanzia miezi 6 hadi 23 ndio wanapatiwa idadi ya milo inayotakiwa kwa siku huku theluthi moja wanapatiwa kiwango kidogo cha mlo ili waweze kuishi.*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapendekeza kuwa ili watoto wapate lishe bora ni vyema Serikali, Wahisani, Mashirika ya Kiraia na Wadau wa Maendeleo washirikiane kubadili mifumo ya vyakula, afya na hifadhi ya jamii kwa kuchukua hatua kama vile kuongeza fursa ya kupata na kumudu vyakula vyenye lishe ikiwemo matunda, mboga za majani, mayai, nyama, samaki na vile vilivyoongezewa virutubisho kwa kuwekea motisha uzalishaji, usambazaji na uuzaaji wake. Halikadhalika kutekeleza sheria na kanuni za kitaifa za kulinda watoto dhidi ya vyakula visivyo na lishe bora na kutokomeza mbinu hatarishi za kibashara zinazolenga watoto na familia zao. Aidha mbinu mbalimbali za mawasiliiano zitumike kuhamasisha matumizi ya vyakula salama na vyenye lishe ili wazazi na watoto waweze kutambua umuhimu wa vyakula hivyo.

**(f) Semina Kuhusu Magonjwa Yasiyoambukiza**

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 15 Mei 2021, Wajumbe walipatiwa mafunzo kuhusu magonjwa yasiyoambukiza yaliyotolewa na Taasisi ya TanCDA yaliyolenga kuwajengea uwezo juu ya madhara yatokanayo na magonjwa ya kisukari, shinikizo la damu, saratani na kiharusi. Katika mafunzo haya ilielezwa kuwa Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (WAVIU) ni kundi

ambalo lipo hatarini sana kuathiriwa na maradhi haya. Vilevile ilielezwa kuwa chanzo kikuu cha maradhi haya ni ulaji usiofaa ambapo watu wengi wanatumia sana chakula cha wanga chenye sukari nyingi, kutofanya mazoezi, kutumia chumvi na sukari nyingi. Imebainika kuwa wananchi wengi hawana tabia ya kufanya mazoezi hali ambayo inachangia sana miili kuathirika kwani mazoezi husaidia kutoa jasho na hivyo kupunguza kiasi kikubwa sana cha chumvi mwilini kwa njia ya jasho. Elimu zaidi inabidi itolewe kwa wananchi waelewe umuhimu wa kula vizuri, kufanya mazoezi na kupima afya Mara kwa Mara na watakapogundulika ugonjwa wowote waanzishiwe dawa mapema.

**Mheshimiwa Spika**, ulevi uliopitiliza, ulaji wa vyakula usiofaa na uzito mkubwa unachangia ongezeko la magonjwa yasiyoambukizwa. Ni ushauri wa Kamati kuwa ili kupunguza tazizo hill ni vema bei ya vilevi ikaongezeka ili kupunguza matumizi ya vilevi hivyo. Vilevile Kamati inasisitiza elimu kuhusu ulaji wa chakula unaofaa itolewe kwa wananchi kuanzia shule za msingi mpaka vyuo vikuu. Kwa kuwa Kamati imebaini sukari huchangia kiasi kikubwa cha ongezeko la uzito mwilini, ni ushauri wa Kamati kuwa Serikali ione umuhimu wa kutoa elimu kwa jamii kuhusu madhara yatokanayo na matumizi ya sukari.

Ni maoni ya Kamati pia kuwa kuwepo na Tume Maalum itakayoshughulikia magonjwa yasiyoambukiza kama ilivyo TACAIDS kwa UKIMWI ambayo itaweka miongozo ya kusimamia maradhi haya na utekelezaji wake ushuke mpaka chini ngazi ya Halmashauri. Vilevile suala la mazoezi ni muhimu hivyo iwepo miongozo katika shule zetu wanafunzi watakiwe kufanya mazoezi na watumishi pia wafanye mazoezi.

**(g) Semina kuhusu Kifua Kikuu (TB) na Ukoma**

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Afya ilifanya mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati kwa lengo la kuwaelimisha kuhusu ugonjwa wa kifua kikuu na ukoma ambapo mafunzo hayo yaliyofanyika tarehe 4 na 5 Aprili, 2021. Mafunzo haya yalihu elimu kuhusu madhara ya kifua kikuu na ukoma na jinsi yanavyoenea. Mwezeshaji alieleza kuwa TB ni ugonjwa sugu

wa kuambukiza kwa njia ya hewa unaosababishwa na vimelea aina ya bacteria ambavyo kitaalam hujulikana kama "*mycobacterium tuberculosis*" pindi mgonjwa anapokohoa, kupiga chafya au kuongea. Ugonjwa huu huathiri sehemu zote za mapafu na husambaa kwa haraka sana katika mwili. Kutogunduliwa mapema kwa wagonjwa na kuwekwa kwenye matibabu kunasababisha ugonjwa huu kuenea kila mahali.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa dalili za mtu anayehisiwa kuwa na vimelea vya TB ni pamoja na kukohoa, homa, kupungua uzito na kutokwa jasho jingi usiku. Mgonjwa ambaye anaugua TB au TB sugu na hajaanza matibabu anaweza kuambukiza watu 10 mpaka 20 kwa mwaka na zaidi ya watu bilioni mbili (30%) duniani wana maambukizi ya TB. Hapa nchini inakadiriwa zaidi ya watu milioni 18 wana maambukizi ya TB ambapo kati ya wagonjwa wanaogunduliwa kila mwaka asilimia 16 ni watoto. Matibabu ya TB sugu yamefupishwa kutoka miezi 18 – 24 hadi 9 kuanzia Januari, 2018. Ni ushauri wa Kamati kwamba, kiundwe chombo maalum kama ilivyo TACAIDS kwa masuala ya UKIMWI ambacho kitakuwa kinashughulikia masuala ya TB tu. Kwa mfano Afrika Kusini kuna chombo maalum kinachoongozwa na Waziri Mkuu kinachoshughulikia masuala ya TB kwa sababu kuna maambukizi makubwa sana.

## **SEHEMU YA TATU**

### **3.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia shughuli zilizotekelizwa na Kamati kuanzia Januari 2021 – Januari 2022 kumekuwa na changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika Wizara/Taasisi zinazosimamiwa na Kamati hii ambazo Kamati inazitolea maoni na ushauri ufuataao: -

#### **3.1 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS)**

**(a) Upatikanaji wa Fedha za ndani kwa ajili ya Afua za UKIMWI**

**KWA KUWA**, Kamati imebaini kwamba Bajeti ya Maendeleo ya fedha za ndani ya TACAIDS kwa mwaka 2020/2021

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

ilitengewa **Shilingi 1,000,000,000** na 2021/2022 imeendelea kutengewa kiasi hicho hicho cha Shilingi 1,000,000,000;

**NA KWA KUWA**, bado Tume hii inahitaji kuongezewa fedha zaidi ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu;

**NA KWA KUWA**, suala la utekelezaji wa afua za UKIMWI linahitaji nguvu nyngi sana za Serikali, Wananchi na Wadau;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inaishauri Serikali iweke mikakati mahususi ya kutenga fedha zake za ndani kwa ajili ya udhibiti wa UKIMWI badala ya kutegemea fedha za wafadhili.

### **(b) Mfuko wa Kudhibiti UKIMWI (ATF)**

**KWA KUWA**, Serikali ilianzisha Mfuko wa UKIMWI wa Taifa mwaka 2015 kwa ajili ya kuongeza nguvu za kupambana na UKIMWI hapa nchini;

**NA KWA KUWA**, Pamoja na malengo mengine Mfuko huu ulilenga kuwezesha nchi kuwa na uwezo wa kifedha wa kupambana na UKIMWI;

**NA KWA KUWA**, Mfuko huu bado una changamoto ya kutojitosheleza kifedha kwa kukosa vyanzo endelevu vya mapato kwa ajili ya mwitiko wa afua za UKIMWI na kutegemea fedha za wafadhili kwa asilimia 90;

**NA KWA KUWA**, lengo la Mfuko huu ni kuhakikisha Serikali inatenga fedha zake za ndani kwa ajili ya kupambana na janga hili;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kuliangalia suala hili kwa uzito unaostahili ili Mfuko wa ATF uweze kuwa na vyanzo vya mapato vya ndani. Aidha, Serikali ifikie mahali ipate ufumbuzi wa upatikanaji wa fedha hizo. Kwa kufanya hivyo, tutapunguza utegemezi mkubwa wa fedha za wafadhili ambapo kwa sasa fedha hizo zimeambatana na masharti magumu. Ni mapendekezo ya Kamati kuwa, mtazamo wa kufikia malengo ya 95 95 95 ifikapo mwaka 2030 inamaanisha wigo wa uhitaji wa dawa

za ARVs unazidi kuongezeka wakati wafadhili wanapungua; hivyo hatuna budi kujipanga ili tusifikie wakati ambapo mahitaji yatazidi uwezo.

**(c) Wanaume kutojitokeza kupima VVU na kufanya tohara KWA KUWA,** Kamati imebaini takwimu zinaonesha wanaume wenye umri mkubwa bado hawajitokezi kupima na kutambua hali ya afya zao za maambuki ya UKIMWI ikilinganishwa na wanawake;

**NA KWA KUWA** imebainika kuwa ufanyaji wa tohara hupunguza kwa kiasi kubwa maambukizi ya VVU kwa asilimia 60 na kusaidia uwezekano wa kuambukiza saratani ya mlango wa shingo ya kizazi kwa akina mama;

**NA KWA KUWA,** Malengo ya Umoja wa Mataifa yanataka kila nchi kufikia 95 – 95 – 95 ifikapo mwaka 2030;

**KWA HIYO BASI,** Kamati inashauri kuwa Serikali kuhakikisha juhudhi zinafanyika za kutoa elimu kuhusu umuhimu wa wanaume kujitokeza kupima afya zao na kufanya tohara.

**(d) Ukatili wa Kijinsia**

**KWA KUWA,** vitendo vya ukatili wa kijinsia vimeendelea kuwepo na kuleta athari ndani ya familia na jamii kwa ujumla;

**NA KWA KUWA,** tarehe 25 Novemba, 2021 Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya uzinduzi wa maadhimisho ya kampeni ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia Tanzania yaliyofanyika Kitaifa katika Mkoa wa Dar es Salaam yenye Kaulimbiu isemayo “EWE MWANANCHI: KOMESHA UKATILI WA KIJINSIA SASA”;

**NA KWA KUWA,** Zaidi ya asilimia 20 ya wanawake wa umri kati ya miaka 15 hadi 29 wanafanyiwa ukatili wa kijinsia hapa nchini;

**NA KWA KUWA,** Kamati imebaini kuwa ukatili wa kijinsia huchangia kuwepo kwa maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwa Wanawake na Wasichana na Wanaume na Wavulana;

**KWA HIYO BASI**, Ni ushauri wa Kamati kuwa Serikali kuelimisha, kukemea na kuchukua hatua kwa pamoja ili kupinga aina zote za ukatili wa kijinsia katika jamii ambazo hupelekea maambukizi ya virusi nya UKIMWI. Aidha, Serikali iendelee kutekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto wa Mwaka 2017/18 hadi 2021/2022) unaolenga kupunguza kiwango cha ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto katika jamii yetu kwa asilimia 50 ifikapo 2022.

**(e) Maambukizi ya VVU kwa vijana**

**KWA KUWA**, takwimu zinaonesha kuwa vijana 80 huambukizwa VVU kwa siku, kwa mwezi ni vijana 2400, sawa na maambukizi 28,800 kwa mwaka; (THIS 2016/17).

**NA KWA KUWA**, vijana wenyе umri wa miaka 15 hadi 24 wanachangia maambukizi kwa asilimia 40 ya maambukizi yote kitaifa ambapo kiwango cha maambukizi kwa wasichana asilimia 2.1 na wavulana ni asilimia 0.6;

**NA KWA KUWA**, Sababu kubwa zinazochangia kuongezeka kwa maambukizi mapya kwa wasichana rika balehe ni kuanza ngono wakiwa na umri chini ya miaka 15 na wavulana asilimia 14.3 hufanya ngono na watu wasio rasmi;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kushirikiana na wadau, wazazi na walezi kutoa mafunzo ya malezi bora ya afya ya uzazi kwa vijana walioko shulen na nje ya shule na hatua za mabadiliko ya tabia. Aidha Wizara kuongeza utoaji wa huduma rafiki za afya kwa vijana rika balehe walioko shulen.

**(f) Maambukizi kutoka kwa mama kwenda mtoto**

**KWA KUWA**, Kamati imebaini bado yapo maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto ambapo kati ya watoto 1,800,000 wanaozaliwa hapa nchini kwa mwaka watoto wapatao 10,000 wanazaliwa na maambukizi ambayo ni sawa na asilimia 0.6;

**NA KWA KUWA**, Watoto wanaozaliwa na maambukizi ya VVU wanaendelea kukua na kuishi katika jamii ambapo familia huendelea kuwa na usiri kutowaambia watoto wanasumbuliwa na maradhi gani pindi wanapougu magonjwa nyemelezi;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali kuweka mikakati madhubuti ya kutoa elimu ya maambukizi kwa akina mama wajawazito pindi wanapofikisha wiki 12 baada ya ujauzito wapime virusi vya UKIMWI, kupima VVU wiki 14 baada ya kujifungua na kuhamasisha kupima VVU wakati wananyonyesha.

### *3.2 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyaa*

#### **(a) Umuhimu wa Serikali kutenga fedha kwa ajili ya bajeti ya Miradi ya Miradi ya Maendeleo**

**KWA KUWA**, kwa kuzingatia majukumu ya Mamlaka ya Kudhibiti na kupambana na Dawa za Kulevyaa ambayo ni udhibiti wa matumizi ya dawa za kulevyaa, kufanya uelimishaji kwa jamii na kufanya afua za kupunguza madhara ya dawa za kulevyaa kwa jamii;

**NA KWA KUWA**, jukumu la pili na la tatu ni ya kimkakati zaidi ikilinganishwa na jukumu la kwanza, na utekelezaji wake unahitaji rasilimali fedha za kukidhi ukubwa wa tatizo la athari za biashara na matumizi ya dawa za kulevyaa, ilihali bado elimu kuhusu matumizi na madhara ya dawa za kulevyaa haijawafikia wanajamii kwa kiasi kikubwa;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri Serikali kuiwezesha Mamlaka hii kwa kutenga fedha kwenye Bajeti yake kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Fedha hizo zitaiwezesha Mamlaka kuimarisha programu za kuhamasisha na kutoa elimu ya madhara ya biashara na matumizi ya dawa za kulevyaa kwa wananchi ili waweze kushiriki kikamilifu katika kupambana na kudhibiti dawa za kulevyaa kwani vita hii ni ngumu na endelevu. Hivyo ni wakati mwafaka kwa Serikali kuchukua hatua za haraka kuhakikisha Mamlaka na wadau wengine wa dawa za

kulevyo wanatoa elimu ya kutosha kwa jamii kuanzia ngazi ya Kaya, Vijijini, Kata, Wilaya, Mkoa na Taifa zima kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kufanya hivyo, kutasaidia kujenga mfumo bora wa kudhibiti na kupambana na dawa za kulevyo nchini pamoja na kujenga jamii ya Watanzania isiyotumia dawa za kulevyo na kutoshiriki katika biashara na matumizi ya dawa za kulevyo. Kwa hali ilivyo, dawa za kulevyo ni tatizo linaloongezeka kwa kiwango kikubwa katika jamii yetu siku hadi siku na linaathiri vijana wengi ambao ndiyo nguvu kazi ya Taifa.

### *3.3 Mapambano ya Dawa za Kulevyo*

**KWA KUWA**, tafiti zinaonesha kuwa zipo mbinu mbalimbali zinazotumika kusafirisha dawa za kulevyo ikiwa ni pamoja na kubebea mizigo ya kawaida na kuficha ndani ya bidhaa nyingine kama magunia na viroba na hata kwa kutumia maiti;

**NA KWA KUWA**, jukumu la kupambana na dawa za kulevyo linahitaji ushirikiano na wadau mbalimbali ikiwemo sekta ya usafirishaji wa anga, barabara, reli na bandari;

**NA KWA KUWA**, utekelezaji wake unaonekana kuwa mgumu kutokana na ukosefu wa vitendea kazi vya kisasa mfano katika baadhi ya viwanja vya ndege kukosa mashine za ukaguzi wa abiria na mizigo kikamilifu;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inaishauri yafuatayo:-

- i) Serikali iwekeze katika vitendea kazi vya kisasa vitakavyorahisisha zoezi zima la upekuzi na ukamataji wa dawa za kulevyo zinazoingizwa nchini kupitia njia mbalimbali lakini pia vitakavyolinda afya za watumishi;
- ii) Wizara ishirikiane na vyombo vya dola katika kuandaan kampeni endelevu ambazo mbali na kuwepo vifaa madhubuti itawajengea uwezo watumishi kutumia kikamilifu vifaa na teknolojia ya kisasa katika kudhibiti dawa za kulevyo;

- iii) Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) kuweka mikakati maalum ya kuhakikisha wanaboresha na kusimamia viwango vya usalama kwa kufunga mashine za kisasa za (*X - Ray Backscatter*) zenyе uwezo wa kung'amuа dawa za kulevya kwenye mizigo ya abiria, vituo vya malori ya mizigo; na
- iv) Uwepo wa mbwa maalum wa kuweza kunusa na kubaini madawa ya kulevya;

### *3.4 Kutokuwepo kwa Sera ya Dawa za Kulevya*

**KWA KUWA**, Mpaka sasa Tanzania haina Sera ya Taifa ya Kupambana na Dawa za Kulevya ambayo kwa umuhimu wake ingeimarisha mapambano yaliyopo dhidi ya matumizi na biashara ya dawa za kulevya;

**NA KWA KUWA**, Sera ina umuhimu mkubwa katika kuweka misingi na mwelekeo wa Taifa katika vita dhidi ya dawa za kulevya kwa ujumla wake.

**KWA HIYO BASI**, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya mchakato wa kuandaa Sera ya Taifa ya kudhibiti na kupambana na Dawa za Kulevya Nchini.

### **3.5 Kifua Kikuu (TB)**

**KWA KUWA**, Kifua kikuu ni ugonjwa unaoenezwа kwa njia ya hewa kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine;

**NA KWA KUWA**, Kamati imebaini kwamba bado wananchi wengi hawana elimu na uelewa wa kutosha kuhusu ugonjwa huu na hivyo kupelekea mambukizi kuenea na vifo kutokea;

**NA KWA KUWA**, utafiti umebainisha kuwa mgonjwa wa Kifua Kikuu akiwahi hospitali kupatiwa matibabu ugonjwa huu unatibika na kupona;

**KWA HIYO BASI**, ni ushauri wa Kamati kuwa Serikali iendelee kutekeleza kampeni mbalimbali za uhamasishaji na upimaji

wa TB na VVU kwa wananchi katika makazi duni yenye msongamano au sehemu za kazi zenye mazingira hatarishi kama vile maeneo ya migodi, magerezani, miji mikubwa na shule za bweni.

### **3.6 Magonjwa Yasiyoambukiza**

**KWA KUWA**, Kamati imebaini kwamba bado wananchi wengi hawana uelewa wa kutosha kuhusu magonjwa yasiyoambukiza;

**NA KWA KUWA**, zipo sababu zinazochangia kuongezeka kwa magonjwa yasiyoambukiza ikiwa ni pamoja na ulaji usiofaa ambapo watu wengi wanatumia sana chakula cha wanga chenye sukari nyingi, kutofanya mazoezi, kutumia chumvi na sukari nyingi;

**NA KWA KUWA**, Magonjwa Yasiyoambukiza yamekuwa ni tishio kwa kwa afya za Watanzania wengi kwa zaidi ya asilimia **73** na pengine kupelekea vifo;

**NA KWA KUWA**, Kamati imebaini kuwa zaidi ya **asilimia 55.6** ya bajeti ya Wizara ya Afya hutumika katika huduma za Saratani, Magonjwa ya Moyo, Magonjwa ya Mishipa ya Damu, Kisukari, Figo, Selimundu na magonjwa sugu ya mfumo wa hewa;

**NA KWA KUWA**, bado elimu ya Magonjwa Yasiyoambukiza hajjawafikia wananchi wengi;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inashauri yafuatayo:-

i) Wizara ya Afya, iweke uratibu wa pamoja wa kuhakikisha shughuli za udhibiti wa magonjwa yasiyoambukiza katika Sekta zote kushiriki kwenye mazoezi, lishe bora, athari za kimazingira na mipango miji, ziratibiwe nje ya Sekta ya Afya;

ii) Pamoja na wananchi kuwa na uelewa mzuri wa baadhi ya visababishi bado hali ya kimaisha, mila, desturi na umaskini, umewazuia kutekeleza kwa vitendo baadhi ya mambo

ambayo yangeweza kuwakinga dhidi ya magonjwa haya. Hivyo ipo haja ya kuendelea kutoa elimu kwa jamii;

iii) Tume Maalum itakayoratibu masuala ya Magonjwa Yasiyoambukiza kwa ajili ya ku-*address NCDs* ianzishwe na hii ni kwa sababu Magonjwa Yasiyoambukiza yanaongoza kwa kuwa chanzo kikubwa cha vifo nchini, visababishi vyta vifo vyake ni mtambuka na matibabu ya yake ni ya gharama kubwa sana. Tume hii itarahisisha uratibu na usimamizi wa afua mbalimbali; na

iv) Mpango Mkakati na Mwongozo wa kufanya mazoezi vishushwe kwenye ngazi za chini kwa ajili ya utekelezaji.

## **SEHEMU YA NNE**

### **4.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, nakushukuru kwa mara nyingine kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu yake hadi kufikia Januari, 2022.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Nd. Nenelwa Joyce Mwihambi, kwa ushirikiano wake kwa Kamati. Namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge – Nd. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi – Nd. Gerald Magili, Makatibu wa Kamati hii, Nd. Happiness Ndalu, Nd. Pamela Pallangyo na Nd. Asia Msangi, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge, Ajira, Vijana na Walemavu - Mhe. Jenista Mhagama, Mb na Naibu Mawaziri; Ummy Khamis Nderiananga na Patrobas Katambi. Vilevile Kamati inapenda kumpongeza Waziri mpya wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge, Ajira, Vijana na Walemavu, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana. Pamoja na hao Kamati inampongeza Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania - Dkt. Leonard Maboko na

Kamishna wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta - Kamishna Jenerali Gerald Kusaya na Watendaji wote wa Tume na Mamlaka kwa ushirikiano walioipatia Kamati kwa kipindi cha mwaka mzima ambapo waliweza kufika mbele ya Kamati kila walipohitajika na kutoa ufanuzi wa masuala mbalimbali kwa umahiri mkubwa.

**Mhesimiwa spika**, Naomba pia kuwashukuru na kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya sambamba na watendaji wao wote kwa kutoa ushirikiano mkubwa wakati wote wa shughuli za kamati na namna wanavyoonesha dhamira ya katatua matatizo yanayowakabili Watanzania.

**Mhesimiwa Spika**, Kwa namna ya pekee napenda niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa uchapakazi wao wakati wote wa kutekeleza majukumu ya Kamati kwa mwaka mzima. Wajumbe wamefanya kazi kubwa katika kuhakikisha Kamati inaisimamia na kuishauri Serikali ipasavyo. Napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa majina kama ifuatavyo: -

- |   |              |
|---|--------------|
| 1. Mhe. Fatma Hassan Toufiq, Mb -               | Mwenyekiti   |
| 2. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb -        | M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Amandus Julius Chinguile, Mb -          | Mjumbe       |
| 4. Mhe. Tecla Mohamedi Ungele, Mb -             | Mjumbe       |
| 5. Mhe. Dkt. Christine Christopher Mnzava, Mb - | Mjumbe       |
| 6. Mhe. Neema Gerald Mwandabila, Mb-            | Mjumbe       |
| 7. Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo, Mb-            | Mjumbe       |
| 8. Mhe. Justin Lazaro Nyamoga, Mb -             | Mjumbe       |
| 9. Mhe. Dkt. Pius Stephen Chaya, Mb-            | Mjumbe       |
| 10. Mhe. Francis Leonard Mtega, Mb -            | Mjumbe       |
| 11. Mhe. Oliver D. Semuguruka, Mb -             | Mjumbe       |
| 12. Mhe. Grace Victor Tendega, Mb -             | Mjumbe       |
| 13. Mhe. Kassim Hassan Haji, Mb -               | Mjumbe       |
| 14. Mhe. Hawa Mchafu Chakoma, Mb -              | Mjumbe       |
| 15. Mhe. Neema Kichiki Lugangira, Mb -          | Mjumbe       |
| 16. Mhe. Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mb-      | Mjumbe       |
| 17. Mhe. Juma Usonge Hamad, Mb -                | Mjumbe       |
| 18. Mhe. Antipas Zeno Mgungusi, Mb              | -Mjumbe      |

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

- |  |        |
|--|--------|
| 19. Mhe. Abdul-Hafar Idrissa Juma, Mb -  | Mjumbe |
| 20. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb -        | Mjumbe |
| 21. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb -      | Mjumbe |
| 22. Mhe. Khalifa Mohamed Issa, Mb -      | Mjumbe |
| 23. Mhe. Ester Amos Bulaya, Mb -         | Mjumbe |
| 24. Mhe. Munde Tambwe Abdallah, Mb-      | Mjumbe |
| 25. Mhe. Rose Syprian Tweve, Mb -        | Mjumbe |
| 26. Mhe. Neema William Mgaya, Mb -       | Mjumbe |
| 27. Mhe. Juliana Shonza, Mb -            | Mjumbe |
| 28. Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb- | Mjumbe |
| 29. Mhe. Esther Malleko, Mb -            | Mjumbe |
| 30. Mhe. Dkt. Faustine Ndugulile -       | Mjumbe |
| 31. Mhe. Agnes Marwa, Mb -               | Mjumbe |
| 32. Mhe. Asia Halamga, Mb -              | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kutoa maelezo kuhusu shughuli zillizotekelawa, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, Maoni na Mapendekezo, sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako lipokee, lijadili na kuikubali Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo kwa ajili ya utekelezaji wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI  
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI  
10 FEBRUARI, 2022**

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa na Mwenyekiti wa Kamati na imeungwa mkono. Sasa tunaanza uchangiaji.

Tunayo orodha ya wachangiaji hapa. Kwa hiyo, tutakwenda kuchangia kwa dakika tano, tano na kengele itakuwa ni moja. Mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa ni

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa Juma, akiafuatiwa na Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, ajiandae.

**MHE. ABDUL-HAFAR IDRISSE JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuchangia katika hoja hizi zilizokuwa mbele yetu. Pamoja na mambo mazuri na ushauri mzuri ulitolewa na Kamati uliowasilishwa na Mwenyekiti, ningependa niendelee kuzungumzia masuala mawili, jambo la kwanza, suala la UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejitahidi sana kama Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Samia katika kupambana na masuala ya UKIMWI. Afua za UKIMWI zimeendelea kupatikana, lakini ripoti ya Kamati na takwimu za Serikali zinaonesha kwamba, vijana hasa walio kati ya miaka 15 na miaka 24 ndio walioathirika zaidi na maradhi haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana 28,800 kwa mwaka, tena vijana hao ni kati ya miaka 15 na miaka 24, ndio ambaao wanaongoza kwa kuathirika. Sasa mimi ningependa nishauri nini pamoja na haya; ningetamani sana Serikali yetu pamoja na Watanzania wote turejeshe nguvu ya kupambana na masuala ya UKIMWI katika ngazi ya familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ngazi ya familia hatuzungumzi sana uwazi kuhusiana na namna ambavyo UKIMWI unaweza kuambukizwa. Ndio maana tunazungumza sana katika kuhakikisha watu wetu hawapati virusi vya UKIMWI kwenye familia kwa kuwashauri wasitende vitendo vile ambavyo vinasababisha kuambikiwa kwa UKIMWI. Moja ya njia kubwa ya kupata virusi vya UKIMWI ni kutenda ngono isiyokuwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dini zote, dini ya Kiislamu, ngono kabla ya wakati ama ngono nje ya ndoa ni dhambi, Dini ya Kikristo, sina mashaka na dini zote. Ngazi ya familia tumekuwa tunawakataza sana watoto wetu kushiriki vitendo vya ngono kwa ku-refertu maelekezo yale yaliyotoka

katika vitabu vyetu vitukufu, lakini shetani yupo kwa ajili ya watu wema. Sasa hawa vijana wetu ambao tunawaambia kwamba, msishiriki ngono, mkishiriki ngono mtapata dhambi tu, shetani yupo kwa ajili yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nadhani katika ngazi ya familia sasa tuwe wawazi kidogo. Tuwaeleze watoto wetu kwamba, ngono ni dhambi, lakini kwa sababu wengi wanashiriki tuwaambie basi siku ukishiriki ngono shiriki ukiwa umevaa *condom*, maana utakuwa umepata dhambi, lakini umelinda afya yako, kuliko akapata dhambi na asilinde afya yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaweza ikanusuru vijana wetu. Kwa siku moja vijana 80, kwa mwezi mmoja vijana 2,400, kwa mwaka mzima vijana 28,000 hali ni mbaya. Sasa tukiendelea kutumia dini peke yake katika kuwakataza vijana wasishiriki tukiamini itatosha peke yake kuwakinga, hapana haitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, dini mpinzani wake mkubwa ni shetani. Jambo zuri sana kushiriki jambo la kimapenzi kwa mtu yeote aliyekuwa juu ya miaka 18 kwa ridhaa yake sio kosa kwa mujibu wa sheria zetu. Sasa katika ngazi ya familia tuwe wawazi, tuwaambie ukitenda utapata dhambi, lakini shetani akikupitia ama kama ukimfuata shetani halafu mkaenda mkatenda, vaa mpira ili kuhakikisha kwamba, hujambukizi virusi vya UKIMWI. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia niongezee katika masuala ya maradhi yasiyoambukiza. Ningetamani niungane na Kamati katika kuishauri Serikali, umefika wakati sasa wa kuunda Tume Maalum ya Kupambana na Maradhi Yasiyoambukiza kama tulivyounda Tume Maalum ya Kupambana na UKIMWI. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote humu ndani na Watananzania karibu wote hakuna familia ambayo hajaathirika na maradhi yasiyoambukiza. Kama hakuna mtu mwenye maradhi ya moyo kuna mwenye maradhi ya kisukari, kuna

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

mwenye uzito uliopitiliza. Sasa tuishauri Serikali ione sababu ya kuunda tume maalum kupambana na maradhi haya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maradhi yasiyoambukiza sio tu ni hatari, lakini ndio maradhi ghali zaidi kuyatibu katika familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja hii. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa fursa na kuweza kuweka mchango wangu katika hoja zillizowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naunga mkono hoja. Baada ya kuunga mkono hoja naomba nijikite katika mambo makuu matatu; jambo la kwanza ni afya, hususan katika taasisi ya *MSD*, jambo la pili nitazungumzia kidogo kuhusu elimu na baadaye nitazungumzia kuhusu Baraza la Michezo Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa ya huduma na maendeleo ya jamii iliyowasilishwa, moja ya changamoto kubwa ambayo imekithiri ni upungufu wa dawa nchini. Ukiuutilia hata katika *ground*, huko *site*, utakubaliana na mimi kwamba, pamoja na upungufu mkubwa wa dawa zipo dawa ambazo katika maeneo yote hazikuwahi kuwa tatizo, dawa hizo ni kama *panadol* na *paracetamol*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siri ya uwepo wa hizo dawa muda wote ni kwa sababu, sehemu kubwa ya dawa hizi zinazalishwa nchini kuititia Kiwanda cha *MSD* pale Keko. Kuititia kiwanda cha Idofi kule Makambako Njombe ambacho kinazalisha vifaatiba na tayari kinajiwekeza katika kuzalisha dawa zaidi nchini. Tumekuwa na fursa nzuri ya kuweza kupata baadhi ya dawa ambazo zinatosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni nini maoni yangu katika jambo hili; Serikali sasa iamue kwa dhati kuwekeza kwa nguvu katika kuanzisha viwanda nya dawa nchini. Viwanda nya dawa nchini ndio njia pekee ambayo itatuondosha kwenye kadhia hii kubwa nchini ya upungufu wa dawa kwa binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan, anafanya kazi kubwa sana katika ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma nchini. Tumeona madarasa mengi sana yamejengwa katika eneo la elimu, tumeona vituo nya afya na zahanati zinaendelea kujengwa kwa wingi sana, lakini majengo hayo hayatakuwa na tija ya kutisha kama hatutakuwa na vifaa pamoja na dawa katika zahanati na vituo vyetu nya afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya eneo ambalo linakwamisha sana upatikanaji wa dawa ni namna ambavyo dawa zinaingizwa nchini. Imeelezwa kwamba, dawa mpaka ifike kwa mlaji ikiagizwa kutoka nje inachukua kati ya miezi sita mpaka miezi nane. Kipindi hicho inawezekana dawa nyingine ikawa tayari imeanza kuelekea kwenye kwisha kwa muda wake wa matumizi. Hilo hii imesababisha hasara kubwa kwa Serikali kupitia *MSD*na dawa nyingi zimeangamizwa kwa kupita muda wake wa matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia kwamba, bado tuna upungufu mkubwa wa dawa katika maeneo yetu, ushauri wangu ni kwamba, namna ambavyo tunaweza tukatatua jambo hili ni kuhakikisha kwamba, sasa tunaenda kwa dhati kuwekeza katika ujenzi wa viwanda nya dawa nchini. Hilo liende sambamba na ajira za watumishi wa idara ya afya, hilo liende sambamba na ule Muswada wa kuhakikisha kwamba, sasa tunapitisha huduma ya afya kwa wote nchini. Tukiwezesha hayo, tutakuwa tumetatua kadhia hii ya huduma ya afya kwa wananchi wetu hapa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni katika suala la elimu. Kwa kipindi kirefu binafsi tangu nimeingia kwenye

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Bunge hili nimekuwa nikiuliza maswali, lakini nilikuwa nikichangia ni namna gani Serikali ina-*accommodate* wale vijana ambao wanashindwa kuendelea na masomo baada ya kuwa wameshindwa mitihani katika /level/ya darasa la sab ana kidato cha nne au kidato cha sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna pekee ya kwenda ku-*accommodate* vijana hawa ni kutoa elimu ya ufundi kwa mikopo. Nashukuru sana maoni ya Kamati yamelimeweka hili jambo vizuri. Nisisitize, kwa kuwa, Serikali hii ni ya watu wote si ya wale ambao wanafaulu peke yake, Serikali hii inawahusu wale pia wanaoshindwa mitihani, ni vizuri sasa ikaja na utaratibu mzuri wa kuweza kuwa-*accommodate* hao kupitia vyuo vya ufundi kwa kuwapa mikopo ya kufanya masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya muda suala la BMT nitalizungumza siku nyngine. Naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko. Sasa namwita Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mheshimiwa Cecilia Paresso na Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo wajiandae.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyopo mezani kwetu. Nianze kwa kuunga hoja mkono, lakini nitajikita katika maeneo matatu. Eneo la kwanza ni lile ambalo ameishia dada yangu Mheshimiwa Husna, ni kuhusu upungufu wa watumishi katika sekta hizi mbili ambazo Kamati yetu inahusika, idara ya elimu na idara ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna upungufu mkubwa sana wa watumishi katika kada hizi mbili. Waheshimiwa Wabunge humu wakitaka watoe takwimu wataonesha wazi kwamba, kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa au kwenye Majimbo kuna changamoto kubwa ya upungufu wa idadi ya Walimu na watumishi katika sekta ya afya. Kazi kubwa ambayo imefanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya

Mama yetu Mama Samia Suluhu Hassan na ujenzi wa madarasa zaidi ya 15,000 na *hostels* 50 na vituo vya afya *impact* yake haitaonekena vizuri sana upungufu huu ukiedealea. Kwa hiyo, naomba Serikali sasa ichukue hatua za makusudi kuhakikisha kwamba, kibali maalum kinatolewa kwa ajili ya ajira ya Walimu na ajira ya watumishi wa sekta ya afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma kulikuwa na upungufu wa Wahasibu katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Serikali ikafumba macho ikatoa ajira ya Wahasibu watano kila halmashauri. Naiomba Serikali yangu sikivu ifanye hivyo, itoe kibali maalum kwa ajili ya watumishi wa sekta ya afya na watumishi wa sekta ya elimu

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye taarifa yetu tumezungumzia villevile kuhusu Chuo Cha Ualimu Mtwara. Wakati tunatekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari mwaka 2005 hadi 2009 kulikuwa na mapendekezo, ili kuongeza idadi ya Walimu wa sayansi vyuo vitatu vibadilishwe kuwa vyuo vikuu vishiriki; Chuo Cha Ualimu Mtwara, Chuo Cha Ualimu Dar-es-Salaam na Chuo Cha Ualimu Mkwawa. Vyuo viwili hivi vimeshabadilishwa kuwa vyuo vikuu vishiriki, Chuo Cha Ualimu Dar es Salaam ni *DUCE* sasa hivi na Chuo Cha Mkwawa kimeshabadilishwa kuwa *MUSE*, ni chuo kikuu kishiriki cha Mkwawa, bado Chuo Cha Ualimu Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Ualimu Mtwara kina *facilities* zote; kuna eneo la kutosha kwa ajili ya upanuzi, kuna bwalo la kutosha, madarasa ya kutosha na majengo ya utawala na vyumba vya mihadhara vya kuanzia viro tayari. Kwa hiyo, naomba Serikali itekeleze ile azma yake ya kukibadilisha Chuo cha ualimu Mtwara kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. *Facilities* zote kama nilivyosema zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye elimu kuna kitu kinaitwa *skill over effect*; tukijenga Chuo Kikuu Kishiriki Mtwara Wana-Mtwara wengi watahamasika kusoma kutoma elimu

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

ya Chuo Kikuu kwa sababu wataona Chuo Kikuu kipo jirani yao. Kwa hiyo, naomba azma hiyo itekelezwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine, wakati tunafanya mahojiano na Wizara hizi mbili za kisekta; elimu na afya, kuna kuingiliana kwa majukumu katika TAMISEMI na Wizara za kisekta; elimu na afya. Hata juzi tulifanya kikao cha kuwakutanisha TAMISEMI na Wizara ya Elimu. Hata kama tunafahamu kwamba kuna *collective responsibility*, siyo vizuri mtumishi au mtumishi wa Wizara fulani kusema Wizara fulani inamwingilia, lakini ukienda kwenye utekelezaji, tunaona kuna changamoto ya kuingiliana, yaani Wizara za kisekta na TAMISEMI wanaingiliana. Hili liko wazi tu kwamba ile (*D by D*) ugatuaji bado haujalelewka vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watumishi wa Serikali bado dhana ya ugatuaji hawajalelewa, lakini mpaka kuna baadhi ya viongozi vile vile dhana ya ugatuaji bado hajaelewka. Udhifu mwengine ni kwamba hakuna sheria ambayo inalinda ugatuaji. Ugatuaji unaongozwa na *policy paper* ya mwaka 1998. Kwa hiyo, naomba vitu viwili kama tulivyoshauri kwenye kamati yetu; kwanza, elimu ya ugatuaji itolewe kwa watendaji na viongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, muda sasa umefika wa kuhakikisha kwamba Serikali inaleta sheria ya kusimamia huu ugatuaji ili kusiwe na kuingiliana katika Wizara na TAMISEMI. Tukifanya hivyo, tutarahisisha utekelezaji wa majukumu katika ngazi ya chini. Huko chini kuna kuingiliana sana katika TAMISEMI na Wizara nyingine za kisekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Umeunga mkono hoja Mheshimiwa?

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishaunga mkono hoja mwanzoni. Kwa hiyo naunga mkono hoja kwa mara ya pili sasa hivi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu muda wetu ni mchache, naomba basi kengele ikipigwa moja basi angalau tumpe nafasi na mtu mwingine. Namwita Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo.

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Kwanza niungane na Mwenyekiti wa Kamati yetu, kupongeza sana juhudzi za Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa ujenzi wa miundombinu ya shule na hasa madarasa yale ambayo tumeyapata. Katika Halmashauri ya Ubungo tumeweza kupata madarasa 151 ambayo yamesaidia sana kupunguza changamoto hizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo nataka nichangie kwa dakika ambazo ninazo, ni haja ya Serikali kushughulikia upotevu katika mfumo wetu wa elimu. Kuna upotevu mkubwa sana na nitatoa mifano mitatu. Mfano wa kwanza, wanafunzi waliofanya mtihani wa *Form IV* mwaka 2021, walianza shule ya msingi mwaka 2011. Walianza wakiwa 1,500,000; waliofanya juzi mwaka 2021 ni wanafunzi 483,820. Inamaanisha watoto 1,000,000 na zaidi wamepotea wakiwa na umri wa miaka 13.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa pili, katika wanafunzi waliofanya mtihani wa *Kidato cha IV* 483,820, katika nchi hii huwa tunapima ufaulu katika madaraja manne; daraja la kwanza, la pili, la tatu na la nne na la mwisho la kufeli. Daraja la nne huwa tunaita ufaulu haffifu.

Kwa hiyo, kwa maana ya ufaulu *proper*, daraja la kwanza mpaka la tatu katika wanafunzi waliofanya mtihani huo, 483,820 waliofaulu daraja la kwanza mpaka la tatu ni wanafunzi 173,000 peke yake sawa sawa na 35.8%. Inamaanisha katika eneo hilo pia, watoto takribani 300,000 wamepotea. Kwa hiyo, mpaka unafika *form four* umeshapoteza watoto 1,300,000, zaidi ya 70%. *Big wastage!*

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa tatu, mwaka 2021 Ofisi ya Waziri Mkuu wamefanya utafiti mzuri sana, unaitwa utafiti wa nguvu kazi katika nchi yetu; na wakabaini kwamba Tanzania tuna watu milioni 33 hivi ambao ni nguvu kazi wanaoweza kufanya kazi ambao ni 54% ya *population* yetu. Katika hao, 16% ya nguvu kazi hiyo hawajawahi kwenda shule kabisa; 65% ndiyo Darasa la Saba na 15% ndiyo *form four*. Inamaanisha kwamba mpaka hapo 96% ya nguvukazi yetu ni nguvukazi ambayo imepita katika mfumo wa elimu bila stadi zozote za kazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya ufundi, *VETA* hii ambayo tunaizungumzia, waliopita katika nguvukazi ni 1%; elimu ya juu ya kati ni 1% nyingine. Vyuo Vikuu ambavyo mnadhani tuko wengi sana, nguvu kazi yetu ni 2% peke yake. Kwa hiyo, ni 4% ya nguvukazi yetu unaweza ukasema angalau wamepita katika mfumo fulani wa stadi za kazi na maisha. *Very big wastage* Maana yake nini? Ni kwamba mfumo mfumo wetu wa elimu haujasambaa. Ni mfumo ambao uko *vertical*, ukishakosea sehemu moja, unatoka katika mfumo. Kwa hiyo, lazima tatizo hili kama Serikali tulione. Ushauri wangu, badala ya kushughulikia changamoto hizi nusu nusu, tuupitie na kuupanga upya mfumo wetu wa elimu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili siyo geni. Mwaka 1982, Rais wetu wa Kwanza Mwalimu Nyerere aliunda Tume ya Makweta, maarufu kama *Makweta Commission* ikaupitia mfumo wetu wa elimu. Ilifanya kazi zaidi ya mwaka mmoja, ikatoka na taarifa ambayo ilitusaidia kwa miaka 20. Ndiyo iliyotupa Sera ya Elimu na Mafunzo ya 1995. Sera ya elimu na mafunzo Mheshimiwa Waziri wa Elimu ya 2014 siyo *product* ya *research* yoyote; sera pekee ambayo ni *product* ya *research* ni ya 1995. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri kwa bidii kwamba Waheshimiwa Mawaziri na Serikali tumshauri Mheshimiwa Rais akubali kuunda *a Presidential Commission* ambayo itapitia upya mfumo wetu wa elimu tupange upya. Jambo hili kugusa tu mtaala wa *Primaryna Sekondari*, haiwezi

kututoa. Tunahitaji elimu ambayo ita-fit katika karne ya 21 na ambayo itatupeleka miaka 20 mingine ijayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri dira yetu inaisha mwaka 2025, kwa hiyo, na hii itatupa nafasi ya kwenda sambamba na dira yetu ya mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso halafu Mheshimiwa Neema Gelard Mwandabila na Mheshimiwa Tecla Mohamed Ungele wajiandae.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika hoja za Kamati zilizoko mbele yetu. Hali ya upatikanaji wa dawa hapa nchini katika hospitali zetu, vituo vyta afya na zahanati kwa ujumla ni mbaya na dawa hazipo na wananchi hawapati huduma zinazostahiki. Tunafahamu tuna bohari ya dawa ambazo kazi yake ni kununua na kusambaza dawa na sasa tumeipa jukumu lingine, tumebadilisha sheria ya kuanzisha viwanda vyta kutengeneza dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba hii *MSD* imezidiwa. Mara nydingi hapa Bungeni tumekuwa tukisema tu Serikali ina idai *MSD*, labda ufanisi wa *MSD* hauonekani kwa sababu inaidai fedha nydingi. Mimi naona kama hicho ni kichaka tu cha kujifichia humo. Ni kweli kwamba inaidai Serikali na ripoti mbalimbali za *CAG* zimeonyesha, lakini *MSD* yenyewe pamoja na kidogo kinachopatikana, bado mfumo wake wa usambazaji wa dawa ni hafifu wa kizamani na hautoi matokeo yale ambayo wananchi wanayatarajia na huduma kule kwenye vituo vyetu, hazipatikani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hata Naibu Waziri wakati anajibu swali hapa akasema shida siyo fedha, fedha zipo lakini shida nadhani nydingine wanaijua. Kwa hiyo, nadhani iko haja sana ya kufanya kufumua *MSD* na kuiunda

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

upya kwa kuangalia mahitaji ya leo na kuweka mfumo ambao usambazaji wa dawa utatosheleza na utafika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, kwenye Mkoa wangu wa Arusha, sasa hivi *MSD* wanapita kwenye vituo wanapeleka dawa. Wananchi wanaona gari limefika, linashusha dawa, lakini wanashusha dawa za wiki moja tu, magari yanaondoka. Hata hilo gari halijafika kwenye Bohari Kuu, huku nyuma dawa zimeisha na mpaka warudi, siyo leo. Kwa hiyo, tusitegemee tena wananchi watapata huduma. Kwa hiyo, ni lazima tuangalie namna gani tutahakikisha wananchi wanapata dawa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwingine, tuliamiwi kwenye Kamati juzi; leo Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kuna uhaba mkubwa sana wa hizi *blood bags*, mifuko ya kuwekeadamu; na wenyewe wamekiri kabisa pale Muhimbili hakuna, lakini maeneo mengine nchini inapatikana, iko mpaka ya ziada. Sasa unajuliza, kuna nini? Maana yake kuna tatizo la mgawanyo na usambazaji na usimamizi wa dawa pamoja na vifaa vyote vya dawa hapa nchini. Kwa hiyo, iko haja sana ya kuitizama *MSD* na kuifumua na kuhakikisha kwamba inafanya huduma ambayo inatakiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, hapa juzi juzi tulisikia tamko la Waziri kuhusiana na kufunga maduka yote ya dawa zilizoko karibu na hospitali au vituo vya afya au vinginevyo; na amerejea sheria ambayo tulipitisha hapa Bungeni. Hiyo sheria inaonesha kabisa kwamba duka la dawa kwenye hospitali itakaa mita 500; kwenye ngazi ya mkoa itakaa mita 400; kwenye ngazi ya wilaya itakaa mita 300; kwenye vituo vya afya na zahanati itakaa mita 200; na akaagiza kwamba ziondoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hili tamko siyo sahihi, kwa sababu kwanza haya maduka ni Serikali wenyewe mmesaidia kuyafanya yashamiri na kustawi, kwa sababu maduka yetu ya dawa zilizopo ndani ya hospitali hakuna

dawa. Kwa hiyo, mwananchi hayuko tayari mgonjwa wake afe kwa sababu hakuna dawa ndani ya hospitali eti asiende kutafuta kwenye duka la dawa. Kwa hiyo, nyle wenyewe mmesaidia kuyafanya yashamiri na hawa watu wanaendesha biashara kihalali, wako kihalali, mmewapa vibali wenyewe, wanalipa leseni, wanalipa kodii, leo mnawaambia waondoke. Hilo siyo suluhisho. Kuwaambia maduka haya yaondoke, siyo suluhisho la kuhakikisha dawa zinapatikana kwenye hospitali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotakiwa ni kuimarisha *MSD*. Kuhakikisha *MSD*inatoa dawa zote na kwa wakati katika hospitali zetu. Hospitali zetu, vituo vya afya na zahanati zikiwa *well equipped* na dawa zote, haya maduka *automatic* yatapotea, hayatakuwepo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani Serikali kwenye hili jambo muiache kama ilivyo. Mwananchi yeoyote hayuko tayari kuona eti mtu wake anafariki hapa kwa kukosa dawa asiende kutafuta dawa kwenye duka la dawa kwa sababu Serikali imetoa tamko, haiwezekani. Kwa hiyo, ni Serikali kuhakikisha *MSD*inaimarishwa, inasambaza dawa zote muhimu kwa wakati na wananchi wanapata dawa ambazo zinatakiwa kulingana na ugonjwa ambao anaugua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni upungufu wa watumishi wa afya. Ripoti mbalimbali za *CAG* zimeonyesha tuna upungufu mkubwa sana wa watumishi wa afya. inakaribia 52% ya watumishi wa afya ambao wanahitajika waajiriwe ili huduma muhimu na stahiki ziweze kutolewa kwenye vituo vyetu vya afya na katika maeneo yote ambayo tunatoa huduma za afya. Hata hivyo, bado ajira hizi hazijatangazwa. Maana yake ni kwamba, huku tuna changamoto ya dawa, huku hatuna watumishi; hivi mnawataka nini Watanzania hawa? (*Makofii*)

Mheshimwia Mwenyekiti, kama tunaweza kukopa fedha tukajenga *SGR*, tukajenga sijui Mwalimu Nyerere *Stiegler's Gorge*, kwa nini tusiwekeze kwenye afya za Watanzania? Hata hiyo *SGR* na *Stiegler's Gorge* tutakuwa

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

tunamjengea nani kama Watanzania wote watakuwa wagonjwa, hakuna dawa? Itakuwa ni kazi bure. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali iliweza kufanya maamuzi yale ikaweza kutafuta fedha kujenga *SGR*, kujenga *Stiegler's* hivyo hivyo fanyeni uamuzi sahihi...

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Mollel.

### **TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sipingani na mawazo mazuri ya Mheshimiwa Mbunge, lakini nilitaka tu nimpe taarifa kwamba unapoajiri, unaajiri kulingana na ukuaji wa uchumi wako na unapokopa, unasisimua uchumi ukue ili uweze kuajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe taarifa kwamba kwa mwaka huu tu tayari tumeruhuswa kuajiri watu 21,000. Hata hivyo, ukikopa ukawekeza hizo fedha, kuna maeneo matatu ya kuwekeza ili uchumi ukue na uweze kuajiri wengi; uwekeze kwenye *human resource capital*, ambayo ndiyo imewekezwa sasa hiyo shilingi bilioni 1.3 kwenye elimu, afya na sehemu nyingine ambazo zinaenda kukuza na kukuza pato letu la Taifa; tunawekeza kwenye teknolojia na maeneo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakubaliana na mawazo yake, lakini anachokifanya Mheshimiwa Rais ni hicho hicho anachokisema yeye. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, pokea taarifa.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tunatambua kwamba uchumi hauwezi kuwa muhimu sana kuliko afya za Watanzania. Yaani inaweza

ikawa inaenda sambamba, lakini naongelea hapa afya za Watanzania kwa ujumla wake. Mnaweza mkawa mmetoa hizo ajira, lakini bado uhitaji ni mkubwa. Si tuko kule tunaona kwenye vituo vyetu vya afya, zahanati na kila mahali.

Kwa hiyo, nadhani waipokee kama ushauri na Naibu Waziri utapata nafasi, utakuja kueleza hayo na tutaendelea kushauri na ndiyo wajibu wetu mkubwa wa Wabunge hapa Bungeni.

**MWENYEKITI:** Sasa endelea kuchangia Mheshimiwa Paresto baada ya kupokea taarifa nzuri ya Serikali.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nasema suala la watumishi wa afya, ajira ni muhimu na ninaendelea kulisisitiza kwamba ni muhimu Serikali iajiri kuhakikisha Watanzania wanapata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naeleza kwamba kama tunaweza kuwekeza nguvu kubwa kwenye masuala ya kiuchumi kwa maana *SGR, Stiegler's*, hawa Watanzania ambao wanategemewa waje watumie hayo kwa kuwa na afya njema, kama hatujawaandalia mazingira ya kuwa na afya njema kwa kuhakikisha dawa na huduma katika hospitali zetu zinapatikana inavyotakiwa, itakuwa ni kazi bure. Tutakuwa na Taifa la watu ambao ni wagonjwa, hakuna dawa. Tutakuwa na Taifa ambalo haya tunayoyatengeneza, hayatakuja kutumiwa kwa sababu watu wote wanaumwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachoshauri ni kwamba uwekezaji kwenye sekta ya afya kwa kuhakikisha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba watumishi wa afya wa kutosha kwenye sekta hii, itiliwe mkazo sawa sawa na mkazo ule ule kwenye sekta nytingine ambazo tunaziona kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo,...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**MWENYEKITI:** Kengele ya kwanza Mheshimiwa. Endelea, hiyo ni ya kwanza itagonga ya pili. Malizia.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala lingne kuhusu mtaala wa elimu ambao tunaufanya marekebisho kwa sasa. Kama ambavyo Serikali imesema na kama ambavyo ripoti yetu imeonyesha, ni kwamba tunatarajia mtaala huu utakuja kuanza utekelezaji 2026. Najiuliza swali moja; Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Marehemu Hayati Dkt. Magufuli, kipindi hicho alitoa agizo kuhakikisha tunaingiza somo la historia kwenye mtaala wetu wa elimu na mtaala ufanyiwe maboresho. Jambo hilo lilitkelezwa *within two months or three months*na ikafanyika na Wizara ikatengeneza vitabu, ikachapisha, wanafunzi wakaanza kufundishwa, ikatekelezeka. Leo kwa nini tunashindwa kuhakikisha kwamba hii sera yetu ya elimu inayofanyiwa maboresho inaenda kutekelezwa *on time*? Kwa nini mpaka 2026? Kuna nini hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kinachoonekana ni kwamba hakuna utayari au utashi wa kuhakikisha suala hili linafanyika. Tukumbuke kwamba dunia ya leo inakimbia, sisi inawezekana tuko nyuma sana. Huko duniani watu wanakimbia, ugunduzi unaendelea, mambo yanaboreka kila siku. Profesa hapa ameeleza vizuri sana, kama tukiwa wagumu, tukiwa na urasimu wa kufanya mabadiliko na kukubali mabadilika kwa wakati...

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Nusrat Hanje.

## **TAARIFA**

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba anachokisema ni ukweli na hata Sera ya Sayansi na Teknolojia

ambayo ilitakiwa iwe Sera ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifufimeishia kwenye Sera ya Sayansi na Teknolojia, lakini pia ni ya mwaka 1996, ina miaka 28. Hata Sheria ya COSTECHni ya mwaka 2000. Yaani sera yenye tunayoizungumzia maana yake itakuwa *outdated* kabla hata haijaanza kutekelezwa, kwa sababu *lifespan* ya sera ni *10 years*. Ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Paresto, taarifa hiyo.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nimeipokea taarifa hiyo nzuri sana na naamini pia wameisikia. Hoja yangu hapa ni kwamba, sijui kwa nini Wizara wanakuwa wagumu au wazito na kunakuwa na urasimu mkubwa. Najua, inaweza ikawa ni mabadiliko ambayo yanahitaji mambo mengi, lakini tujaribu, tufanye huo uthubutu, tuhakikishe kwamba Sera ya Elimu tunaitekeleza kwa wakati na tuendane na dunia na teknolojia ya leo, kuhakikisha kwamba tunazalisha na tunatoa wataalam ambao wanakubalika duniani katika kuingia kwenye soko la ajira na kuisaidia nchi kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo tu, nakushukuru sana, na naunga mkono hoja ya Kamati.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Nitajikita kwenye mambo mawili, sana sana katika suala la ustawii wa jamii na suala la pili litakuwa kuhusu dawa za kulevyaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa huu mwezi wa kwanza tumekuwa tukishuhudia matukio mbalimbali ya watu kufanya mauaji kwa watoto wadogo, wanandoa na watu mbalimbali katika familia. Tunafahamu chanzo cha mauaji hayo na kwa taarifa zilizopo mengi yametokana na masuala ya mahusiano, migogoro ya ndoa, uchawi pamoja na mirathi. (*Makofii*)

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukianza kuangalia masuala haya kwa jicho la kawaida unaweza ukalichukulia hili kama ni suala dogo sana, lakini kadiri siku zinavyozidi kwenda ndivyo wimbi hili litakavyokuwa linaendelea kuongezeka kukua kwa watu tofauti fofauti na mikoa tofauti tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema nini, najaribu kuonesha *role* ya watu wa ustawi wa jamii ilivyo muhimu kwenye jamii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningependa nimpongeze Mheshimiwa Rais, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kutupatia Wizara mpya ya Maendeleo ya Jamii ambayo ameitofautisha na Wizara ya Afya. Hapa nadhani ndipo *roles* za hawa watu wa maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii zitakavyoanza kutofautishwa kwa uzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawa wa ustawi wa jamii ni watu muhimu sana katika kufanya *counselling* kwa ajili ya ku-restore *psychological status* ya watu katika jamii zetu. Hata hivyo, unakuta watu hawa katika jamii hawatambuliki na hawapewi kipaumbele na hata bajeti yao ipo chini. Kwa hiyo kupitia taarifa hii ya Kamati ya Huduma ya Jamii nilitamani walichukue hili na kuweza kulifanyia utafiti vizuri au kulipa kipaumbele kwa namna tofauti ili watu hawa ajira zao ziongezwe, hata ikiwezekana wafikie angalau kwenye *level* ya kata ili wawe na uwezo wa kubainisha haya mambo yanayoendelea kwenye jamii haraka kabla mauaji hayajatokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kuongelea suala la dawa za kulevyta. Kama tuliviosikia kwenye taarifa, kwamba changamoto ya dawa za kulevyta katika nchi yetu bado ni kubwa na hususan kwa watu wanaotoka mipakani suala hili limekuwa ni gumu zaidi kwa sababu vijana wengi wanaathirika na dawa za kulevyta. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema kuwa kuna ongezeko, japokuwa taarifa hazijawa bayana katika taarifa ya Kamati, lakini niseme tu kuwa ongezeko la dawa za

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

kulevya ni kubwa na warahibu hawa wana athari nydingi kwenye jamii. Tumeanzisha *clinic* mbalimbali katika maeneo mbalimbali ambapo warahibu hawa wamekuwa wakiendelea kupewa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto inayokuja, unakuta mrahibu yuko kwenye *methadone clinic* lakini unakuta askari bado wanaendelea kumbughudhi na wakati huo huo wakimkamata na wakimpeleka *Central Police* wanamkatisha hii dozi ya *methadone*. Kwa hiyo natamani kwamba hili liweze kupewa kipaumbele, kwamba mrahibu anapokamatwa apewe fursa ya kwenda kupata huduma hii ya *methadone* kwenye zile *clinic* ili asiweze kukatisha ile dose yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hizi *methadone clinics* hakuna huduma za lishe. Tunafahamu kabisa kuwa mtu ambaye anatumia dawa za kulevya anakuwa katika mazingira hatarishi ya kuwa na lishe duni. Anaweza akawa na *overweight* au akawa na *underweight*, kitu ambacho tunajua kabisa, kwamba uwezo na ufanisi wake wa *recovery* mwilini unakuwa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, natamani kuona kwamba katika vituo hivi suala la lishe linapewa kipaumbele ili hawa wanapoendelea na matibabu wapone haraka, kama lishe itakuwa vizuri wataweza kupona haraka.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia naomba dakika moja tu.

**MWENYEKITI:** Haya, nakuongezea dakika moja Mheshimiwa Neema, malizia.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile hawa watu wakishapewa matibabu wanashindwa kurudi kwenye jamii kwa sababu wanakuwa hawana kazi.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Kwa hiyo kama tunaweza kutenga asilimia mbili za mikopo kwa walemavu, asilimia kwa vijana na wanawake, basi kungekuwa na hili kundi pia lipewe kipaumbele kwenye jamii kama sehemu ya kukopeshwa fedha ili waweze kuingia kwenye jamii wakiwa na kipato. Ahsante. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Tecla Ungele, Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya pamoja na Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage wajiandae.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ili nami nichangie hoja hii iliyotolewa na Kamati ya Masuala ya UKIMWI, dawa za kulevyo, kifua kikuu na magonjwa yasiyoambukiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote tunamshukuru na tunampongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendeleza na kuongeza ujenzi wa madarasa katika shule zetu ili kupunguza msongamano wa wanafunzi katika madarasa hayo. Msongamano huo ndio uliokuwa unaleta magonjwa ya maambukizi ikiwa ni pamoja na kifua kikuu na mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nitauelekeza kwenye kifua kikuu na ukoma. Kifua kikuu ni ugonjwa mkubwa na ni tatizo kubwa nchini Tanzania. Tunaona Tanzania ni mionganoni mwa nchi 30 ulimwenguni zenye maambukizi makubwa ya kifua kikuu; mwaka 2019 kulikuwa na wagonjwa 137,000. Kikubwa zaidi, kwa kifua kikuu kama mgonjwa hakugundulika mapema na hakupata matibabu mapema basi kuna hatari ya kwenda kwenye kifua kikuu sugu na hatimaye kusababisha kifo. Mgonjwa wa kifua kikuu asipopata matibabu anaambukiza watu wengine 10 mpaka 20 kwa siku. Hilo ni tatizo kubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitachangia kuhusu ugonjwa wa ukoma. Bado ukoma ni tatizo kwenye nchi yetu; na ukoma nao unaambukiza kwa njia ya hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha mwaka 2019 kulikuwa na wagonjwa 1,600 nchini, lakini pia hata kihistoria ugonjwa wa ukoma una asili fulani ya unyanyapaa. Kwa hiyo kuna hatari wagonjwa hawajitokeza. Sasa, ushauri wangu ni kwamba, kuimarisha elimu ya afya katika jamii, lakini pia kutumia kikamilifu kada ya *community health workers* nchini kwetu. Tumeona sasa hivi wanaajiriwa kama *medical attendance*, lakini kada hii ilikuwa *specifically* kwa ajili ya kwenda kwenye jamii na ndiko watakakoshughulika na magonjwa haya sugu, kugundua wagonjwa wa kifua kikuu na maambukizi mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri kuwe na mafunzo maalum, iwe *short courses ama course* za muda mrefu kwa ajili ya kukabiliana na magonjwa ambukizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja.

**MNEYEKITI:** Ahsante sana Dkt. Tecla Mohamed Ungele. Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, wakati huo huo Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage anajienda.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii uliyonipatia. Vilevile nichukue nafasi hii nimshukuru Rais wetu, Mama Samia, pia nimshukuru Waziri wa Afya na Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitajikita kwenye magonjwa yasiyoambukizwa. Takwimu zinatuambia kuwa zaidi ya asilimia 40 ya Wabunge humu wamewahi kuvuta sigara, aidha kwa kukusudia au kwa kutokusudia. Vilevile kidunia takwimu inatuambia kwamba zaidi ya asilimia 70 ya vifo vinavyotokea duniani ni kwa sababu ya magonjwa yasiyoambukizwa. Kwa Tanzania, zaidi ya asilimia 40 ya vifo vinavyotokea vinasababishwa na magonjwa yasiyoambukizwa. (*Makofii*)

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivi? Tatizo la magonjwa sasa hivi ni kubwa saba. Wakati UKIMWI unaanza miaka ya 1980 tuliona ni janga kubwa sana la kitaifa, lakini naomba niseme kwamba sasa magonjwa yasiyo ya kuambikiza ikiwemo kansa, ugonjwa wa moyo pamoja na ugonjwa wa figo, ni hatari sana na ni janga la kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikwambie *burden* ya magonjwa haya ya kuambukiza, nitatolea mfano mmoja tu kwenye ugonjwa wa figo. Wakati tunakwenda kupeleka wagonjwa wetu kutibiwa India kwa ajili ya *dialysis* na hususan kubadilishiwa figo tulikuwa tunatumia takribani milioni 60 kwa mgonjwa mmoja. Baada ya kuboresha huduma zetu za afya na tunamshukuru Rais, sasa hivi tunatumia takribani milioni 20, ambayo bado ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika wiki moja kuna *session* nne za kufanya *dialysis*, kusafisha figo kwa mgonjwa wa figo. Kila *session* moja inatumia si chini ya 200,000. Kwa hiyo, kwa wiki nzima mgonjwa wa figo anahitaji 800,000 ili afanyiwe usafishajji wa figo. Hili ni zoezi *routine* mpaka pale Mungu atakapomwita. Tatizo la magonjwa ya kuambikiza *is a burden*, ni tatizo kubwa sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba bado takwimu, hata hii ninayoisema ya asilimia zaidi ya 40 bado iko *under-reported*. Kuna watu wengi sana wapo vijijini ambao wameathirika na magonjwa haya yasiyo ya kuambukizwa lakini hatujawatambua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ushauri wangu; natambua kwamba kuna *initiatives* mbalimbali zimechukuliwa kitaifa na kimataifa. Katika *level* ya kimataifa tuna *Global Action Fund 2020/2025* ambayo lengo lake ni kupunguza magonjwa yasiyoambukiza kwa asilimia 25 ifikapo mwaka 2025. Katika ngazi ya Taifa tuna mkakati wetu wa kitaifa wa kupunguza haya magonjwa yasiyoambukiza. Tumeanzisha mwongozo wa kitaifa wa kufanya mazoezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo mawili ya kushauri. La kwanza, naomba nimshauri Mheshimiwa Waziri wa Afya, tuboreshe na tuhuishe *DHS2*, mfumo wa kukusanya taarifa. Ule mfumo wa kukusanya taarifa una taarifa chache sana zinazoonesha watu wangapi wanaumwa magonjwa yasiyoambukizwa. Hiyo inasababisha tunatoa *report ambazo ni under reported*, tunaacha watu wengi sana ambao tungeweza kuwasaidia kupata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, hili ni kwa upande wa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naishauri Serikali; suala la magonjwa yasiyoambukizwa ni *multisectoral*, ni suala mtambuka. Kuiachia Wizara ya Afya kushughulika na magonjwa yasiyoambukizwa inasababisha tunashindwa *ku-deal*/na tatizo hili. Nishauri sasa, kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu alichukue hili ili liwe kwenye ofisi yake na tuanzishe tume kama tulivyoanzisha Tume ya UKIMWI ili tuweze kuratibu wadau wote ambao wanahusika katika kusaidia suala la kupambana na magonjwa yasiyoambukizwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage aweze kuchangia.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie. Nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais na Serikali yake kwa kuendeleza mapambano dhidi ya matatizo haya makubwa na ambayo ni mtambuka, masuala ya UKIMWI, kifua kikuu, dawa za kulevyaa na magonjwa yasiyoambukizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunafahamu kwamba magonjwa yasiyo ya kuambukiza ni magonjwa yale ambayo tunasema hayana vimelea vinavyosambazwa. Hata hivyo, tafiti zinaonesha kabisa kwamba magonjwa yasiyo ya kuambizwa limekuwa ni tatizo kubwa sana na bahati mbaya niseme kwamba *the latest study* ni ya mwaka 2016 ambayo imekuwa-*reported* na Shirika la Afya Duniani (*WHO*), inasema

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

katika vifo 43 vya mwaka 2016 asilimia 71 vilikuwa ni vya magonjwa yasiyo ya kuambukizwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *study* nyingine zinazoendelea duniani, zinasema kufikia mwaka 2050 kutakuwa kuna ongezeko kubwa sana la wazee, wanamaanisha kuanzia miaka 65 kwenye *study* yao. Wanasema asilimia 68 ya wazee hao itakuwa Afrika, Tanzania ikiwa mojawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni suala lisilopingika kwamba magonjwa yasiyoambukiza kweli sasa hivi yanayakuta makundi yote, lakini asilimia kubwa ni wazee na ni magonjwa yanayochukua muda mrefu na tiba yake takriban ni ya kila siku, ni magonjwa ya kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hilli illi kuonesha ukubwa wa tatizo. Kwa hivyo naungana na wenzangu waliotangulia, lakini labda niwe *specific* zaidi. Niseme, Wizara ya Afya inafanya kazi nzuri sana katika kupambana na janga hilli, lakini ifikie mahali sasa, kwa sababu magonjwa haya kwa asilimia zote ni magonjwa yanayozuiliwa, ni kwamba watu tu hawana uelewa. Hata tunapokaa sisi hutakiwi kukaa zaidi ya saa moja, lazima uinuke utembee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna alimu kubwa ambayo jamii halifahamu. Kwa hiyo utaona msingi wa matatizo haya ni sehemu ya kuzuia (*prevention*). Tungeiachia Wizara ifanye suala la tiba, lakini suala la *prevention*, kama tulivyoshauriana liwekwe chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na liundiwe tume. Kwanza tukishazuia pia tutapunguza *burden* kwa Serikali na kwa Wizara. Kwa hiyo tume hii ikiundwa, au chombo hiki kikiundwa, kwanza hawa watu watakuwa *dedicated* na watakuwa *answerable* na wataweza kusimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo sheria nyingi sana, tumezipata humu humu ndani, sheria zisizopungua 60 ambazo zinasaidia kuzuia magonjwa ya kuambukiza. Hata hivyo, sheria zile ni nani anazisimamia? Wizara imeelemewa. Kuna miongozo imewekwa, hata hivi siku za karibuni umetoka

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

mwongozo, umeshaenda kwenye halmashauri zetu zote, lakini, ni nani anazisimamia? Wizara imeelemewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, suala la *prevention* ya magonjwa yasiyoambukiza na ambayo ndio msingi wa kuzuia magonjwa haya, hebu tuangalie namna ya kulifanya. Wawe watu ambao watakuwa *very dedicated*, watakuwa na mipango na watatupa taarifa.

Nashauri hivyo, kwamba sasa ifikie mahali tutambue ukubwa tatizo hili, tuishauri Serikali iangalie utaratibu wa kupambana, kwa maana ya kuzuia. Kwa sababu tukizuia, ukitoa elimu, kwa sababu ukishaunda chombo cha kuzuia kitatoa elimu kwa wakati, kitakuwa kina bajeti na kitafanya mambo yote. Ukiphasua na ukishatoa elimu ina maana hakuna matokeo ya ugonjwa kwa ukubwa wake.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika moja.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa, hitimisha kwa dakika moja.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba pia nishauri kuhusu kuongeza bajeti kwa Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevyia. Huku tunaona *operations* zao ni nyeti, wanahitaji vyombo muhimu vya maabara, watu wanao-graduate kwenye *methadone* wanahitaji pia wapate *study* za kazi; mambo ni mengi sana kwenye mamlaka hii.

Kwa hiyo nazidi kushauri, kama nilivyoshauri mara ya kwanza, hebu tuanglie bajeti ya hawa watu ili kuwawezesha waweze kufanya kazi kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, sasa ninamuita Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, wakati huo Mheshimiwa Hassan Ziddu Kungu na Mheshimiwa Philipo Mulugo wanajiaandaa.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa ili niweze kuchangia. Nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa fedha za madarasa, tumejenga madarasa 73 ya sekondari kule Kilolo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa na mambo machache ya kuchangia kwa haraka kulingana na muda. Kwanza ni suala la *Aids Trust Fund*, Mfuko ulioko chini ta *TACAIDS* pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifuko mingi tunayoianzisha hapa Bungeni huwa ina chanzo mahsusini cha mapato, lakini Mfuko huu ulianzishwa kwa kutegemea kwanza baeti ya Serikali, imetengwa shilingi bilioni moja na ndiyo inayotengwa kila mwaka, harambee pamoja na michango mbalimbali inayotokana na wahisani mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, kama ilivyo katika Mifuko mingine, uwe Mfuko wa Maji, Barabara na Mifuko mingine mbalimbali, Mfuko huu pia utafutiwe chanzo mahsusini kutockana na tozo au da mbalimbali mahali fulani ambazo tayari zipo ili uweze kuwa *stable* zaidi. Kwa sababu tunazungumzia jambo ambalo bado mpaka sasa kuna watu 200 wanaambukizwa UKIMWI kila siku, ambayo ni 73,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii bado ni idadi kubwa, lakini hatuko *sustainable*. Zaidi ya 90% ya bajeti inatokana na misaada na kama ikitokea siku moja wafadhili tukatikisika kidogo tu, hatuna uwezo wa hata 5% wa kuweza kujifadhilli. Kwa hiyo, huu mfuko lengo lake tungeujenga taratibu ili wafadhili watakapokuja kutikisika kidogo, basi angalau tuwe *stable* tuweze kununua angalau *paracetamol* kwa muda kadhaa wakati tunaendelea kujipanga.

**MHE. ENG. STELLA I. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mtoa taarifa, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya.

## TAARIFA

**MHE. ENG. STELLA I. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba pia nimpe taarifa Mheshimiwa anayechangia kwamba ni kweli kabisa naungana naye katika kuongeza fedha kwenye mfuko huu, kwa sababu katika eneo la kutoa elimu, tuko nyumba sana. Kwa mfanu, sasa hivi kuna hatari kubwa inayoendelea kwamba hizo *condom* tunazosisitiza kwamba watu wawe wanazitumia, kwenye maeneo ya vijiji na siyo vijiji tu, hata mjini, lakini hasa suala hilli nimeliona vijiji, unakuta watoto wanachukua hizo *condom* ndiyo wanageuza kuwa mipira na unakuta mtoto analia kabisa naomba *condom* yangu, *condom* yangu, kumbe ameiokota tu kwenye majalala huko. Kwa hiyo, bado inahitajika elimu ya kutosha na iwafikie wananchi wote. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nyamoga, unapokea taarifa?

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea taarifa hiyo. Sasa naomba kuchangia pia kuhusu magonjwa yasiyo ya kuambukiza, lakini mimi nitachangia kipengele kimoja kuhusu suala la wataalam wa mazoezi (*physiotherapists*). Wizara ya Afya inafahamu kwamba chuo kinachotoa taaluma hiyo kwa sasa ni kimoja tu cha *KCMC*; na hivi tunavyozungumza, tuna *Physiotherapist* 500 tu ambao wana *practice* nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kawaida, magonjwa kama kisukari, *pressure* na hayo mengine yanahitaji mazoezi. Hizi Idara kwa sasa hivi, nyingi ziko kwenye ngazi ya Mkoa tu, lakini sasa siyo kama zamani. Zamani vijiji tulikuwa tunapelekewa tu dawa za matumbo, kikohozи na

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

kadhalika; lakini kwa jinsi magonjwa yasiyo ya kuambukizwa yanavyoendelea, hali inahitaji *Physiotherapist* hadi kwenye Hospitali za Wilaya; na hizi Idara hazipo kwenye Hospitali za Wilaya na ni Idara muhimu sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza kwamba Wizara ya Afya iangalie kuongeza vyuo vinavyotoa taaluma ya *Physiotherapist*, yaani wale watu wa mazoezi. Pia katika ikama, wakati wa ujenzi wa hospitali za Wilaya na hata vituo vya afya, tuangalie uwezekanao wa kuweka hizo ili kuweza kuendana sasa na kasi ya maradhi yasiyo ya kuambukiza, yanayohitaji sana hii huduma ya *Physiotherapist*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ninalotaka kuzungumza ni kuhusu bajeti ya maendeleo kwa Tume ya Dawa za Kulevy. Kwasababu tuna chaguzi mbili; au tuwe na watu wengi sana humu ndani (hapa nchini) wanaotumia madawa ya kulevy, au tuzuie yasiingie kwa kiwango kikubwa. Kuzuia ni kwa kununua mitambo kwenye maeneo mbalimbali na mitambo hiyo inahitaji bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza bajeti hii iangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naunga mkono hoja. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, sasa hivi ikipiga kengele tu, hapo hapo unahitimisha hoja yako, hatutaongeza hata sekunde moja, kwa sababu bado wachangiaji ni wengi na upande wa Serikali nao pia kuna watu wanataka kuongezea michango yao.

Sasa namwita Mheshimiwa Hassan Zidetu Kungu aweze kuchangia.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Naomba njielekeze kwenye eneo dogo

tu ama eneo moja la michezo. Kwenye michezo changamoto kubwa tuliyonayo ni uwekezaji na uvezeshwaji hafifu wa makampuni ya taasisi za kiserikali kwenye michezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyikiti, nashauri mambo yafuatayo: Moja, Serikali ijaribu kushawishi makampuni na taasisi za kiserikali; kwenye fungu la *Corporate Social Responsibility* kwa kiasi kikubwa ielekezwe kwenye michezo. Mfano mzuri ni Geita *Gold Mine*, kwenye CSR yao wamewekeza kwenye upande wa *Geita Football Club*. Pia Kampuni ya Barrick imeweza kuwekeza kwenye timu ya *Biashara United*. Kwa hiyo, nashauri Serikali isukume makampuni hayo na taasisi za kiserikali ziweze kuelekeza CSR ziente kwenye michezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Serikali itoe *Incentives* kwa makampuni yote yanayowekeza kwenye michezo. Hii inafanywa sana na nchi nyingi zilizopiga hatua. Mfano, Serikali inaweza ikaamua makampuni yote yanayowekeza kwenye michezo, pale wanapokwenda kulipa *Corporate Tax*, basi lile fungu ambalo wamewekeza kwenye michezo lihesabiwe kwenye *Corporate Tax*. Hii italeta hamasa kwenye makampuni mengine yote kuweza kuwekeza kwenye michezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na machache tu. Naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Phillipo Augustino Mulugo, wakati huo Mheshimiwa Benardeta Kasabago Mushashu na Mheshimiwa Samwel Xaday Hhayuma wanajiandaa.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia wasaa nami niweze kuchambua hoja, lakini mimi nijikite kwenye mambo makubwa mawili hasa sekta ya elimu, nami ni mdau wa elimu hapa nchini.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wabunge mnisikilize. Lipo jambo linaendelea kwenye mashule yetu nchi nzima ambalo jipya mno halijawahi kutokea toka tumepata uhuru. Jambo hilo linaitwa utekelezaji wa Kalenda mpya katika mtaala uliopo hapa nchini. Jambo hilo limetolewa mwezi wa Kwanza na Ofisi ya TAMISEMI, kitu ambacho hakijawahi kutokea TAMISEMI akatoa miongozi ya *implementation za curriculum*. Anayetakiwa kutoa masuala yote ya kitaaluma nchini ni Mtaaluma Mkuu kwa suala la elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kisheria, Mtaaluma Mkuu Tanzania hii ni mmoja tu na yuko Wizara ya Elimu. Sasa TAMISEMI leo wamevaa utaaluma wa kutoa maagizo kwenye shule zetu zote, tena wanaingilia mpaka kwenye shule za *private*. Jambo hili ni gumu na limeshindwa kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAMISEMI wametoa mwongozo, ninao hapa nitakuletea kwa sababu upo kwenye simu, lakini kesho naweza nikauchapa vizuri nikakuletea. Nchi nzima, mashule yote binafsi na mashule ya TAMISEMI wameagizwa wafuate Kalenda ya Utekelezaji iliyotolewa na maafisa wa *secondary* ya *primary* pale TAMISEMI kwamba kuanzia mwaka huu shule zote nchini zifuate kalenda hiyo kwa vipindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama shule hii haina somo la mwalimu wa *physics*, basi wanaachwa wanakwenda kwenye somo lingine, ndiyo wanakuwa hawawezi kutekeleza ile kalenda. Shule ambayo imeshapata mwalimu wa *physics* na wanafundishwa, basi wasiende mbele mpaka wasubiriane kwa huyu mwalimu ambaye hakuwepo. Sijawahi kuona jambo kama hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali imeharibika mashulenii. Ukiwauliza wanasema maagizo yametoka juu. Yametoka juu kwa nani? Ukiwauliza Wizara ya Elimu wanasema yametoka TAMISEMI, ukiwauliza TAMISEMI wanasema Wizara ya Elimu haiwezi kutuingilia mambo kama haya. Jamani tunakwenda wapi katika nchi hii? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mheshimiwa Profesa hapa amezungumza jambo kubwa sana, hebu tutafute *regulator* wa elimu ni nani hapa nchini? Kwa sababu kama nilivyosema mwaka juzi, TAMISEMI wana shule zao, wanatakiwa wawe na mikakati yao namna ya kuendesha vipindi mashulenii na kufaulisha. Shule za Seminari zina utaratibu wao na shule za *private* zina utaratibu wao. Haya mambo yanatokea wapi? Leo hii wanasoma katika ile Kalenda yao, maana yake hakutakuwa na *revision* za *topics*. Maana wameacha wiki moja kabla ya mtihani wa mwisho kwa mwanafunzi wa Darasa la Saba ama wa *Form Four* ama wa *Form Two* ama *Form Six* maana yake nchi nzima hakutakuwa na *revision* katika masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kama ni somo gumu la hesabu, hakutakuwa na *topic* ya kufanya *revision* kwa sababu Kalenda ile inamtaka mwanafunzi asome hiki na kile, hata kama shule inakuwa kwenye mfumo wa michepuo; kwa mfano, shule niliyosoma mimi *O'level*, Mbeya Sekondari, ina 15. Masomo kama ya *cookery* yako pale, masomo ya dini yako pale na masomo mengine na vile vile masomo ya sayansi na ya biashara. Pia kuna shule za Kata kule Kapalala ina masomo nane mpaka tisa, unakuja kuwawekea ratiba moja katika mwaka mzima kwamba wataenda Pamoja; haliwezekani jambo kama hilli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali isitishe jambo hilli, ni baya. Siyo kwa shule za *private* tu, hata kwa shule za Serikali jambo hilli ni baya, haliwezekani. Wanatuvurugia elimu nchini. Kila mtu akiamka, anakuja anasema hilli. Umekuta mtu anasema kwenye *TV*; mara, kuanzia leo hakuna likizo za wanafunzi. Yaani mtu anaamka tu anakuja kuongea jambo kama hilli. Elimu ni shirikishi. Watushirikishe wadau, tuwe tunaongea masuala ya elimu. Hakuna mtu ambaye amezaa mtoto wake peke yake hapa. Wote wamezaa watoto hapa, twendeni kwa pamoja. (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui kama dakika zimeisha!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ahsante sana...

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Lah!

**MWENYEKITI:** ...kwa mchango mzuri sana. Hujaunga mkono hoja.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyikiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Benardeta Kasabago Mushashu.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wetu, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa mambo mazuri makubwa ambayo imeweza kutekeleza katika kipindi kifupi. Wametujengea madarasa 15,000 na kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania tumeweza kujenga madarasa mengi kiasi hicho na wanafunzi wote wameingia kwa mkupuo wote walioshinda kuingia kidato cha kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii vile vile imepunguza *pressure* kwa wazazi ambapo kwa kipindi hiki huwa wanahangaika kutafuta michango. Sasa hivi Serikali imepanga wanaenda kujenga shule 1,000 za Sekondari ili kuhakikisha kwamba kila Kata ambayo haikuwa na shule ya sekondari itakuwa imejengewa shule ya sekondari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mama ametoa shilingi bilioni 30, wanaenda kujenga shule za wasichana katika Mikoa 10. Kwa hiyo, sisi akina mama mnaotuona hapa, ambaao ni wasichana wa zamani, tulisoma kwenye shule za

wasichana za bweni, tukalelewa, tukalindwa, tukaepukana na mimba na ndoa za utotoni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaipongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita. Pamoja na kwamba tumejenga mashule mengi, lakini kwa sasa hivi tuna upungufu mkubwa sana wa walimu na hasa katika Mkao wa Kagera tuna upungufu mkubwa. Bila mwalimu huwezi kutoa elimu bora, mwalimu ni *centra/katika* kutoa elimu bora. Bila walimu wa hisabati na walimu wa sayansi, huwezi kuwa na watalaam ambao wanaweza kuleta hiyo tecknolojia tunayohitaji kwa ajili ya uchumi wa kati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza kwa Serikali kwamba watoe vibali walimu waajiriwe. Ila pale ambapo Serikali itakuwa hajatoa vibali, tunao walimu wengi waliohitimu wako mitaani, tunaomba vibali vitolewe kwa Halmashauri. Wawaajiri hawa walimu kwa kutumia own source kama part time teachers, watoto wetu wakasomeshwe. Itakapotokea kwamba vibali vya ajira vimetoka, hawa watimu wapewe kipaumbele cha kupewa ajira, lakini waendelee kufundisha watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu magonjwa yasiyoambukiza (*noncommunicable disease*) ni matatizo makubwa sana. Huko nyuma tulifikiri kwamba ni magonjwa ya matajiri, ni ya wazee, lakini sasa hivi wataalam wanatuambia, mtu ye yote yule anaweza kuugua. Hata watoto nao wameanza kuugua magonjwa kama kisukari, kansa, pumu, magonjwa ya akili, selimundu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia sasa hivi haya magonjwa yasiyo ya kuambukiza yanaua Watanzania kuliko hata magonjwa kama Malaria, Corona na Kipindupindu. Hata hivyo, haya yanababishwa na mtindo wa maisha. Tumeacha kutembea, tunakaa kwenye viti kwa muda mrefu, hatufanyi mazoezi, ulaji usiofaa; tunakula chumvi zaidi, tunakula mafuta zaidi; tunakula sukari zaidi, tunakunywa pombe kuzidi, tunavuta tumbaku, tunatumia madawa ya

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

kulevya, tuna misongo ya mawazo na vile vile hatupati usingizi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi huko kwenye Majimbo, huyu anaanguka na pressure, huyu anakufa na kisukari, na kadhalika. Ndugu zangu, haya magonjwa yasiyoambukiza yanaweza kuzuilika. Kwa hiyo, ni jukumu la kila mmoja kudhibiti haya magonjwa. Therefore, tunahitaji ushiriki wa wadau mbalimbali, tuyape umuhimu. Ndiyo maana sisi kama Wabunge, baada ya kuona kwamba kuna umuhimu wa kila mtu kushiriki katika kudhibiti haya magonjwa, tumeanzisha mtandao wa Wabunge katika kudhibiti haya magonjwa yasiyoambukiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali ipange bajeti ya kutosha kwa Wizara ya Afya ili waweze kutekeleza afua mbalimbali za kudhibiti haya magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile hata kwenye Wizara ya Michezo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma, wakati huo huo Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze anajiardaa.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nami nipongeze kwa kazi nzuri inayofanywa na Serikali kwa uwekezaji mkubwa uliofanyika kwenye sekta ya elimu na afya. Pia nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, ametembelea Mkoa wetu wa

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Manyara hasa Wilaya yetu ya Hanang, amehimiza wananchi na wananchi wamechangamka, wameelewa Serikali yao inachapa kazi kweli kweli na kazi inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie eneo la usambazaji wa dawa ambayo inafanywa na *MSD*. Kweli kuna changamoto kubwa kwenye maeneo na vituo vyetu nya afya kuna uhaba mkubwa wa dawa. Ninachoshauri, Serikali iangalie namna ya muundo mzima wa *MSD*. Tukiacha *MSD* kwenye utaratibu huu wa kawaida wakati, wengine mtu akiamka anaweza akanunua akapelekwa kwenye maduka, lakini *MSD* inapita kwenye mchakato wa manunuzi. Tuangalie namna muundo mwenyewe wa *MSD* ulivyokaa na namna ambavyo watatekeleza taratibu za manunuzi ya dawa kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ifanyike tathimini ya kina ya wadau wa *MSD* kwenye ule mnyororo wa usambazaji wa dawa. Ifanyike tathmini ya kina: Je, ni kweli kwamba wale wadau wote sio washindani wa *MSD* ambao wakati mwingine wako kwenye vituo vyetu na wao ni wafanyabiashara? Kwa sababu wanataka kufanya biashara, wanasababisha kwa makusudi dawa zisifike kwa wakati kwenye vituo ili zile dawa zilizoko kwenye maduka yao ziweze kuuzwa? Kwa hiyo, tathmini ya kina hiyo ifanyike ili tujue nani ambaye wakati mwingine anakwamisha dawa hizi kufika kwenye vituo vyetu nya kutolea huduma za afya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Mamalaka ya Dawa na Vifaatiba; kwenye eneo la kufuatilia ufanisi na ubora wa vifaa vile vikubwa, hasa vinavyotumika kwenye uchunguzi na tiba; Serikali imewekeza sana faida nyngi kwenye eneo hilo. Hivyo vifaa vikinunuliwa tuvifuatilie ufanisi wake. Hata hivyo ili vifaa hivyo vifanye kazi vizuri, vinahitaji matangenezo kinga (*prevent maintenance*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuhakikishe kwamba tunawaajiri wataalam wa kutosha wa kufanya hiyo kazi ya matangenezo ya vifaa tiba, lakini tuhakikishe kwamba tunawashirikisha kwenye hatua za awali zile za kufanya

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

manunuzi kwa maana ya kufanya uchaguzi wa teknolojia sahihi, lakini kufanya uchambuzi wa kina wa teknolojia wa vifaa tiba na hatimaye tuwashirikishe kwenye hatua ya uhamishaji wa teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwashirikishe vizuri hao wataalam. Sasa tunao wataalam wa kutosha wa vifaatiba, lakini Serikalini bado wataalam hao hawapo. Ninaishauri Serikali watoe ajira kwa wataalam kwa wataalam wa vifaa tiba. Tunavyo vifaa vingi kwenye sehemu zetu na vifaa vingi havifanyi kazi na sehemu kubwa ukiangalia, hatuna wataalam wa kuviangalia hivyo vifaa. Serikali iwekeze kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwekeze kwenye eneo la mafunzo ya wataalam wa vifaatiba. Walipo, ngazi ya mwisho ni Shahada. Tuwekeze kwenye Shahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamivu ili tafiti zifanyike hapa nchini tuanze kutengeneza vifaatiba vyetu wenye na hatimaye tuanze kujitegemea kama nchi badala ya kutegemea vifaa vingi tunavyoviagiza kutoka nje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niunge mkono hoja kwa sababu Kamati hii ni yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo anafanya kazi vizuri na pia kwenye jimbo langu amenijengeta madarasa 196. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nimshukuru na kumpongeza Mwenyekiti wetu wa Kamati kwa kuwasilisha taarifa vizuri.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najikita kwenye eneo moja kulingana na dakika ambazo ni chache; eneo la watoto wanaopata mimba katika shule zetu za Sekondari na Msingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza Serikali kwa jinsi ambavyo imeruhusu sasa watoto wale amba wamepata ajali ya kupata mimba watarudi tena shulen kusoma baada ya kuwa wanaendelea kunyonyesha. Hilo ni jambo jema na wananchi wamelifuarahia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili isije kuonekana Serikali sasa imeruhusu mimba za shulen. Hili ni jambo la kuangalia sana; kwamba kwanza kwenye familia zenyewe ambako hawa watoto ndiyo wanatoka, tuvunje ukimya, tuzungumze hili suala la mimba, tusiwafiche watoto wetu. Kama mwanaume utashindwa kuongea na kijana wako, basi tafuta namna ambavyo ujumbe utamfikia kijana wako, lakini kama huna uwezo wa kuongea na msichana basi tafuta hata shangazi aweze kuongea na huyu msichana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ni vizuri pia ije na mpango mwingine. Niliwahi kuzunguza wakati fulani kwenye semina nikasema Serikali ilete mtaala amba utasababisha kufundishwa wale watoto wafikie hatua ya kujua kwamba mimba inapatikana wakati gani. Kwa sababu ile ni ajali. Ni ajali. Hakuna mtoto anayetegemea kupata mimba, hakuna. Anakwenda kusoma ilia pate elimu. Kwa nini anapata mimba; anapata mimba kwa sababu ni ajali. Na anapata mimba kwa sababu wakati mwingine hajui kwamba ile mimba anaipatapataje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa wale ni wanafunzi na wanasoma, basi wafikishwe kwenye eneo la kalenda, kwamba ukitaka kuthubutu kufanya jambo hilo, basi tarehe hii na hii usithubutu hicho kitendo. Kabisa. Kama mwenzangu aliyechangia aliposema kwamba...

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, taarifa.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba kitendo cha ngono kwa mila na desturi za Mtanzania na kwa imani za dini zetu zote haipaswi mtoto kufundishwa namna ya kukifanya na kwamba kufanya hivyo ni sawa na kuhalalisha dhambi hiyo ya uzinzi. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendeleee.

**MWENYEKITI:** Unapokea taarifa Mheshimiwa Bidyanguze?

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendeleee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo lazima tulizungumze kwenye familia zetu lakini pia tulipeleke na shuleni. Bila kufanya hivyo Serikali itaonekana sasa kuruhusu hawa watoto waliopata mimba shuleni na warudi tena kusoma shuleni, itaonekana imehamasisha wanafunzi kupata hizo mimba. Naamini kabisa mimba zile zinapatikana kama vile ajali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niishauri Serikali; habari ya kukataa kufundisha somo hili tutakuwa tunajipoteza muda kwa sababu tunaposema kwamba kujamiihana ni dhambi, ni sawa ni dhambi, lakini lazima tufikie mahali kwamba *no*, usifanye ngono kipindi hiki na hiki, ndiyo. Tufike mahali hilo tuliseme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja tena. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa naita wachangiaji kutoka upande wa Serikali tutaanza na Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

(Sera, Bunge na Uratibu, Mheshimiwa Ummy Hamisi Nderiananga wakati huo Mheshimiwa Naibu Waziri, Pauline Gekul ajiandae. Muda wetu usizidi dakika zile zile tano, ukiongea dakika tatu au nne siyo mbaya.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote nipende kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuniamini na kunituea ili niwe Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu ninayeshughulikia Sera, Bunge na Uratibu. Namhakikishia Mheshimiwa Rais Samia kwamba sitamwangusha na kazi iendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitumie fursa hii pia kuwashukuru sana Kamati yetu chini ya Mheshimiwa Mwenyekiti, Fatma Toufiq na Wajumbe, kwa kazi kubwa na nzuri wanayofanya ya kuishauri Serikali katika mapambano dhidi ya Virusi Vya UKIMWI na dawa za kulevyta nchini. Niseme kwamba ushauri walioutoa sisi kama Serikali tumeupokea, tutaufanya kazi na tutaleta maendeleo ya yale tuliyofanya kazi katika Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la kuhamasisha wanaume kupima, naomba niseme kwamba Serikali imeendelea na mkakati wa kuwahamasisha wanaume kupima VVU na kujua afya zao. Tuna Mkakati unaitwa *Male Engagement Strategy*. Kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa Majaliwa, kwa kukubali kuwa balozi wa kuhamasisha wanaume kupima Virusi Vya UKIMWI. Kazi hiyo imeendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadri tulivyokuwa tunakwenda mbele tukaona tuboreshe programu hii na kuhamasisha kwamba tumeanzisha *plan* nyngine ambayo inaitwa *Male Involvement Culture Plan* ambayo itawajumuisha sasa watu wengi; wanawake, viongozi wa dini,

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

watu ambao ni maarufu katika maeneo yetu kuhakikisha kwamba wanashirikiana na wanaume kuwahamasisha. Nitumie fursa hii kuwahamasisha wanaume mliopo humu Bungeni na ninyi kumuunga mkono Mheshimiwa Waziri Mkuu ili kupima afya zenu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika programu ya vijana Kamati imetushauri vizuri sana na tunawashukuru sana Kamati kwa kutambua na kuona kwamba eneo hili la vijana linatakiwa kupewa mkazo wa hali ya juu. Nipende kuwaambia vijana wote nchini Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan na Serikali nzima tunawathamini na tunawapenda sana vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana hata mimi kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nilizindua programu maalum ya vijana kwenye redio na tv inaitwa *Ongea Programme* ipo katika *East Africa Radio* na *Clouds Media* tunashirikiana nao pia na mtandao wa *Instagram* kuhakikisha tunatoa elimu kwa vijana wetu na tutaendelea kuhakikisha kwamba tunawafikia vijana wengi zaidi na zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwatoe wasiwasi; kazi inaendelea vizuri, Ofisi ya Waziri Mkuu tumejipanga vizuri na maoni yote ya Waheshimiwa Wabunge tumeyachukua na tutayafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Sasa namwita Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Pauline Gekul, aweze kuhitimisha.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi. Pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kutupa afya njema siku ya leo kutimiza wajibu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami pia kwa niaba ya Waziri wangu, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, nimshukuru Mheshimiwa Rais kuendelea kutuamini tuweze kuhudumu katika Wizara hii muhimu ya Sanaa, Utamaduni na Michezo. Mheshimiwa Rais tunakushukuru sana pamoja na Makamu wa Rais na Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu ni Wizara mtambuka, ina sekta tatu, inagusa maisha ya Watanzania lakini ajira kwa vijana wetu. Nishukuru Kamati yetu ya Bunge ya Huduma za Jamii chini ya Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti pamoja na Wabunge wenzetu, wamekuwa wakitushauri kwa dhati namna gani tunaweza tukafanya vizuri katika sekta hizi ambazo ni muhimu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi nimshukuru Mheshimiwa Rais pamoja na Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Wamekuwa wakituelekeza tufanye nini kwenye sekta ya sanaa, sekta ya michezo na sekta ya utamaduni. Nianze kwenye sekta ya utamaduni; Kamati kwa ujumla imezungumzia mambo matatu, imezungumzia suala la BMT, suala la Bodi ya Filamu na BAKITA, nami nitajikita huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa utamaduni nishukuru sana jitihada ambazo anazifanya Mheshimiwa Rais wetu, mama Samia Suluhu Hassan. Rais wetu wakati anakuza diplomasia ya uchumi pamoja na wasaidizi wake wametusaidia sana kwa upande wa utamaduni na kwa upande wa kukuza Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana UNESCO imetangaza Siku ya Kiswahili Duniani tarehe 7 Julai. Hizi ni jitihada za Mheshimiwa Rais wetu, mama Samia Suluhu Hassan, pamoja na wasaidizi wake. Sisi Wizara tunawashukuru kwa sababu kazi yetu inakuwa imerahisishwa na viongozi wetu na wamekuwa wakitupa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo halitoshi, chini ya Mheshimiwa Rais wetu, mama Samia Suluhu Hassan tumeona juzi tarehe 6, mwezi huu wa Februari wakati Makamu wa Rais

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

akituwakilisha, akimwakilisha Mheshimiwa Rais wetu katika vikao nya Wakuu wa Nchi na Serikali katika Makao Makuu ya Afrika, pale Ethiopia, Makamu wa Rais alipeleka maombi maalum kwa niaba ya nchi yetu na kwa niaba ya Mheshimiwa Rais wetu kwamba Kiswahili sasa iwe lugha ya kazi. Mheshimiwa Rais tunakushukuru sana na AU waliridhia hili. Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu, hii ni hatua kubwa sana kwa Taifa letu lakini pia kwa sekta yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge na sisi tumefanya nini? Kwa kuwa mmezungumzia kupitia Kamati hii, kazi ambayo tumefanya, tumeielekeza BAKITA – Mheshimiwa Waziri Mkuu tunamshukuru sana, alikuwa BAKITA juzi, ametupa maelekezo mahususi. Sisi na BAKITA tumeandaa mpango mkakati wa kubidhaisha Kiswahili wa miaka kumi, kuanzia 2021 mpaka 2031 ambao una thamani ya bilioni 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hii inaendelea chini ya BAKITA, dada yetu Consolatha na timu yake wanafanya kazi nzuri na hata balozi mbalimbali wameshaanza kupata wataalam kupitia BAKITA; Ubalozi wa Korea Kusini, Nigeria na Balozi zingine kazi hii imeanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kazi hii tunaifanya kwa kasi kubwa na tunaamini pia kadri ambavyo wanatupitishia bajeti kazi hii itakuwa rahisi sana. Hii ni heshima kwa Taifa letu na tunaomba tumpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kweli kwa kazi hii ya kubidhaisha Kiswahili na kutuelekeza na tunamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu na kubwa, tunamshukuru pia Makamu wa Rais kwa hili. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine lilikuwa ni suala la Baraza la Michezo (BMT). Kamati imeshauri mambo kadhaa na wamekuwa wakitusshauri sana kwa upande wa michezo. Wametushauri tuongeze mahusiano na Serikali za Mitaa, ma-DAS na ma-RAS wetu ni Wenyeviti katika Mikoa yetu kusimamia michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati wamezungumzia pia kuhakikisha utawala bora unapatikana katika vyama na vilabu vya michezo. Kwa niaba ya Waziri wangu, Mheshimiwa Mchengerwa, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba. kazi hii tunafanya, na tumekuwa tukifanya vikao na Maafisa Utamaduni na Maafisa Michezo, lakini ma-RASna ma-DASwetu tukipeana maelekezo nini cha kufanya kuboresha michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisipowapongeza Waheshimiwa Wabunge...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja.  
(Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy Mwalimu.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kuongea katika Bunge hili la Kumi na Mbili kama Waziri wa Afya, niruhusu nianze kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniamini kuendelea kuwa msaidizi wake. Nimwahidi Mheshimiwa Rais, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwamba mimi na Mheshimiwa Dkt. Mollel tutaifanya kazi hii kwa kasi, ubunifu na weledi katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze pia kwa kuunga mkono hoja za Kamati zetu mbili; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii pamoja na Kamati ya UKIMWI. Niishukuru sana Kamati zetu zote mbili na Waheshimiwa Wabunge kwa maoni na ushauri. Tumepokea na niwaahidi kwamba tutafanyia kazi.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda niseme mambo makubwa matatu. Jambo la kwanza ambalo limeongelewa kwenye Kamati na Waheshimiwa Wabunge ni suala la upatikanaji wa dawa. Katika Bunge hili zamani tunapoongea suala la dawa tulikuwa tunaongea ukosefu wa fedha za dawa, lakini tunamshukuru Rais Samia suala la dawa siyo suala la ukosefu wa fedha za dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kukiri kwamba tunahitaji kujipanga zaidi katika kuhakikisha kwamba dawa zinapatikana, kwa sababu tangu Rais Samia ameingia madarakani tayari Serikali imeshapeleka *MSD* zaidi ya bilioni 333. Sasa hivi kila mwezi tunapokea bilioni 15 kwa ajili ya dawa, vifaa na vifaatiba.

Kwa hiyo nikiri kweli, maana ukificha maradhi kifo hukuumbua, halii ya upatikanaji wa dawa hairidhishi. Kwa hiyo tunaangalia, tutaendelea kuboresha utendaji wa *MSD* ili iweze kutekeleza kikamilifu majukumu yake ya ununuzi, utunzaji na usambazaji wa dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili nilishafika *MSD* nikawaambia badala ya kupima upatikanaji wa dawa kwa kuwa na dawa za mwezi mmoja tutawapima kwa kuangalia dawa za miezi mitatu. Kuna Mheshimiwa Mbunge amesema dawa zinapelekwa wiki moja zinaisha kwa sababu dawa za miezi mitatu zinapelekwa dawa za siku mbili au tatu. Kwa hiyo hili tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, siyo tu *MSD*, *MSD* anaweza aka-*procure* dawa, lakini upatikanaji wa dawa katika ngazi za vituo vya kutoa huduma za afya kuanzia zahanati hadi hospitali zetu. Kwa hiyo pia tutaimarisha usimamizi wa suala zima la upatikanaji wa dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye usimamizi tumeona, na nashukuru Kamati pia imezungumzia suala la ulinganifu wa usambazaji wa dawa kwenye vituo. Kwa hiyo tutafufua zile timu za upembuzi yakinifu wa mahitaji ya dawa kulingana na magonjwa katika eneo husika.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, saa nyingine navyo vituo vyetu kila mtu anajua *top ten diseases* katika eneo lake. Sasa badala ya kufanya *quantification* ya dawa anazohitaji kwa watu anaowahudumia analeta makisio madogo; kwa hiyo hili pia tutalifanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kwa upande wa usimamizi wa dawa, kuna Mwongozo wa Taifa wa Matibabu (*Standard National Treatment Guidelines*), inasema dawa gani zinatakiwa zitolewe katika *level* gani. Tumeona, watu wetu badala ya kutoa, sisi kama Serikali tunatumia dawa ambazo ni *generic*, siyo *brand*, kwa hiyo unakuta mtu ameandikiwa *paracetamol/daktari anamuandikia Panadol, Panadol/hazipo* katika vituo vyetu vya kutoa huduma za afya kwa sababu ile ni *brand*, sisi tunatumia *generic*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dawa ya matibabu ya maambukizi kwa mfano, *flagyl*, *flagyl* ni *brand*, kwa hiyo daktari unapomwandikia mgonjwa *flagyl*/wakati mwongozo unakwambia ni *metronidazole*, tumeona pia ni tatizo, kwa hiyo tutaimarisha wataalam wetu wazingatie Mwongozo wa Taifa wa Matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda unakwenda. Suala la pili ni suala la bima ya afya kwa wote... kabla ya hili, *MSD* kuhusu uzalishaji wa ndani wa dawa tunashukuru sheria imepita na tayari Serikali imeshatoa fedha zaidi ya bilioni 15.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja...

**MWENYEKITI:** Nakuongeza dakika moja uzungumzie hilo suala la bima ya afya kwa wote.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bima ya afya kwa wote, tumepokea maoni na ushauri. Tayari tulishakwenda kwenye Baraza la Mawaziri, tumepokea

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

maelekezo ya Baraza la Mawaziri, tumeyafanya kazi sasa hivi tuko tayari kurudi tena kwenye Baraza la Mawaziri kwa ajili ya kuomba kuitisha Sheria hiyo ya Bima ya Afya kwa kila Mtu. Kwa sababu tunaamini kwa kweli ndiyo itaweza pia kuwawezesha Watanzania kupata huduma bora za afya bila ya kikwazo cha fedha. Tunaona Watanzania wanauza mashamba yao, wanauza baiskeli pale ambapo wanapata mgonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tumepokea maoni na ushauri kuhusu *non-communicable diseases* (magonjwa yasiyo ya kuambukiza), tutawekeza kwenye elimu pamoa na *community health workers* (wahudumu wa afya ngazi ya jamii) ili waweze kutoa elimu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, tayari ameshaanza kuratibu *implementation* ya *activities* mbalimbali katika mapambano dhidi ya magonjwa yasiyo ya kuambukiza. Kwa hiyo suala hili tayari Waziri Mkuu yupo *on-board* na analisimamia kwa ukaribu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, tunashukuru kwa maoni na ushauri na tutayafanya kazi. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda aweze kuchangia hoja.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa sababu nami ni mara yangu ya kwanza kuzungumza baada ya Mheshimiwa Rais kunitua kuwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kutoa shukrani nyingi kwa Mheshimiwa Rais kwa uteuzi huu na kumwahidi kwamba tutafanya kazi kwa bidi, timu yote, kwa ajili ya kuleta mabadiliko ambayo sote tunayatarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vilevile kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa fedha hizi za ahueni

ya UVIKO ambazo sekta ya elimu kwa ujumla wake ndani ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na TAMISEMI tumepata zaidi ya bilioni 300 ambayo kwa kweli inatusaidia sana kusonga mbele, hasa katika suala la miundombinu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeisikiliza vizuri Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii. Tunamshukuru sana Mwenyekiti, Mheshimiwa Stanslaus Nyongo na Wajumbe wote kwa taarifa nzuri ambayo tutazingatia sana ushauri ambao wameutoa. Napenda kuhukakishia vilevile tutazingatia ushauri ambao umetolewa na Waheshimiwa Wabunge kwa mapana yake katika utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda kueleza vitu vichache ambavyo vinahitaji uafanuzi. La kwanza ambalo linaweza likawa linazusha tataruki ni kuhusu *transition* ya wanafunzi kutoka darasa la kwanza mpaka la saba kuanzia *form four* kwenda *form five, form six*, kwamba tuna *dropout* kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zetu hazzoneshi kama *net enrollment rate* hata *gross enrollment rate* Tanzania ni mbaya. Tulipata *peak* kubwa sana ya *enrollment* baada ya Serikali kutangaza kutoa elimu bure, na *enrollment* iliongezeka sana mwaka 2016. Ili tuweze kuona picha vizuri najaribu kutoa takwimu za wanafunzi waliofanya mtihani Darasa la Nne na waliofanya mtihani Darasa la Saba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia wanafunzi waliofanya mtihani Darasa la Nne mwaka 2018, walikuwa ni 1,362,642 na walipofika Darasa la Saba 2021, waliofanya mtihani ni 1,132,084. *Noteworthy alarming* lakini haturidhiki na *transition* hiyo na hao ambao wame-drop hapo katikati. Hata hivyo, *figure* siyo kubwa kama ambavyo imekuwa *alluded to*, hapo mwanzoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hizi takwimu ni vizuri kama tunataka kuziangalia kwenye *NBS, net enrolment rate* ambayo inaonesha watu ambao kwa umri fulani

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

walitakiwa wawe darasa fulani, na wangapi bado wapo katika darasa hilo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hivyo, ningependa nieleze kwamba Serikali hasa chini ya Uongozi wa Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, imejikita sana kuhakikisha kwamba wale wote ambao wana-*drop* shulenii kwa sababu mbalimbali, wanarudi shulenii. Ndiyo maana ya maelekezo ya Mheshimiwa Rais tumetoa mwongozo, tumeusambaza, kuonesha namna gani ya kuwarudisha tena wanafunzi ambao walilacha shule kwa sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na wale ambao walipata ujauzito; na wengine kwa sababu walikuwa na changamoto ambazo hawakuzijua. Kwa mfano, mwanafunzi alikuwa na matatizo ya kusoma hakujua kwamba anahitaji miwani, akaacha shule. Baadaye akagundua kumbe nahitaji miwani, anataka kurudi shulenii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunajaribu kutoa fursa kwa kila mwanafunzi ambaye hata kama alikuwa ameshaacha shule, aweze kurudi shule na kuendelea kusoma ili tuhakikishe kwamba namba zinaongezeka kutoka hizi namba ambazo nilikuwa nimezieleza hapo katikati. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeshauri sana suala la kuongeza ajira hasa ya walimu; na ni kweli kuna upungufu mkubwa wa walimu. Serikali imewekeza sana sasa hivi kama tulivyoona katika miundombinu ya ufundishaji hasa madarasa na vifaa vilevile vimenunuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ukweli ni kwamba bado tuna upungufu mkubwa wa walimu. Wengine mtakuwa mlimsikia Mheshimiwa Rais wakati anapiga simu kuongea na walimu na wanafunzi wa *Benjemin Mkapa Secondary School* pale Dar es Salaam. Alieleza kwamba baada ya miundombinu, kazi kubwa sasa hivi ni kuajiri walimu ili kuhakikisha kwamba tunapata walimu wa kutosha.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika moja nielezee suala la mitaala ambalo kidogo ni muhimu, niache haya mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati vilevile imeeleza na Waheshimiwa Wabunge wamesisitiza tumalize mapema iwezekanavyo mapitio ya mitaala na ndicho tunachojaribu kukifanya. Hata hiyo tarehe ambayo imewekwa tungetaka tumalize kabla ya hapo. Pia ningependa tuzingatie kwanza kwamba mitaala hii inaongozwa na Sera. Sera ya 2014 inafanyiwa mapitio, Sheria, halafu mitaala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukiangalia Sera ya 2014 inaelezea miaka sita ya elimu ya msingi; elimu ya lazima mpaka *Form Four*. Maana yake ni kwamba hata mitaala inapotengenezwa lazima izingatie suala hili, endapo sera itakapofanyiwa mapitio, tutabaki na vigezo hivyo hivyo. Kwa hiyo, tunafanya mapitio ya sera na wakati huo huo tunapitia mapitio ya sheria na tunapitia vilevile mitaala. Pia kama Kamati ilivyoshauri, tunapitia mitaala siyo kwenye elimu ya msingi tu, ni pamoja na Vyuo na Vyuo Vikuu, na miongozo imetolewa na kazi inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naona kengele imeshagongwa, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Prof. Mkenda kwa kutoa mchango wako. Sasa nawaita watoa hoja. Tutaanza na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Stanslaus Nyongo ili aweze kuhitimisha hoja yake kwa ufupi na kisha tutakukaribisha Mwenyekiti mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, karibu. (*Makofii*)

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA YA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Niendelee

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

tu kushukuru na kupongeza sana Wabunge wote. Tumepata wachangiaji 15; na kwa kweli Wabunge wote wameunga mkono hoja, hakuna hata mmoja aliyepinga. Vilevile, tumepata wachangiaji ambapo tunesikia Naibu Mawaziri wawili ambao wamechangia pamoja na Mawaziri wawili ambao wametoa ufanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati niendelee kupongeza sana Mawaziri hawa, wamefanya kazi vizuri na Kamati yangu kama unavyoifahamu ina sasa Wizara nne. Kwa kweli mambo ni mengi na tulipata muda mdogo kidogo wa kuweza kutoa ufanuzi. Pia tumetoa kwenye maandishi na kila Mbunge anaweza akapitia na imeonesha ni jinsi gani ambapo Kamati imeweza kutoa ushauri kwa kina kwa wizara zote hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nisilitize mambo mawili matatu kwa kila sekta. Mambo makubwa yaliyojitekeza, kubwa ni hili suala la; kwanza kabisa tunaipongeza Serikali kwa kutoa fedha nyingi kwenye fedha hii ya mkopo ambayo ni shilingi triliuni 1.3 ambapo kwa kweli Mheshimiwa Rais ameitendea haki nchi yetu kwa kuweza kuelekeza hizi fedha ziende zikajenge miundombinu ya elimu na afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika fedha hizi zimekwenda karibu shilingi bilioni 800 na ushei, ambazo zimekwenda kwenye miundombinu ya elimu na afya. Nii sawa sawa na kama 75% hivi zimekwenda kujikita kwenye kupeleka huduma kwa wananchi. Jambo hili kwa kweli Mheshimiwa Rais tunapongeza sana kwa sababu hii changamoto ilikuwa ni kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulivjosikia Wabunge, pamoja na kutoa pongezi hii, ni kwamba tuna upungufu mkubwa sana wa watumishi wa afya na elimu. Kwa wastani, kwa sekta zote hizi mbili tunaona kabisa tuna upungufu wa watumishi karibia 50% kwa kila sekta. Walimu pamoja na madaktari na watumishi wa afya, kwa kweli naipongeza Serikali, Waheshimiwa Mawaziri wamezungumza, lakini kwa

kweli Serikali ichukue juhudzi za kipekee kuhakikisha kwamba tunaajiri watumishi wa sekta ya elimu na afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa walimu, tuhakikishe tunazalisha walimu wenye ubora. Tunaweza tukawa na madarasa ya kutosha lakini kama hakuna walimu, bado watoto wetu wanawea wasipate elimu inayostahili.

Kwa hiyo, tunapenda kuishauri Serikali na kuisisitiza kwamba tuzalishe walimu wa kutosha ili waende wakawafundishe watoto hawa. Kwa kweli juhudzi zilizofanyika ni kubwa, kwa hiyo, lazima tukamilishe kwa kuweza kupeleka walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo, tunawapongeza sana Wizara ya Afya, walitoa mwongozo wa masuala ya kuulinda au kuhakikisha kwamba wale wafanyakazi au watumishi wasiokuwa na ajira, wanaojitolea (*volunteers*) waweze kwenda kufanya kazi kwenye vituo vya afya na zahanati. Kwa kweli hili nalo lifanyike kwa Wizara ya Elimu. *Volunteerism* ifanyike ili kusudi watu wapelekwe kule hata ambao hawana ajira, basi itafutwe namna bora au *program* bora ya kuajiri kama *parttime* ili waweze kutoa huduma kwa wananchi, kwa sababu wananchi wanahitaji huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fikiria kijiji kilikuwa hakina zahanati, leo kina zanahati, majengo yamejengwa pale, lakini hakuna mganga; *what do you expect?* Wale ambao hawajaajiriwa, basi waende pale wakatoe huduma kwa wananchi halafu iangaliwe namna ya Serikali kuwalipa hawa hata kama ni kidogo, basi waweze kutoa huduma. Ajira ikija, siku mkiamua kuajiri hawa waliojitolea muwape kipaumbele cha kuwapa ajira. Kama ni walimu wapewe ajira kwa kipaumbele kwa sababu walijitolea; na kama ni waganga na manesi, nao wapewe kipaumbele cha kupewa ajira kwa sababu wamejitolea na kwa kweli wametoa huduma na wameshirikiana na Serikali katika wakati mgumu, nao muweze kuwajali. (*Makof*)

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *MSD* limezungumzwa na kila Mbunge hapa. Suala la upatikanaji wa dawa, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri ametoa ufanuzi, lakini *MSD* iwezeshe. *MSD* kama haijawezeshwa, bado litakuwa ni tatizo. Tunashukuru kwamba fedha zimetolewa shilingi bilioni 373 lakini kuwezeshe huko, na mfumo urekebishwe wa kuweza ku-monitor usambazaji wa dawa. Kama hakuna mfumo thabiti, upotevu wa dawa utakuwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunawapongeza sana *MSD* kwa kuamua kuzalisha dawa, tumeona *essential drugs* zinazalishwa na Keko *Pharmaceuticals*; tumekuta uzalishaji *a hundred percent*. Sasa kama uzalishaji wa *essential drugs* upo kwa 100%, kwa nini kunakuwa na upotevu na huu upungufu wa dawa kwenye vituo vyta dawa? Kwa sababu wanaangalia mahitaji na uzalishaji, sasa huu upungufu umetokea wapi? Inaonekana hapa katikati kuna upotevu wa dawa. Basi ingaliwe namna ya kuwekeza katika kuweka mifumo mizuri ya kuweza kuhakikisha dawa inasimamiwa wakati wa kuzalisha, wakati wa kununua, wakati wa *ku-stock*, kusambaza na kupeleka kwa wagonjwa na watumiaji. Hili ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasisitiza hivi kwa sababu gani? Kama tumeweza kujenga Kituo cha Afya kwa shilingi milioni 400, umejenga zahanati kwa shilingi milioni 100, umejenga Hospitali ya Mkoa kwa mabilioni ya fedha, tunashindwa nini *ku-invest* kwenye Kituo cha Afya shilingi milioni tano ya kuweka mfumo ambao uta-*monitor* mapato, dawa, matumizi na kuwezesha kujua kwamba *stock* hii ipo eneo hili na hili na *stock* hii kuna upungufu eneo lingine, mfumo unakueleza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri, kwenye *blood bag* imeonekana. Kuna maeneo *MSD* wametueleza *blood bag* ipo Mkoa X, halafu Mkoa Y hakuna *blood bag*. Maana yake nini? Pangokuwa na mfumo unao-*monitor* Mkoa X una *blood bag in excess*, basi huo mfumo umwelekeze *blood bag* zitoke Mkoa X kwenda ku-*supply* Mkoa Y ili hawa watu wa

Mkoa Y nao wapate *blood bags*. Hili ni suala la mfumo tu. Kwa hiyo, tunasisitiza sana mfumo ufungwe katika *ku-monitor* hizi shughuli za *ku-control stock*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *issue* ya mitaala, tunaishukuru sana Serikali, wameeleza vizuri na mwaka 2026 tunategemea kwamba tutapata mitaala mipya na ianze kufundishwa. Tunasisitiza waendelee kufanya kwa haraka, lakini lazima uangalie, mtoto anayemaliza Kidato cha Nne ambayo sasa hivi tumesema ndiyo *basic education*, mnapomfundisha, basi afundishwe na utaalam, atoke na utaalam fulani ili hata asipoendelea Kidato cha Tano, akienda mtaani awe utaalamu fulani wa kuweza kufanya kazi. Atakapomaliza chuo cha kat, awe na ujuzi, yaani tupate namna ya kupata wataalam wadogo wadogo ambao wanaweza kwenda kuzalisha katika viwanda vidogo vidogo. Hili ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la michezo limezungumzwa vizuri, tuwekeze. Hizi kampuni zinapotoa misaada kwenye michezo, basi ile gharama inayotolewa kwenye michezo iwe inatambulika kwenye mahesabu ya kikodi, kwamba mtu anaye-*finance*; mfano, kampuni imetoe fedha ya kununua mipira, iweze kutambulika kikodi ili waweze kupunguziwa katika *corporate tax*. Hili ni jambo la muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie suala la Mheshimiwa Mulugo; suala hili linatisha kwa kweli kama kweli hiyo hali ipo. Tunaomba wadau pamoja na Serikali tukae, tujadili tuone. *Ku-control*/ufundishaji kwamba mwezi wa Tatu *topic* moja na mbili ziwe zimeshafundishwa, hiyo sawa; lakini kumzuia mtu kufundisha zaidi eti kwa sababu anawahi sana, hilo tunaomba tukae na kuweza kuli-review. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kuhusu mimba za utotonii Mheshimiwa Bidyanguze amezungumza vizuri, tunahitaji elimu, watoto tuwafundishe. *Biologically* mtoto akishakuwa *matured* anapokwenda kwenye *secondary growth* ana-develop kitu kinaitwa *ovulation period*, ndiyo kipindi cha hatari yeye kupata ujauzito. Aambilie kipindi hiki

## **NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

kina dalili zipi, ili asijihusishe. Bila ya kufanya hivyo, tutaendelea na *dropouts* kwa watoto na utoro utaongezeka na hii inakuwa ni hasara kwa Taifa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA YA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Basi baada ya kusema hivyo, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**MHE. KASSIM HASSAN HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja IIitolewa Iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunashukuru, tutawahoji hapo baadaye.

Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi, Mheshimiwa Fatma Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge waliochangia katika Taarifa yetu ya Kamati ya Masuala ya UKIMWI kwa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia ni saba, lakini pia upande wa Serikali tumepata ufanuzi kutoka kwa Mawaziri wawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wabunge waliochangia, naomba kwanza nianzie upande wa Serikali ambapo Naibu Waziri wetu Mheshimiwa Ummy Nderiananga, ameipongeza sana Kamati na amekubali kwamba ushauri wote ambao Kamati tumeutoa utachukuliwa na utakwenda kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, naomba kwa niaba ya Kamati niendelee kuipongeza sana Serikali na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa kinara wa kuhamasisha wanaume kwenda kupima. Naamini kabisa, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kinara, basi wanaume wengi zaidi watajitokeza na jamii kwa ujumla watakwenda kupima ili kusudi tuweze kupunguza hili suala zima la maambukizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Naibu Waziri amezungumzia kuhusu *programs* za vijana, tunashukuru sana. Basi nasi tunaendelea kusisitiza *program* hizi ziendelee ili kusudi tuweze kuwanusuru vijana wetu, kwa sababu tumeona kwamba kundi ambalo limeonesha kabisa kwamba linaathirika kwa sana ni la vijana kati ya miaka 15 – 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy Mwalimu amezungumzia kuhusu suala zima la elimu hasa kwa *Community Health Workers* kuhusu magonjwa yasiyo ambukiza. Tunashukuru sana kulichukua hilo, tunaamini kabisa yote yatafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, amezungumzia kwamba uratibu umeshaanza chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa hiyo, hili nalo sisi kama Kamati tunaendelea kuishauri Serikali ione namna bora kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu *i-take lead* kwa sababu hili Jambo ni suala mtambuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, naomba niendelee kuipongeza sana Serikali hasa kwenye hili suala la magonjwa yasiyoambukiza kwa sababu kumekuwa na *political will*, tumeona kabisa jinsi gani Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan amekuwa akiongoza matembezi ili kuhakikisha kwamba Watanzania tunaendelea kuwa afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, tumeona Mheshimiwa Makamu wa Rais akiongoza matembezi na Mheshimiwa Waziri Mkuu; yote haya

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

inaonesha kabisa kwamba Serikali ina nia ya dhati kabisa kuhakikisha kwamba suala zima la magonjwa yasiyoambukiza nchini kama siyo kupungua basi linakwisha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niende kwa Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia hoja hii. Jumla ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia ni saba, akiwemo Mheshimiwa Abdul-Hafar, Mheshimiwa Neema Mwandabila, Mheshimiwa Tecla Ungele, Mheshimiwa Dkt. Chaya, Mheshimiwa Dkt. Alice, Mheshimiwa Dkt. Nyamoga na Mheshimiwa Mama Mushashu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ushauri wao, tumegundua kwamba jambo kubwa ambalo limezungumziwa hasa kwenye suala zima la Ukimwi, ni kuhusu *Aids Trust Fund*. Miongoni mwa ushauri ni kwamba hii kuwe kuna chanzo mahususi cha kutunisha mfuko huu. Naamini kwamba hili Serikali watakuwa wamelipokea, kwa sababu tunatamani hili suala la afua ya Ukimwi, fedha zitokane na sisi kwa fedha zetu za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwenye suala zima la elimu ya Ukimwi ni kuhusu matumizi ya *condom*. Mheshimiwa Abdul-Hafar amesisisitiza suala la matumizi ya *condom* na pia kuhabarisha vijana wetu ili kusudi wasiende kuianza ngono mapema, lakini kama ikibidi, basi waweze kutumia zile njia za kujizua ili mwisho wa siku wasiweze kupata maambukizi mapya.

Meshimiwa Spika, jambo lingine ambalo limezungumziwa ni kuwepo na Tume itakayoshughulikia maradhi yasiyoambukiza. Hapa Waheshimiwa Wabunge watatu wamelizungumzia hili, nami kama Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Kamati yetu, katika taarifa yetu, maoni na ushauri pia tumelizungumzia hili kwamba, kama ikiwezekana, basi tunaishauri Serikali iundwe tume maalum ya kuweza kushughulika na masuala ya magonjwa yasiyoambukiza; na ikiwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu,

itakuwa ni nzuri zaidi kwa sababu hili ni jambo linahusu masuala mtambuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine uliotolewa kwenye *issue* ya elimu ya magonjwa yasiyoambukiza ni kwamba lazima kuwepo na suala la elimu ili watu waweze kujua, waweze kuchukua tahadhari mapema na kuweza kujinrusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Waheshimiwa Wabunge wote wameongelea kuhusiana na suala zima la elimu ili kusudi wananchi au jamii iweze kuchukua tahadhari mapema wasiweze kupata magonjwa yasiyoambukiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limetolewa ushauri ni kuhusiana na wataalam wa *physiotherapy*. Mheshimiwa aliyetoea ushauri huu ni Mheshimiwa Nyamoga, kwamba wataalam hawa inhabidi waende hadi katika ngazi ya Wilaya na ikiwezekana Serikali ione umuhimu sasa wa kujenga vyuo vya kutosha vya *physiotherapy* kwa sababu inaonesha kabisa kwamba magonjwa ya kuambukiza yanaongezeka. Kwa hiyo, hii itasaidia kukidhi magonjwa yasiyoambukiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limezungumziwa ni kubadili mtindo wa maisha. Kwamba ili kuweza kukabiliana na suala zima magonjwa yasiyoambukiza, tuweze kubadilisha mtindo wetu wa maisha ili mwisho wa siku tuweze kuyazuia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limezungumziwa ni kuhusiana na madawa ya kulevyo, ambapo imezungumziwa kuhusiana na waraibu kwamba itakuwa ni vizuri waweze kupatiwa miradi. Kwamba, kuna vituo ambavyo vimekuwa vikitoa hii huduma ya *methadone* na kuna waraibu wengine ambao wamekuwa wakipona kabisa. Sasa je, baada ya kupona wanakwenda wapi? Basi, Serikali ione umuhimu sasa wa kutafuta miradi midogo midogo kama ikiwezekana kuwapa mikopo na kadhalika hao waraibu ili kusudi waweze kurudi katika maisha yao.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, suala la lishe limeonekana kwamba nalo pia ni muhimu ili mwisho wa siku hawa vijana wanaotumia *methadone* waweze kupata lishe ambayo ni bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Haya yote naamini kabisa kwamba Serikali itayachukua na kuyafanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu kuunga mkono hoja yetu ya Kamati ya Masuala ya Ukimwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

*(Hoja IIitolewa lamuliwe)*

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa tutakwenda kwenye hatua nyingine kwa mujibu wa Kanuni ambapo nitawahoji.

*(Hoja IIitolewa lamuliwe)*  
*(Hoja IIiamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Maoni na Mapendekezo ya Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii Pamoja na Maoni na mapendekezo Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI yalipitishwa kuwa maazimio ya Bunge)*

**MWENYEKITI:** Tunaishukuru sana Serikali kwa jitihada zake ambazo imezifanya ambapo kwa kuitia Kamati yetu tumeona kazi kubwa iliyofanyika, imeweza kuchambua mambo mengi, lakini hasa juu ya kazi kubwa iliyofanyika kwa zile fedha; shilingi trillioni 1.3. Sisi kama Bunge tumeona na tumeshuhudia zaidi ya shilingi bilioni 800 zimeingizwa kule na

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

tumejenga madarasa zaidi ya 15,000. Kati ya hayo 12,000 shule za Sekondari na 3,000 shule za Msingi; madawati karibu 600,000 ya Sekondari na 120,000 shule za msingi na hivyo kuwezesha wanafunzi zaidi ya 907,000 na kitu kuweza kuanza bila shida mwaka huu. Tunaipongeza sana Serikali. (*Makofi*)

Tunampongeza sana Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa usimamizi thabiti katika eneo hili. Tunashukuru pia kwa maoni mazuri ambayo yametolewa na Kamati, tunaamini Serikali itakwenda kuweka mkakati mzuri wa kufanya kazi ikiwemo ku-*fast-track* Mfuko wa Bima kwa Wote ambao tunaamini unakwenda kuwa na tija kubwa kwa wananchi wa nchi yetu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa tumefika mwisho wa shughuli yetu ya leo. Hivyo naahirisha Bunge mpaka kesho tarehe 11 Februari, 2022 saa 8.00 mchana.

*(Saa 12.45 Bunge lilahirisha hadi siku ya Ijumaa,  
Tarehe 11 Februari, 2022 Saa Nane Mchana)*